

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 27 Aprili, 2020

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Naomba tukae Waheshimiwa. Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani Na:-

NAIBU WAZIRI WA MAJI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

MHE. ZUBEDA H. SAKURU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA MAJI:

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. KHADIJA H. ABOUD - MWENYEKITI WA KAMATI YA
KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA YA BUNGE YA KILIMO,
MIFUGO NA MAJI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa Maji kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

SPIKA: Ahsante sana. Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH -KATIBU MEZANI

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yameuillezwa na kujibilwa kwa njia ya mtandao)

Na. 154

Kumtua Mama Ndoo Kichwani

MHE. MARY P. CHATANDA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza matatizo ya maji na kumtua ndoo mama kichwani nchini?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda Mbunge wa Korogwe Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Tanzania. Katika jitihada za kukabiliana na tatizo hilo, tangu mwaka 2006 Serikali inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inayolenga kuhakikisha tatizo la maji nchini kufikia mwaka 2025 linakuwa historia. Programu hii

inatekelezwa kwa awamu ya miaka mitano mitano ambapo kwa sasa tupo katika awamu ya pili ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalilmbali mikubwa na midogo katika maeneo yote nchini mijini na vijijini. Lengo kuu la miradi hiyo ni kuhakikisha huduma hiyo inafikia asilimia 85 kwa wananchi wa vijijini na asilimia 95 kwa wakazi wa mijini ifikapo Desemba, 2020.

Na. 155

Changamoto Zinazokabili Sekta ya Kilimo

MHE. HASSAN E. MASALA aliuliza:-

Kumekuwa na changamoto nyingi sana katika Sekta ya Kilimo.

Je, ni upi Mpango wa Serikali katika kusambaza pembejeo za zao la Korosho kwa msimu wa mwaka 2019?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hassan Elias Masala Mbunge wa Jimbo la Nachingwea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuratibu na kusimamia upatikanaji wa pembejeo katika zao la Korosho ili kuongeza uzalishaji na ubora wa korosho nchini. Katika mwaka 2019, mfumo wa upatikanaji wa pembejeo za zao la korosho ulisimamiwa na Bodi ya Korosho na udhibiti wa ubora wa viuatilifu umefanywa na taasisi ya *TPRI*. Kampuni za pembejeo pamoja na vyama vya ushirika viliagiza viuatilifu na kuvisambaza kwa wakulima baada ya kuingia mikataba na Bodi ya Korosho. Aidha, utaratibu huo pamoja na faida nyiningine umerahisisha upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na kwa bei nafuu ya shilingi 32,000 kwa mfuko wa kilo 50 ya salfa ya unga.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2019/2020 jumla ya tani 19,631 za salfa ya unga na lita 280,201 za viuatilifu vya maji zilisambazwa kwa wakulima kupita vituo vya mauzo vilivyopo katika halmashauri mbalimbali. Aidha, hadi mwezi Desemba 2019, kulikuwa na bakaa ya jumla ya tani 20,110.79 za salfa ya unga na lita 280,830.5 za viuatilifu vya maji.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Korosho ilikusanya takwimu za mahitaji ya pembejeo kutoka Sekretarieti za Mikoa inayozalisha korosho nchini ambapo mahitaji ya viuatilifu kwa mwaka 2020/2021 yanakadiriwa kufikia tani 30,000 za salfa ya unga na lita 350,000 za viuatilifu vya maji. Kutokana na bakaa iliyopo, jumla ya tani 9,889.213 salfa ya unga na lita 99,169.5 za viuatilifu ya maji vitahitajika ili kukidhi mahitaji ya viuatilifu vya Zao la Korosho kwa mwaka 2020/2021.

Aidha, Serikali kupitia Bodl ya Korosho inaendelea kuratibu upatikanaji na usambazaji kwa kuongeza vituo vya usambazaji, kutoa elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo, na kuimarisha udhibiti wa ubora kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduka ya pembejeo.

Na. 156

Kukamilisha Mradi wa Umwagiliaji Kinamwigulu – Maswa

MHE. MASHIMBA M. NDAKI aliuliza:-

Mradi wa Umwagiliaji uliopo kata ya Buchambi, kijiji cha Kinamwigulu Wilayani Maswa haujakamilika kwa muda mrefu sasa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha mradi huo ili utele tija kwa wananchi?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, skimu ya Kinamwigulu iliyopo Kijiji cha Kinamwigulu kata ya Buchambi Wilayani Maswa ni moja ya skimu zilizokuwa zinatekelezwa chini ya Mradi wa *DASIP* ambao utekelezaji wake uliishia Desemba 2013 na kuacha baadhi ya skimu hazijakamilika ikiwemo Kinamwigulu.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na mapungufu hayo, Serikali iliunda Timu ya wataalam waliopitia miradi yote iliyokuwa inatekelezwa chini ya *DASIP* na kuainisha kazi ambazo zimetekelawa na ambazo bado hajijatekelezwa ili iweze kujuua gharama halisi inayohitajika kwa ajili ya kukamilisha mradi huu na miradi mingine kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuitia mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan – NIMP 2018*), Serikali imepanga kujenga, kukarabati na kuboresha jumla ya skimu kumi (10) zilizopo Mkoa wa Simiyu ikiwemo skimu ya Kinamwigulu. Aidha, Serikali imeanzisha Ofisi za Umwagiliaji kwa kila Mkoa na Wilaya ili kusogeza karibu huduma kwa wakulima kwa lengo la kuungeza ufanisi katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile wananchi wanaolima katika skimu hiyo wanawajibika kulipa tozo za kisheria kama vile kuchangia Mfuko wa Umwagiliaji kwa ajili ya upanuzi na uendelezaji wa Skimu ya Kinamwigulu iliyopo kata Buchambi.

Na. 157

Ujenzi wa Barabara ya Mkiwa - Noranga

MHE. YAHAYA O. MASSARE aliuliza:-

Mwaka 2017 Serikali ilionesha nia ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mkiwa - Noranga yenyewe urefu wa kilometra 56.9.

Je, ni lini ujenzi wa barabara hii utaanza?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, (Mbunge wa Manyoni Magharibi) kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mkiwa – Noranga (km 56.9) ni sehemu ya barabara Kuu ya Mkiwa – Rungwa – Makongorosi (km 413) na inayohudumiwa na Wakala wa Barabara *TANROADS* Mkoa wa Singida. Barabara hii ni ya kiwango cha changarawe na hufanyiwa matengenezo kila mwaka ili iweze kuitika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kujenga barabara ya Mkiwa – Noranga (km 56.9) kwa kiwango cha lami ambapo tayari Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakini na usanifu wa kina wa barabara ya Makongorosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa ikiwemo sehemu ya barabara hiyo ya Mkiwa – Noranga.

Aidha, ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami utafanya kulingana na upatikanaji wa fedha.

Na. 158

Idadi ya Wahandisi Nchini

MHE. RUTH H. MOLLEL aliuliza:-

(a) Je, kuanzia mwaka 1961 hadi sasa Tanzania imezalisha Wahandisi wangapi katika kada mbalimbali?

(b) Je, kwa nini wakati wa ujenzi wa barabara kuu (*Highway*) kwenye miji mikubwa hayatengwi maeneo ya kufanyi biashara?

(c) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuepusha ajali zinazotokea mara kwa mara kwenye miji inayofanywa biashara pembeni mwa barabara?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, (Mbunge Viti Maalum) lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Spika, Tangu mwaka 1961, Tanzania imezalisha wahandisi 25,401 katika makundi mawili yaani Wahandisi Wahitimu wa Kitanzania (*Graduate Engineers*) 18,727 na Wahandisi Wataalam wa Kitanzania (*Professional Engineers*) 6,674. Aidha, katika kada hizo Wahandisi wamegawanyika katika fani zifuatazo: Uhandisi wa Ujenzi (Barabara, Majengo na Maji) (10,435); Uhandisi wa Umeme (4,164); Uhandisi wa Mitambo na fani zinazoelekeana (3,882); Uhandisi wa Mazingira (1,029); Uhandisi katika Kilimo na Umwagiliaji (1,085); Uhandisi katika Mawasiliano na Kompyuta (2,812) na Uhandisi katika Madini na Uchimbaji wa Gesi (1,994).

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007, Kanuni na Miongozo yake eneo la hifadhi ya barabara lina jumla ya upana wa meta 60. Eneo hili limetengwa kwa ajili ya barabara na samani zake tu. Halihusishi maeneo ya kufanya biashara. Ujenzi wa Barabara Kuu (*Highway*) kwenye miji mikubwa huhusisha njia za watembea kwa miguu, waendesha baisikeli na vituo vya mabasi (*Bus Bays*). Vile vile kulingana na mwangozo, hifadhi ya barabara hutengwa kwa ajili ya kuweka huduma za kijamii zikiwemo maji, simu, gesi na mikongo ya mawasilianno. Wizara yangu haijapewa jukumu la kutenga maeneo yakufanya biashara katika eneo la barabara. Jukumu hilo ni la Halmashauri za Miji na Majiji.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliiano kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imechukua hatua mbalimbali za kuizua ajali zinazoweza kutokea pembezoni mwa Barabara Kuu ambako kuna wafanyabiashara ndogo ndogo kama ifuatavyo: Kutoa elimu na kuhamasisha Umma mara kwa mara juu ya Sheria

ya Barabara ya Mwaka 2007 ambayo inakataaza kufanya shughuli zozote za maendeleo ndani ya hifadhi ya barabara, Kujenga uzio kwenye maeneo maalum, mfano: maeneo ya ujenzi wa barabara unaoendelea ili kutenganisha barabara za magari na sehemu za watembea kwa miguu; na kuweka alama na mabango makubwa yenye katazo la kufanya biashara au shughuli zozote za maendeleo ndani ya hifadhi ya barabara.

Na. 159

Barabara ya Lami Kutoka Katoma Hadi Bukwali

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA aliuliza: -

Je, ujenzi wa barabara ya lami kutoka Katoma hadi Bukwali utakamilika lini?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
aliibuu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala Mbunge wa Nkenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Katoma hadi Bukwali yenye urefu wa kilometra 39.8 ni barabara ya mkoa na inasimamiwa na wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS*).

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni kukamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami barabara kuu zinazounganisha makao makuu ya mikoa na nchi jirani. Baada ya ujenzi wa barabara hizi kukamilika, ujenzi wa barabara za mikoa ikiwemo barabara ya Katoma hadi Bukwali utafuata kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Kwa kutambua umuhimu wa barabara ya Katoma – Bukwali, Wizara yangu kupitia Wakala

wa Barabara nchini, imekuwa ikijenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu katika maeneo korofi kuhakikisha inapitika majira yote. Hadi kuflikia Machi 2020, jumla ya Kilometra 2.6 zimejengwa kwa kiwango cha lami katika barabara hiyo.

Na. 160

Uwepo wa Malighafi ya Kutengeneza Saruji Eneo la Uvinza na Makere

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO aliuliza:-

Katika eneo la Uvinza na Makere Mkoani Kigoma kuna uwepo mkubwa wa malighafi ya kutengeneza saruji kwa mujibu wa taarifa za kijiolojia Kituo cha Dodoma.

Je, ni hatua gani zinachukuliwa na Shirika letu la *STAMICO* kuchimba madini hayo ili yanufaishe Taifa na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla?

WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko (Kasulu Mjini) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (*GST*), Mkoa wa Kigoma una maeneo mengi yenye viashiria vya uwepo wa madini ya chokaa ikiwemo Uvinza, Makere, Nyamori, Ulombola, Milima ya Nyakachaka, Lugufu na Mto Mugundozi (Mkondossi).

Mheshimiwa Spika, kawaida madini ya chokaa yanayofaa kwa ajili ya viwanda vya saruji ni yale yenye ubora angalau kuanzia asilimia 48 ya *Calcium Oxide (CaO - lime)* na kiwango cha *Magnesium oxide (MgO)* kisizidi asilimia 5 kwenye miamba ya chokaa. Aidha, miamba inayopatikana katika maeneo ya ukanda wa magharibi ya nchi kwa sehemu

kubwa ina *Calcium Oxide* chini ya asilimia 48. Kulingana na taarifa zilizopo, maeneo ya Makere na Uvinza yana chokaa yenye *Calcium Oxide (CaO)* asilimia 30 -35 na *Magnesium Oxide (MgO)* asilimia 16. Hivyo, kutokana na uwepo wa asilimia hizo kwenye mashapo ya chokaa inasababisha gharama za uzalishaji wa saruji kuwa wa juu ukilinganisha na saruji ya maeneo ya ukanda wa pwani.

Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania chokaa ambayo ina ubora mkubwa na haina *impurities* nyingi ni ile inayopatikana katika maeneo ya ukanda wa Pwani ambayo kwa sehemu kubwa ina ubora wa kati ya asilimia 48 hadi 56 ambacho ni kiwango cha juu sana katika ubora wa madini ya chokaa.

Mheshimiwa Spika, *STAMICO* itaandaa mafunzo ya namna ya wachimbaji na wajasiriamali wa Uvinza na Makere wanavyoweza kutumia teknolojia rahisi ili kuzalisha malighafi ya chokaa kwa wingi na kwa ajili ya matumizi mengine ikiwa ni pamoja na viwanda vya mbolea, mitambo ya kuchenjua dhahabu (*elution plants*), viwanda vya ujenzi na rangi, viwanda vya chuma, dawa, vipodozi na utunzaji wa mazingira kwa kutibu majitaka.

Na. 161

Kusuasua kwa Mradi wa REA Wilayani Meatu

MHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza:-

Utekelezaji wa mradi wa umeme Vijiji (REA) katika Wilaya ya Meatu uko nyuma na unasuasua sana kwani ni Vijiji 21 tu kati ya Vijiji 109 sawa na 19% ndiyo vyenye umeme.

(a) Je, ni Vijiji gani vya Wilaya ya Meatu vimo kwenye REA III kwa mwaka wa fedha 2017/2018?

(b) Je, ni lini vijiji vilivyobaki vitapewa umeme wa *REA*?

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijiji (REA) inatekeleza mradi wa kusambaza umeme vijiji ambapo jumla ya vijiji 59 katika Wilaya ya Meatu vinaendelea kupatiwa umeme kupitia utekelezaji wa mradi wa REA Awamu ya Tatu (REA - III) Mzunguko wa Kwanza. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2020 vijiji 12 vya Dakama, Mwakisandu, Mwalwilo, Mnadani, Tindaburigi, Mwagwila, Itaba, Kisesa, Mwaukoli, Mwakasumbi, Mwanjoro na Bukundi vimekwishawashiwa umeme na wateja wa awali zaidi ya 276 wameunganishiwa huduma ya umeme kupitia *transfoma 19.*

Mheshimiwa Spika, Kazi za mradi katika Wilaya ya Meatu zinajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 94.1, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 84 pamoja na ufungaji wa *transforma 42* za KVA 50, 100 na 200; na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 1,127. Gharama ya mradi ni shilingi Bilioni 5.6 na mradi unatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2020.

(b) Mheshimiwa Spika, Vijiji vilivyobaki katika Wilaya ya Meatu vitapatiwa umeme kupitia utekelezaji wa mradi wa REA Awamu ya Tatu (REA - III) Mzunguko wa Pili ambao unatarajiwa kuanza Mwezi Mei, 2020 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

Na. 162

Vitabu Vitakavyotumika Katika Ufundishaji wa Fasihi

MHE. ALLY SALEH ALLY aliuliza:-

Je, ni utaratibu gani hutumika katika kuchagua vitabu ambavyo hutumika katika viwango vya ufundishaji wa fasihi;

katika viwango vya mitihani ya darasa la 12 na ile ya darasa la 14 hapa nchini?

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshiniwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Saleh Ally (MB) Malindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuchagua vitabu vya ufundishaji wa fasihi katika darasa cha 12 na 14 hapa nchini, unaongozwa na Waraka wa Elimu Na. 4 wa mwaka 2014 unaohusu Utayarishaji wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi huo hufuata hatua mbalimbali ambazo ni; uhakiki wa maudhui ambao hufanywa na jopo la wataalam wa somo la fasihi. Baada ya uhakiki kukamilika, Miswada ya vitabu hivyo hupelekwa kwenye Baraza la Taasisi ya Elimu Tanzania kwa lengo la kuthibitisha uhakiki uliofanyika. Aidha, Baada ya Baraza kujiridhisha, Miswada hupelekwa kwa Kamishna wa Elimu kwa ajili ya utoaji wa ithibati.

SPIKA: Karibuni sana Waheshimiwa Wabunge kwenye Mkutano wetu wa Kumi na Tisa. Kikao cha Leo ni Kikao cha Kumi na Saba. Nawakaribisha sana Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na *sanitizer*. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Wizara ya Maji

SPIKA: Ahsante sana. Moja kwa moja sasa nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa karibu sana uwasilishe. Una nusu saa, karibu sana Profesa.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kupokea Taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa ambaye alichambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji ya Mwaka 2019/2020 sasa likubali kupokea, kujadili na kuitisha Mpango na Makadirio ya Mapato ya Matumizi na Fedha ya Wizara ya Maji ya Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa dhati kabisa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushauri, maoni na maelekezo iliyotoa wakati nilipowasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2019/2020 na Mpango wa Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Fedha ya Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuniamini kusimamia Sekta ya Maji. Kupitia uongozi wake shupavu katika kipindi cha Mwaka 2015 - 2020 amesimamia kikamilifu utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015/2020 na mafanikio makubwa yamepatikana katika nyanja zote za maendeleo. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, yaani *SADC*na ninamtakia kila la heri na mafanikio makubwa katika kuiongoza Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wapya waliochaguliwa kuwa Wabunge kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka wa fedha uliokwisha.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko, ninaomba kutoa pole kwako, Wabunge na wananchi wa Jimbo la Newala Vijijini kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Mheshimiwa Alhj. Rashid Akbar. Pia natoa pole kwako na kwa Wabunge kufuatia kifo cha Mbunge wa Viti Maalum,

Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Lwakatare. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, ninapoenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni ambayo imetoa dira na mwongozo wa utekelezaji kwa kazi za Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu hi imegawanyika katika maeneo manne ambayo ni:-

(i) Hali ya Sekta ya Maji;

(ii) Utekelezaji wa Bajeti wa Mwaka 2019/2020;

(iii) Malengo na Mpango wa Kurekebisha Huduma ya Maji kwa Mwaka 2020/2021; na

(iv) Maombi ya fedha kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya maji; kiasi cha maji ya mito, mabwawa na maziwa nchini kimeongezeka kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini ambapo kwa ujumla zimekuwa juu ya wastani katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2019 hadi mwezi Machi, 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Ziwa Victoria, vipimo vilivyochukuliwa tarehe 4 Machi, 2020 vimeonyesha kuwa usawa wa maji katika ziwa hilo umefikia mita 1,134.28 juu ya usawa wa Bahari. Kiwango hicho ni cha juu zaidi tangu vipimo vianze kuchukuliwa Ziwa Victoria. Taarifa ya kina kuhusu hali ya rasilimali za maji inapatikana kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa nne mpaka ukurasa wa 17.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini na mjini; tangu *program* ya

maendeleo ya Sekta ya Maji ianze kutekelezwa mwaka 2007 hadi Desemba, 2019 jumla ya miradi 2,450 imetekelzwa mijini na vijijini. Kati ya miradi hiyo, 1,423 imetekelzwa kati ya mwaka 2015 mpaka 2019 ambapo miradi 1,268 imetekelzwa vijijini na miradi 155 imetekelzwa mijini.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa wastani wa iddai ya watu wanaopata huduma ya maji safi na salama vijijini imeongezeka kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi asilimia 71.1 mwezi Machi, 2020. Kwa upande wa mijini, hali ya upatikanaji wa maji imeongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi asilimia 84 mwezi Machi, 2020. Kwa kuzingatia miradi ya maji mbalimbali inayotekelzwa hapa nchini, Serikali ina matumaini makubwa kwamba malengo ya Kitaifa katika Sekta ya Maji yatafikiwa ifikapo mwisho wa mwaka huu 2020.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Bajeti wa mwaka 2019/2020; katika mwaka wa fedha 2019/2020, Fungu Na.49 - Wizara ya Maji iliadhinishiwa Bajeti ya shilingi bilioni 634.196. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 23.726 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 610.469 ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Machi, 2020, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 470.34 sawa na asilimia 74 ya bajeti. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni 553.697 ni za miradi ya maendeleo sawa na asilimia 74 ya bajeti ya fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa fedha za matumizi ya kawaida, jumla ya shilingi bilioni 16.667 zilipokelewa sawa na asilimia 70 ya bajeti ya fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 12.072 ni fedha za mishahara na shilingi bilioni 4.604 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu *program* na miradi mbalimbali inayotekelzwa katika mwaka 2019/2020; usimamizi na uendelezaji wa rasilimali maji.

Mheshimiwa Spika, rasilimali za maji zinajumuisha maji yaliyomo ndani ya nchi na maji shirkishi. Rasilimali hizo

zinasimamiwa na kuendelezwa na Wizara kupitia Bodi ya Maji za Mabonde tisa zilizopo chini ya Wizara. Hatua zilizochukuliwa katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji katika mwaka 2019/2020 zimeelezwa kwa kina ndani ya kitabu changu cha bajeti kuanzia ukurasa wa 18 hadi 37.

Mheshimiwa Spoika, katika Mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kufuatilia ubora wa maji kwenye vyanzo na kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa lengo la kulinda ikolojia na afya za wananchi. Hadi mwezi Machi, 2020, sampuli mbalimbali kutoka vyanzo mbalimbali zimehakikiwa na zimeonyeshwa kwenye kitabu changu cha Bajeti kutoka ukurasa wa 38 hadi ukurasa wa 45.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya usambazaji maji Vijijini; katika kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio maeneo ya vijijini, Wizara ya Maji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutekeleza miradi na *program* mbalimbali za kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira. Miradi na *program* hizo zinatekelezwa kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira katika maeneo husika.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara kupitia RUWASA imetekeliza miradi ya maji 652. Hadi kufika mwezi Machi, 2020, miradi 94 yenye vituo vya kuchotea maji 2,495 imekamilika na miradi 558 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, linguine ni kuhusu programu ya kuimarisha uendelevu wa huduma ya maji vijijini; program ya malipo kwa matokeo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa maendeleo inatekeleza program mbalimbali kwa lengo la kuimarisha uendelevu wa miradi ya maji vijijini. *Program* hizo ni programu ya malipo kwa matokeo (*Payment by result*) inayotolezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Serikali ya Uingereza. *Program*

hii ilianza mwezi Aprili, 2016 na itafika ukomo mwezi Machi, 2022. Inatekelezwa kwa garama ya Paundi za Uingereza milioni 65.4 sawa na takribani shilingi bilioni 190.

Mheshimiwa Spika, kazi zinazofanyika ni pamoja na kupanua mtandao wa kusambaza maji, kukarabati vituo mbalimbali vya maji na kuhakikisha vituo vilivyopo vinaendelea kutoa huduma kwa awamu ya tatu inayotekelawa. Katika kipindi cha Julai mpaka Desemba, 2019, kiasi cha shilingi bilioni 29.668 kilitolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira katika Halmashauri 181. Sehemu kubwa ya utekelezaji wa miradi hiyo inahusisha wataalam wa ndani wa RUWASA kwa utaratibu wa *Force Account* na ilihuisha ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji 1,215 katika vijiji 2,476 ambapo vituo 11,354 vimefuliwa na wananchi milioni 2,431,313 wananaufaika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya *program* hiyo yenye jumla ya Paundi za Uingereza milioni 23.34 sawa na shilingi bilioni 70 imeanza kutekelezwa kuanzia mwezi Februari, 2020 ambapo Halmashauri 181 zitanufaika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza *program* ya uendelevu wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini inayotekelawa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka 2019 hadi 2024 katika Halmashauri za Wilaya 84 kwenye Mikoa 17.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya *program* hii, jumla ya Dola za Kimarekani milioni 350 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali hususani miradi ya ukarabati, upanuzi wa mitandao pamoja na ujenzi wa miradi mipya itakayoibuliwa na Halmashauri zilizo katika program hiyo. *Program* inatekelezwa kupitia RUWASA katika Wilaya husika. Hadi Mwezi Desemba, 2019, Serikali ilipokea shilingi bilioni 119.99 kutoka Benki ya Dunia. Fedha hizo zitatumika kutekeleza jumla ya miradi 513 yenye vituo 9,286 vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao milioni 2,321,500 katika vijiji 1555.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira kupitia *Force Account*; Awamu ya Kwanza ya *program* ya maendeleo ya Sekta ya Maji ilikumbwa na changamoto pamoja na dosari nyingi za kiutekelezaji zilizosababisha baadhi ya miradi iliyokamilika kushindwa kufanya kazi kama ilivyotarajiwa. Mojawapo ya changamoto iliyotekelawa katika utekelezaji wa awamu hiyo ni baadhi ya wakandarasi na wataalam washauri kuwasilisha gharama za juu za vifaa vyta utekelezaji zisizoendana na uhalsia wa bei zilizopo katika soko.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara iliamua kutekeleza baadhi ya miradi ya maji kwa kutumia wataalam wa ndani (*Force Account or Direct labour*) unaohusisha wataalam na wahandisi walio katika mamlaka za maji na usafi wa mazingira mjini, Wakala wa maji na usafi wa mazingira (*RUWASA*) au kwa kushirikiana kwa pamoja baina ya mamlaka hizo. Aidha, kutoka na wingi wa miradi inayotekelawa katika maeneo mbalimbali nchini, baadhi ya miradi itaendelea kutekeleza na wakandarasi lakini Wizara itaweka utaratibu mzuri zaidi wa kusimamia na ufuatiliaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Wizara ilipitia gharama ya kutekeleza miradi 23 chini ya Wakandarasi yenyeye thamani ya shilingi bilioni 43.613 kulingana na *Indigeneous estimate*. Baada ya mapitio na kuamua kutekeleza miradi hiyo kwa kutumia *Force Account*, gharama halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo ilishuka kutoka shilingi bilioni 43.613 hadi kufikia shilingi bilioni 27.517 na hivyo kuiwezesha Serikali kukoa shilingi bilioni 16.069. Kwa sasa Wizara inatekeleza miradi 199 kwa kutumia utaratibu huu wa *Force Account*.

Mheshimiwa Spika, katika miradi ya usambazaji maji vijiji; katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya kuboresha huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na miradi ya Kitaifa. Hadi mwezi Machi, 2020, miradi 75 inatekelezwa katika maeneo mbalimbali ya mijini nchini ambapo miradi

miwili imekamilika na miradi 73 inaendelea kutekelezwa. Orodha ya miradi hiyo inayotekeliza imeonyeshwa kwenye tovuti ya Wizara www.maji.go.tz. Hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi ni kubwa kimkakati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, Wizara imeanza kutekeleza miradi mipya mikubwa na ya kimkakati miwili. Miradi hii ni miradi ya kuboresha huduma ya maji katika miji 28 na mradi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi wa Simiyu. Kutoka ana ukubwa na umuhimu wa miradi hii, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa mwaka 2019 nilipokuwa nikiwasilisha Bajeti yangu, nilitoa taarifa kuhusu Serikali kupata mkopo nafuu wa Dola za Kimarekani milioni 500 kutoka Serikali ya India kuititia *Exim Bank* ya India kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28 Tanzania Bara na mji mmoja huko Zanzibar. Hatua iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kusainiwa kwa mkataba wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28, taratibu za kumpata mtaalam mshauri wa kufanya usanifu wa kina, kuandaa vitabu vyat zabuni pamoja na kusimamia ujenzi wa mradi zilianza. Mtaalam mshauri alipatikana tarehe 14 Mei, 2019 na kuanza kazi rasmi tarehe 1 Juni, 2019 kwa muda wa miezi mitatu ambapo alikamilisha kazi na kukabidhi taarifa yake ya mwisho tarehe 24 Agosti, 2019.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliwasilisha taarifa ya usanifu kwa Serikali ya India tarehe 29 Agosti, 2019. Serikali ya India ilirejesha taarifa hiyo na maoni yake na Wizara iliifanyia kazi na kuwasilisha taarifa hiyo iliyofanyiwa marekebisho tarehe 4 Novemba, 2019. Tarehe 31 Januari, 2020, Serikali ya India iliidhinisha rasmi taarifa hiyo na kuruhusu hatua nyingine kuendelea.

Mheshimiwa Spika, aidha, Benki ya *Exim* ya India wamekamilisha kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kupata orodha ya awali ya Makandarasi. Tangazo la zabuni lilitolewa na Benki ya *Exim* tarehe 24 Machi, mwaka huu na mwisho wa kupokea maombi ilikuwa tarehe 21 Aprili, mwaka huu. Benki ya *Exim* India wanatarajia kufanya tathimini ya zabuni kwa wakandarasi kuanzia tarehe 12 Mei, 2020 na kukamilisha tarehe 19 Machi, 2020. Baada ya hapo orodha ya Wahandisi Wakandarasi watakaopita katika mchujo wa awali itawasilishwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuendelea na taratibu za manunuzi kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Tanzania. Tunatarajia mchakato wa manunuzi kwa upande wa Tanzania utakamilika mwezi Julai mwaka huu na wakandarasi wataanza kazi mwisho wa mwezi Julai mwaka huu. Mradi huu utakapokamilika unatarajiwa kunufaisha wananchi wapatao milioni nne kwa kuanzia na baadaye wananchi millioni sita ifikapo mwaka 2040 katika miji 28.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi wa Simiyu; tarehe 03 Mei, 2019 Serikali ya Tanzania na Benki ya *KfW*kwa niaba ya Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi na Serikali ya Ujerumani zilisaini Mkataba wa fedha kwa lengo la taasisi hiyo kuipatia Tanzania msaada wa *Euro* milioni 102.7. Fedha hizo ni kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Mkoani Simiyu. Aidha, katika mradi huu Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania itachangia *Euro* milioni 40.1 na wananchi watakaonufaika na mradi huu watachangia *Euro* milioni 1.5 kuititia nguvu zao katika ujenzi wa mradi. Hivyo, jumla ya gharama ya mradi ni jumla ya *Euro* milioni 144.3, sawa na takribani shilingi bilioni 370.

Mheshimiwa Spika, usanifu wa mradi umekamilika na zoezi la kutathmini ardhi itakayochukuliwa katika ujenzi wa mradi huo linaendelea ili wahusika walipwe fidia. Aidha, Serikali inaendelea na mchakato wa kuwapata wataalam washauri watakaosimamia ujenzi wa mradi wanaotarajiwa kupatikana kabla ya mwisho wa mwezi Mei mwaka huu. Vile

vile wakandarasi wa ujenzi wa mradi wanatarajija
kupatikana ifikapo mwishoni mwa mwezi Julai mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Usafi wa Mazingira; Serikali inaendelea kuboresha huduma ya usafi wa mazingira katika miji mbalimbali nchini kwa kujenga na kupanua mifumo ya uondoaji wa majitaka na mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka. Lengo ni kuongeza wastani wa upatikanaji wa huduma hiyo kutoka asilimia 15 za sasa hadi asilimia 30 ifikapo Oktoba mwaka huu. Katika kufikia azma hiyo, miradi mbalimbali ya usafi wa mazingira inatekelezwa na inapatikana katika tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Taasisi zilizo chini ya Wizara; maelezo ya kina kwa taasisi za chini ya Wizara, Mfuko wa Maji wa Taifa, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini, *EWURA* na Chuo cha Maji yameelezwa kwa kina kwenye kitabu changu cha bajeti kuanzia ukurasa wa 61 mpaka ukurasa wa 72.

Mheshimiwa Spika, Masuala Mtambuka; Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa masuala mtambuka kwa Sekta ya Maji; maelezo ya kina yameelezwa kwenye kitabu changu cha bajeti kuanzia ukurasa 72 hadi 83.

Mheshimiwa Spika, Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2019/2020 na hatua zinazochukuliwa; katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2019/2020, Wizara imekabiliana na changamoto mbalimbali katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwezo mdogo wa wakandarasi, udanganyifu mkubwa unaofanywa na wakandarasi wakishirikiana na wataalam wa Wizara ambao sio waaminifu, miradi mingi kujengwa chini ya viwango na mingine kuwa na gharama kubwa ikilinganishwa na bei ya soko, uharibifu wa vyanzo vya maji, upotevu wa maji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu changamoto hizi na hatua zilizochukuliwa zimeonyeshwa kwenye kitabu changu kuanzia ukurasa wa 84 mpaka 91.

Mheshimiwa Spika, malengo na mpango wa kuboresha upatikanaji wa huduma kwa mwaka 2020/2021; programu ya uvunaji wa Maji; katika kuhakikisha program maalum ya uvunaji wa maji ya mvua inafanikiwa na kero ya maji kwa wananchi inapungua, Wizara inatekeleza mikakati mbalimbali ya uvunaji wa maji ya mvua. Makadirio ya awali katika utekelezaji wa programu hiyo ni shilingi bilioni nne. Maelezo ya kina ya mpango huo yameelezwa kwenye kitabu changu cha bajeti kuanzia ukurasa wa 92 mpaka 94.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa kuanzisha Mfumo wa Taifa wa Usambazaji Maji (*National Water Supply Grid*); Mfumo wa Taifa wa Usambazaji Maji ni mfumo unaobuniwa na Serikali na unalenga kuhakikisha maji yanapatikana kwenye maeneo yote nchini na katika kipindi chote cha mwaka bila kujali eneo husika lina vyanzo vya maji au uhaba wa maji. Mfumo huo utahusisha ujenzi wa mtandao wa kusimamia maji kutoka maeneo yenye maji mengi na kuyapeleka kwenye maeneo yenye maji haba.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini, Mradi wa Kutoa maji Ziwa Victoria na kuyapeleka kwenye maeneo mbalimbali kama vile Shinyanga, Tabora na Simiyu ni mfano mmojawapo wa mtandao unaotoa maji kutoka kwenye eneo lenye maji mengi na kuyapeleka kwenye maeneo yenye maji haba. Katika mwaka 2020/2021, Serikali itafanya utafiti wa kubainisha vyanzo vya maji na njia zitakazotumika katika mfumo wa *National Water Supply Grid* itaanza matayarisho ya awali ya ujenzi wa mtandao huo.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa ujenzi wa Mabwawa; katika mwaka 2019/2020, Serikali imebainisha maeneo 217 katika Wilaya 42 zilizopo kwenye mikoa 10 yanayopendekezwa kujengwa mabwawa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa matumizi ya maji ya Maziwa Makuu; Mradi wa Kutoa maji Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria; Mtaalam Mshauri amekamilisha usanifu wa kina wa Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria utakaohudumia wananchi wanaoishi maeneo ya pembezoni

mwa maziwa hayo. Kwa upande wa Ziwa Tanganyika mradi huo utatekelezwa katika Mkoa wa Kigoma, Rukwa na Katavi na utahusisha vijiji 73. Kwa upande wa Ziwa Victoria, mradi huo utatekelezwa katika Mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita, Mara na Simiyu na utahusisha vijiji 301 ya mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Nyasa; Mtaalam Mshauri anaendelea na usanifu wa kina wa Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Nyasa utakaohudumia wananchi wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini; katika mwaka 2020/2021, Wizara imeendelea kukamilisha miradi ya maji vijijini inayoendelea na kutekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini. Jumla ya shilingi bilioni 235.96 zimepangwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo, ambapo fedha za ndani shilingi bilioni 124.16 na fedha za nje ni shilingi bilioni 111.8

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Maji Mijini; katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kukamilisha miradi ya maji mijini inayoendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini. Jumla ya Shilingi bilioni 558.63 zimepangwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo, ambapo fedha za ndani ni Shilingi bilioni 280.93 na fedha za nje ni Shilingi bilioni 277.7.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa *corona*; kama tunavyofahamu dunia nzima imekubwa na mlipuko na ugonjwa wa homa ya mapafu yaani *corona* na hatua muhimu ya kujikinga na ugonjwa huo ni kunawa mikono kwa maji yanayotiririka na sabuni. Wizara inaendelea kuziagiza Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira pamoja na RUWASA kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yote nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wadau wote waliochangia kwa njia moja ama nyingine kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa kipindi cha mwaka 2019/2020 ambao

wameorodheshwa kwenye kitabu changu cha bajeti kuanzia ukurasa 101 hadi samahani...

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Taarifa, Msekwa.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri sekunde, ndiyo Msekwa anayetoa taarifa.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa hotuba ya Mheshimiwa Waziri asilimia 90 ya Wabunge tulipo Msekwa hatuipati kwa sababu *tablet* hizi hazifunguki na huku kuna mtu mmoja tu wa *IT*. Tunaomba tuongezewe watu waweze kutufungulia hizi ili tuweze kuipitia hotuba kwa pamoja. Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Humu ndani pia *tablet* hazifunguki?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

SPIKA: Sawa, Mheshimiwa Waziri endelea na hotuba, watu wa *IT* hebu changamkeni na hilo na nipate ripoti.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba nitumie fursa hii niwashukuru Watumishi wote wa Wizara ya Maji kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2020/2021; baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.733,284,075,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni Sh.28,275,145,000 ambapo Sh.11,171,714,000 sawa na asilimia 40 ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo na Sh.17,103,431,000 sawa na asilimia 60 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni Sh.705,008,930,000 ambapo kati ya fedha hizo, Sh.349,449,000,000 sawa na asilimia 49.6 ni fedha za ndani na Sh.355,559,930,000 sawa na asilimia 50.4 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara www.maji.go.tz.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofij*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI, MHE. PROF. MAKAME MNYAA
MBARAWA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI KWA
MWAKA 2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kupokea taarifa iliowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini**, ambayo ilichambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji ya Mwaka 2019/2020, sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2020/2021.

2. Mheshimiwa Spika, ninapenda kwa dhati kabisa kumshukuru Mwenyekiti na wajumbe wote wa **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji** kwa ushauri, maoni na maelekezo walivotoa wakati nilipowasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2019/2020 na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara kwa mwaka 2020/2021. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii ninayoiwasilisha leo.

3. Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumshukuru kwa dhati **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Daktari John Pombe Joseph Magufuli**, kwa

kuendelea kuniamini kuisimamia Sekta ya Maji; sekta ambayo ina mchango mkubwa kwa uhai wa binadamu na maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa nchini. Kupitia uongozi wake shupavu, katika kipindi cha 2015 - 2020 amesimamia kikamilifu utekelezaji wa **Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 – 2020** na mafanikio makubwa yamepatikana katika nyanja zote za maendeleo. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), na ninamtakia kila la heri na mafanikio makubwa katika kuiongoza Jumuiya hiyo.

4. Mheshimiwa Spika, ninaomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wapya waliochaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mwaka wa fedha unaoisha. Wabunge hao ni **Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo** wa Jimbo la **Arumeru Mashariki** na **Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu** wa Jimbo la Singida Mashariki. Ni mategemeo yetu kuwa katika kipindi hiki kilichobaki katika Bunge hili tutashirkiana nao katika kufanikisha majukumu yaliyo mbele ya Bunge letu na Taifa kwa ujumla.

5. Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa pole kwako wewe mwenyewe Mhe. Spika, Bunge lako Tukufu, Familia za Marehemu, Ndugu, Jamaa na Watanzania wote kwa misiba iliyo tupata kwa kuondokewa na aliye kuwa **Mbunge wa Newala Vijiji, Mhe. Ajali Rashid Akibar** pamoja na aliye kuwa **Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare**. Michango ya Wabunge hao katika shughuli za maendeleo ya Taifa letu itakumbukwa milele daima. Vilevile, ninatoa pole kwa wananchi waliopoteza jamaa zao kutokana janga la ugonjwa wa Corona, pamoja na wale waliopoteza maisha kutokana na ajali na mafuriko yaliyotokea katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. **Amin**.

6. Mheshimiwa Spika, ninapenda nichukue fursa hii kumpongeza **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, kwa

hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni, ambayo imetoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali katika mwaka ujao wa fedha. Ninawapongeza pia Waheshimiwiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hoja zao.

7. Mheshimiwiwa Spika, Hotuba yangu ina maeneo makuu manne, ambayo ni hali ya sekta ya maji nchini; utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2019/2020; malengo na mpango wa kuboresha huduma ya maji kwa Mwaka 2020/2021; na maombi ya fedha kwa Mwaka 2020/2021. Muundo na mfumo wa Bajeti ya Mwaka 2020/2021 umeongozwa na kuzingatia malengo ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (*Five Year Development Plan – FYDP*) 2015/2016 – 2020/2021; Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2020/2021; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020; Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP II* 2016/2017 – 2020/2021); na Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals – SDGs* 2015-2030) hususan Lengo Na. 6, linalohusu sekta ya maji.

2. HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI

8. Mheshimiwiwa Spika, hali ya Sekta ya Maji nchini inaelezwa kwa kuzingatia hali ya rasilimali za maji; hali ya huduma za ubora wa maji; hali ya upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini na uwezo wa kitaasisi wa kutoa huduma hizo.

Hali ya Rasilimali za Maji

9. Mheshimiwiwa Spika, kiasi cha maji katika mito, mabwawa na maziwa nchini kimeongezeka kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali hapa nchini, ambazo kwa ujumla zimekuwa juu ya wastani katika kipindi cha mwezi Oktoba 2019 hadi Machi 2020. Hali hii imesababisha mafuriko katika maeneo mbalimbali na baadhi ya mabwawa yamefurika kutokana na mvua hizo. Mabwawa hayo ni pamoja na mabwawa ya Mindu (Morogoro), Kazima

(Tabora), Igombe (Tabora), Nyumba ya Mungu (Kilimanjaro), na mabwawa ya Mtera na Kidatu yaliyopo mkoani Iringa. Kwa upande wa Ziwa Victoria, kwa mfano, vipimo vilivyochochukuliwa tarehe 04 Machi, 2020 vimeonesha kuwa usawa wa maji katika ziwa hilo umefikia **mita 1,134.28** juu ya usawa wa bahari. Kiwango hiki ni cha juu zaidi tangu vipimo vianze kuchukuliwa katika ziwa hilo. Kipimo cha awali cha juu kabisa katika ziwa kilikuwa **mita 1,134.27** kutoka usawa wa bahari kilichorekodiwa tarehe 12 Mei, 1965.

10. Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina mito mingi ya msimu na ile inayotiririsha maji katika kipindi chote cha mwaka. Mito mikubwa ambayo hutririsha maji kwa kipindi chote cha mwaka ni Mto Ruvuma, Mto Rufiji, Mto Kilombero, Mto Pangani, Mto Wami, Mto Ruvu, Mto Malagarasi, Mto Ruhuhu, Mto Kiwira, Mto Kagera, Mto Bubu, Mto Simiyu na Mto Mara. Katika kipindi cha Oktoba 2019 na Februari, 2020 mito hiyo imekuwa na maji mengi juu ya wastani.

11. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Atlas ya Taifa ya rasilimali za maji (Toleo la Mwaka 2019), nchi yetu inakadiriwa kuwa na rasilimali za maji zinazofaa kwa matumizi ya binadamu kwa wastani wa **mita za ujazo bilioni 126**, zikiwemo **mita za ujazo bilioni 105** juu ya ardhi na **mita za ujazo bilioni 21** chini ya ardhi. Kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu **milioni 54** katika mwaka 2018, kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa **mita za ujazo 2,300**. Kiasi hicho ni juu ya wastani wa **mita za ujazo 1,700** ambacho ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa; chini ya kiwango hiki cha maji nchi huhesabika kuwa na uhaba wa maji (*water stress*).

12. Mheshimiwa Spika, mahitaji ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali nchini, kama vile majumbani, umwagiliaji, viwanda na mazingira ni wastani wa **mita za ujazo bilioni 40** kwa mwaka. Inakadiriwa mahitaji hayo ya maji yataongezeka hadi kufikia wastani wa **mita za ujazo bilioni 57** kwa mwaka ifikapo mwaka 2035. Hii inaonesha nchi yetu itaendelea kuwa na rasilimali za maji za kutosha kwa ajili ya

shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, kutokana na mwenendo wa kuongezeka kwa mahitaji ya maji nchini, ni muhimu nchi yetu ikaendelea kuimarisha uhifadhi wa rasilimali za maji ili taifa lisiingie kwenye hali ya ubaba wa maji siku za usoni.

Hali ya Huduma za Ubora wa Maji

13. Mheshimiwa Spika, mipango na matumizi ya rasilimali za maji hutegemea ubora wa maji katika vyanzo na mifumo ya usambazaji maji. Ufuatiliaji wa ubora wa maji katika vyanzo na mifumo hiyo vijiji ni mijini ni muhimu katika kulinda afya ya jamii pamoja na mifumo ya ikolojia. Katika kuhakikisha jamii inapata maji safi na salama na vyanzo vya maji vinalindwa, Wizara kupitia maabara 16 za ubora wa maji zilizopo katika mikoa mbalimbali nchini ina jukumu la kuhakiki ubora na usalama wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya kusambaza maji mijini na vijiji. Maabara hizo huhakiki viashiria vya ubora wa maji kwa kufanya uchunguzi wa kibaiolojia na kikemia kwa lengo la kubaini hali halisi ya mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji na maji yanayosambazwa kwa jamii. Takwimu za ubora wa maji ni moja ya viashiria muhimu vinavyotumika kufanya maamuzi katika kupanga na kuendeleza rasilimali za maji nchini.

14. Mheshimiwa Spika, ubora wa maji katika vyanzo vya maji nchini hutofautiana kutoka eneo moja hadi jingine. Tofauti ya ubora wa maji kutoka eneo moja hadi jingine husababishwa na hali ya miamba ya asili, jiografia ya eneo, mabadiliko ya tabianchi na shughuli za kibinadamu. Kwa upande wa maji juu ya ardhi (*surface water*), changamoto kwa baadhi ya maeneo nchini ni kuwepo kwa kiwango kikubwa cha viashiria vya Nitrogen na Phosphorous katika maziwa na tope (*turbidity*) katika mito vinavyosababishwa na shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji. Vilevile, kiwango kikubwa cha chumvichumvi, Nitrate, Madini ya Flouride, Chuma na Manganese vimeonekana kuwa changamoto kwa upande wa maji chini ya ardhi kwa baadhi ya maeneo. Kwa ujumla, hali ya ubora wa maji katika vyanzo vya maji kwa maeneo mengi nchini kwa kipindi cha mwaka

2019/2020 imeendelea kuimarika na maji katika vyanzo hivyo yanaendelea kutumika baada ya kuchakatwa kulingana na matumizi yaliyokusudiwa.

15. Mheshimiwa Spika, maji ya kunywa yanayosambazwa kwa jamii nayo yameonesha kuwa na ubora unaoridhisha licha ya changamoto zilizopo kwenye maeneo machache, kama vile uwepo wa madini ya *fluoride* kwenye ukanda unaopitiwa na Bonde la Ufa katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Singida na Shinyanga; na madini ya chumvichumvi kwenye maeneo ya Pwani na Ukanda wa Kati katika mikoa ya Dodoma na Singida. Katika kukabiliana na changamoto za ubora wa maji, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeanza kuweka mitambo inayotumia teknolojia ya kisasa kama vile mitambo ya kuondoa chumvichumvi (*reverse osmosis plant*) iliyofungwa Galro na Arusha kwa ajili kuondoa chumvichumvi na madini ya *fluoride*.

Hali ya Upatikanaji wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na Mijini

16. Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002 inalenga kuboresha huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini ili wapate huduma hiyo kwa umbali usiozidi mita 400 kutoka kwenye makazi yao. Vilevile, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inalenga kuboresha huduma za maji vijijini kufikia asilimia 95 ifikapo Mwaka 2025. Malengo ya kati ni kuboresha huduma ya maji vijijini kufikia asilimia 85 mwaka 2020. Ili kutimiza malengo haya, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ya mwaka 2006 – 2025, ikiwa ni awamu ya pili ya utekelezaji wake kwa sasa. Aidha, katika kuboresha na kuleta ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maji vijijini, Serikali imeanzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*Rural Water Supply and Sanitation Agency – RUWASA*) ulioanza kutekeleza majukumu yake rasmi mwezi Julai, 2019. Katika kufikia malengo yaliyowekwa, Serikali kuititia RUWASA inaendelea kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya maji, kujenga visima na kujenga mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini.

17. Kwa upande wa mijini, Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira zinaendelea kutekeleza majukumu yao kama kawaida. Pamoja na kutoa huduma ya maji na usafi wa mazingira kwa wananchi, Mamlaka za Maji pia zimekabidhiwa jukumu la kusimamia ujenzi wa miradi ya maji katika maeneo yao na katika maeneo ya vijiji vilivyo katika mikoa yao. Aidha, katika kuimarisha mamlaka hizo na kupunguza gharama za uendeshaji, Serikali imefanya mabadiliko makubwa katika muundo wa mamlaka kwa kuziunganisha baadhi ya mamlaka za miji midogo na makao makuu ya wilaya kwenye Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira za Makao Makuu ya Mikoa.

18. Mheshimiwa Spika, lengo la Wizara kwa Mwaka 2020 ni kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini unafikia **asilimia 85**. Katika kufikia lengo hilo, Wizara imepanga kutekeleza miradi itakayoongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa haraka na pia kutekeleza miradi kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa zaidi wa maji. Hadi kufikia Machi 2020 kuna miradi **558** vijijini inayoendelea kutekelezwa kupitia bajeti ya Serikali na kati ya miradi hiyo, miradi **268** yenye uwezo wa kuhudumia wananchi **1,539,509** kupitia vituo **7,540** katika vijiji **880** inatarajjiwa kukamilika katika mwaka 2020. Katika kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati uliopangwa Wizara itawasimamia kwa karibu Wakandarasi wanaotekeleza miradi hiyo. Aidha, utekelezaji wa miradi ya maji kwa mfumo wa **Force Account** unatarajjiwa kuharakisha na kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi ya maji na hivyo kufikia malengo ya kitaifa katika sekta ya maji kwa muda uliopangwa.

19. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inatekeleza Programu mbili za "malipo kwa matokeo" zinazojulikana kama *Payment by Results (PbR)* inayofadhiliwa na Serikali ya Uingereza kupitia shirika lake la maendeleo (*DFID*) na *Program For Results (PforR)* inayofadhiliwa na Benki ya Dunia. Programu zote mbili zinalenga kuimarisha uendelevu wa huduma ya maji vijijini. Kupitia *PbR*, ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji **1,215**

katika vijiji **2,476** utafanyika ambapo **vituo 11,354** vitafufuliwa na wananchi **2,431,313** watanufaika. Aidha, kupitia programu ya *PforR*, jumla ya miradi **513** yenye jumla ya vituo **9,286** vya kuchotea maji itatekelezwa na kuhudumia wananchi wapatao **2,321,500** katika vijiji **1,055**.

20. Mheshimiwa Spika, tangu Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ianze kutekelezwa mwaka 2007 na hadi kufikia Desemba 2019, jumla ya miradi **2,450** imetekelezwa mijini na vijijini. Kati ya hiyo, miradi **1,423** imetekelezwa kati ya mwaka 2015 na mwaka 2019, ambapo miradi **1,268** imetekelezwa vijijini na miradi **155** imetekelezwa mijini. Takwimu zinaonyesha kuwa wastani wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji ya safi na salama vijijini imeongezeka kutoka **asilimia 47** mwaka 2015 hadi kufikia **asilimia 70.1** mwezi Machi mwaka 2020. Kwa upande wa mijini, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji imeongezeka kutoka **asilimia 74** mwaka 2015 hadi kufikia **asilimia 84** mwaka 2020.

21. Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia miradi ya maji **631** inayoendelea kutekelezwa nchini, Serikali ina matumaini makubwa kuwa malengo ya kitaifa katika sekta ya maji yafikiwa ifikapo mwishoni mwa mwaka huu. Aidha, Wizara imeweka mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma ya maji mijini na vijijini, ikiwemo kushirikiana na wadau mbalimbali katika kujenga na kupanua miundombinu ya maji; kuhakikisha miradi ya maji iliyo katika hatua mbalimbali za utekelezaji inakamilika na kuanza kutoa huduma; kuhakikisha kiasi cha fedha kinachopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika sekta ya maji kinaelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi yenye kuleta matokeo makubwa; kuboresha uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya maji; kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji; kuongeza makusanyo ya maduhuli kwenye mamlaka za maji ili kuziwezesha kuwekeza katika utekelezaji wa miradi; na kutumia wataalam wa ndani kutekeleza miradi ya maji kuitia mfumo wa *force account*.

22. Mheshimiwa Spika, Huduma ya usafi wa mazingira ni muhimu katika kuhakikisha Wananchi wanaishi katika

mazingira bora na kuepusha maradhi yanayotokana na uchafu yakiwemo maradhi ya mlipuko kama vile magonjwa ya matumbo na kipindupindu. Huduma za usafi wa mazingira katika Mamlaka hutolewa kwa wateja kuunganishwa kwenye mtandao wa majitaka na uondoaji wa majitaka kwa kutumia magari maalum (*bowsers*) na kuyamwaga majitaka katika mabwawa ya kusafisha na kutibu majitaka. Hadi mwezi Machi 2020 huduma ya uondoaji wa majitaka imefikia **asilimia 15** ambapo lengo ni kufikia **asilimia 30** ifikapo mwezi Oktoba 2020. kwa ujumla, huduma ya uondoaji majitaka nchini kuititia mitandao ya majitaka bado ni changamoto kutokana na uwekezaji mdogo uliofanyika kwenye ujenzi wa miundombinu hiyo, na mwamko mdogo wa wananchi kujunga kwenye mtandao wa majitaka kwenye maeneo ambayo miundombinu hiyo ipo.

Mfumo wa Kitaasisi wa Kusimamia Huduma Katika Sekta ya Maji

23. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha sekta ya maji inatekeleza majukumu yake kulingana na sheria, taratibu na kanuni, Bunge lako tukufu lilitunga sheria katika maeneo muhimu matatu, ambayo ni rasilimali za maji; utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira; na udhibiti wa utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira. Eneo la rasilimali za maji linasimamiwa na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya **Na. 11** ya Mwaka 2009; wakati eneo la utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira linasimamiwa na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira **Na. 5** ya Mwaka 2019. Eneo la udhibiti wa utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira linasimamiwa na Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji **Na. 11** ya Mwaka 2001. Aidha, Wizara iliandaa Kanuni mbalimbali za kuwezesha utekelezaji wa sheria hizo.

24. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya **Na. 11** ya Mwaka 2009 inasimamia rasilimali za maji zilizopo juu na chini ya ardhi zikiwemo mito, maziwa, mabwawa, chemchemi, na ardhi oevu pamoja na kuzuia uchafuzi wa maji katika vyanzo. Aidha, sheria hiyo inazuia

uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji na inaelekeza kutumia maji baada ya kupata kibali kutoka kwenye Bodi za Maji za Mabonde. Adhabu ya faini na/au kifungo jela hutolewa kwa wanaobainika kukiuka masharti ya Sheria hiyo. Kanuni mbalimbali zimeandalishi ili kuwezesha utekelezaji wa sheria hiyo.

25. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya **Na. 5** ya Mwaka 2019 inasimamia utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira katika mijii na vijiji katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Sheria hiyo ndiyo inaunda Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*RUWASA*), Jumuiya za Huduma za Maji Ngazi ya Jamii (*CBWSOs*) na Mfuko wa Taifa wa Maji (*National Water Fund - NWF*). Sheria hiyo imeanza kutekelezwa rasmi tarehe 1 Julai 2019, baada ya kupitishwa na Bunge mwezi Januari 2019 na kuridhiwa na Mheshimiwa Rais mwezi Februari 2019.

26. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji **Na. 11** ya Mwaka 2001 inahusika na udhibiti wa huduma za umeme, mafuta, gesi asilia na huduma za majisafi na majitaka. Sheria hiyo inaunda Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) ili kudhibiti utoaji wa huduma hizo. Katika kutekeleza majukumu yake ya udhibiti, *EWURA* inatoa leseni kwa watoa huduma hizo ikiwa ni pamoja na mamlaka za maji; inaidhinisha bei za huduma zinazotolewa na watoa huduma; na inatoa miongozo mbalimbali ya kuhakikisha huduma inakuwa bora.

27. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa sekta ya maji, Serikali ipo katika mchakato wa kupitia upya Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002 ili sera hiyo iendane na mazingira ya sasa. Umuhimu wa kupitia upya sera hiyo umetokana na ukweli kwamba kipindi cha miaka 18 kimepita tangu ianze kutumika na katika kipindi hicho kuna mabadiliko mengi ya kimwelekeo na kimalengo ambayo yametokea kitaifa na kimataifa, ikiwemo kuanza kutumika kwa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP 2016/17 - 2020/21) na

kutungwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDGs 2015-2030). Mapitio ya Sera hiyo ikiwa ni pamoja na maandalizi ya Mkakati wake wa utekelezaji yanatarajiwa kukamilika katika mwaka 2020.

28. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji inatekeleza majukumu yake ya kiutendaji kupitia taasisi zake mbalimbali. Taasisi hizi ni Mfuko wa Taifa wa Maji; Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira; Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji; na Chuo cha Maji. Majukumu ya taasisi hizi yanafafanuliwa kwa kifupi hapa chini.

29. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Maji umeanzishwa kupitia Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira **Na. 5** ya Mwaka 2019. Majukumu ya Mfuko ni pamoja na kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya maji na usafi wa mazingira; kutuma fedha kwa watekelezaji wa miradi ya maji; kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya utoaji huduma za maji; kufuatilia matumizi ya fedha zinazotumwa kwa watekelezaji; kuzijengea uwezo mamlaka za utekelezaji wa miradi ya maji ili ziweze kusimamia kwa ufanisi miradi inayotekeliza; kumshauri Waziri mwenye dhamana ya sekta ya maji kuhusu miongozo mbalimbali ya matumizi ya fedha za Mfuko huo.

30. Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira **Na. 5** ya Mwaka 2019, Bunge lako Tukufu Iliananza Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji (*Rural Water Supply and Sanitation Agency-RUWASA*). Wakala huu umechukua majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia ujenzi wa miradi na utoaji wa huduma ya maji vijiji na ulianza kazi rasmi tarehe 01 Julai, 2019. Ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako kuwa Serikali imekamilisha hatua zote za msingi za kuanzisha wakala huu, ikiwemo kutengeneza muundo wa wakala; kuunda Bodi ya Wakurugenzi; na kuteua menejimenti ya wakala. Aidha, taratibu zote za kuhamisha majukumu, mikataba na rasilimali kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekamilika. Ninaomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Mheshimiwa Waziri-Ofisi ya Rais TAMISEMI,

Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ushirikiano mkubwa waliotupa katika mchakato wa kuanzisha RUWASA.

31. Mheshimiwa Spika, huduma za maji na usafi wa mazingira mijini zinaendeshwa na Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira zilizopo katika miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa. Mamlaka hizo zinasimamiwa na Bodi za Wakurugenzi zinazoteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya maji kwa kushirikiana na uongozi wa mikoa husika. Lengo la utaratibu huo ni kuziwezesha mamlaka hizo kutoa huduma endelevu na hatimaye kujitegemea kwa gharama zote za uendeshaji, matengenezo na uwekezaji kupitia maduhuli yanayotokana na mauzo ya maji.

32. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi wa utendaji wa mamlaka za maji na usafi wa mazingira, Serikali imefanya mabadiliko kadhaa katika mfumo wa uendeshaji wa mamlaka hizi. Mabadiliko haya ni pamoja na kuongeza/kupanua maeneo ya huduma kwa mamlaka. Kwa sasa eneo la huduma kwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira itakuwa ni eneo la utawala katika mji husika. Aidha, ili kuongeza tija na kupunguza gharama za uendeshaji, baadhi ya mamlaka za maji na usafi wa mazingira katika miji midogo na makao makuu ya wilaya zimeunganishwa na mamlaka za maji za makao makuu ya mikoa, na baadhi ya mamlaka za maji za miji mikuu ya wilaya na miji midogo zimefutwa na maeneo yao yatahudumiwa na mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa na/au na RUWASA katika maeneo husika. Orodha mpya ya Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 1**.

33. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maji ni Wakala unaosimamiwa na Bodi ya Ushauri ya Wizara ya Maji. Chuo hicho Kimeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuanda wataalam, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam unaohitajika katika sekta za maji. Utekelezaji wa majukumu hayo unazingatia Sera, mikakati na miongozo ya Wizara pamoja na Baraza la Taifa la Vyuo vya Ufundis (*NACTE*). Wizara

imeendelea kukiimarisha Chuo cha Maji kwa kujenga na kukarabati majengo kama vile madarasa, mabweni na maabara na miundombinu mengine ili kukiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Vilevile, Wizara itaendelea kugharamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi katika fani mbalimbali katika sekta ya maji.

3. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2019/2020

Hali ya Upatikanaji wa Fedha

34. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Fungu 49 – Wizara ya Maji - liliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi 634,196,197,530**; kati ya fedha hizo **Shilingi 23,726,309,000** zilikuwa ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 610,469,888,530** zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Machi 2020, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 470,374,480,186.31** sawa na **asilimia 74** ya bajeti. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi 453,697,256,871.41** ni za kutekeleza miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 74** ya bajeti ya fedha za maendeleo. Kwa upande wa fedha za Matumizi ya Kawaida, jumla ya **Shilingi 16,667,223,314.90** zilipokelewa sawa na **asilimia 70** ya bajeti ya fedha za Matumizi ya Kawaida na kati ya fedha hizo, **Shilingi 12,072,957,217** ni fedha za mishahara (*PE*) na **Shilingi 4,604,266,097.90** ni fedha za matumizi mengineyo (*OC*).

Miradi na Programu Mbalimbali Zilizotekelzwa kwa Mwaka 2019/2020

35. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi na programu kwa Mwaka 2019/2020 umefafanuliwa katika maeneo matano ambayo ni usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; huduma za ubora na usafi wa maji; miradi ya huduma za usambazaji majisafi mijini; na miradi ya usafi wa mazingira. Aidha, sehemu hii ya taarifa inaeleza pia utekelezaji wa kazi mbalimbali katika Taasisi zilizo chini ya Wizara na masuala mtambuka.

Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

36. Mheshimwa Spika, rasilimali za maji zinajumuisha maji yaliyomo ndani ya nchi na majishirikishi (*transboundary waters*). Rasilimali hizo zinasimamiwa na kuendelezwa na Wizara kuititia Bodi za Maji za Mabonde **tisa** yaliyopo nchini. Kwa upande wa majishirikishi, nchi yetu inashirikiana na nchi nyingine na taasisi mbalimbali za kikanda na kimataifa katika kusimamia rasilimali hizo. Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji umegawanyika katika maeneo **matano**, ambayo ni tathmini na ufuatiliaji wa rasilimali za maji; uhifadhi na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji, ugawaji na uendelezaji wa rasilimali za maji, usimamizi wa rasilimali za majishirikishi na uimarishaji wa taasisi zinazosimamia rasilimali za maji. Hatua zilizochukuliwa katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji katika mwaka uliopita wa fedha ni kama ifuatavyo:-

Tathmini na Ufuatiliaji wa Rasilimali za Maji

(a) Mwenendo wa Rasilimali za Maji

37. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu na kufuatilia mwendendo wa rasilimali za maji ili kutambua wingi na ubora wa rasilimali za maji zilizopo kwa sasa na baadaye. Upatikanaji wa takwimu sahihi na za muda mrefu za rasilimali za maji ni muhimu katika kuiwezesha Serikali kutoa taarifa sahihi za hali ya maji nchini, kuchukua tahadhari dhidi ya majanga ya ukame na mafuriko, pamoja na kuibua na kusanifu miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

38. Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina vituo **794** vya kufuatilia mwenendo wa maji juu na chini ya ardhi vilivyojengwa katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kukusanya takwimu za mvua, hali ya hewa, mtiririko wa maji katika mito, pamoja na kupima kina cha maji katika maziwa na mabwawa; kiasi cha tope (*sediment*) katika mito, maji chini ya ardhi na ubora wa maji. Katika mwaka 2019/2020, Wizara imefanya tathmini ya hali ya mtandao wa vituo vya kukusanya takwimu za mwenendo wa maji ili kufahamu hali ya ufanyakaji kazi wa vituo hivyo. Kufuatia tathmini hiyo, vituo **saba (7)** vya kufuatilia

mwenendo wa maji mitoni vimejengwa ambapo katika Bonde la Ziwa Victoria vimejengwa vituo **sita (6)** na kituo **Kimoja** katika mradi wa kufua umeme wa Nyerere katika Mto Rufiji. Aidha, ukarabati wa vituo vya kufuatilia mwenendo wa maji mtoni umefanyika katika Bonde la Ziwa Victoria vituo tisa **(9)**; Bonde la Ziwa Rukwa **(22)**, Bonde la Ziwa Nyasa **(11)**, Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini **(31)**, Bonde la Ziwa Tanganyika **(5)**, Bonde la Wami/Ruvu **(3)**, Bonde la Mto Rufiji **(8)** na Bonde la Kati vituo **11**. Vilevile, vituo **19** vya kufuatilia hali ya hewa vimejengwa katika Bonde la Mto Rufiji.

39. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa hali ya mwenendo wa maji katika maziwa, mabwawa na mito ilikuwa juu ya wastani kwa mwaka wa kihaidrolojia 2018/2019. Hali hiyo imedhihirishwa katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa na Rukwa; mabwawa ya Mtera, Kihansi, Kidatu, Nyumba ya Mungu na Mindu; na mito ya Pangani, Ruvuma, Malagarasi, Wami, Ruvi, Rufiji, Mara na Kagera ambapo kiwango cha maji kilikuwa juu ya wastani. Katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa ufuatilaji wa takwimu za hali ya rasilimali za maji ili kujua hali na mwenendo wa rasilimali hizo kwa ajili ya kuwezesha Wizara kutoa taarifa na takwimu mbalimbali za rasilimali za maji nchini.

(b) Udhibiti wa Uchimbaji Holela wa Visima

40. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde zimeendelea kudhibiti uchimbaji wa visima kwa lengo la kuhakikisha misingi ya kitaalam inafuatwa katika uchimbaji wake. Jukumu hilo linatekelezwa kwa kuratibu na kusajili kampuni za utafiti na uchimbaji wa visima pamoja na kutoa leseni na vibali vya uchimbaji kwa makampuni yanayokidhi vigezo. Hadi mwezi Machi 2020, leseni mpya **52** za uchimbaji visima zimetolewa na vibali **225** vya kuchimba visima vya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kuhakikisha taratibu za uchimbaji wa visima zinafuatwa na kuchukua hatua stahiki kwa wale watakaokiuka taratibu hizo.

(c) Matumizi Bora ya Rasilimali za Maji na Udhibiti wa Migogoro

41. Mheshimiwa Spika, kazi ya kusimamia ugawaji wa maji kwa matumizi mbalimbali katika mabonde ya maji ina changamoto nyingi kutokana na kuwepo kwa ongezeko la watumia maji linalotokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi na kuongezeka kwa idadi ya watu. Katika kuhakikisha uwiano katika ugawaji wa maji unakuwepo, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde inaratibu na kusimamia ugawaji wa rasilimali hiyo kwa kutoa vibali vya matumizi ya maji kulingana na mahitaji ya watumiaji maji mbalimbali na kiasi cha maji kilichopo. Hadi mwezi Machi 2020, vibali **793** vya matumizi ya maji vimetolewa kwa watumiaji mbalimbali. Vilevile, ukaguzi wa vibali vya kutumia maji ulifanyika ambapo watumia maji **28** walibainika kutokuwa na vibali na kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009.

42. Mheshimiwa Spika, vilevile, Bodi za Maji za Mabonde kwa kushirikiana na Jumuia za Watumiaji Maji zimekuwa zikidhibiti migogoro ya matumizi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Jumla ya migogoro **10** ya matumizi ya maji ilijitokeza katika mwaka huu wa fedha, ambapo migogoro **tisa (9)** imetatuliwa na utatuzi wa mgogoro **mmoja** unaendelea. Aidha, elimu kuhusu matumizi bora ya maji yanayozingatia sheria, taratibu na kanuni za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji imetolewa kwa wadau mbalimbali kupitia warsha, makongamano na majukwaa ya wadau wa sekta ya maji.

43. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kupokea maombi mapya ya vibali vya matumizi ya maji; na kuhakikisha watumiaji wa maji wote wanakuwa na vibali vya matumizi ya maji ili kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza kutokana na matumizi holela ya rasilimali hiyo.

Uhifadhi na Udhibiti wa Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji

(a) Uhifadhi wa Mazingira na Vyanzo vya Maji

44. Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya mazingira na vyanzo vya maji ni muhimu katika kuhakikisha uendelevu wa vyanzo hivyo. Kumekuwa na changamoto za hifadhi ya utunzaji wa vyanzo vya maji kutokana na shughuli za kibinadamu ndani ya vyanzo au karibu na vyanzo. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imekuwa ikifanya jithiada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubainisha vyanzo vya maji na kuvihifadhi pamoja na kuunda Jumuiya za Watumia Maji (*Water User Associations – WUAs*) kwa lengo la kuwashirikisha wananchi katika mipango ya matumizi ya maji kwenye kidakio husika. Wizara imeendelea kuzijengea uwezo na kuziimarisha Jumuiya za Watumia Maji kwa kutoa mafunzo, vitendea kazi na kuwajengea ofisi

45. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2020, vyanzo **575** vya maji vimebainishwa kwa ajili ya kuvihifadhi na kati ya hivyo mabwawa ni **33**, chemichemi **280**, maeneo ya visima **36**, mito **185**, maeneo ya ardhi oevu **22** na maziwa **19**. Kati ya vyanzo hivyo, vyanzo **18** tayari vimehifadhiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kama maeneo tengefu na vyanzo **120** vimewekewa mipaka kama hatua ya awali ya kuhifadhi vyanzo hivyo. Vilevile, Jumuiya **123** za watumia maji zimeundwa katika mabonde yote tisa ya maji nchini; jumuiya **23** zimeanzishwa Mwaka huu wa fedha (2019/2020) katika mabonde mbalimbali kama ifuatavyo: Pangani (**13**), Rufiji (**1**), Ziwa Victoria (**2**), Ziwa Nyasa (**2**), Ziwa Rukwa (**2**), Ruvuma na Pwani ya Kusini (**1**) na Kati (**2**). Aidha, jumuiya **10** za watumia maji zimeimarishwa kwa kupatiwa mafunzo kuhusu utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za maji, na kupatiwa vitendea kazi kama vile baiskeli, vifaa vya ofisi na nyenzo ndogondogo kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa rasilimali za maji.

46. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2020/2021, Serikali imepanga kutangaza vyanzo **45** kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji, na kuendelea kuhifadhi vyanzo vilivyopo na kubaini vyanzo vypya kwa lengo la kuvitunza kwa ajili ya

mahitaji ya kizazi cha sasa na baadaye. Vilevile, Wizara itaendelea kusimamia uundwaji wa Vyombo vyat Watumia Maji ikiwa ni pamoja na kuvijengea uwezo.

(b) Udhibiti wa Uchafuzi wa Vyanzo vyat Maji

47. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kudhibiti uchafuzi wa mazingira na vyanzo vyat maji unaotokana na majitaka yanayotiririshwa katika vyanzo vyat maji kwa kufanya ukaguzi mara kwa mara. Hadi mwezi Machi 2020, ukaguzi huo umefanyika katika migodi ya ukubwa wa kati **21** iliyopo kanda ya Ziwa ambapo miongozo na ushauri katika kudhibiti uchafuzi wa maji unaotokana na kemikali za kuchakatia madini ulitolewa. Matokeo ya ukaguzi huo yanaonesha kupungua kwa uchafuzi wa vyanzo vyat maji na mazingira kwenye maeneo hayo ya migodi. Aidha, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde imetoa vibali vyat muda **28** vyat kutiririsha majitaka katika mabonde ya Pangani, Wami/Ruvu na Ziwa Victoria. Katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vyat maji katika maeneo mbalimbali nchini ili kunusuru afya za binadamu na viumbe wengine pamoja na mazingira.

(c) Mradi wa Kunusuru Vyanzo vyat Maji Kupitia Mpango Endelevu wa Matumizi Bora ya Ardhi Katika Mabonde Madogo ya Mto Zigi na Mto Ruvu

48. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kunusuru Vyanzo vyat Maji kupitia Mpango Endelevu wa Matumizi Bora ya Ardhi katika Mabonde Madogo ya Mto Zigi na Mto Ruvu unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) pamoja na Mfuko wa Mazingira Duniani (*Global Environment Facility - GEF*) kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 27.65**. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016 hadi 2021 na unalenga kujenga uwezo wa kitaasisi ili kuimarisha uratibu na usimamizi wa rasilimali za maji na kutekeleza mipango endelevu ya matumizi ya ardhi. Mradi huo unatekelezwa katika milima ya Uluguru na Usambara Mashariki ambapo jumla ya vijiji **20** katika Halmashauri za Wilaya za Morogoro, Mvomero,

Muheza, Mkinga na Korogwe vinanufaika. Mradi unatekelezwa katika milima hiyo ya Uluguru na Usambara kutokana na umuhimu wake wa kuwa na vyanzo vya maji kwa mito ya Zigi na Ruvu ambayo ndio tegemeo la maji kwa sehemu kubwa ya ukanda wa Pwani na miji ya Morogoro na Tanga.

49. Mheshimiwa Spika, mradi huo umefanikisha kuanzishwa kwa miradi mbadala midogo midogo ya kijamii ambayo ni rafiki kwa mazingira kama vile ufgajji nyuki na samaki ipatayo **12**. Vilevile, umehamasisha matumizi ya majiko banifu na sanifu na hivyo kupunguza matumizi ya mkaa na kuni katika maeneo ya vyanzo vya mito ya Ruvu na Zigi. Aidha, mradi unatoa elimu ya ujasiriamali hususan kwa wakinamama wanaojishughulisha na *VICOBA* ili waweze kujiongezea kipato kupitia shughuli mbalimbali mbadala ambazo ni rafiki kwa mazingira. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, mradi huu umetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wananchi wapatao **125** ambaao ni wanavikundi wa *VICOBA* na umesaidia kuanzishwa kwa *VICOBA vitano* katika vijiji vya Kimbo, Shembekeza, Kiwanda, Mangubu na Bombani vilivyo katika dakio la Mto Zigi. Kwa ujumla mradi umechangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa uharibifu wa mazingira na kuongeza kipato kwa wananchi, na ni matarajio yetu kwamba uharibifu wa mazingira utaendelea kupungua kuprtitia jitihada zilizopo.

Ugawaji na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

(a) Utafutaji wa Vyanzo Vipyta vya Maji

50. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2019/2020, Wizara ilifanya utafiti wa uwepo wa maji chini ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini. Kazi hiyo ilitekelezwa kupitia Bodi za Maji za Mabonde yote nchini. Hadi mwezi Machi 2020, maeneo **157** yanayofaa kuchimbwa visima yalifanyiwa utafiti katika mabonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini maeneo **47**, Ziwa Victoria (**31**), Bonde la Kati (**20**), Bonde la Ziwa Rukwa (**15**), Bonde la Ziwa Tanganyika (**14**), Bonde la Mto Pangani (**13**), Bonde la Wami/Ruvu (**12**) na Rufiji (**5**). Kulingana na matokeo ya utafiti huo, maeneo husika yanaweza kuendelezwa kama

vyanzo vya maji. Aidha, katika jitihada za kuboresha upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma, kazi ya utafiti wa maji chini ya ardhi imefanyika katika maeneo 18 ambayo ni Zuzu maeneo manne (4), Miyuji (4), Mahomanyika (3), Mpamaa (2), Michese (2) na Mbwanga (3). Kati ya hayo, maeneo matano (5) yalipendekezwa kuchimbwa visima vya utafiti ambapo hadi mwezi Machi 2020, jumla ya visima vinne (4) vimechimbwa kwenye maeneo ya Mpamaa chenyе uwezo wa kutoa maji **lita 20,000** kwa saa, Mbwanga (**12,000** kwa saa), Zuzu (**18,000** kwa saa) na Michese (**lita 10,000** kwa saa). Matokeo ya utafiti huo yamesaidia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (*DUWASA*) kuchimba kisima kimoja eneo la Zuzu chenyе uwezo wa kutoa maji zaidi ya mita za ujazo **40** kwa saa. Katika Mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya kijamii na kiuchumi.

(b) Ujenzi wa Mabwawa ya Kimkakati

51. Mheshimiwa Spika, Wizara imepanga kujenga mabwawa makubwa ya kimkakati kwa ajili ya kuhifadhi maji na kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa matumizi mbalimbali. Mabwawa hayo ni Farkwa (Dodoma), Ndembera (Iringa) na Kidunda (Morogoro). Hadi mwezi Machi 2020, Serikali imelipa fidia **Shilingi bilioni 11.4** kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa bwawa la Kidunda; na **Shilingi bilioni 7.134** kwa wananchi **2,612** kati ya **2,868** wa vijiji vya Bubutole na Mombose wilayani Chemba wanaopisha ujenzi wa Bwawa la Farkwa. Kwa upande wa Bwawa la Ndembela, tathmini ya fidia imekamilika na Serikali inaendelea kutafuta **Shilingi bilioni 4** kwa ajili ya kuwalipa wananchi watakaopisha ujenzi wa bwawa hilo. Katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha malipo hayo ya fidia na ujenzi wa mabwawa hayo pamoja na fedha za kukarabati mabwawa mengine ya kimkakati ya Itobo wilayani Nzega na Enguikumet II wilayani Monduli.

(c) Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

52. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini, Wizara imeandaa na kukamilisha Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji kwa Bodi za Maji za Mabonde **saba** kati ya **tisa** ambayo ni Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini, Mto Rufiji, Bonde la Kati na Wami/Ruvu. Uandaaji wa Mpango huo kwa bonde la Ziwa Victoria unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwaka 2020/2021. Katika mwaka 2020/2021, Wizara imepanga kuanza maandalizi ya mpango kwa bonde la Mto Pangani. Aidha, Wizara itakamilisha Tathmini ya Kimkakati ya Kimazingira na Kijamii kwa Mabonde ya Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini, Wami/Ruvu na Bonde la Kati.

(d) Uanzishwaji wa Majukwaa ya Wadau wa Maji

53. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji na kuhakikisha maendeleo endelevu ya rasilimali hiyo, Wizara inaendelea kuanzisha majukwaa ya wadau wa sekta ya maji katika mabonde yote ya maji nchini yenye lengo la kuongeza ufanisi katika ugawaji wa maji, uhifadhi wa vyanzo vya maji, utatuzi wa migogoro ya matumizi ya maji na kuongeza ushiriki wa wadau katika kutekeleza Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji. Hadi mwezi Machi 2020, majukwaa mapya yalianzishwa katika Bodi za Maji za Mabonde ya Ziwa Rukwa, Pangani, Ruvuma na Pwani ya Kusini, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, Wami/Ruvu na Bonde la Kati pamoja. Vilevile, majukwaa kama hayo yameanzishwa katika Vidaka Maji vya Mto Kilombero, Kiwira, Rutikira na Mngaka. Majukwaa hayo hujadili masuala mbalimbali yanayohusu usimamizi wa rasilimali za maji, ikiwa ni pamoja na changamoto zake na kuweka maazimio ya kuboresha usimamizi na uhifadhi wa rasilimali hiyo. Katika Mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kuanzisha majukwaa ya wadau katika ngazi za Bodi za Maji za Mabonde na Vidaka Maji kwa kadri ya uhitaji.

Usimamizi wa Rasilimali za Majishirikishi

54. Mheshimiwa Spika, kati ya kiasi cha maji cha **mita za ujazo bilioni 126** zinazokadiriwa kupatikana hapa nchini kwa mwaka, **asilimia 43.4** ya maji hayo yapo katika vyanzo vya majishirikishi. Vyanzo hivyo vipo katika Mabonde saba kati ya tisa yaliyopo nchini ambavyo ni Maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa, Natron, Chala na Jipe pamoja na Mito ya Kagera, Mara, Malagarasi, Momba, Mwiruzi, Umba, Ruvuma na Songwe. Kwa idadi hiyo ya vyanzo kunaifanya Tanzania kuwa nchi yenye vyanzo vingi vya majishirikishi vinavyotumiwa na nchi nyingine. Katika hali hiyo, ushirikiano katika usimamizi wa rasilimali za majishirikishi ni muhimu katika mustakabali wa kulinda maslahi ya nchi yetu katika kuhifadhi na kutumia maji katika vyanzo hivyo. Ushirikiano katika majishirikishi unahusisha nchi nane majirani, ambazo ni Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Uganda, Malawi, Msumbiji na Zambia. Nchi nyingine tunazoshirikiana nazo ni Angola, Botswana, Ethiopia, Misri, Namibia, Sudan, Sudan Kusini, Zimbabwe na Eritrea. Ushirikiano huo unaotokana na Tanzania kihaidrolojia kuwa ni sehemu ya mabonde makubwa matatu Barani Afrika ambayo ni Bonde la Mto Nile, Bonde la Mto Zambezi na Bonde la Mto Kongo.

55. Mheshimiwa Spika, usimamizi wa rasilimali za majishirikishi unafanyika kupitia Taasisi za Kikanda na Kimataifa zilizoundwa kwa ushirikiano wa nchi wanachama. Tanzania ni mwanachama katika Taasisi zifuatazo: Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika (*AMCOW*); Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (*Zambezi Watercourse Commission - ZAMCOM*); Taasisi ya Mpito ya Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative- NBI*); Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe; Mamlaka ya Usimamizi wa Bonde la Ziwa Tanganyika (*Lake Tanganyika Authority - LTA*); na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria. Katika kipindi cha Mwaka 2019/2020, shughuli za usimamizi wa rasilimali za majishirikishi kupitia Taasisi zake umefanyika kama ifuatavyo:-

(a) Kamisheni ya Bonde la Mto Nile

56. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Bonde la Mto Nile inajumuisha nchi wanachama **11** ambazo ni Burundi, Ethiopia,

Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Tanzania, Uganda na Eritrea ambaye ni mtazamaji. Kamisheni hiyo inatekeleza miradi miwili (2), ambayo ni mradi wa ujenzi wa vituo vya kufuatilia mwenendo wa maji katika bonde la Mto Nile (*Nile Basin Hydromet*) na mradi wa utabiri wa hali ya maji katika mito (*Nile Basin River Flow Forecasting*). Mradi wa *Nile Basin Hydromet* kwa upande wa Tanzania unatekelezwa katika Bonde la Ziwa Victoria na unahusisha kujenga vituo **vinane (8)** vya kisasa kwa ajili ya kufuatilia mwenendo na ubora wa rasilimali za maji katika mito ya Kagera na Mara. Hadi mwezi Machi 2020, usanifu wa mradi huo unaendelea na ujenzi wa mradi unatarajwa kukamilika mwezi Mei, 2021. Vilevile, utekelezaji wa mradi wa *Nile Basin River Flow Forecasting* katika ukanda wa Ziwa Victoria unaolenga maeneo **11** ya vyanzo vya maji unaendelea na utakamilika Mwezi Agosti, 2020. Miradi yote miwili inaijengea uwezo Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria kufanya utabiri wa maji katika mito, mabwawa na maziwa ili kuimarishe mfumo wa kugawa maji, kuwasaidia wadau kupanga shughuli zinazotegemea maji kulingana na kiasi cha maji kilichopo, pamoja na kuchukua tahadhari na kujikinga na majanga ya mafuriko na ukame.

(b) Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe

57. Mheshimiwa Spika, nchi za Tanzania na Malawi zimekubaliana kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe ambayo makao yake makuu yapo Mjini Kyela nchini Tanzania. Kamisheni hii ilizinduliwa tarehe **11 Machi, 2019**. Katika mukutano wa wakuu wa nchi hizi mbili uliofanyika Jijini Lilongwe **tarehe 24 Aprili, 2019**, viongozi wa nchi hizi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Profesa Arthur Peter Mutharika, Rais wa Jamhuri ya Malawi, walikubaliana kwa pamoja kutafuta mkopo nafuu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza kwa pamoja mradi wa Bonde la Mto Songwe ambaeo utazalisha **megawati 80** za umeme zitakazotumika kuendeleza viwanda. Hadi mwezi Machi 2020, Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe inaendelea na majadiliano na washirika wa maendeleo kwa ajili ya kupata mkopo wa masharti nafuu wa kiasi cha **Dola za Marekani milioni 577** kwa

ajili ya ujenzi wa mabwawa makuu matatu, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na usambazaji maji, na kudhibiti mafuriko katika bonde hili.

(c) Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi

58. Mheshimiwa Spika, Tanzania pamoja na nchi za Angola, Botswana, Malawi, Msumbiji, Namibia, Zambia na Zimbabwe ni mwanachama wa Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (*Zambezi Watercourse Commission - ZAMCOM*). Kamisheni hii imekamilisha Mpango Mkakati wa Bonde la Mto Zambezi wa Mwaka (2018-2040) na mwelekeo wa sasa ni kuimarisha Kamisheni kwa kujengea mfumo thabiti wa kitaasisi. Katika Mwaka 2019/2020, Tanzania imeshiriki katika uimarishaji wa Taasisi na utafutaji wa fedha kupitia maeneo makuu manne ambayo ni uendelezaji wa miundombinu ya maji; uhifadhi na ulinzi wa mazingira, kuinua hali ya maisha ya jamii; pamoja na usimamizi wa rasilimali za maji.

(d) Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

59. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya SADC ya Usimamizi wa Maji chini ya Ardhi (*SADC Groundwater Management Institute*) inaendelea kutekeleza mradi wa ufuatilaji wa hali ya maji chini ya ardhi katika maeneo ya Kimbiji na Mpera, Jijini Dar es Salaam kwa gharama ya **Dola za Marekani 165,000**. Vilevile, kupitia Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Afrika inayoratibiwa na Umoja wa Afrika kupitia ukanda wa SADC, Tanzania imeshiriki katika tathmini ya awamu ya kwanza ya programu hiyo iliyotekelizwa kati ya mwaka 2011-2020 na maandalizi ya awamu ya pili ya programu hiyo kwa kipindi cha mwaka 2021-2030. Katika awamu ya pili ya programu hiyo, Tanzania imewasilisha mapendekezo ya miradi kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji, ambayo ni mradi wa ujenzi wa mabwawa ya kuzuia mafuriko na kuzalisha umeme katika Mto Songwe kati ya Tanzania na Malawi (*Songwe River Basin Development Programme - Hydropower Project*); mradi wa umeme wa Rumakali; mradi wa maji wa Tunduma/ Nakonde kati ya Tanzania na Zambia; mradi wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mto Ngono kati ya

Tanzania na Uganda; ujenzi wa bwawa la Borenga kati ya Tanzania na Kenya; na mradi wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika bonde la Mto Mara kati ya Tanzania na Kenya.

(e) Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika (AMCOW)

60. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mwanachama wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika (*African Ministers' Council on Water - AMCOW*) lenye jukumu la kushughulikia masuala ya maji katika nchi za Afrika. Kwa sasa, Tanzania ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Maji wa Afrika (*African Water Facility - AWF*) ambao ni chombo cha *AMCOW* kinachosimamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank - AfDB*) kwa lengo la kugharamia miradi ya maji na usafi wa mazingira barani Afrika. Katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Tanzania imekuwa mwenyeji wa mkutano wa 19 wa Baraza la Uongozi la Mfuko huo uliofanyika kuanzia tarehe 25 hadi 26 Novemba, 2019 Jijini Dar es Salaam, Tanzania. Mkutano huo ulipitisha mpango kazi wa mwaka 2020/2021 na kuweka mikakati ya kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya miradi ya maji barani Afrika.

(f) Bonde la Mto Mara

61. Mheshimiwa Spika, nchi za Tanzania na Kenya zinashirikiana katika kuhifadhi mazingira ya Bonde la Mto Mara ambalo maji yake ni muhimu kwa ustawi wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Katika kuendeleza ushirikiano huo, nchi zote mbili zilifanya uhamasishaji wa kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti na kuweka mipaka kupitia maadhisho ya siku ya Bonde la Mto Mara yaliyofanyika mwezi Septemba 2019, Wilayani Serengeti Mkoani Mara. Vilevile, Tanzania inaendelea na uandaaji wa kanuni na miongozo ya mgawanyo wa rasilimali za maji katika Mto Mara. Kanuni na miongozo hiyo inalenga kuhakikisha maslahi na haki za Taifa katika matumizi ya maji ya Bonde la Mto Mara yanalindwa. Vilevile, Tanzania inashiriki katika programu ya hifadhi ya maeneo oevu ya Bonde la Mto Mara inayoratibiwa na Bonde

la Mto Nile Ukanda wa Maziwa Makuu kwa kufanya tathmini ya mahitaji ya maji kwa ajili ya mazingira ambayo yatajumuishwa katika mlongozo ya matumizi ya maji katika bonde hilo.

(g) Programu ya Pamoja ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji ya Bonde la Ziwa Victoria

62. Mheshimiwa Spika, Tanzania inashirikiana na nchi za Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda katika kutekeleza Programu ya Pamoja ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji ya Bonde la Ziwa Victoria (*Lake Victoria Basin Integrated Water Resources Management Programme (LVB - IWRM)*). Programu hiyo ya miaka mitano (2019 – 2023) inalenga kuchangia katika usimamizi endelevu wa rasilimali za maji ya Ziwa Victoria. Hadi mwezi Machi 2020, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria imepata ufadhili wa **Euro 30,000,000** kutoka Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya. Fedha hizo zitatumika katika utekelezaji wa miradi katika majiji ya Mwanza, Kampala, Kigali na Kisumu. Kazi zinazoendelea kufanyaika ni pamoja na mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi iliyopendekezwa; taratibu za kuingia mikataba na Taasisi za kitaifa zitakazotekeleza miradi; na taratibu za uundwaji wa mfumo wa usimamizi wa Programu katika ngazi za kitaifa.

(h) Kamati ya Kitaifa ya Programu ya Kihaidrolojia (*Hydrological Programme National Committee*)

63. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*). Moja ya Programu za *UNESCO* ni Sayansi kwa ajili ya Amani na Maendeleo Endelevu (*Science for Peace and Sustainable Development*) ambayo ina programu ndogo ya Haidrolojia (*International Hydrological Programme - IHP*). Programu hiyo, huwa na Kamati za Kitaifa kwa ajili ya kushughulikia masuala ya maji. Kufuatia umuhimu huo, katika mwaka 2019/2020, Wizara imeunda Kamati ya Kitaifa ya Programu ya Kimataifa ya Haidrolojia (*International Hydrological Programme National Committee*) inayojumuisha wajumbe kutoka sekta mtambuka katika rasilimali za maji itakayofanya kazi kwa kushirikiana na

UNESCO. Kamati hiyo ina jukumu la kujadili masuala yanayohusu usimamizi wa rasilimali za maji hapa nchini na kutoa ushauri kuhusu namna bora ya kupata ufumbuzi wa changamoto za sekta ya maji katika ngazi ya kitaifa na kikanda.

64. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza ushirikiano katika usimamizi wa rasilimali za maji kwa ajili ya kulinda maslahi ya Taifa; katika Mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kikanda na kimataifa pamoja na kuimarisha ushirikiano katika usimamizi na uendelezaji wa majishirikishi kwa manufaa ya nchi yetu. Vilevile, Wizara itaendeleza mchakato wa kukubali, kuridhia na kuijunga na Mkataba wa Kulinda na Kutumia Majishirikishi na Maziwa ya Kimataifa wa Mwaka 1992 (*The Convention on The Protection and Use of Transboundary Watercourses and International Lakes*) kwa kifupi (*Water Convention*) pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mwaka 1997 kuhusu matumizi ya majishirikishi (*The 1997 UN Convention on the Law of the Non-Navigational Uses of International Watercourses*).

Uimarishaji wa Taasisi zinazosimamia Rasilimali za Maji

(a) Mradi wa Kuimarisha Taasisi Zinazosimamia Rasilimali za Maji

65. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Taasisi Zinazosimamia Rasilimali za Maji (*Water Sector Support Project - WSSP II*) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 50** kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji nchini. Mradi huo unatekeleza katika Mabonde **tisa (9)** ya maji nchini ambapo Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu imepewa kipaumbele na kutengewa zaidi ya **asilimia 40** ya fedha zote kutohana na idadi kubwa ya watumia maji na wingi wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika bonde hilo, hususan katika Jiji la Dar es Salaam.

66. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2020, Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro imechimba visima **vinne (4)** kwa ajili ya

maji kwa mifugo na usanifu wa mabirika **matano (5)** ya kunyweshea mifugo umekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Machi 2020. Vilevile, Bonde la Wami/Ruvu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na Wilaya ya Mvomero linaendelea kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji **20** ambapo vijiji **sita (6)** vya Langali, Nyandira, Kibigiri, Tchenzema vilivyopo katika Wilaya ya Mvomero na vijiji vya Kibwaya na Tegetero vilivyopo katika ya Wilaya ya Morogoro tayari mipango yao imeandaliwa. Bonde limefanya kampeni ya uhamasishaji kijiji hadi kijiji ambapo jumla ya vijiji **50** vimeelimishwa juu ya uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji; na kukamilisha uundwaji wa Jumuiya **tatu (3)** za watumia maji katika bonde la Mto Mgeta. Aidha, mradi huo kupitia Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/ Ruvu unajenga miradi midogo ya maji **minne (4)** katika vijiji vya Mngazi, Dakawa, Tulo na Mgeta Juu ambapo kwa sasa ipo katika hatua ya usanifu. **(b) Ukusanyaji wa Maduhuli**

67. Mheshimiwa Spika, Bodi za Maji za Mabonde zimeendelea kukusanya maduhuli yanayotokana na ada za maombi ya vibali na ada za matumizi ya maji pamoja na tozo mbalimbali katika usimamizi wa rasilimali za maji. Maduhuli hayo huchangia katika kuziwezesha Bodi hizo kutekeleza majukumu yake ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa ufanisi. Hadi mwezi Machi 2019, **Shilingi bilioni 7.1** zilikusanywa ambazo ni sawa na **asilimia 100** ya lengo la **Shilingi bilioni 7** liliowekwa. Kiwango hicho bado hakikidhi mahitaji ya Bodi hizo ya kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji. Katika kuhakikisha bodi za maji zinajitegemea, Serikali ilifanya utafiti wa namna ya Bodi hizo zitakavyoongeza mapato na kujidoresha. Serikali inaendelea kuyafanyia kazi mapendekezo ya utafiti huo. Katika mwaka 2020/2021, Bodi za Maji za Mabonde zimepanga kukusanya **Shilingi bilioni 7.5** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato. **Kiambatisho Na. 2** kinaonesha mchanganuo wa maduhuli yaliyokusanywa na Bodi za Maji za Mabonde hadi mwezi Machi 2020 na makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2020/2021.

Huduma za Ubora wa Maji

68. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kufuatilia ubora wa maji kwenye vyanzo na kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa lengo la kulinda ikolojia na afya za wananchi. Hadi mwezi Machi 2020, jumla ya sampuli **5,252** za maji zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake. Kati ya hizo, sampuli kwa ajili ya matumizi ya majumbani ni **4,218**, viwandani sampuli **268**, umwagiliaji (**60**), ujenzi (**56**), utafiti (**116**) na sampuli **534** ni kwa ajili ya kubaini mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo. Aidha, katika kuhakikisha kuwa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira yanakidhi viwango vya ubora vilivyowekwa jumla ya sampuli **387** za majitaka zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake. Vilevile, jumla ya sampuli **30** za madawa ya kusafisha na kutibu maji zilihakikiwa ubora wake kabla ya kununuliwa.

69. Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu matokeo ya uchunguzi wa hali ya ubora wa maji katika vyanzo na kwa matumizi mbalimbali pamoja na kazi nyingine zilizoteklezwa ni kama ifuatavyo:-

Ubora wa Maji Katika Vyanzo

70. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2019/2020, Wizara ilikusanya **sampuli 534** kutoka vyanzo **24** vya maji vya kimkakati kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji. Matokeo yanaonesha kuwa vyanzo hivyo vina hali nzuri na vinawezza kuendelea kutumika au kuendelezwa kwa matumizi yaliyokusudiwa. Aidha, Wizara ilifanya uchunguzi wa ubora wa maji ya viziwa (*satelite lakes*) vya Rushwa na Karenje vilivyopo eneo la Kyerwa Mkoani Kagera ili kuona kama maji hayo yanawezza kutumika kwa matumizi ya majumbani. Matokeo yalionesha kuwa viziwa hivyo havifai kuendelezwa kwa sababu maji yake hayana ubora hata kama kutawekwa miundombinu ya kusafisha na kutibu maji. Kutokana na matokeo hayo, Wizara ilisitisha hatua zozote za kutumia maji kutoka chanzo hiki kwa matumizi ya binadamu.

Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Majumbani na Matumizi Mengine

71. Mheshimiwa Spika, katika kulinda afya ya jamii na shughuli za kiuchumi, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji yanayosambazwa kwa matumizi ya majumbani, viwanda, ujenzi, umwagiliaji na utafiti. Hadi mwezi Machi 2020, jumla ya sampuli za maji **4,218** zimekusanywa kutoka katika mifumo ya kusambaza maji ya kunywa vijijini na mijini na kuhakikiwa usalama wake kwa kuzingatia viwango vya ubora wa maji vya nchi. Matokeo yalionesha **asilimia 90.8** sawa na sampuli **3,832** zilikidhi viwango vinavyokubalika. Changamoto za ubora na usalama wa maji zilizobainika katika Mamlaka za Maji na Vyombo vya Watumiaji Maji vijijini ni uwepo wa viwango vikubwa vya madini ya chuma, *Manganese* na chumvichumvi kwa mikoa ya Lindi na Mtwara, *Fluoride* kwa mikoa ya Arusha na Singida, *Nitrate* na chumvichumvi kwa Mkoa wa Dodoma. Changamoto hizo zinaendelea kutatuliwa kwenye ngazi husika. Kwa upande wa maji kwa matumizi ya viwandani, ujenzi na umwagiliaji jumla ya sampuli 384 zilifanyiwa uchunguzi na matokeo yalibainisha kuwa maji kwa matumizi hayo yanakidhi viwango vinavyokubalika.

72. Mheshimiwa Spika, sampuli **116** kwa ajili ya utafiti zilihakikiwa ubora wake ambapo sampuli 98 zilikuwa za utafiti wa madini ya *arsenic* katika vyanzo vya maji katika Halmashauri ya Mji wa Geita na Halmashauri ya Wilaya ya Geita; na sampuli 18 ni kwa ajili ya tafiti nyingine. Kwa upande wa utafiti wa madini ya *arsenic* vyanzo vilivyochanguzwa ni pamoja na visima, chemchemi na mabwawa ambapo matokeo yalionesha **asilimia 97** ya sampuli zilizochukuliwa zilikidhi viwango. Aidha, takwimu katika maeneo mengine ya nchi zinaendelea kukusanywa ili kupata taarifa za mwenendo wa viashiria vya madini tembo (*heavy metal*) katika vyanzo vya maji hususan maeneo ya migodini.

73. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ufuatiliaji wa ubora wa maji katika mwaka 2019/2020 Wizara imeendelea kutoa mafunzo kuanzia ngazi ya kijiji juu ya utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji pamoja na

Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango ya Usalama wa Maji. Katika kuhakikisha maji yanayosambazwa yanasa fishwa na kutibiwa ipasavyo ili kukidhi viwango vya ubora wa maji ya kunywa, Wizara ipo katika hatua za mwisho kukamilisha Mwongozo wa Kitaifa wa Kusafisha na Kutibu Maji utakaotumika katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), pamoja na Vyombo vya usambazaji maji ngazi ya kijiji na wadau wengine wanaojihu shisha na usambazaji wa maji ya kunywa.

Ubora wa Majitaka Yanayorudishwa Kwenye Mazingira

74. Mheshimiwa Spika, ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira ni lazima udhibitiwe ili kuzuia uchafuzi wa vyanzo vya maji na mazingira. Wizara kupitia Maabara za Maji imeendelea kufuatilia ubora wa majitaka ili kuhakikisha yanaporudishwa kwenye mazingira au vyanzo vya maji yanakidhi viwango vilivyowekwa. Hadi mwezi Machi 2020, jumla ya sampuli **387** zilikusanya katika mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka ya Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Dodoma, Iringa, Morogoro na Mbeya na katika viwanda vya kuchakata samaki, maziwa, vinywaji baridi na vikali, viwanda vya nguo na rangi. Matokeo yalionesha asilimia **60** ya sampuli za majitaka zilikidhi viwango vya kurudishwa kwenye mazingira. Ushauri wa kitaalam wa namna ya kuboresha mifumo ya kusafisha na kutibu majitaka ulitolewa kwa Mamlaka za Maji pamoja na viwanda ambavyo majitaka yake hayakukidhi viwango vinavyokubalika kurudishwa kwenye mazingira au vyanzo vya maji. Katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kufuatilia ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira kwa lengo la kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

Ubora wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji

75. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakiki ubora wa madawa ya kusafisha na kutibu maji ya kunywa kabla ya manunuzi kufanyika. Hadi mwezi Machi 2020, jumla ya sampuli **30** za madawa ya kusafisha na kutibu maji kutoka Taasisi

mbalimbali za ugavi zilichunguzwa ubora wake. Sampuli hizo ni za madawa ya kusafisha maji aina ya *Aluminium Sulphate* (Shabu) sampuli **14**, *Polymerblend (5)*, *Anionic Polymer (1)*, *Algal floc (1)* na *Zeta Floc (1)*. Vilevile, sampuli **nane (8)** aina ya *Calcium Hypochlorite* kwa ajili ya kutibu maji zilichunguzwa ubora wake. Matokeo yamebaini kuwa sampuli zote za madawa hayo zilikidhi viwango vinavyokubalika kwa ajili ya kusafisha na kutibu maji na ushauri ulitolewa kwa Taasisi husika kuendelea na manunuzi husika. Katika mwaka 2020/2021, Wizara imepanga kuendelea kufuatilia na kuhakiki ubora wa madawa ya kutibu maji katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira pamoja na Taasisi zinazohusika na usambazaji wa madawa hayo. Aidha, ili kuimarisha upatikanaji, thamani ya fedha na ubora wa madawa ya kutibu maji yanayotumiwa na mamlaka za maji nchini, Wizara kwa kushirikiana na Bohari Kuu ya Madawa (Medical Stores Department -MSD) inaandaa utaratibu utakaotumika katika uagizaji wa madawa ya kutibu maji kwa pamoja kwa lengo la kupunguza gharama za ununuzi wa madawa hayo.

Mkakati wa Uondoaji wa Madini ya Fluoride katika Maji

76. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mkakati wa Kuondoa Madini ya Fluoride (*Defluoridation Strategy*) kwenye maji, Wizara imeendelea kusambaza teknolojia ya kutumia chengachenga za mifupa ya ng'ombe ili kuondoa madini ya fluoride katika maji ya kunywa na kupikia. Hadi mwezi Machi 2020, mitambo 200 ya ngazi ya kaya imesambazwa kwenye maeneo ya Minjingu na Olasiti katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati na imenufaisha wananchi wapatao **1,600** kwa kupata maji safi na salama. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu ya athari za kiwango kikubwa cha madini ya fluoride katika maji ya kunywa na kupikia katika Kijiji cha Majengo Mkoani Kilimanjaro; maeneo ya Minjingu na Olasiti Mkoani Manyara; na Mwandu, Wilaya ya Mkalama Mkoani Singida. Vilevile, Kituo cha Utafiti wa Madini ya Fluoride cha Ngurdoto kimeandaa *documentary* kuhusu masuala ya fluoride na itasambazwa ili kujenga uelewa kwa wananchi. Pia, Kituo kimeshiriki katika Mkutano Mkuu wa mwaka wa Mabonde ya Maji na Mkutano Mkuu wa Tume ya Sayansi na

Teknolojia (*COSTECH*) na kutoa elimu juu ya masuala ya athari za madini ya fluoride na teknolojia ya kuondoa madini hayo kwa kutumia chengachenga za mifupa ya ng'ombe katika maji ya kunywa na kupikia.

Maabara za Maji Kupata Ithibati (*Accreditation*)

77. Mheshimiwa Spika, Wizara iliweka lengo la kuongeza idadi ya maabara za maji zenyetibati (*accreditation*) kufikia saba (7) kutoka maabara moja ya sasa ambayo ni Mwanza. Katika kufikia azma hiyo, mafunzo yalitolewa kuhusu Mwongozo mpya wa Kimataifa wa Uendeshaji wa Maabara za Uchunguzi (*ISO 17025:2017*) kwa maabara zote za maji **16** nchini ili ziweze kupata ithibati. Hadi mwezi Machi 2020, maabara sita (6) za Dar es Salaam, Singida, Shinyanga, Musoma, Bukoba na Kigoma zimeainishwa kupata ithibati katika Mwaka 2019/2020 ambapo maandalizi ya mlongozo inayohitajika kuwasilishwa katika Bodi ya *SADCAS* kwa ajili ya kupata ithibati hiyo imekamilika na maombi ya kupewa ithibati tayari yamewasilishwa.

78. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa takwimu sahihi za uchunguzi wa ubora wa maji kimaabara zinatolewa, mwezi Julai na Agosti, 2019 maabara za ubora wa maji zilishiriki zoezi la kujipima uwezo wa utendaji kazi kimaabara linaloratibiwa na Shirika la Maji la Namibia (*NamWater*). Matokeo yalitoka mwezi Novemba, 2019 na yalionesa maabara zetu kufanya vizuri katika upimaji wa viashiria vyatvijidudu na vile vyatvya *physical chemical*.

79. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kufuatilia ubora wa maji yanayosambazwa kwa matumizi ya majumbani kwa kukusanya na kuchunguza sampuli **10,000** za maji na kuendelea kuimarisha maabara za maji na kuhakikisha kuwa zinapata ithibati.

Miradi na Programu za Kuboresha Huduma ya Maji Vijijini

80. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea kuboresha hali ya

upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa wananchi waishio maeneo ya vijijiini kwa kutekeleza miradi na programu za uendelevu wa huduma. Kazi zinazotekelizwa ni pamoja na kujenga miradi mipya na kukarabati na kupanua miradi ya maji iliyopo.

Miradi Inayotekelizwa Vijijiini

81. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia RUWASA inatekeleza miradi ya maji **652** ambapo hadi mwezi Machi 2020, miradi **94** yenye vituo vya kuchotea maji **2,495** imekamilika na miradi **558** ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. **Kiambatisho Na. 3** kinaonesha orodha ya miradi ya maji inayoendelea kutekeleza vijijiini.

Programu za Kuimarisha Uendelevu wa Huduma ya Maji Vijijiini

82. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inatekeleza programu maalum kwa lengo la kuimarisha uendelevu wa miradi ya maji vijijiini. Programu hizi ni Programu ya Malipo kwa Matokeo (*Payment by Results - PbR*), inayotekelizwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Serikali ya Uingereza (*DFID*) na Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijiini (*Sustainable Rural Water Supply and Sanitation Program - Program-for-Results - PforR*), inayotekelizwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Benki ya Dunia. Maeleo mafupi kuhusu program hizi ni kama ifuatavyo:-

(a) Programu ya Malipo kwa Matokeo (*Payment by Results - PbR*)

83. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (*DFID*) inatekeleza Programu ya Malipo kwa Matokeo (*PbR*) iliyoanza mwezi Aprili 2016 na itafika ukomo mwezi Machi 2022. Programu hiyo inatekeleza kwa gharama ya **Paundi za Uingereza milioni 65.4** sawa na takribani **Shilingi bilioni 190** na inalenga kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa

mazingira katika Halmashauri mbalimbali nchini. Kupitia programu hii, kazi zinakazofanyika ni pamoja na kupanua mitandao ya kusambaza maji; kukarabati na kujenga vituo vya kuchotea maji; na kuhakikisha vituo vilivyopo vinaendelea kutoa huduma.

84. Mheshimiwa Spika, kulingana na utaratibu wa utekelezaji wa programu ya *PbR*inayotekelawa katika awamu na fedha hutolewa kwa watekelezaji baada ya kukidhi vigezo vilivyokubalika vya kiutendaji na matokeo. Baadhi ya vigezo hivyo ni pamoja na idadi ya vituo vya maji vilivyokarabatiwa na vituo vipyta vilivyojengwa na vinafanya kazi katika maeneo husika. Kupitia programu hiyo, **Paundi 300** hutolewa kwa kila kituo kilichohakikiwa na kinachofanya kazi na **Paundi 150** kwa kila kituo cha kuchotea maji kitakachothibitika kuwa kinafanya kazi lakini wakati wa uhakiki kitaonekana kimefungwa kwa sababu tu ya kukosa huduma ya nishati au kwa utaratibu uliowekwa na jamii yenyewe wa kutoa maji kwa mgao.

85. Kwa sasa, awamu ya tatu ya utekelazaji wa Programu hiyo iliyoanza mwezi Julai 2019 unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2020. Katika awamu hiyo, Halmashauri **181** zilifuzu na kiasi cha **Shilingi 29,668,865,000** kilitolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira katika maeneo yao. Sehemu kubwa ya utekelezaji wa miradi hiyo unatumia wataalam wa ndani wa RUWASA kwa utaratibu wa *force account* na kuhusisha ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji **1,215** katika vijiji **2,476** ambapo **vituo 11,354** vitafufuliwa na wananchi **2,431,313** watanufaika na huduma ya maji. Miradi mbalimbali inayotekelawa vijijini kupitia *PbR* inapatikana kwenye tovuti ya Wizara: www.maji.go.tz

86. Mheshimiwa Spika, awamu ya nne ya programu hii yenyeye jumla ya **Paundi milioni 21.94** (sawa na **Shilingi bilioni 63**) itaanza kutekelezwa mwezi Mei, 2020 ambapo Halmashauri **181** zitanufaika. Kiasi hiki cha fedha kinafikisha jumla ya fedha zilizotolewa tangu kuanza kutekelezwa kwa programu hiyo Mwaka 2016 kuwa **Paundi milioni 38.09** (sawa na **Shilingi bilioni**

114.27), sawa na asilimia **58** ya fedha zote zilizopangwa kutumika kwenye programu hiyo.

(b) Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Sustainable Rural Water Supply and Sanitation Program - Program-for-Results - PforR)

87. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*Sustainable Rural Water Supply and Sanitation Program - Program-for-Results - PforR*) inayotekelawa kwa kipindi cha miaka sita (2019-2024) katika Halmashauri za Wilaya **86** kwenye Mikoa **17**. Katika awamu ya kwanza ya Programu hiyo, jumla ya **Dola za Marekani milioni 350** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali, hususan miradi ya ukarabati, upanuzi wa mtandao pamoja na ujenzi wa miradi mipyta itakayoibuliwa na Halmashauri zilizopo katika programu. Programu inatekelezwa kuititia *RUWASA* katika wilaya husika. Hadi mwezi Desemba 2019, Serikali ilipokea **Shilingi bilioni 119.99** kutoka Benki ya Dunia za kutekeleza miradi ya maji vijijini. Fedha hizo zitatumika kutekeleza jumla ya miradi **513** yenye vituo **9,286** vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao **2,321,500** katika vijiji **1,055**. Vilevile, sehemu ya fedha hizo zitatumika kuzijengea uwezo Jumuiya **286** za Watoa Huduma za Maji ngazi ya jamii katika vijiji **1,720**. Miradi mbalimbali inayotekelawa vijijini kuititia *PforR* inapatikana kwenye tovuti ya Wizara: www.maji.go.tz

88. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2020, hatua iliyofikiwa katika maeneo mengi ni kukamilika kwa taratibu za ununuzi vifaa, ikiwemo pampu na mabomba ya maji. Aidha, utekelezaji wa miradi hiyo kwa sehemu kubwa unahusisha wataalam wa ndani (*force account*). Awamu ya pili itaendelea baada ya kufanyika kwa tathmini ya utekelezaji wa awamu ya kwanza.

Utekelezaji wa Miradi ya Maji na Usafi wa Mazingira kupitia Force Account

89. Mheshimiwa Spika, Awamu ya Kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP I) ilikumbwa na changamoto pamoja na dosari nyingi za kiutekelezaji zilizosababisha baadhi ya miradi iliyokamilika kushindwa kufanya kazi kama ilivyotarajiwu. Mojawapo ya changamoto iliyojitokeza katika utekelezaji wa awamu hiyo ni baadhi ya Wakandarasi na Wataalamu Washauri wasio waaminifu kuwasilisha gharama za juu za vifaa vya kutekeleza miradi ya maji zisizoendana na uhalisia wa bei. Katika kukabiliana na changamoto hiyo na kuhakikisha miradi ya maji inajengwa kwa gharama nafuu, Wizara ya Maji imeamua kufanya yafuatayo:-

90. Mheshimiwa Spika, kwanza, kuweka utaratibu mzuri wa kutoa vibali vya kuingia mikataba kwa miradi mipya inayotarajiwu kutekelezwa na Wakandarasi; na miradi hiyo kusimamiwa na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini au Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji (RUWASA). Utaratibu huo unaenda sambamba na kuwa na makisio ya kihandisi ya bei za vifaa vya kutekeleza miradi zitakazokokotolewa kulingana na bei za vifaa hivyo viwandani. Utaratibu huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ongezeko la gharama za miradi zisizokuwa na uhalisia ambazo zimekuwa zikiwasilishwa na Wakandarasi.

91. Mheshimiwa Spika, pili, kutekeleza baadhi ya miradi ya miundombinu ya maji kwa kutumia Wataalamu wa ndani (*force account* au *direct labour*) unaohusisha Wataalamu na Wahandisi waliopo katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini; Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji (RUWASA); au kwa ushirikiano wa pamoja baina ya Mamlaka hizo na RUWASA. Aidha, kutokana na wingi wa miradi inayotekeliza katika maeneo mbalimbali nchini, baadhi ya miradi itaendelea kutekelezwa na Wakandarasi lakini Wizara itaweka utaratibu mzuri zaidi wa usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo ili kuhakikisha inajengwa kwa ubora na kuzingatia thamani ya fedha.

92. Mheshimiwa Spika, Wizara imeamua kutumia utaratibu wa *force account* katika kutekeleza baadhi ya miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji kwa kuwa uzoefu unaonesha gharama za ujenzi wa miradi kupungua kwa takribani katika **asilimia 30** hadi **asilimia 70** ikilinganishwa na gharama zilizowasilishwa na Wakandarasi. Vilevile, miradi mingi ya maji inayotekelawa na Wakandarasi imekuwa haikamiliki kwa wakati. Katika utaratibu huo wa kutumia Wataalamu wa ndani miradi iliyotekelawa na inayoendelea kutekelezwa, imeonekana kukamilika katika muda uliopangwa na kwa ubora uliotarajiwa ikilinganishwa na miradi inayotekelawa na Wakandarasi. Pia, kuititia utaratibu huo kumesaidia wataalam wa ndani kupata fursa za kujengewa uwezo na uzoefu ikiwa ni pamoja na kuongeza uwajibikaji na kuwepo kwa uendelevu wa miradi inayojengwa.

93. Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara ilipitia gharama za kutekeleza **miradi 23** (*Kiambatisho Na. 4a*) yenye thamani ya **Shilingi 48,509,042,963.57** kulingana na *Engineer's estimate* na kubaini kuwa gharama halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo kuititia utaratibu wa *force account* ni **Shilingi 27,499,674,190.42** ambapo Wizara imeamua kutekeleza miradi hiyo kuititia utaratibu huo. Kutekelezwa kwa miradi hiyo, kutawezesha Serikali kuokoa kiasi cha fedha **Shilingi 21,009,368,773.15**. Baada ya Wizara kuona faida ya kutekeleza miradi kwa njia ya *force account* inaendelea kutekeleza miradi mingine **169** (*Kiambatisho Na. 4b*) kwa utaratibu huu ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Gharama za miradi hiyo ni **Shilingi 133,827,567,744.45** ukilinganisha na makadirio ya **Shilingi 161,554,090,013.48** kama miradi hii ingetekelawa kwa njia ya wakandarasi ambapo kiasi cha **Shilingi 27,726,522,269.04** kitaokolewa. Hivyo, kwa ujumla Serikali itaokoa **Shilingi 48,735,891,042.19** kwa kuamua kutekeleza miradi kwa utaratibu wa *force account*.

94. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kubainisha miradi inayoweza kutekelezwa na wataalam wa ndani kuititia *force account* ili miradi hiyo itekelawezwe kwa haraka na kwa ufanisi na wananchi wapate huduma bora za maji na usafi wa mazingira. Kwa miradi

mikubwa, Wizara itaendelea kutumia wataalam washauri na wakandarasi katika kuitekeleza ambapo Wizara itaongeza umakini na kusimamia kwa ukaribu hususan kwenye manunuzi ya vifaa, utaalam na uwezo wa wakandarasi.

Matumizi ya Teknolojia ya Nishati Jadidifu (Renewable Energy)

95. Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto za gharama kubwa za uendeshaji wa miradi ya maji vijijini hususan miradi inayotumia nishati ya mafuta ya dizeli ambayo ni ghali. Hali hiyo imesababisha wananchi washindwe kumudu gharama za uendeshaji kwa baadhi ya miradi ya maji vijijini. Katika kupunguza gharama za uendeshaji wa miradi hiyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatekeleza programu ya kubadilisha teknolojia ya uendeshaji wa miradi ya maji vijijini inayotumia mafuta ya dizeli ili itumie nishati ya jua ambayo teknolojia nafuu.

96. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na *Ohio State University – OSU* chini ya ufadhili wa Taasisi ya Kiraia (*Water Development Alliance-WADA*) inatekeleza mradi wa Uboreshaji wa Mifumo Endelevu ya Maji Vijijini (*Sustainable Village Water Systems Project*) kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 2.4**. Kiasi hicho cha fedha kimepangwa kutumika katika vijiji **36** katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Mara, Mwanza na Kilimanjaro. Programu hii inahusisha ukarabati wa miundombinu ya kusambaza maji; kuongeza vyanzo vya maji; na kufunga mfumo wa umeme wa jua. Mradi huo pia unatekelezwa katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na vijiji **28**. Hadi mwezi Machi 2020, mradi umekamilika katika vijiji **saba (7)** vya Ghalunyangu, Mughanga, Sagara, Nduamughanga (Singida Vijijini); Unyankhanya (Ikungi), Rungwa (Itigi), Muhalala (Manyoni) pamoja na Chuo Kikuu cha Dodoma. Utekelezaji unaendelea katika vijiji 21 ambavyo ni Mwarufyu/Mvae, Msange, Mdillu, Ngimu (Singida Vijijini); Majiri (Manyoni); Nghong' onha (Dodoma); Mwandihimji, Matinje, Mwalala, Simbo (Igunga); Mahene, Nawa, Sojo (Nzega); Sangu A, Sangu B, Gulumwa (Kwimba); Kitaramanka, Kamgendi (Butiama); Kebweye (Tarime); na Hunyari (Bunda).

Mradi utakapokamiliika utawanufaisha wananchi wapatao **120,000**.

97. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kuititia Ufadhilli wa GPOBA (*Global Partnership on Output-Based Aid*) wanatekeleza mradi wa Kubadili Miradi ya Maji inayotumia Teknolojia ya Nishati ya Dizeli kwenda Nishati Jua (*Accelerating Solar Pumping via Innovative Financing Project*). Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 8.5** ambapo Benki ya Dunia watatoa **Dola za Marekani milioni 5.1** na Benki ya Uwekezaji Tanzania (*TIB*) watatoa **Dola za Marekani milioni 3.4**. Utekelezaji wa mradi umegawanywa katika awamu tatu ambapo awamu ya kwanza utatekelezwa katika vijiji **280** na kuwanufaisha wananchi wapatao **840,000**. Awamu ya pili itatekelezwa katika vijiji **430** na kuwanufaisha wananchi wapatao **1,290,000** na awamu ya tatu itahusisha vijiji **1,500** na wananchi wapatao **4,500,000** watanufaika.

98. Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza, mradi umeanza kwa majaribio katika mikoa **12** ya Dodoma, Morogoro, Geita, Kagera, Mara, Shinyanga, Mtwara, Rukwa, Singida, Tabora, Arusha na Manyara. Hadi mwezi Machi 2020, kazi ya kukusanya takwimu imekamilika katika mikoa **mitano (5)** ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Tabora na Mtwara. Vilevile, wakandarasi wa kununua, kufunga na kufanya matengenezo ya mitambo ya mfumo wa umeme jua katika mikoa ya Dodoma na Singida wamepatikana ambapo jumla ya miradi **43** kutoka Mkoa wa Singida na miradi **39** kutoka Mkoa wa Dodoma itaanza kufungwa mitambo ya umeme jua. Kazi hizo zitahusisha pia, kufunga mita za LUKU za maji (*pre-paid water meter*) katika miradi ya mikoa hiyo.

Uimarishaji wa Jumuiya za Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs)

99. Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa awali, miradi ya maji vijijini inapokamiliika ilikuwa ikitabidiwa kwa wananchi ambao huunda Jumuiya (*Community Based Water Supply Organisations - CBWSOs*) kwa ajili ya kuiendesha miradi hiyo.

Muundo wa Jumuiya hizo haukuzingatia utaalam kwenye nafasi zake za usimamizi. Hali hiyo ilisababisha kukosekana kwa uendelevu wa miradi ya maji vijijini kwa kuwa wajumbe wengi wa jumuiya hizo hawakuwa na utaalam kwenye nafasi walizopewa. Kupitia Sheria **Na. 5** ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019, muundo wa jumuiya hizo kwa sasa umeboreshwa na kuweka hitaji la kuwa na watalaaam wa ufundi na uendeshaji wa fedha. Aidha, RUWASA wametakiwa kuhamasisha sekta binafsi kuunda jumuiya za kuendesha miradi ya maji vijijini kwa utaratibu maalum watakaoingia kati ya taasisi binafsi na Meneja wa RUWASA wa Wilaya.

100. Mheshimiwa Spika, Wizara iliandaa Kanuni za Usajili na Uendeshaji wa Jumuiya za Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (*The Water Supply and Sanitation Registration and Operations of Community Based Water Supply Organisations Regulations, 2019*). Kupitia kanuni hiyo, RUWASA imeweza kuandaa miongozo mitatu ambayo ni Mwongozo wa Uundaji na Usajili wa CBWSOs; Mwongozo wa Kushirikisha Sekta Binafsi katika Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii; na Mwongozo wa Uunganishaji wa Jumuiya za Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii. Kuunganishwa kwa Jumuiya hizo kutasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa miradi ya maji na kuongeza ufanisi katika usimamizi wa miradi ya maji vijijini.

101. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2020, kuna jumla ya jumuiya za Watoa huduma ya Maji Ngazi ya Jamii zipatazo **3,236** kwenye vijiji **4,490** kati ya vijiji **10,630** vyenye huduma ya maji. Jumuiya hizo zilisajiliwa kwa Sheria ya Na. 12 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2009. Kutokana na mabadiliko ya Sheria, Jumuiya za Watumiaji Maji Ngazi ya Jamii zilizopo zinatakiwa kuhuishwa kwa kutumia kuzingatia matakwa ya sheria mpya. Katika kipindi hicho, RUWASA imefanikiwa kuunda na kusajili jumuiya mpya **21** katika mikoa ya Mwanza, Ruvuma, Iringa na Songwe. Katika mwaka 2020/2021, RUWASA imepanga kuunda na kusajili Jumuiya **860** pamoja na kuhuishwa jumuiya **3,236** katika mikoa yote ya Tanzania Bara. **Kiambatisho Na. 5** kinaonesha idadi ya CBWSOs zilizosajiliwa.

Miradi ya Usambazaji Maji Mijini

102. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo imeendelea kutekeleza miradi ya kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa. Kazi zilizotekelizwa ni pamoja na kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya majisafi na salama, pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini kwa kuzipatia mafunzo na kujenga ofisi.

103. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, jumla ya miradi **75** inatekelezwa katika maeneo mbalimbali ya mijini nchini. Kati ya miradi hii, hadi kufikia Machi 2020, jumla ya miradi **2** imekamilika na miradi **73** inaendelea kutekelezwa. Orodha ya miradi ya maji mijini inayotekelizwa na hatua iliyofikiwa imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 6.**

Hatua Zilizofikiwa katika Utekelezaji wa Miradi ya Maji Mipyä Mikubwa na ya Kimkakati

104. Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha Wizara imeanza kutekeleza miradi mipyä mikubwa na ya kimkakati miwili. Miradi hii ni Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji **28** na Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadilki ya Tabia Nchi wa Simiyu. Kutokana na ukubwa na umuhimu wa miradi hii, ninaomba kutoa maelezo mafupi kuhusu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake.

(a) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28

105. Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa mwaka jana wakati nikiwasilisha Bajeti yangu nilitoa taarifa kuhusu Serikali yetu kupata mkopo nafuu wa dola milioni 500 kutoka Serikali ya India kuitia Benki ya Exim India kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28 Tanzania Bara na mji mmoja visiwani Zanzibar. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:

106. Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Fedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya India kupitia Benki ya EXIM India ulisainiwa tarehe 10 Mei, 2018. Mara ya baada ya kusainiwa kwa Mkataba wa Fedha, taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya kazi ya usanifu wa kina, kuandaa vitabu vya zabuni pamoja na kazi ya usimamizi wa ujenzi wa miradi zilanza. Mtaalam Mshauri alipatikana tarehe 14 Mei, 2019, na kuanza kazi rasmi tarehe 01 Juni, 2019 kwa muda wa miezi mitatu, na alikamilisha kazi na kukabidhi taarifa yake ya mwisho tarehe 24 Agosti, 2019. Wizara iliwasilisha taarifa ya usanifu kwa Serikali ya India tarehe 29 Agosti, 2019. Serikali ya India ilirudhisha taarifa hiyo na maoni yake na Wizara iliwayfanyia kazi na kuwasilisha taarifa iliyofanyiwa marekebisho tarehe 04 Novemba, 2019. Tarehe 31 Januari, 2020 Serikali ya India iliidhinisha rasmi taarifa hiyo na kuruhusu hatua zingine kuendelea, ikiwemo kuandaa hadidu rejea kwa ajili ya kazi zitakazofanywa na wakandarasi.

107. Mheshimiwa Spika, ninapenda kulitaarifu Bunge lako kuwa hadidu rejea za wakandarasi zilishakamilika na kukubaliwa na pande zote mbili, yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya India. Aidha, Benki ya Exim ya India wameshakamilisha kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kupata orodha ya awali ya wakandarasi (prequalified list of contractors). Tangazo la zabuni lilitolewa na Benki ya Exim tarehe 24 Machi, 2020 na mwisho wa kupokea maombi ilikuwa tarehe 21 Aprili, 2020. Benki ya Exim wanatarajia kufanya tathimini ya zabuni za wakandarasi kuaniza tarehe 12 Mei, 2020 na kukamilisha tarehe 19 Mei, 2020. Baada ya hapo orodha ya wakandarasi waliopita katika mchujo wa awali itawasilishwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuendelea na taratibu za manunuzi kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Tanzania. Tunatarajia mchakato wa manunuzi kwa upande wa Tanzania ukamilike ifikapo mwezi Julai 2020 na wakandarasi wawe wameshaanza kazi ifikapo mwisho wa Mwezi Julai 2020.

108. Mheshimiwa Spika, mradi huu utakapokamilika unatarajiwa kunufaisha wananchi wapatao **milioni 4** kwa

kuanzia na wananchi **milioni 6** ifikapo mwaka 2040 katika miji 28.

(b) Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi wa Simiyu

109. Mheshimiwa Spika, tarehe 03 Mei, 2019 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya *KfW* kwa niaba ya Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund-GCF*) na Serikali ya Ujerumanzi zilisaini Mkataba wa Kifedha kwa lengo la taasisi hiyo kuipatia Tanzania msaada wa **Euro milioni 102.7**. Fedha hizi ni kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi Mkoani Simiyu. Aidha, katika mradi huu Serikali ya Jamhuri ya Muungano itachangia **Euro milioni 40.1** na wananchi watakaonufaika na mradi huu watachangia **Euro milioni 1.5** kupitia nguvu zao katika ujenzi wa mradi huu. Hivyo, gharama za mradi ni jumla ya **Euro milioni 144.3**, sawa na takribani **Shilingi bilioni 370**.

110. Mheshimiwa Spika, usanifu wa mradi umekamilika na zoezi la kutathmini ardhi itakayochukuliwa katika ujenzi wa mradi huo linaendelea ili wahusika waweze kufidiwa. Aidha, Serikali inaendelea na mchakato wa kuwapata wataalam washauri watakaosimamia ujenzi wa mradi huo. Wataalam washauri wanatarajiwa kupatikana kabla ya mwisho wa mwezi Mei 2020 na wakandarasi wa ujenzi wa mradi wanatarajiwa kupatikana ifikapo mwishoni mwa mwezi Julai 2020.

111. Mheshimiwa Spika, lengo kuu la mradi huo ni kuboresha afya na kuongeza uzalishaji mali ili kuinua hali ya maisha ya wananchi walioathirika na mabadiliko ya tabianchi katika maeneo husika ya mradi. Mradi una maeneo makubwa manne yafuatayo:-

(i) Kusambaza huduma ya maji kwa kutumia chanzo cha Ziwa Victoria na kuyapeleka katika Miji Mikuu ya Wilaya za Busega, Bariadi na Itilima na vijiji zaidi ya 200 vilivyoko pembezoni mwa bomba kuu umbali wa kilomita 12 kila upande.

- (ii) Ukarabati na ujenzi wa mabwawa ya kilimo cha umwagiliaji endelevu (*Smart Agriculture*) ambayo pia yatatumika kupunguza adha ya maji kwa ajili ya kilimo na mifugo.
- (iii) Kuimarisha huduma za usafi wa mazingira hususani ujenzi wa mabwawa ya majitaka (*Sludge Digester*) na vyoo vya mfano katika mashule na vituo vya afya.
- (iv) Kujenga uwezo wa watumishi wa sekta ya maji kwa halmashauri zote husika, Mkoa pamoja na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira ili kutimiza malengo ya Mradi kwa ufanisi na kwa muda muafaka na uendelevu wa Mradi (*project sustainability*).

112. Mheshimiwa Spika, mradi huu utatekelezwa katika Mkoa wa Simiyu na unatarajiwu kunufaisha wananchi laki nane (**800,000**) katika Wilaya tano za Mkoa wa Simiyu ambazo ni Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu. Kwa kuanzia, katika awamu ya kwanza mradi huu utatekelezwa katika Wilaya za Busega, Itilima na Bariadi.

Miradi ya Usafi wa Mazingira

113. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya usafi wa mazingira katika miji mbalimbali nchini kwa kujenga na kupanua mifumo ya uondoaji wa majitaka na mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka, pamoja na kununua magari maalum ya uondoaji wa majitaka. Lengo ni kuongeza wastani wa upatikanaji wa huduma hiyo kutoka **asilimia 15** za sasa hadi **asilimia 30** ifikapo mwezi Oktoba 2020. Katika kufikia azma hiyo, miradi mbalimbali ya usafi wa mazingira inatekelezwa na inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Maji: www.maji.go.tz

TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

Mfuko wa Taifa wa Maji

114. Mheshimiwa Spika, katika kutimiza matakwa ya Sheria, Mfuko umeendelea kutekeleza majukumu yake ili kuchangia

katika kufikia malengo makuu ya Serikali ya kuwa na huduma bora ya maji kwa wote katika maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2025; kuwa na huduma bora za maji vijijini kwa zaidi ya asilimia 90 ifikapo mwaka 2025; na kuwa na rasilimali za maji endelevu kwa kuivilinda, kuvitunza, kuviendoeleza na kutafuta vyanzo vypya nya maji.

115. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 05 ya mwaka 2019 imeainisha vyanzo mbalimbali nya mapato ya Mfuko vikiwemo fedha zitakazoidhinishwa na Bunge, misaada pamoja na fedha nyingine zitakazolipwa kwenye Mfuko kwa mujibu wa Sheria nyingine. Hadi sasa chanzo cha mapato ya Mfuko ni tozo ya Shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya dizeli na Shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya petroli.

116. Mheshimiwa Spika, kupitia chanzo hicho, katika mwaka 2019/2020, Mfuko wa Taifa wa Maji ilitengewa **Shilingi 169,949,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi mwezi Machi 2020, kiasi kilichopatikana ni **Shilingi 124,863,295,133.58** sawa na **asilimia 73** ya fedha zilizotengwa na zimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya utoaji huduma ya maji kwenye maeneo ya vijijini na mijini pamoja na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini.

117. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Mfuko wa Taifa wa Maji umepanga kuendelea kutafuta vyanzo vingine zaidi nya fedha kwa ajili ya kuongeza wigo wa kuwekeza kwenye miradi ya maji nchini. Aidha, katika jitihada za kuziwezesha Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa kuijendesha kwa kuongeza mapato yao ya ndani, Mfuko wa Taifa wa Maji umepanga kuanza kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa Mamlaka hizo kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya utoaji huduma ya maji.

Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)

118. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma, uendeshaji na

utekelezaji wa miradi ya maji vijijiini, Serikali kuititia Sheria **Na. 5** ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019, ilianzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijiini (*Rural Water Supply and Sanitation Agency – RUWASA*) ulioanza rasmi utekelezaji wa majukumu yake mwezi Julai 2019. Kuanzishwa kwa RUWASA kumetokana na changamoto zilizokuwepo katika uendelezaji, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji vijijiini. Changamoto hizo ni pamoja na ujenzi wa baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati, baadhi ya miradi kujengwa chini ya kiwango stahili cha ubora, baadhi ya miradi kuwa na gharama kubwa ikilinganishwa na bei ya soko na baadhi ya miradi iliokamilika na kukabidhiwa kwa wananchi kutokuwa endelevu.

119. Mheshimiwa Spika, kulingana na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019, RUWASA inasimamiwa na Bodi Tendaji yenye wajumbe tisa. Majukumu ya RUWASA ni pamoja na kupanga, kusanifu na kujenga miradi ya maji vijijiini na kusimamia uendeshaji na uendelevu wa miradi hiyo. Kimuundo RUWASA ina ngazi kuu tatu ambazo ni RUWASA – Makao Makuu; Ofisi za Mikoa na Ofisi za Wilaya. RUWASA – Makao Makuu inaandaa na kuweka mifumo, miongozo, kufuatilia na kusimamia matumizi yake katika kutekeleza miradi ya maji, utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijiini na baadhi ya miji midogo; na uendelevu wa miradi vijijiini na baadhi ya miji midogo. Ofisi za RUWASA Mkoa zina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maji kwenye wilaya husika pamoja na kuzijengea uwezo ofisi za RUWASA za wilaya. Ofisi za RUWASA Wilaya zina jukumu la kutekeleza miradi ya maji ndani ya wilaya na kuunda, kusimamia na kuzijengea uwezo Jumuiya za Huduma za Maji Ngazi ya Jamii (*Community Based Water Supply and Sanitation Organization-CBWSOs*). Katika mwaka 2020/2021, RUWASA itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali nchini.

Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

120. Mheshimiwa Spika, jukumu la Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira mijini ni kutoa huduma za maji safi na

salama pamoja na uondoaji wa majitaka ambapo Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Miji Mikuu ya Mikoa zimeweza kupiga hatua katika utoaji wa huduma ya majisafi na kuweza kuongeza maunganisho ya wateja kutoka wateja **803,613** mwezi Juni 2019 na kufikia wateja **869,275** mwezi Machi 2020. Vilevile, wastani wa makusanyo ya maduhuli kwa mwezi yalikuwa **Shilingi bilioni 23.79** mwezi Juni 2019 na hadi kufikia mwezi Machi 2020 wastani wa makusanyo ya maduhuli ni **Shilingi bilioni 22.61** ambapo mvua nyingi za vuli zilizonyesha zimeathiri makusanyo. Aidha, wastani wa upotevu wa maji kwa mwezi kwenye miji mikuu ya mikoa umepungua kutoka **asilimia 40.63** mwezi Juni 2019, hadi asilimia **33** mwezi Machi 2020. Hatua hiyo ya kuongeza makusanyo ya maduhuli imeziwezesha mamlaka hizo za maji kuchangia katika kutekeleza miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya maji kwa kutumia fedha za makusanyo yao na kwa kiasi kikubwa kumeipunguzia Serikali mzigo wa kuwekeza kwenye mamlaka hizo.

121. Mheshimiwa Spika, huduma ya uondoaji majitaka, kwa wateja waliouanganishwa kwenye mtandao wa majitaka hutolewa katika Miji **11** ambayo ni Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Tabora, Moshi, Tanga, Songea na Iringa. Idadi ya wateja waliouanganishwa kwenye mtandao wa majitaka katika miji hiyo imeongezeka kutoka **49,864** mwezi Juni 2019 hadi kufikia wateja **50,685** mwezi Machi, 2020. Vilevile, huduma ya uondoaji wa majitaka kwa kutumia magari maalum ya kuondoa majitaka hutolewa na Mamlaka za Sumbawanga, Bukoba, Musoma, Geita, Kigoma, Nansio na Sengerema ambapo kumejengwa mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka. Aidha, katika miji ya Kahama, Misungwi, Lindi, Magu na Lamadi kumejengwa mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka ambayo yapo katika hatua za mwisho kuanza kutumika.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA)

122. Mheshimiwa Spika, *EWURA* imepewa majukumu ya kudhibiti utoaji wa huduma za nishati na maji. Kwa upande wa sekta ya nishati, *EWURA* inadhibiti huduma za umeme,

mafuta na gesi asilia na huduma hizo zinasimamiwa na Wizara ya Nishati. Kwa upande wa sekta ya maji, *EWURA* inadhibiti masuala ya ubora wa huduma za maji na usafi wa mazingira zinazosimamiwa na Wizara ya Maji. Katika mwaka 2019/2020, *EWURA* imeendelea na udhibiti wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

123. Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti ubora wa huduma, *EWURA* ilikagua miundombinu inayotoa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka katika mamlaka za maji **74** na kuzishauri kuhusu taratibu bora za uendeshaji, matengenezo, ukarabati na uboreshaji wa miundombinu; vilevile, ilihakiki ubora wa majisafi katika mamlaka **62** na ubora wa majitaka yanayotoka katika mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka katika mamlaka **tisa (9)** ili kujiridhisha kama majitaka hayo yanakidhi viwango vya ubora unaokubalika kurudishwa kwenye mazingira; pia, ilifanya ukaguzi maalum kwa mamlaka **nne (4)** za maji nchini za Bariadi, Kigoma, Mahenge na Kilindoni. Kupitia matokeo ya kaguzi hizo, *EWURA* ilitoa ushauri na maelekezo mbalimbali ya kuboresha utoaji wa huduma hizo kwenye Mamlaka husika.

124. Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti bei za maji, *EWURA* ilitathmini na kuidhinisha bei mpya za huduma ya maji kwa mamlaka za maji **tatu (3)** za Mwanza, Namtumbo na Morogoro; vilevile, ilifanya tathmini na kuidhinisha mikataba miwili ya huduma kwa mteja kwa Mamlaka za Maji za Tunduru na Ruangwa; pia, kupitisha Mipango ya Kibiashara kwa Mamlaka **nne (4)** za Bariadi, Dodoma, Same na Sumbawanga; na kufanya ufuatilaji wa bei za maji kwa mamlaka zote za maji nchini na kuchukua hatua za kiutendaji na kisheria kwa mamlaka za maji zilizokiuka taratibu. Aidha, *EWURA* imeendelea kutoa elimu kwa wadau wake kuhusu masuala mbalimbali ya kiudhibiti ikiwa ni pamoja na taratibu za kupanga bei za maji.

125. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa mamlaka za maji zinatoa huduma zinazokidhi viwango vya ubora vinavyotakiwa, *EWURA* ilipitia upya na kuboresha Mwongozo

wa Kusimamia Ubora wa Majisafi na Majitaka (*Water and Wastewater Quality Monitoring Guidelines*) wa mwaka 2014 na kutoa mwongozo mpya wa mwaka 2020. Vilevile, *EWURA* ilipitia upya na kuboresha Kanuni za Utoaji wa Huduma za Maji za mwaka 2011 na Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji [*Water Supply and Sanitation (Quality of Service) Rules*] za mwaka 2016 na kutoa kanuni mpya za mwaka 2020.

126. Mheshimiwa Spika, vilevile, *EWURA* ina jukumu la kuanda taarifa za utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kila mwaka na kwa mwaka 2018/2019, taarifa hiyo iliandaliwa na kutolewa mwezi Julai 2019. Taarifa hizo husaidia Wizara pamoja na Wadau wa sekta ya maji kuanda na kutekeleza mipango mbalimbali ya kuimarisha na kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira. Aidha, *EWURA* imeendelea kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu hatua mbalimbali za kuchukua ili kuimarisha utendaji na ufanisi wa mamlaka za maji nchini. Hii ni pamoja na ushauri wa kuzunganisha baadhi ya mamlaka za maji (*clustering*) ili kuunda mamlaka kubwa zitakazotekeliza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

127. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ndogo ya umeme, *EWURA* iliendelea kupanua wigo wa utoaji huduma hiyo kwa kuidhinisha leseni **nane (8)** za miradi ya kuzalisha umeme. Kati ya hizo, leseni **tatu (3)** ni za muda mfupi na **tano (5)** ni za muda mrefu. Vilevile, *EWURA* ilitoa leseni **351** za ufungaji mifumo ya umeme kwa wataalam mbalimbali wanaofanya kazi hiyo. Katika mwaka 2019/2020, *EWURA* imefanya ukaguzi wa miundombinu ya umeme katika mikoa **17** ambapo kaguzi **11** zilifanyika kwenye miundombinu ya ugavi na **sita (6)** kwenye vyanzo vya uzalishaji umeme. Lengo la ukaguzi huo ni kuhakikisha miundombinu ya umeme inayojengwa na kuendeshwa inakuwa bora ili kupunguza uvezakano wa kuleta madhara kwa watu, mali na mazingira. Matokeo ya kaguzi hizo yaliwasilishwa kwa watoa huduma na kupewa ushauri wa kuboresha.

128. Mheshimiwa Spika, katika sekta ndogo ya mafuta, *EWURA* imeendelea kutoa leseni za biashara ya mafuta,

pamoja na kupanga bei kikomo za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa kwa Tanzania Bara. Vilevile, iliendelea kudhibiti ubora wa mafuta hayo ili watumiaji waweze kutumia mafuta bora na kwa bei ambayo imepangwa na *EWURA*. Hadi mwezi Machi 2020, *EWURA* imetoa leseni **337** kwa vituo vya mafuta na kati ya hizo, leseni **107** ni za vituo vipyta na leseni **220** ni kwa vituo vya zamani.

129. Mheshimiwa Spika, *EWURA* imeendelea kusimamia mfumo wa uagizaji wa mafuta wa pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*). Kupitia mfumo huo mikoa mbalimbali hupata mafuta kupitia bandari ya karibu. Mwezi Julai 2018, Bandari ya Mtwara ilianza kupokea mafuta kupitia *Mfumo wa BPS* na wananchi wa Mikoa ya Kusini ya Mtwara, Lindi na Ruvuma wananaufaika kwa kushuka kwa bei za mafuta zilizokuwa juu kutokana na usafirishaji wa mafuta. Kanda ya Kaskazini tayari inanufaidika na mfumo huo kwa mafuta yake kupokelewa Bandari ya Tanga.

130. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ndogo ya gesi asilia, *EWURA* imeendelea kukagua miundombinu ya kuchakata, kusafirisha na kusambaza gesi asilia ili kuhakikisha kuwa miundombinu hiyo inakuwa salama kwa matumizi yake na mazingira. Aidha, *EWURA* imekamilisha kanuni mbalimbali zitakazowezesha upokeaji wa taarifa kutoka kwa wazalishaji na wasambazaji wa gesi asilia kuanzia mkondo wa juu, wa kati na wa chini wa sekta ndogo ya gesi asilia; na udhibiti wa miundombinu ya gesi asilia kiufundi, kiusalama, kiafya na kimazingira kama Sheria ya Mafuta (*Petroleum Act 2015*) inavyotaka. Kanuni hizo zitaimarisha ushirikishwaji wa wazawa kwenye shughuli za uendeshaji wa sekta ndogo ya gesi asilia hapa nchini.

131. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, *EWURA* itaendelea kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake ya kiudhibiti katika sekta za nishati na maji kwa kutoa miongozo na kanuni mbalimbali kwa huduma inazoidhibiti; kukagua ubora wa miundombinu ya utoaji wa huduma na taratibu za utoaji wa huduma hizo; kudhibiti ubora wa huduma na bei ili watumiaji wapate huduma bora kwa bei zilizoidhinishwa na

EWURA; kuzijengea uwezo mamlaka za maji ili kupunguza tatizo la upotevu wa maji; na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya kiudhibiti pamoja na haki na wajibu wao.

Chuo cha Maji

132. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maji ni Taasisi ya Wizara yenye jukumu la kuandaa wataalam wa sekta za maji na umwagiliaji. Majukumu mengine yanayotekelawa na chuo ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya maji. Chuo kinatoa mafunzo katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada. Katika ngazi ya Astashahada na Stashahada mafunzo yanayotolewa ni Uhandisi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*Water Supply and Sanitation Engineering*), Uhandisi wa Umwagiliaji (*Irrigation Engineering*), Haidrojolojia na Uchimbaji wa Visima (*Hydrogeology and Water Well Drilling*), Haidrojolojia na Hali ya Hewa (*Hydrology and Meteorology*) pamoja na Teknolojia ya Maabara na Ubora wa Maji (*Water Quality Laboratory Technology*). Katika ngazi ya Shahada, mafunzo yanayotolewa ni katika fani ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation Engineering*). Vilevile, Chuo kinaendesha kozi za muda mfupi zinazombwa na wadau mbalimbali katika sekta za maji na umwagiliaji.

133. Mheshimiwa Spika, chuo kimeendelea kufanya udahili kwa wanafunzi wapya katika ngazi za astashahada, stashahada na shahada. Katika mwaka 2019/2020, wanafunzi **450** wa astashahada na stashahada; na wanafunzi **206** wa shahada ya kwanza ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji walidahiliwa. Kwa sasa, chuo kina jumla ya wanafunzi **2,238** ikilinganishwa na wanafunzi **2,151** mwaka 2018/2019 ambapo wanafunzi wa astashahada na stashahada ni **1,539** na shahada ni **699**. Aidha, katika mahafali ya Desemba 2019, jumla ya wanafunzi **586** walihitimu mafunzo yao na kati yao, wanafunzi **146** ni wa Shahada, **431** wa Stashahada na wahitimu tisa (**9**) walikuwa wa ngazi ya Astashahada. Hili ni ongezeko la asilimia **89.6** ikilinganishwa na wanafunzi **309** waliohitimu mwaka uliopita.

134. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha taaluma bora inatolewa, Chuo kinaendeleza watumishi wake kimasomo ambapo jumla ya watumishi **22** wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu. Kati ya hao, watumishi **16** wako katika mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*); watumishi wawili ni wa shahada ya uzamili (*Masters*); na wanne ni wa shahada **ya kwanza**. Vilevile, kupitia fedha za ndani, Chuo kimeanza ujenzi wa zahanati mpya ya kisasa ambapo ujenzi wake umefikia hatua ya kuezekwa; na kununua vifaa nya maabara ya *Hydraulics*. Aidha, katika kuhakikisha taaluma bora inatolewa, Chuo kimepanga kuwaendelea watumishi wake kimasomo.

135. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Chuo kimepanga kutekeleza majukumu mbalimbli yakiwemo kuongeza wataalam wanaohitajika kwenye sekta ya maji kwa kudahili jumla ya wanafunzi **1,000** katika fani mbalimbali zinazotolewa; kuboresha miundombinu mbalimbali katika mifumo ya majisafi, majitaka na TEHAMA; kuongeza vifaa nya kufundishia katika maabara; kununua vitabu mbalimbali nya rejea; na kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi. Vilevile, kupitia mradi wa "*Sustainable Rural Water Supply and Sanitation 2018 – 2024*" unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, Chuo kitaendelea kuboresha mazingira ya kazi na utoaji mafunzo kwa kufanya ukarabati (*Vertical Extension*) wa majengo ya madarasa, maabara na karakana. Aidha, chuo kitaendelea na kazi za utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo mbalimbali nchini.

MASUALA MTAMBUKA

Sheria

136. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa sheria zinazosimamia sekta ya maji na kutoa ushauri wa kisheria kwa wadau mbalimbali wanaoguswa na hatua za kuchukua dhidi ya ukiukwaji wa sheria hizo. Sheria zinazosimamia sekta ya maji ni Sheria Na. 11 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2009; Sheria Na. 5 ya Huduma za

Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019; na Sheria Na. 11 ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ya mwaka 2001. Sheria hizo zinapatikana kwenye tovuti ya Bunge (www.parliament.go.tz) na kanuni za Sheria za Maji zinapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Maji (www.maji.go.tz). Hali ya utekelezaji wa sheria hizo imefafanuliwa katika Aya zifuatazo:-

Sheria Na. 11 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Mwaka 2009

137. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2020, Wizara imekamilisha kuandaa kanuni **moja** (1) inayohusiana na kuweka mfumo wa kupanga ada za maji na kufanya marekebisho ya kanuni **nne** (4) ambazo ni kanuni ya leseni za usalama wa mabwawa; kanuni ya leseni za utafutajji na uchimbaji wa maji chini ya ardhi; kanuni ya vibali vya matumizi ya maji na kutiririsha majitaka; na kanuni ya uteuzi wa wajumbe wa bodi. Lengo la kufanya marekebisho hayo ni kuimarisha usimamizi wa kazi za usalama wa mabwawa, kuongeza ufanisi katika utoaji wa vibali vya uchimbaji wa visima vya maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani; na kuimarisha mfumo wa ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi wa rasilimali za maji kwa kuanzisha majukwaa ya wadau katika ngazi za mabonde ya maji na kitaifa.

138. Mheshimiwa Spika, kanuni zilizofanyiwa marekebisho ni zifuatazo:-

(i) *The Water Resources Management (Fee Setting) Regulations, 2019, GN. No. 825 dated 8th November 2019;*

(ii) *The Water Resources Management (Water Abstraction, Use and Discharge) (Amendment) Regulations, 2020, GN. No. 53 dated 31st January, 2020;*

(iii) *The Water Resources Management (Exploration and Drilling Licensing) (Amendment) Regulations, 2019, GN. No. 54 dated 31st January, 2020;*

(iv) *The Water Resources Management (Dam Safety) (Amendment) Regulations, 2020, GN. No. 55 dated 31st January, 2020;* na

(v) *The Water Resources Management (Procedure for Nomination of Board Members) (Amendment) Regulations, 2020, GN. No. 56 dated 31st January, 2020.*

Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019

139. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanza kutekeleza rasmi Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019 mwezi Julai 2019 na imeendelea kutoa elimu ya Sheria hiyo kwa wadau mbalimbali wanaohusika na utekelezaji wake. Aidha, Wizara imeandaa kanuni na miongozo ya utekelezaji wa Sheria hiyo ambapo kanuni zifuatazo zimeandaliwa:-

(i) Uunganishaji wa Mamlaka za Maji - Tangazo la Serikali Na. 826 la tarehe 8/11/2019 (*The Water Supply and Sanitation (Clustering of Water Authorities) Regulations, 2019 - GN. No. 826 of 8th November 2019*);

(ii) Usimamizi na Utoaji wa Huduma za Majitaka - Tangazo la Serikali Na. 827 la tarehe 8/11/2019 (*The Water Supply and Sanitation (Provision and Management of Sewage and Wastewater Services) Regulations, 2019 - GN. No. 827 of 8th November 2019*);

(iii) Usambazaji wa Maji - Tangazo la Serikali Na. 828 la tarehe 8/11/2019 (*The Water Supply Regulations, 2019 - GN. No. 828 of 8th November 2019*);

(iv) Usajili na Uendeshaji wa Vyombo vya Watumiaji Maji - Tangazo la Serikali Na. 829 la tarehe 8/11/2019 (*The Water Supply and Sanitation (Registration and Operations of Community Based Water Supply Organisations) Regulations, 2019 - GN. No. 829 of 8th November 2019*); na

(v) Mfuko wa Taifa wa Maji - Tangazo la Serikali Na. 981 la tarehe 13/12/2019 (*The National Water Fund Regulations 2019* - GN. No. 981 of 13th December 2019).

140. Mheshimiwa Spika, vilevile, katika utekelezaji wa Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019, Wizara imeandaa notisi za kuunganisha mamlaka za maji ambapo baadhi ya mamlaka hizo zimeongezewa maeneo ya utoaji wa huduma na nyingine kufutwa. Lengo ni kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji kwa mamlaka za maji. Hadi mwezi Machi, 2020 Notisi zilizoandaliwa ni za kuziongezea maeneo ya utoaji wa huduma mamlaka za maji zifuatizo:-

(i) *The Water Supply and Sanitation (Iringa Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2019; GN. No. 658 dated 6th September 2019;*

(ii) *The Water Supply and Sanitation (Dodoma Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2019; GN. No. 659 dated 6th September 2019;*

(iii) *The Water Supply and Sanitation (Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2019; GN. No. 660 dated 6th September 2019;*

(iv) *The Water Supply and Sanitation (Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2020; GN. No. 71 dated 31st January, 2020;*

(v) *The Water Supply and Sanitation (Arusha Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2019; GN. No. 661 dated 6th September 2019;*

- (vi) *The Water Supply and Sanitation (Babati Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2019, GN. No. 662 dated 6th September 2019;*
- (vii) *The Water Supply and Sanitation (Masasi- Nachingwea Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2019, GN. No. 664 dated 6th September 2019;*
- (viii) *The Water Supply and Sanitation (Manyoni Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2019, GN. No. 665 dated 6th September 2019;*
- (ix) *The Water Supply and Sanitation (Tanga Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2019, GN. No 666 dated 6th September 2019;*
- (x) *The Water Supply and Sanitation (Tabora Urban Water Supply and Sanitation Authority)(Extension of Service Area and Dis- establishment of Authority) Notice, 2019, GN. No. 667 dated 6th September 2019;*
- (xi) *The Water Supply and Sanitation (Maswa Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2019, GN. No. 668 dated 6th September 2019;*
- (xii) *The Water Supply and Sanitation (Morogoro Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis- establishment of Authority) Notice, 2019 GN. No. 669 dated 6th September 2019;*
- (xiii) *The Water Supply and Sanitation (Mwanza Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis- establishment of Authority) Notice, 2019, GN. No. 670 dated 6th September 2019;*

- (xiv) *The Water Supply and Sanitation (Mwanza Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2020, GN. No. 70 dated 31st January 2020;*
- (xv) *The Water Supply and Sanitation (Mtwara Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2019; GN. No. 671 dated 6th September 2019;*
- (xvi) *The Water Supply and Sanitation (Same - Mwanga Water Supply and Sanitation Authority) (Establishment) Notice, 2019, GN. No. 672 dated 6th September 2019;*
- (xvii) *The Water Supply and Sanitation (Kyela - Kasumulu Water Supply and Sanitation Authority) (Establishment) Notice, 2019, GN. No. 673 dated 6th September 2019;*
- (xviii) *The Water Supply and Sanitation (Moshi Urban Water Supply and Sanitation Authority (Extension of Service Area) Notice, 2019, GN. No. 585 dated 9th August 2019;*
- (xix) *The Water Supply and Sanitation (Kahama Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area and Dis-establishment of Authority) Notice, 2020; GN. No. 72 dated 31st January, 2020; na*
- (xx) *The Water Supply and Sanitation (Shinyanga Urban Water Supply and Sanitation Authority (Extension of Service Area) Notice, 2020, GN. No. 111 dated 7th February, 2020.*

Sheria Na. 11 ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ya Mwaka 2001

141. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2019/2020, Wizara ilikamilisha na kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu, mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Na. 11 ya Mwaka 2001. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisheso kupitia Sheria Na. 13 ya Marekebisheso ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2019 (*Written*

Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Act, 2019. Lengo la kurekebisha sheria hiyo ni kuongeza na kuimarisha ushirikishwaji wa Wizara zote zinazohusika katika kusimamia sekta zote zinazodhibitiwa na EWURA; na vilevile, kuipa EWURA mamlaka ya kufifilisha makosa ya jinai kwa kuzingatia misingi na kanuni zilizoainishwa kwenye sheria hiyo.

142. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kuhakikisha sheria zinazoisimamia sekta ya maji zinatekelezwa kikamilifu; kuandaa kanuni chini ya Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019; kufanya mapitio ya Sheria Na. 11 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2009 ikiwa ni pamoja na kukusanya maoni ya wadau kwa ajili ya kuifanyia mapitio ya sheria hiyo; na kutoa elimu kuhusu sheria zinazosimamia utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Maji katika Bodi za Maji za Mabonde, Mamlaka za Maji Mijini, Ofisi za Mikoa na Wilaya za RUWASA na wadau wengine wa Sekta ya Maji pamoja na jamii kwa ujumla. Aidha, Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kisheria juu ya utekelezaji wa sheria hizo na hatua za kuchukua dhidi ya ukiukwaji wake.

Ujenzi wa Majengo Katika Wizara

143. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kukabiliana na changamoto ya uhaba wa ofisi, Wizara imeanza utekelezaji wa Awamu ya Pili ya ujenzi wa ofisi za Wizara katika Mji wa Serikali, Mtumba Jijini Dodoma. Hadi mwezi Machi 2020, michoro ya jengo hilo ilikuwa imekamilika na kazi inayoendelea ni kuandaa gharama za ujenzi (*BOQ*). Ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2020/2021.

144. Mheshimiwa Spika, vilevile, katika kuimarisha Taasisi zinazosimamia rasilimali za maji, Wizara imeendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi kwa Bodi za Maji za Mabonde na Maabara za Maji nchini kote. Kwa upande wa Bodi za Maji za Mabonde, ujenzi na ukarabati unaendelea katika mabonde ya Wami/Ruvu, Ruvuma na Pwani ya Kusini, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Rufiji na Bonde la Kati. Hadi mwezi Machi 2020, ujenzi

wa majengo ya ofisi za Bodi ya Bonde la Wami/Ruvu-Morogoro pamoja na Ofisi ya Jumuiya ya Watumia Maji ya Kilosa umefikia **asilimia 55**, Ofisi ndogo za Bonde la Wami/Ruvu Dodoma **(60)**, Ruvuma na Pwani ya Kusini-Lindi **(95)**, Ziwa Nyasa-Njombe na ukarabati wa ofisi ndogo za Bonde la Ziwa Nyasa - Songea **(50)**, Ziwa Rukwa - Mbeya na Sumbawanga **(70)**, Rufiji - Iringa **(35)** na Ofisi za Jumuiya za Watumia Maji za Kimani na Mkoji **(70)**; na Bonde la Kati-Singida ujenzi wake umefikia **asilimia 98**.

145. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa Maabara ya Maji Shinyanga na ukarabati wa maabara ya Dar es Salaam. Hadi mwezi Machi 2020, ujenzi wa Maabara ya Maji Mtwara umefikia asilimia **95**, Morogoro **(65)**, Iringa **(35)** Sumbawanga **(85)**, Mbeya **(50)** na Songea **(95)**.

Mapambano Dhidi ya Rushwa

146. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kukabiliana na vitendo vya rushwa katika maeneo ya kazi kupitia Kamati ya Uongozi na Usimamizi pamoja na Kamati ya Uadilifu zenye majukumu ya kusimamia mapambano dhidi ya rushwa ngazi ya Wizara na Taasisi zake. Kamati hizo ziliundwa kufuatia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu (*National Anti-Corruption Strategy and Action Plan – NACSAP III*) uliolenga kupambana na vitendo vya rushwa kwenye maeneo yote ya kazi. Kutekelezwa kwa mkakati huo, kumepunguza malalamiko dhidi ya viashiria vya rushwa hususan kwenye manunuzi ya wataalam washauri, wakandarasi na watoa huduma wengine kwa wizara. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa watumishi wa wizara na taasisi zake kuhusu uadilifu ili kujiepusha na vishawishi na vitendo vya rushwa.

UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY)

147. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudimbalimbali za kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI na Magonjwa sugu yasiyoambukiza mahali pa kazi. Magonjwa hayo ni pamoja na kisukari, kansa, magonjwa sugu katika

mfumo wa upumuaji, magonjwa ya moyo na magonjwa ya akili. Hadi mwezi Machi 2020, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu magonjwa hayo kwa watumishi na kusambaza kondomu katika vituo vya kazi kama kinga dhidi ya maambukizi ya VVU. Katika mwaka 2020/21 Wizara itaendelea kuandaa mipango kwa ajili ya kulinda afya za watumishi, kutoa elimu na kuhamasisha watumishi kuendelea kupima afya zao na kujikinga dhidi ya magonjwa hayo.

Rasilimali Watu Katika Sekta ya Maji

148. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha sekta ya maji inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija hususan baada ya mabadiliko ya kimuundo na kimfumo, katika mwaka 2019/2020 Wizara ilifanya zoezi la kutathmini uwezo wake katika kusimamia majukumu ya sekta kwa kuangalia rasilimali watu iliyopo na uwezo wake (*HR Audit*). Matokeo ya tathmini hiyo yameonesha kuwa Sekta ya Maji ina jumla ya watumishi 8,257 ikilinganishwa na mahitaji wa watumishi 10,276 ambapo upungufu ni watumishi 2,019. Aidha; Wizara inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais-UTUMISHI kwa ajili ya kupata kibali cha kuajiri wataalam wa kutosha katika sekta ya maji ili kukabiliana na upungufu uliopo na itaendelea kuzisimamia Mamlaka za Maji ili zitenge fedha kila mwaka kwa ajili ya kuajiri watumishi wenye sifa katika Taasisi zao.

149. Mheshimiwa Spika, vilevile, tathmini hiyo imeonesha kuwa Wizara ina jumla ya Wahandisi (*Engineers*) *675 ambapo wahandisi 331* sawa na **asilimia 49.4** wamesajiliwa na Bodi ya Usajili ya Wahandisi nchini (*Engineers Registration Board-ERB*) kama wahandisi wataalam na wahandisi 344 sawa na **asilimia 50.95** wapo kwenye hatua mbalimbali za kusajiliwa. Lengo ni kuona kuwa wahandisi wanajesiliwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu tangu walipoajiriwa.

Watumishi Wenye Ulemavu

150. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha haki ya ajira na utumishi kwa watu wote hususan wenye ulemavu, Wizara imeendelea kutekeleza Mwongozo wa Huduma kwa

Watumishi wa Umma Wenye Ulemau kwa kufuata kanuni za kuwawezesha watu wenye ulemau kutekeleza majukumu yao katika mazingira wezeshi kwa kuweka mahala pa kazi miundombinu wezeshi kwa ajili yao. Katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kuzingatia haki ya ajira kwa watu wote na kudumisha kazini watu wenye ulemau ikiwa ni pamoja na kuandaa mipango na bajeti ya mazingira wezeshi kwa watumishi hao kwa kuzingatia sheria, haki na wajibu.

CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2019/2020 NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA KATIKA KUZITATUA

151. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2019/2020, Wizara imekabiliana na changamoto mbalimbali zikiwemo uharibifu wa vyanzo vya maji; upotevu wa maji; mtazamo wa wananchi katika kuchangia huduma ya maji; uwezo mdogo wa vyombo vya watumiaji maji wa kusimamia miradi ya maji vijijini; na upungufu wa wataalam kwenye sekta ya maji. Hatua mbalimbali zimechukuliwa katika kukabiliana na changamoto hizo kama ifuatavyo: -

Upatikanaji wa Fedha za Kutekeleza Miradi

152. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali imeendelea kutoa fedha za kutekeleza miradi ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira pamoja na usimamizi wa rasilimali za maji nchini, kwa kuzingatia mahitaji muhimu na hati za madai zinazowasilishwa. Pamoja na juhudzi za Serikali za kutenga fedha mahitaji halisi ya sekta ya maji ni makubwa ikilinganishwa na bajeti ya fedha za maendeleo zinazotengwa kila mwaka. Kwa mfano, kuna miradi ambayo tayari imesanifiwa lakini kutohana na ukosefu wa fedha bado haijaanza kutekelezwa. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa maji kutoka Mto Ruvuma kwenda katika Manispaa ya Mtwara-Mikindani, ujenzi wa Bwawa la Dongo, ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda, Farqwa na Ndembera na mradi wa kuboresha huduma katika Wilaya ya Kyerwa Mkoani Kagera.

153. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imekuwa ikichukuwa hatua mbalimbali zikiwemo za kuishawishi sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo na Asasi Zisizo za Kiserikali kuwekeza katika sekta ya maji. Washirika wa Maendeleo wameendelea kuunga mkono juhudzi zinazofanywa na Serikali za kuboresha huduma ya maji kwa kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi ya maji nchini. Aidha, Serikali ipo katika mazungumzo na washirika mbalimbali wa maendeleo kwa ajili ya kupata fedha za kugharamia baadhi ya miradi iliyotajwa hapo juu. Baadhi ya wadau hawa ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia, na Serikali ya Jamhuri ya Korea kuitia Benki ya Exim Korea.

Uwezo Mdogo wa Wakandarasi

154. Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo muda mrefu wa ukamilihaji wa mradi na gharama kubwa za utekelezaji zinazosababishwa na mchakato mzima wa kutekeleza miradi hiyo kuanzia ngazi ya usanifu, usimamizi na ujenzi wa mradi. Changamoto nyingine ni za kiuadilifu ambapo baadhi ya wakandarasi wamekuwa wakitoa taarifa zisizo za ukweli kuhusu aina na ubora wa vifaa vya kazi walivyonavyo, wataalam walionao na uwezo wao kifedha. Mfano, wakati wa mchakato wa manunuzi, wakandarasi hao wanaonesha vifaa wasivyovimiliki na wataalam wasiokuwa wao ili wapate ajira. Changamoto hutokea wakati wa utekelezaji wa miradi ambapo wakandarasi wamekuwa na visingizio vingi visivyo na msingi hususan ucheleweshaji wa kazi unapotokea. Matokeo ya hali hiyo ni wakandarasi kuomba nyongeza ya muda, *addendum* kwenye miradi, na miradi kuchukuwa muda mrefu kukamilika. Vilevile, gharama za vifaa vya ujenzi (*Bill of Quantities - BOQ*) zinazotolewa zimekuwa kubwa na wakati mwininge bei zinakuwa mara mbili ya gharama halisi ya vifaa hivyo kutoka kwa wagavi.

155. Mheshimiwa Spika, matokeo ya changamoto zilizotajwa ni miradi kutekelezwa kwa gharama kubwa zisizolingana na thamani ya fedha, miradi kutokuwa na ubora unaolingana

na thamani ya fedha, miradi kuchelewa kukamilika na wananchi kukosa huduma waliostahili kwa wakati. Katika kukabiliana na changamoto hizo, mojawapo ya hatua zilizochukuliwa ni Wizara kuvunja mikataba na kutekeleza baadhi ya miradi inayoweza kutekelezwa na wataalam wa ndani kupitia utaratibu wa *force account*. Utaratibu huo umepunguza kwa kiasi kikubwa changamoto zilizotajwa za mchakato wa manunuzi, uwezo wa wataalam na udanganyifu kwenye bei ya vifaa. Wataalam wa ndani kumekuwa na faida kubwa kwa kupunguza gharama za miradi kwa kiasi kikubwa ambapo kupitia *Force Account* miradi inatekelezwa kwa gharama halisi inayolingana na thamani ya fedha.

Uharibifu wa Vyanzo vya Maji Unaosababishwa na Shughuli za Kibinadamu

156. Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kuongezeka kwa uvamizi wa vyanzo vya maji kunakosababishwa na ongezeko kubwa la shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo hivyo zikiwemo shughuli za kilimo, ufugaji na ujenzi wa makazi. Hali hiyo inasababishwa na kukosekana kwa miundombinu ya kusambaza maji; kilimo cha umwagilaji; na unyweshaji wa mifugo katika maeneo ya vijiji. Matokeo ya uharibifu huo ni vyanzo kukauka, mabwawa ya maji kujaa mchanga (*siltation*) na baadhi ya maeneo kuwa na migogoro kwenye matumizi ya maji. Mikoa ilioathirika zaidi na uharibifu wa vyanzo vya maji ni pamoja na Rukwa, Katavi, Morogoro, Tanga, Mbeya, Iringa na Ruvuma.

157. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya uharibifu wa vyanzo vya maji, Wizara imeendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa rasimali za maji kupitia Bodi za Maji za Mabonde kwa kuendelea kuanzisha na kuimarisha Jumuiya za Watumia Maji (*Water User Associations - WUA*) ambapo hadi sasa kuna Jumuiya za Watumia Maji **123** nchini kote, kuunda makujwaa ya wadau kwa ajili ya kujadili kuhusu utunzaji na uhifadhi wa rasimali za maji ambapo hadi sasa kuna majukwaa **10**; kuainisha vyanzo vya maji, kuvivekea mipaka na kuvitangaza kama maeneo

tengefu ili kuimarisha usalama wa vyanzo hivyo. Vilevile, Wizara imeendelea na programu/miradi mbalimbali ya utunzaji wa rasilimali za maji na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa usimamizi na utunzaji bora wa rasilimali za maji, mfano Mradi wa Utunzaji wa Vyanzo vya Maji Kupitia Matumizi Bora ya Ardhi (*Sustainable Land Management-SLM*) unaotekeliza kupitia Bonde la Wami-Ruvu; na Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa Simiyu (*Simiyu Climate Resilient Program*). Vilevile, Mipango Shirikishi ya Uendelezaji wa Rasilimali za Maji iliyoandalika kwenye mabonde **nane (8)** itasaidia kuwaleta pamoja wadau wote wa sekta ya maji katika kupanga kwa pamoja masuala yanayohusiana na hii ikiwa ni pamoja na utunzaji, uhifadhi na uendelezaji wa vyanzo vya maji.

Upotevu wa Maji

158. Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kupunguza upotevu wa maji katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Miji Mikuu ya Mikoa hadi kufikia **asilimia 25** ifikapo mwezi Juni 2020. Hadi mwezi Machi 2020, wastani wa upotevu wa maji umefikia **asilimia 33** ambapo mwezi Juni 2019 upotevu huo ulikuwa ni **asilimia 40.63**. Wizara kupitia mamlaka za maji inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kupunguza upotevu huo ikiwemo kuhakikisha wateja wote wanafungiwa dira za maji, ukarabati wa mabomba chakavu ya kusambaza maji, ufuatiliaji wa taarifa zinazotolewa na wananchi kuhusu mivujo ya maji na kuwachukulia hatua stahiki wale wote wanaokamatwa wakijihuisha na hujuma kwenye miundombinu ya maji na wizi wa maji.

Mtazamo kwa Baadhi ya Wananchi Kuchangia Huduma ya Maji

159. Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 imeelekeza juu ya umuhimu wa jamii kuchangia gharama za uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji vijijini na jitihada mbalimbali zimechukuliwa kuwahamasisha wananchi kushiriki katika kuchangia gharama hizo. Hata hivyo, kwenye baadhi ya maeneo kumeendelea kuwepo na

changamoto katika kuchangia huduma ya maji kwa sababu wananchi kuwa na mtazamo tofauti ambapo baadhi wanaona si haki kulipia huduma za maji kwa kuwa ni rasilimali ya asili. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara kupitia RUWASA imeendelea kuwajengea uelewa wananchi na kuwashamasisha kushiriki kikamilifu katika uendeshaji na matengezo ya miradi yao.

Uwezo mdogo wa Jumuiya za Watumiaji Maji (CBWSOs) Kusimamia Miradi

160. Mheshimiwa Spika, baadhi ya Jumuiya za Watumiaji Maji (CBWSOs) zilizoanzishwa kwa ajili ya kusimamia na kuendesha miradi ya maji zimekuwa na uwezo mdogo wa kusimamia utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa vijiji. Hali hiyo imesababisha baadhi ya miradi ya maji vijiji kutoa huduma isiyordhisha na kutokuwa endelevu. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imebadilisha muundo wa jumuiya za watumiaji maji vijiji katika fani za ufundi na usimamizi wa fedha. Kwa sasa, jumuiya hizo zitaajiri wataalam wenyewe uwezo katika fani hizo ili waweze kusimamia masuala ya kifedha pamoja na ya kiufundi ikiwemo matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya maji.

Upungufu wa Wataalam wa Sekta ya Maji

161. Mheshimiwa Spika, sekta ya maji kwa muda mrefu imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa wataalam. Zoezi la ukaguzi wa rasilimali watu (*Human Resources Audit*) lililofanyika katika mwaka 2018/2019 kwenye sekta ya maji ili kubaini hali halisi ya rasilimali watu. Matokeo ya ukaguzi huo yameonesha kuwa sekta ya maji ina jumla ya watumishi **8,257** ikilinganishwa na mahitaji wa watumishi **10,276** na ina upungufu wa watumishi **2,019**. Aidha, zoezi hilo lilibaini kwamba Wahandisi **344** kati ya wahandisi **675** sawa na **asilimia 50.95** bado hawajakamilisha taratibu za usajili kwenye Bodi ya Usajili ya Wahandisi (*Engineering Registration Board - ERB*) kama Wahandisi Wataalam. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wataalam waliopo na kuwashamasisha kujiedeleza kwenye

fani zao za kitaaluma ili kuwa na sifa kamili. Lengo la Wizara ni kuhakikisha kuwa wahandisi wote katika sekta ya maji wanasaajiliwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu tangu walipoajiriwa. Vilevile, Wizara imewaaagiza wataalam wa fani nyingine katika sekta ya maji ambao bado hawajasajiliwa kwenye bodi za kisheria kuanza taratibu za kujisali ili watambulike kisheria.

162. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa wataalam, Wizara itaendelea kuomba vibali vya ajira Ofisi ya Rais- UTUMISHI ili kuajiri wataalam wa kutosha na wenye sifa katika sekta ya maji. Aidha, Wizara itazisimamia mamlaka za maji zitenge fedha kila mwaka kwa ajili ya kuajiri watumishi wenye sifa katika Taasisi zao.

Ugonjwa wa Corona

163. Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, dunia nzima imekumbwa na mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu, ujulikanao kama Corona (COVID 19). Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) za tarehe 24 Aprili 2020, zinaonesha takriban watu **milioni 2.5** duniani walikuwa wameambukizwa virusi vya Corona na takriban watu **175,825** walikuwa wamepoteza maisha kutokana na ugonjwa huu. Nchini Tanzania jumla ya watu **284** walikuwa wameambukizwa na watu **10** walikuwa wamefariki dunia kutokana na ugonjwa wa Corona.

164. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hatua ya kwanza ya kujikinga na ugonjwa huu ni kunawa mikono kwa maji yanayotiririka na sabuni, Wizara ilizlagiza Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuhakikisha kuwa wanaimarisha upatikanaji wa huduma ya majisafi katika maeneo yao hususan katika kipindi hiki. Aidha, taasisi hizi zilielekezwa kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa katika kuhakikisha kuwa huduma ya majisafi na vifaa vya kunawia mikono vinawekwa katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu wengi kama vile masoko, vituo vya mabasi na minada. Katika maeneo mengi nchini maelekezo haya yalitekelezwa na

wananchi wengi wamekuwa wakichukua hatua muhimu za kunawa mikono kama njia mojawapo ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu.

165. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya tathmini ya awali kuhusu athari za ugonjwa wa Corona katika sekta ya maji. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa, pamoja na athari zingine, kuna uwezekano wa kuchelewa kukamilika kwa baadhi ya miradi ya maji kutokana na wadau tunaoshirikiana nao kutoka nje kushindwa kusafiri kuja kusaini mikataba na/ au kushindwa kusafirisha vifaa vya ujenzi wa miradi. Wizara inaendelea kufanya tathmini ya kina na itachukua hatua stahiki katika kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza.

MALENGO NA MPANGO WA KUBORESHA UPATIKANAJI WA HUDUMA YA MAJI KWA MWAKA 2020/2021

Programu ya Uvunaji wa Maji ya Mvua

166. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa nchi yetu imebahatika kuwa na vyanzo vingi vya maji vikiwemo maziwa, mito, chemichemi na maji chini ya ardhi hata hivyo, mtawanyiko wa vyanzo hivyo hauko sawia. Baadhi ya maeneo yamekuwa na uhaba mkubwa wa maji kutokana ufinyu wa vyanzo. Aidha, kwa sababu za mtawanyiko wa watu, kuna maeneo hayajaweza kufikishiwa huduma ya maji kutokana na gharama kubwa za ujenzi wa miundombinu ya maji

167. Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, nchi yetu imebahatika kupata kiwango kizuri cha mvua ambapo wastani wa mvua kwa mwaka katika maeneo mengi nchini ni milimita **900** hadi milimita **1,200** wakati wastani wa mvua katika maeneo kame ya katikati ya nchi ni kat i ya milimita **400** hadi milimita **550** kwa mwaka. Kwa upande wa maeneo yenye mvua nyingi kama vile Nyanda za Juu Kusini na maeneo ya milima ya Usambara, kiasi cha mvua ni wastani wa milimita **2,200** hadi milimita **2,500** kwa mwaka. Takwimu hizo zinaonesha fursa ya kuvuna maji ya mvua yanayoweza kutumika kwenye maeneo kame na katika vipindi vya

kiangazi. Katika kutumia fursa hiyo ya kuwa na mvua za kutosha, na ili kupunguza kero kubwa ya uhaba wa maji kwenye baadhi ya maeneo nchini, Serikali imeona upo umuhimu wa kuandaa programu maalum ya kuhamasisha uvunaji wa maji kuititia teknolojia mbalimbali rahisi zilizopo ambapo wananchi wa kawaida wanaweza kufundishwa na kutekeleza kwa ufanisi. Teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua inaweza kutekelezwa kwa kuzingatia mahitaji na uwezo wa mwananchi. Hivyo, hata kaya zenyenye kipato kidogo zinaweza kujenga miundombinu ya gharama nafuu ya kuvuna maji ya mvua.

168. Mheshimiwa Spika, programu hiyo inatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu 2020/2021 – 2022/2023 na inalenga kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kutumia teknolojia mbalimbali za uvunaji wa maji ya mvua hususan kuititia mapaa ya nyumba zao; ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua katika vituo vya kutolea huduma za jamii kama vile vituo vya afya, mashulenii na vituo vya usafiri; pamoja na viwandani. Aidha, kwa maeneo ya vijiji yanayotegemea shughuli za kilimo na ufugaji, programu hiyo inalenga kuhamasisha ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua kama vile malambo na mabwawa madogo yatakayosaidia kuhakikisha maji yanapatikana katika kipindi chote cha mwaka. Hivyo, kupunguza kutegemea kilimo cha mvua na ufugaji wa kuhamahama ambao husababisha uharibifu wa mazingira; pamoja na kuhujumu miundombinu ya maji kwa ajili ya kupata maji ya kunyweshea mifugo. Vilevile, miundombinu ya uvunaji maji ya mvua kama vile mabwawa, itasaidia kupunguza athari za mafuriko hususan kwenye maeneo yanayokumbwa na mafuriko ya mara kwa mara.

169. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Programu Maalum ya Uvunaji wa Maji ya Mvua (*Special Programme for Rain Water Harvesting*) inafanikiwa na kero ya maji kwa wananchi inapungua, Wizara inatekeleza mikakati mbalimbali ya uvunaji wa maji ya mvua ikiwemo kuhamasisha kwa vitendo uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga miundombinu kwenye Taasisi za Serikali kama vile mashulenii, zahanati na majengo

mengine ya Serikali. Katika hatua hiyo, wananchi watashirikishwa moja kwa moja wakati wa mipango ya ujenzi na watapewa taarifa za faida ya uvunaji wa maji ya mvua kwa takwimu na kiasi cha fedha kinachookolewa kwa kuwa na miundombinu hiyo. Vilevile, Wizara itahamasisha kwa vitendo uvunaji wa maji ya mvua kupitia malambo madogo kwa kujenga ‘malambodarasa’ kwenye maeneo yatakayobainishwa. Pia, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo ifatanya kampeni za uvunaji wa maji ya mvua nchi nzima (*National Rain Water harvesting Campaign*). Makadirio ya awali ya utekelezaji wa programu hiyo ni **Shilingi bilioni 4.**

Mpango wa Kuboresha Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira katika Vituo vya Afya na Shule

170. Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira katika vituo vya afya nchini pamoja na shule zisizo na huduma hizo. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kunakuwa na huduma bora ya majisafi na usafi wa mazingira ili Taasisi hizo zitoe huduma bora kwa wananchi. Vilevile, kupatikana kwa huduma ya maji kwenye vituo vya afya kutasaidia kulinda afya za wananchi hususan akina mama wanaokwenda kujifungua katika vituo hivyo. Vilevile, wanafunzi mashulenzi watapata maji ya kunywa, na maji kwa ajili ya usafi wa mazingira hivyo, kuboresha mahudhurio hususan kwa watoto wa kike.

171. Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa huduma ya maji katika vituo vya afya na shule umekuwa ukitekelezwa na Wizara kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI); Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Jitihada zimefanyika za kupeleka maji kwenye vituo vya afya na shule hata hivyo, bado vituo vya afya na shule ambazo bado hazijafikiwa na huduma hiyo. Kutokana na hali hiyo, Wizara inaandaa Mpango Maalum wa Kuboresha Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira katika Vituo vya Afya na Shule kusiko na huduma hiyo (*Special WASH Programme for Medical*

Centers and Schools). Mpango huo unaotarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023. Kupitia mpango huo, Serikali imepanga kuvunganisha vituo vyote vya afya nchini na shule kwenye mtandao wa maji katika maeneo yenyenye mitandao ya maji na kwa maeneo yasiyo na mtandao, Serikali itafanya usanifu kwa ajili ya kupata vyanzo vya maji ili kuvipatia vituo vya afya na shule huduma ya maji.

172. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2020, Wizara inaendelea na zoezi la kukusanya takwimu za vituo vya afya na shule zisizo na huduma ya maji ya uhakika ili vinufaiki na mpango huo. Tathmini ya awali imebaini vituo vya afya **1,195** visivyo na huduma ya maji kati ya vituo **6,134**; na shule **5,721** kati ya shule **19,965** zilizopo nchini. Katika mwaka 2020/2021, kiasi cha **Shilingi bilioni 2** kimetengwa kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira kwenye vituo vya afya na shule.

Mpango wa kuanzisha Mfumo wa Taifa wa Usambazaji Maji (National Water Grid)

173. Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Taifa wa Usambazaji Maji (*National Water Supply Grid*) ni mfumo wa usambazaji wa maji unaobuniwa na Serikali na unalenga kuhakikisha maji yanapatikana kwenye maeneo yote nchini na katika kipindi chote cha mwaka bila kujali iwapo eneo husika lina vyanzo vya maji au lina uhaba wa maji. Mfumo huo utahusisha ujenzi wa mtandao wa kusafirisha maji kutoka maeneo yenyenye maji mengi na kuyapeleka kwenye maeneo yenyenye uhaba (*Intra Basin Water Transfer - IBWT*). Mfumo huo utakuwa ni msingi wa kuwa na mkakati wa kitaifa wa kuwa na miundombinu ya kusambaza maji ya kutosha kwenye maeneo yote ya mijini na vijijiini kwa sasa na miaka ya baadaye.

174. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mfumo huo ni rahisi na unawezekana kwa kuwa nchi yetu imezungukwa na maziwa makuu matatu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa, na imepitiwa na mito mikubwa **11** inayotiririsha maji kipindi chote cha mwaka ambayo ni Ruvuma, Rufiji, Kilombero,

Pangani, Wami, Ruvu, Malagarasi, Ruhuhu, Kiwira, Kagera na Mara. Vilevile kuna mito midogo na chemchemi nyingi zilizopo kwenye maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, nchi yetu ina hazina ya maji chini ya ardhi ambayo inaweza kuvunwa na kuingizwa kwenye mtandao huo ili yatumike kwenye maeneo yenye uhaba wa maji. Mfumo huo wa taifa utaunganishwa kwenye mitandao ya Mamlaka za Maji ili kuziwezesha kuwa na maji ya kutosha katika kipindi chote cha mwaka.

175. Mheshimiwa Spika, hapa nchini, mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria na kuyapeleka kwenye maeneo mbalimbali kama vile Shinyanga, Tabora na Simiyu ni mfano mojawapo wa mtandao unaota maji kutoka kwenye eneo lenye maji mengi na kuyapeleka kwenye maeneo yenye uhaba. Maeneo mengi ya katika nchi yetu kama Dodoma, Singida, Shinyanga na Babati ni kame na yanaathiriwa na uhaba wa maji kwa kipindi kirefu cha mwaka, hivyo, jitihada ya aina hili itasaidia kuondoa kabisa kero ya maji kwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo hayo. Vilevile, mtandao huo utakidhi mahitaji makubwa ya maji yanayoongezeka kutokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi kama viwanda, madini na kilimo.

176. Mheshimiwa Spika, uzoefu kutoka nchi nyingine unaonesha uhamishaji wa maji kutoka maeneo yenye maji mengi kwenda maeneo yenye uhaba wa maji (*Intra Basin Water Transfer - IBWT*) unawezekana. Nchi kama China, India na Lesotho wametumia mfumo huo kwa mafanikio makubwa na kuweza kuondoa kero ya uhaba wa maji kwenye maeneo kame. Nchini China, mradi wa *South-North Water Transfer Project* unatoa maji kutoka Mto Yangtze ulioko kusini mwa nchi hiyo na kuyapeleka maeneo ya kaskazini mwa nchi hiyo umbali wa **kilomita 1,152** ambako kuna uhaba mkubwa wa maji. Nchini India, mradi wa Telugu Ganga uliopo kusini mwa nchi hiyo unasafirisha maji umbali wa **kilomita 406** kutoka Mto Krishna na kuyapeleka katika majimbo manne yenye uhaba wa maji ya Maharashtra, Karnataka, Andhra Pradesh na Tamil Nadu. Katika Bara la Afrika, mradi wa *Lesotho Highlands Water Project* uliopo nchini Lesotho unatoa maji kwenye maeneo

ya milima ya Lesotho na kuyapeleka Jimbo la Gauteng nchini Afrika Kusini.

177. Mheshimiwa Spika, mifano hiyo inadhihirisha kuwa Tanzania inaweza kuwa na *water national grid* na ukawa ndio ufumbuzi wa kudumu wa changamoto ya uhaba wa maji nchini. Ili kufikia lengo hilo, katika mwaka 2020/2021, Serikali itafanya utafiti wa kubainisha vyanzo vya maji na njia zitakazotumika katika mfumo na kuchora ramani ya namna mtandao huo utakavyojengwa.

Mkakati wa Ujenzi wa Mabwawa ya Maji Nchini

178. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali imebainisha maeneo **217** katika Wilaya **42** zilizopo kwenye mikoa **10** yanayopendekezwa kujengwa mabwawa. Mikoa hiyo ni Geita, Kagera, Pwani, Songwe, Rukwa, Arusha, Mara, Tabora, Manyara na Ruvuma. Katika mwaka 2020/2021, maeneo hayo yatafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa. Aidha, Serikali itaendelea kufanya utafiti wa maeneo mengine yanayofaa kujengwa mabwawa ili yahifadhiwe.

Mchango wa Sekta Binafsi katika Ujenzi wa Miradi na Utoaji wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Nchini

179. Mheshimiwa Spika, sekta binafsi nchini imekuwa ikichangia katika kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira hususan kwenye maeneo ambayo huduma hizo hazijafika. Kuna Taasisi zisizo za kiserikali na watu binafsi ambao wameendeleza vyanzo vya maji na kusambaza maji kwa majirani. Pia, kuna Taasisi binafsi ambazo zimechimba visima na kuvikabidhi kwa wananchi kwa ajili ya kuviedesha. Vilevile, kuna watu binafsi wenye magari yanayobeba maji na kuyapeleka kwenye maeneo yenye uhaba wa maji. Pia, kwenye maeneo yasiyo na miundombinu ya majitaka, watu binafsi wanamiliki magari (*cesspit emptiers*) ya kusafirishia majitaka ambapo hutoa huduma hiyo kwa wenye uhitaji.

180. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019, Serikali kupitia RUWASA imefanya tathmini ya mchango wa sekta binafsi katika mikoa **14**. Tathmini hiyo, imebaini kuwa sekta binafsi imechangia kiasi cha **Shilingi 90,908,785,121** na kunufaisha wananchi wapatao **736,777** waishio vijijini. Aidha, katika kuhamasisha uendelevu wa miradi na utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini, Serikali inatoa wito kwa sekta binafsi kushiriki kwenye uendeshaji wa miradi ya maji na utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Vilevile, Serikali kupitia RUWASA imeandaa mwongozo utakaoweka utaratibu madhubuti wa ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini. **Kiambatisho Na. 7** kinaonesha baadhi ya Taasisi binafsi zinazotoa huduma za maji na usafi wa mazingira nchini.

181. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuipongeza sekta binafsi kwa mchango huo katika kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira nchini. Katika mwaka 2020/2021, Serikali itazitambua kampuni binafsi na watu binafsi wanaotoa huduma za maji na usafi wa mazingira na itaweka miongozo ya kuwawezesha kutoa huduma hiyo katika mazingira mazuri.

Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Kutekeleza Miradi Kwenye Sekta ya Maji (Private Sector Participation – PSP & PPPs)

182. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira (*Private Sector Participation*). Ushirikishaji huo unahusu sekta binafsi kutoa ushauri wa kitaalam, na kufadhili, kusanifu, kujenga na kuendesha miradi ya maji na usafi wa mazingira. Kwa sasa ushiriki wa sekta binafsi umekuwa zaidi katika usanifu na ujenzi miradi; na ugavi wa vifaa vyta ujenzi wa miundombinu ya maji na usafi wa mazingira. Wizara imekuwa ikipokea maombi mbalimbali ya kusanifu na kujenga miradi kutoka kampuni nydingi binafsi ambapo kampuni zenye sifa zimekuwa zikipewa miradi hiyo na kuitekeleza. Hata hivyo, sekta binafsi haijahamasika katika ufadhili na uendeshaji wa miradi. Pamoja na hali hiyo, Wizara imeendelea kuandaa mazingira ya sekta binafsi kusaidia kutekeleza miradi ya maji kwa kuzihamasisha mamlaka za

maji kuandaa miradi ya ubia (*Public Private Partnership - PPPs*). Hadi sasa, Mamlaka tano (5) za Vwawa-Mlowo, Moshi, Tanga, Mwanza na DAWASA zimewasilisha maandiko ya miradi ambayo baada ya Wizara kuyapitia iliyawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya hatua zinazofuata.

183. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwaalika sekta binafsi kuja kuwekeza kwenye sekta ya maji kwa kuwa mazingira wezeshi yapo. Serikali tayari imeweka misingi kwa ajili kutekeleza miradi ya ubia (*PPP Framework*) kwa kutunga Sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*National PPP Policy, 2009*), Sheria ya *PPP* ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2018 pamoja na kanuni na miongozo mbalimbali ya kusimamia miradi ya *PPP*. Aidha, Serikali imewajengea uwezo watendaji mbalimbali katika ngazi ya Wizara na mamlaka za maji ili wapate uelewa wa masuala ya *PPP* ikiwa ni pamoja na kundaa miradi.

184. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kukamilisha maandalizi ya miradi ya *PPP* kwa kuajiri mtaalam mshauri (*Transaction Advisor*) kwa ajili ya kufanya usanifu kwa miradi iliyowasilishwa na mamlaka za maji. Aidha, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo mamlaka za maji na kuzihamasisha kuandaa maandiko ya miradi ya *PPP* ili kuishirikisha sekta binafsi katika kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira.

Mpango wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Dodoma kupitia Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria

185. Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dodoma kupitia mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria. Katika kufikia azma hiyo, Wizara iliunda kikosi kazi (*Task Force*) kwa ajili ya kuandaa andiko la awali la upembusi yakinifu. Aidha, utekelezaji wa mradi huo utanufaisha maeneo litakapopita bomba kuu ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Singida na vijiji vitakavyokuwa umbali wa kilomita 12 pembezoni mwa bomba kuu.

Mpango wa Matumizi ya Maji ya Maziwa Makuu

186. Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kutekeleza miradi ya maji katika maeneo ya pembezoni mwa Maziwa Makuu ya Tanganyika, Nyasa na Victoria kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma ya majisafi. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Tanganyika

187. Mheshimiwa Spika, mtaalam mshauri amekamilisha usanifu wa kina wa mradi wa kutoa maji Ziwa Tanganyika utakaohudumia wananchi wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa ziwa hilo. Mradi huo utatekelezwa katika mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi na utahusisha vijiji **73** vya Halmashauri za Wilaya za Kigoma, Uvinza, Nkasi, Kalambo, Mpimbwe na Mpanda.

(b) Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Nyasa

188. Mheshimiwa Spika, mtaalam mshauri anaendelea na usanifu wa kina wa mradi wa kutoa maji Ziwa Nyasa utakaohudumia wananchi wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa ziwa hilo. Mradi huo utatekelezwa katika mikoa ya Njombe na Ruvuma na utahusisha vijiji **41** vya Halmashauri za Wilaya za Ludewa na Nyasa.

(c) Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria

189. Mheshimiwa Spika, mtaalam mshauri amekamilisha usanifu wa kina wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria utakaohudumia wananchi waishio maeneo ya pembezoni mwa ziwa hilo. Mradi utatekelezwa katika mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita, Mara na Simiyu na utahusisha vijiji **301** vya mikoa hiyo.

Miradi Mingine ya Kimkakati ya Maji Vijijini Inayotarajiwa Kutekelezwa kwa mwaka 2020/21

(a) Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Mkoani Kigoma

190. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Maendeleo ya Serikali ya Ubelgiji - *Enabel*, inatekeleza mradi

wa majisafi na usafi wa mazingira Kigoma (*Water and Sanitation Kigoma Regional Project - WASKIRP*) kwa gharama ya **Euro milioni 8.8** ambapo kati ya fedha hizo, Serikali ya Ubelgiji itatoa **Euro milioni 8** na Serikali itatoa **Euro 800,000**. Lengo la mradi huo ni kutoa huduma endelevu ya majisafi na salama kwa wananchi wapataao **128,919**. Mradi huo ulipangwa kutekelezwa katika vijiji **26** vilivyo chaguliwa katika wilaya sita za mkoa huo katika kipindi cha miaka **mitano** kuanzia Novemba 2017 hadi Julai, 2022. Hata hivyo, vijiji nya mradi vilipunguzwa na kubaki vijiji **15** kutokana na gharama halisi ya utekelezaji wa miradi iliyopendekezwa.

191. Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizosababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa mradi, kwa sasa utekelezaji umeanza ambapo *Enabel* kwa kushirikiana na *RUWASA* inatekeleza miradi katika Wilaya ya Kigoma Vijijini ambapo usanifu wa mradi wa Mkongoro Na.1 umekamilika na zabuni ya ujenzi wa mradi huo imetangazwa. Ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi April, 2020 na kukamilika mwezi Desemba, 2020. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wananchi wapataao **44,137**. Vilevile, katika Wilaya ya Buhigwe, mtaalam mshauri anaendelea na kazi ya usanifu wa mradi wa maji katika Kijiji cha Mwayaya na ujenzi kuanza mwezi Mei, 2020 na kukamilika mwezi Januari 2021. Mradi huo utawanufaisha wananchi wapataao **13,419**.

192. Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Uvinza, visima **viwili (2)** vimechimbwa katika Kijiji cha Kazuramimba. Usanifu wa miundombinu ya kusambaza maji unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2020 na ujenzi kuanza mwezi Juni, 2020. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2021 na kuwanufaisha wananchi wapataao **30,812**. Katika Wilaya ya Kibondo, mtaalam mshauri anaendelea na kazi ya usanifu wa mradi wa kutoa maji Mto Mkugwa kwenda Kijiji cha Kifura unaotarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2021. Mradi huo utawanufaisha wananchi wapataao **12,095**.

193. Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa visima virefu unaendelea katika vijiji nya Kiyobera na Kabingo kwa ajili ya kupeleka maji katika vijiji vinne nya Kabingo, Kiyobera,

Kiziguzigu na Ruyenzi Wilaya ya Kakonko. Ujenzi wa miundombinu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2020 na ukikamilika utawanufaisha wananchi wapatao **15,595** wa vijiji hivyo. Aidha, Serikali itakarabati mradi wa maji uliokuwa unahudumia vijiji vya Kabingo, Kiyobera, Kiziguzigu na Ruyenzi ili kupunguza kero ya maji kwenye vijiji hivyo wakati wakisubiri kukamilika kwa mradi utakaotumia visima virefu. *RUWASA* katika Wilaya ya Kasulu itagharamia uchimbaji wa kisima kirefu na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika Kijiji cha Kidyama utakaowanufaisha wakazi wapatao **12,861**.

(b) Mradi wa Maji Isimani

194. Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa maji Isimani uliopo katika Halmashauri za Wilaya ya Iringa na Kilolo kwa gharama ya **Shilingi bilioni 10.8**. Mradi huo unahuishwa ujenzi na ukarabati wa matanki, ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya usambazaji maji, ujenzi wa vituo vya kuchotea maji, ujenzi wa mabirika ya kunyweshea mifugo, ufungaji wa mfumo wa nishati ya jua kwenye vijiji ambavyo umeme wa TANESCO haujafika, uchimbaji wa visima **saba (7)** na ufungaji wa pampu katika visima hivyo. Mradi huo unatekelezwa na wataalam wa ndani kutoka Mamlaka za Maji za Makambako, Iringa na RUWASA kwa kutumia mfumo wa *Force Account*. Hadi mwezi Machi 2020, utekelezaji wa mradi huo umeanza na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2021 na kuwanufaisha wananchi wapatao **46,980** wa vijiji **29** vilivypo Wilaya ya Kilolo (vijiji **vitano**) na Iringa Vijijini (vijiji **24**).

(c) Mradi wa Maji Lukululu

195. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Hispania imekamilisha usanifu wa mradi wa maji Lukululu Mkoani Songwe. Mradi huo utahuishwa vijiji vya Lukululu, Mbewe, Mlangali, Shomola, Shaji na Ndolezi katika Kata ya Mlangali na vijiji vya Igunda, Mahenje, Mbulu, Myovizi, Ichesa na Ivgula vilivypo katika Halmashauri ya Mbozi. Gharama za kutekeleza mradi huo zinakadiriwa kufikia **Shilingi bilioni 5** na utekelezaji wa mradi utaanza katika mwaka 2020/2021 na utakapokamiliika utawanufaisha wananchi wapatao **35,277** wa vijiji hivyo.

Miradi ya Maji Mijini Inayotarajiwa Kutekelezwa Katika Maeneo Mbalimbali

(d) Mradi wa Maji Katika Miji ya Nyashimo, Bariadi, Lagangabilili, Maswa na Mwanhuzi

196. Mheshimiwa Spika, mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Mkoa wa Simiyu unalenga kuwapatia huduma ya maji wananchi wa miji ya Busega, Bariadi, Lagangabilili, Maswa, Mwanhuzi pamoja na vijiji vipatavyo **256** vilivypo kilomita 12 pembezoni ya litakapopita bomba kuu. Mradi utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*) pamoja na *Green Climate Fund (GCF)* na utakuwa na awamu mbili. Awamu ya kwanza itagharimu **Euro milioni 127.7** na kati ya hizo, **Euro milioni 25** zitatolewa na *KfW* na **Euro milioni 102.7** zitatolewa na *Green Climate Fund (GCF)*. Awamu hiyo ya kwanza itahusisha miji ya Nyashimo, Bariadi, Lagangabilili pamoja na vijiji **256**. Hadi mwezi Machi 2020, mtaalamu mshauri amekamilisha usanifu wa awali na taratibu za manunuzi kwa ajil ya kuwapata wataalam washauri wa kupitia usanifu na kusimamia mradi zinaendelea. Aidha, Wizara inaendelea na tathmini ya kulipa fidia kwenye maeneo ambayo miundombinu ya maji itapita.

197. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya pili utakaohusisha miji ya Mwanhuzi na Maswa.

(e) Mradi wa Maji katika Mji wa Morogoro

198. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*) itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa gharama ya **Euro milioni 70**. Mradi huo utahusisha kuongeza urefu wa tuta la bwawa la Mindu kwa mita 2.5 ambapo ujazo wa maji katika bwawa hilo utaongezeka kutoka **lita bilioni 12** za sasa hadi **lita bilioni 20**. Bwawa hilo ndiyo chanzo kikuu cha maji kwa Mji wa Morogoro. Vilevile, kupitia mradi huo, Serikali itajenga miundombinu ya majitaka katika maeneo ya Kipera/Tungi. Serikali inaendelea na majadiliano na AFD

ya kukamilisha taratibu za kupata fedha za kutekeleza mradi huo.

Mpango wa Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji 2020/2021

199. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Wizara kuititia Bodi za Maji za Mabonde nchini itaendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji ambapo Wizara imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 39** kwa ajili ya kuiwezesha Wizara pamoja na Bodi tisa za Maji za Mabonde ambapo fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 11** na fedha za nje ni **Shilingi bilioni 28**.

Mpango wa Utekelezaji wa Huduma za Ubora wa Maji 2020/2021

(a) Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Mbalimbali na Ubora wa Majitaka

200. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kufuatilia ubora wa maji katika vyanzo na mifumo ya usambazaji maji kwa kukusanya na kufanya uchunguzi jumla ya sampuli 10,000 za maji. Vilevile, katika kudhitibi uchafuzi wa vyanzo vya maji na mazingira Wizara imepanga kufuatilia ubora wa majitaka kwa kukusanya na kufanya uchunguzi wa sampuli 1,000 za majitaka kutoka katika Mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira, viwanda na Taasisi mbalimbali. Vilevile, katika kuimarisha ufuatiliaji wa ubora wa maji, Wizara imepanga kuendelea kutoa mafunzo kuanzia ngazi ya kijiji kuhusu utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji, Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango ya Usalama wa Maji pamoja na kukamilisha na kusambaza nakala za Mwongozo wa Kusafisha na Kutibu Maji kwenye Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini pamoja na Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii.

(b) Ubora wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji

201. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Wizara imepanga kuendelea kufuatilia na kuhakiki ubora wa

madawa ya kutibu maji katika mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira pamoja na Taasisi zinazohusika na usambazaji wa madawa hayo.

(c) Mkakati wa Uondoaji wa Madini ya Fluoride katika Maji

202. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kutekeleza mkakati wa kuondoa madini ya *fluoride* katika maji ya majumbani kwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara yatokanayo na uwepo wa kiwango kikubwa cha madini ya fluoride katika maji; kuhimiza matumizi ya teknolojia rahisi ya kutumia chengachenga za mifupa ya ngombe kwa ajili ya kupunguza madini hayo katika maji ya kunywa na kupikia; kuongeza uzalishaji wa chengachenga za mifupa ya ng'ombe; kutengeneza mitambo midogo 1,000 na kufuatilia ufanisi wa mitambo inayotumika. Vilevile, Wizara itaendelea kutafiti vyanzo vya maji vilivyoathiriwa na madini ya fluoride katika mikoa ya Simiyu, Geita na Mara; na kuandaa kanzidata ya vyanzo vya maji vyenye madini hayo.

(d) Maabara za Maji Kupata Ithibati (Accreditation)

203. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Wizara itakamilisha lengo la kuongeza idadi ya maabara za maji zenyetibati (*accreditation*) kufikia **saba (7)** kutoka maabara moja ya sasa ambayo ni Mwanza. Vilevile, Wizara itaendelea kuhakikisha uendelevu wa ithibati za maabara hizo kwa kuzijengea uwezo na kuzipatia madawa na vifaa vya kisasa vya kufanyia uchunguzi wa ubora wa maji. Aidha, kwa lengo la kutimiza mahitaji ya Mwongozo mpya wa Kimataifa wa Uendeshaji wa Maabara za Uchunguzi (*ISO 17025:2017*), Wizara itakamilisha uwekaji wa mfumo wa kieletroniki (*Laboratory Information Management System*) katika maabara zote 16 za ubora wa maji pamoja na kituo cha utafiti wa madini ya fluoride cha Ngurdoto.

Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini 2020/2021

204. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kukamilisha miradi ya maji vijijini inayoendelea

kutekelezwa na miradi mipyä katika maeneo mbalimbali nchini. Jumla ya **Shilingi bilioni 235.96** zimepangwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 124.16** na fedha za nje ni **Shilingi bilioni 111.8**. Mchanganuo wa fedha za maendeleo zilizotengwa katika mwaka 2020/2021 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini inayoendelea umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 8**. Aidha, miradi mipyä iliyopangwa kutekelezwa katika Halmashauri mbalimbali nchini kwa mwaka 2020/2021 inapatikana kwenye tovuti ya Wizara: www.maji.go.tz

Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Maji Mijini 2020/2021

205. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kukamilisha miradi ya maji mijini inayoendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini. Jumla ya **Shilingi bilioni 558.63** zimepangwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 280.93** na fedha za nje ni **Shilingi bilioni 277.7**. Mchanganuo wa fedha za maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji mijini katika mwaka 2020/2021 umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 9**.

4. SHUKRANI

206. Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wadau wote waliochangia kwa njia moja ama nyingine kufanikisha majukumu ya sekta ya maji katika kipindi cha mwaka 2019/2020. Shukrani za pekee ziwaendee nchi marafiki, washirika wa maendeleo, mashirika ya misaada ya kimataifa, taasisi za kiserikali, mashirika ya kidini pamoja na wadau wengine. Ninapenda kuwashukuru wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika kutekeleza miradi ya maji. Kwa namna ya kipekee, ninapenda kuzishukuru nchi rafiki ambazo zimechangia katika maendeleo ya sekta ya maji nchini. Nchi hizo ni Uingereza, Ujerumani, Korea Kusini, China, Marekani, India, Japan, Uhlanzi, Hispania, Ubelgiji, Ufaransa, Kuwait, Misri, na Saudi Arabia. Ninakiri kwamba, maendeleo hayo yanatokana na jithada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa washirika hao.

207. Mheshimiwa Spika, vilevile, ninapenda kuyashukuru mashirika ya maendeleo na Taasisi za kimataifa za fedha kwa misaada ya kitaalam na fedha katika kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na Benki ya Dunia (*World Bank-WB*), Benki ya Maendeleo ya Africa (*AfDB*), Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (*AFD*), Benki ya Maendeleo ya Ujeruman (*KfW*), Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (*EIB*), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (*OPEC Fund for International Development-OFID*), Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (*Kuwait Fund*), Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD*), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (*DFID*), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (*JICA*), Shirika la Maendeleo la Ujeruman (*GIZ*), *Global Environment Facility (GEF)*, *Green Climate Fund*, Shirika la Afya Duniani (*WHO*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (*BTC*), Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID*).

208. Mheshimiwa Spika, Mashirika na Taasisi za Kidini yameendelea kuongeza hamasa katika kuyafikia malengo tulyojeweke. Hivyo, ninapenda kuyashukuru mashirika na Taasisi hizo ambazo ni *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)*, *Adventist Development Relief Agency (ADRA)*, *Norwegian Church Aid*, *Livingwater International*, *World Islamic League*, Shirika la Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania, *Islamic Foundation*, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (*BAKWATA*), Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (*KKKT*), Kanisa Katoliki Tanzania na Kanisa la Kianglikana Tanzania.

209. Mheshimiwa Spika, vilevile, nazishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali zinazoshiriki katika kuendeleza sekta ya maji. Taasisi hizo ni pamoja na *Association of Tanzanian Water Suppliers (ATAWAS)*, *WaterAid*, *Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET)*, Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya (*WAMMA*), *World Vision*; *World Wide Fund for Nature (WWF)*, *Water Resources Integration Development Initiatives*

(WARIDI), Netherlands Volunteers Services (SNV), Plan International, Concern Worldwide, Bill and Melinda Gates Foundation, Water Mission (T), Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Mali Asili (IUCN), African Medical Research Foundation (AMREF) na Clinton HIV Aids Initiative.

210. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati Mhe. Jumaa Hamidu Aweso (Mb), Naibu Waziri wa Maji; Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Katibu Mkuu; Mhandisi Anthony Damian Sanga, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wataalam na Watumishi wote wa Wizara ya Maji; pamoja na Maafisa Watendaji Wakuu na Watumishi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha majukumu ya Wizara ya Maji yanatimizwa. Vilevile, naishukuru familia yangu kwa upendo, ushirikiano na msaada wao katika kipindi chote na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi.

5. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021

211. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 733,284,075,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2020/2021. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 28,275,145,000** ambapo **Shilingi 11,171,714,000** sawa na **asilimia 40** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 17,103,431,000** sawa na **asilimia 60** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **Shilingi 705,008,930,000** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 349,449,000,000** sawa na **asilimia 49.6** ni fedha za ndani na **Shilingi 355,559,930,000** sawa na **asilimia 50.4** ni fedha za nje.

212. Mheshimiwa Spika, ninaomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara www.maji.go.tz.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maji Profesa Mbarawa kwa kutoa hoja na hoja imeungwa mkono. Tunakushukuru kwa kuwasilisha hotuba hiyo kwa umakini mkubwa na kwa kuzingatia wakati. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji. Atupatie taarifa yake kwa muda wa dakika 20. Mheshimiwa Mwenyekiti, endelea.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako tukufu.

Pia naomba nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwakilisha ripoti inayohusu taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maji. Nichukue fursa hii tena kukupongeza kwa kazi nzuri unayoifanya hapa Bungeni kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi mkubwa, pia hatua ulizozichukuwa za kupambana na janga kubwa la maambukizi ya *corona*.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya ya kizalendo kwa miaka mitano. Tunamtakia afya njema Jemedari wetu na Mwenyezi Mungu ampe afya njema ili aweze kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa kipindi kijacho cha miaka mitano inayokuja. Ana ushindi mkubwa usiotarajia na usiokuwa na mashaka.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kutoa pole kwa vifo vyta ndugu zetu walitangulia mbele ya haki akiwepo marehemu Dkt. Getrude Rwakatare aliyekuwa Mbunge mwenzetu na Marehemu Abdulkarimu Shaa aliyekuwa Mbunge katika Bunge la Kumi; bwana ametoa na bwana ametwaa, jina la bwana lihimidiwe; *Inna lillah wainna ilayh rajiiun.*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwashukuru wapiga kura wangu katika Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa ushirikiano

mkubwa wanaonipatia. Mwisho, niwatakie kila heri Waislam kote dunia katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani; Ramadhani Karim.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yetu ya Kamati iingie kwenye *Hansard* kama iliyokuwa kwenye *tablet* zenu. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6(7) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kimeipa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwa madhumuni ya taarifa hii, taarifa ninayoiwasilisha inahusu Wizara ya Maji - Fungu 49.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yafuatayo:-

(1) Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji - Fungu 49 kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

(2) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

(3) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

(4) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na

(5) Maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati ya ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji na kutoa maoni na ushauri kwenye maeneo yafuatayo:-

- (a) Kuimarisha utengaji wa fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo;
- (b) Kuongeza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji kwa kuimarisha makusanyo ya Mfuko wa Maji;
- (c) Mikakati ya uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi mbalimbali;
- (d) Ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika Miji na Makao Makuu ya Mikoa nchini;
- (e) Kuimarisha na Kutekeleza Mipango na Mikakati ya Kutumia Maji kutoka Ziwa Tanganyika;
- (f) Kuimarisha Tafiti za Rasilimali Maji na kuboresha Mitaala ya Elimu kwa Umma kuhusu kutunza vyanzo vya Maji; na
- (g) Umuhimu wa Kukamilisha miradi mbalimbali ya Maji inayotekelze wa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Fungu 49, liliidhinishiwa jumla ya Sh. 624,415,131,530.00. Kati ya fedha hizo Sh.6,266,714,000 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na Sh.610,469,888,530.00 zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi Sh.349,449,000,000.00 sawa na asilimia 57 ni Fedha za Ndani ambapo kati ya fedha hizo, Sh.158,500,000,000 ni za Mfuko wa Taifa wa Maji na Sh.284,714,034,677 ni fedha zinazotokana na vyanzo vingine vya ndani. Aidha, Sh.261,020,888,530 sawa na asilimia 43 ni Fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2020, Wizara ya Maji (Fungu 49) liliikuwa limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida Sh.6,266,741,000.00 sawa na asilimia 73 na ya kiasi

kilichoidhinishwa. Aidha, kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa zilikuwa Sh.453,697,256,871.41 sawa na asilimia 72.2 ya Fedha zote za Bajeti ya Maendeleo zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo Sh.175,036,818,847.08 sawa na asilimia 50 ya bajeti ni fedha za ndani na kati ya hizo fedha zilizotokana na Mfuko wa Maji ni Sh. 108,574,476,547.40.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara ya maji ilikuwa imepokea asilimia 72.2, ikikilinganishwa na asilimia 51 ya Bajeti ya Mwaka 2018/2019 kwa kipindi kama hicho. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga asilimia kubwa ya fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ukusanyaji wa maduhuli; kwa upande wa maduhuli, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Maji illipanga kukusanya mapato yenye jumla ya Sh.7,678,502,000.00 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Machi, 2020, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Sh.7,917,721,588.30 sawa na asilimia 103 ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato hayo kuvuka lengo la ukusanyaji kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha mwezi Juni.

Mheshimiwa spika, Maoni ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ulikabiliwa na changamoto mbalimbali zinazojumuisha changamoto za upatikanaji wa rasilimali fedha, kutotekeleza miradi kwa wakati, uharibifu katika vyanzo vya maji na upotevu wa maji.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa wataalam wa maji...

TAARIFA

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Ndiyo Mheshimiwa Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, samahani, bado na sisi tuna tatizo kama ambalo walikuwa wameripoti wenzetu, hatuna watu wa *lThumu* ndani, tukinyoosha mikono ili watusaidie hatuwapati. Kwa hiyo, tunaomba kama *lTwapo* watusaidie.

SPIKA: Nimehakikishiwa linatatuliwa baada ya muda si mrefu. Endelea Mwenyekiti.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Spika, upungufu wa wataalamu wa maji. Utafiti uliofanywa na Wizara umebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 sekta ya maji inakabiliwa na upungufu wa watumishi takribani 2,019.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Maji inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Sh.28,275,145,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Sh.11,171,114,000 sawa na asilimia 40 ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (*OC*) na Sh.17,103,330,000 sawa na asilimia 60 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazoomba kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Wizara ya Maji inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.7,008,930,000. Kati ya fedha hizo Sh.349,449,000,000 sawa na asilimia 49.6 ni fedha za ndani na Sh.355,539,000,000 sawa na asilimia 59.4 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya maduhuli. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Maji inakadiriwa kukusanya jumla ya Sh. 8,187,042, 210 kwa ajili ya eneno la maduhuli.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati. Baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na

maombi ya fedha kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuataao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*RUWASA*). Kuanzishwa kwa wakala huu ni juhudzi za Serikali katika kutatua changamoto za utatuaji huduma ya maji. Tangu kuanzishwa kwa *RUWASA* mwezi Julai 2019 mafanikio yameanza kuonekana kutokana na kuongezeka kwa utekelezaji wa miradi kutoka asilimia 53 Julai 2019 hadi kufikia wastani wa asilimia 64.8 Novemba 2019. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa wakala huu hakutakuwa na maana endapo Serikali haitaweza kushughulikia changamoto zinazoikabili *RUWASA* ili iweze kutekeleza majukumu inayokabidhiwa kisheria kwa ufanisi. Changamoto zinazoikabili *RUWASA* zimealnishwa kwa kirefu kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sekta ya maji imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa wataalamu, kuna upungufu wa watumishi takribani 2019 katika kada mbalimbali. Uhaba huu mkubwa wa watumishi katika sekta ya maji umekuwa ukikwamisha huduma ya maji safi na usafi wa mazingira kutolewa kikamilifu. Kamati inashauri Wizara ya Maji kupeleka maombi Ofisi ya Rais Utumishi ili kuomba kibali cha kuajiri. Aidha, ni muhimu pia kwa Serikali kuona ukubwa wa tatizo la uhaba wa wataalam katika sekta ya maji na kutenga fedha kwa ajili ya kuajiri watumishi ili kukabiliana na upungufu huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini katika kutekeleza miradi ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira pamoja na usimamizi wa rasilimali za maji nchini kwa mwaka 2019/2020 Wizara ilikabiliwa na changamoto ya fedha kutokupatikana kwa wakati. Athari zinazojitokeza kwa kutokupatikana fedha kwa wakati ni pamoja na kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi ambako huathiri kuendelea kwa utekelezaji wa miradi. Kamati inashauri Serikali kuititia Wizara ya Fedha na Mipango kushughulikia mapema iwezekanavyo

hati za madai za wakandarasi ambazo hazijalipwa ili madai haya yalipwe na hatimaye kukamilisha miradi ya maji iliyosimama kutokana na ukosefu wa fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya mapitio ya sekta kuu tano za kipaumbele cha matumizi ya Serikali na kubaini kuwa licha ya kuwepo kwa ahadi kwa umma kukuza uchumi wa nchi na kuboresha mazingira ya biashara kuitia kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu na ujuzi, chakula na lishe pamoja na maji safi na salama, Kamati imebaini sekta kuu tano zilizotengewa fedha nyingi kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo ni elimu, miundombinu, afya na nishati. Kamati inashauri Serikali kama kweli sekta ya maji ni moja ya sekta kuu tano za kipaumbele ni vyema sekta hii ikatengewa bajeti ya kutosha kama inavyotengwa katika sekta ya elimu, miundombinu, afya na nishati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza miradi ya maji safi na salama pamoja na usimamizi wa rasilimali maji kwa mwaka 2019/2020, Wizara ya Maji inaendelea kukabiliwa na changamoto ya kuchelewa kupatikana kwa misamaha ya kodi kwa miradi inayostahili kutokana na makubaliano ya kifedha katika Serikali na watoa fedha. Hali hii imesababisha kusuasua kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi na kutishia azma ya Serikali kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliiana na changamoto hii, Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kufuata taratibu zote katika utoaji wa misamaha kodi ili kuhakikisha upatikanaji wa misamaha hiyo kwa wakati kwani Makubaliano ya Kifedha (*Financial Agreement*) yako wazi na yanaelekeza kuwa miradi haipaswi kutozwa kodi. Kamati inashangazwa na ucheleweshaji unaofanywa na taasisi za Serikali kwenye misamaha ya kodi hadi kupelekea vifaa inavyotumika katika ujenzi wa miradi hiyo kuzuiliwa bandarini kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi ambavyo mmekuwa

mkituongoza kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge hili la Kumi na Moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kumbukumbu naomba Wajumbe wote wa Kamati majina yao yaingizwe katika Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kama yalivyoordheshwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hiki ni kipindi cha mwisho katika Bunge hili la Kumi na Moja, napenda kutumia fursa hii kuwatachia kheri Wajumbe wa Kamati na Wabunge wenzangu wote katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Oktoba, 2020. Panapo majaliwa Mwenyezi Mungu aturejeshe sote katika Bunge la Kumi na Mbili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Juma Aweso, Katibu Mkuu Prof. Mkumbo Kitila, Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Anthony Sanga pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Maji kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakati inatekeleza majukumu yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai; Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati, Ndugu Michael Chokokoto; Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati ya Bunge, Ndugu Gerald Magili kwa kuisaidia na kuweza Kamati kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kwa namna ya kipekee naishukuru sana Sekretarieti ya Kamati ambao ni Ndugu Virgil Mtui, Ndugu Rachel Nyega na Ndugu Jane Ndulesi kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maeleo haya, sasa naliomba Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama yalivowasilishwa katika hoja ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA
WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019
PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA
WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 KAMA
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 (7) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvubi. Kwa madhumuni ya taarifa hii, taarifa ninayoiwasilisha inahusu Wizara ya Maji- Fungu 49.

Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yafuatayo:-

(a) Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji - fungu 49, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

(b) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

- (c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;
- (d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na
- (e) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo yatakayotolewa ni matokeo ya uchambuzi wa nyaraka zilizowasilishwa mbele ya Kamati, majadiliano kati ya Kamati na wadau mbalimbali na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelawa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

SEHEMU YA PILI

UCHAMBUZI WA MASUALA MBALIMBALI

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii inabainisha masuala muhimu yaliyojitekeza katika uchambuzi uliofanywa na Kamati kwa kuzingatia masuala yaliyoorodheshwa katika Kipengele 1.2 cha Sehemu ya Kwanza.

Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji na kutoa maoni na ushauri kwenye maeneo saba (7) ya kipaumbele yafuatayo:-

- (a) Kuimarisha utengaji wa fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo;
- (b) Kuongeza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji Kwa kuimarisha makusanyo ya Mfuko wa Maji;
- (c) Mikakati ya uvunaji wa Maji ya mvua kwa ajili ya Matumizi mbalimbali;

- (d) Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka katika Miji na Makao Makuu ya Mikoa nchini;
- (e) Kuimarisha na Kutekeleza Mipango na Mikakati ya Kutumia Maji kutoka Ziwa Tanganyika;
- (f) Kuimarisha Tafiti za Rasilimali Maji na kuboresha Mitaala ya Elimu kwa Umma kuhusu kutunza vyanzo vya Maji; na
- (g) Kukamilisha miradi mbalimbali ya Maji inayotekelzeza nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati umetekelzeza. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo ya kutekeleza ushauri wa Kamati kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi. Hata hivyo, baadhi ya ushauri haujatekelezwa kikamilifu hususan kwenye ushauri uliohusu umuhimu wa kuwa na Mpango Mkakati wa kuhakikisha uvunaji wa maji ya mvua unakuwa endelevu kwa matumizi ya akiba hasa wakati wa kiangazi pamoja na ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika miji na makao makuu ya mikoa.

Mheshimiwa Spika, tafiti zinaonyesha kiasi cha maji kwa mtu kinaendelea kushuka mwaka hadi mwaka. Ni muhimu kuchukua hatua kuhusu uvubaji wa maji ya mvua na kuyahifadhi kwa ajili ya matumizi ya badae, Wabunge watakubaliana na Kamati jinsi mwaka huu nchi yetu ilivyopata baraka kwa kuwa na mvua nyngi, hata hivyo tujilize ni maji kiasi gani ya mvua yaliyopotea bila kuhifadhiwa wakati wa kipindi hiki cha masika.

Mheshimiwa Spika, rai ya Kamati kwa Serikali haikuwa tu uvunaji wa maji kupitia mapaa na majengo (majumbani, au kwenye majengo ya Serikali) ambao utekelezaji wake pia umekuwa mgumu, Kamati iliitaka Serikali kufikiri zaidi kwa kuwa na mipango ya muda mfupi, kati na endelevu ya kuvuna maji mengi ya mvua yanayopotea barabarani kipindi kama hiki cha masika.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati ilishauri umuhimu wa ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika miji na makao makuu ya mikoa kutokana na ukweli kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja wa hali ya afya na usafi wa mazingira, tafiti zinaonyesha kuwepo uwiano wa moja kwa moja katika uondoaji majitaka katika miji na majiji, usafi wa mazingira wa afya za watu na ustawi wa jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali kuongeza kasi ya kutekeleza mipango na miradi mbalimbali ya majitaka na kwamba mipango hiyo iende sambamba na mipango ya upatikanaji majisafi pamoja na ujenzi wa barabara unaondelea katika miji na majiji kupitia mpango wa uboreshaji miji na majiji (Strategic Cities) unaofadhiliwa na mkopo kutoka Benki ya Dunia kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwamba ujenzi wa barabara hizo uende sambamba na ujenzi wa miundombinu ya majitaka. Hata hivyo, bado utekelezaji wa ushauri huu sio wa kuridhisha kwani miundombinu ya majitaka huwekwa baada ya barabara kukamilika na hivyo kuharibu barabara zilizojengwa kwa kubomoa na kuacha mashimo ambayo ni hatari kwa matumizi ya binadamu na magari.

Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 yalijielekeza katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika na eneo la ukusanyaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi Machi, 2020.

Kiasi cha Fedha Kilichoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Fungu 49, liliidhinishiwa jumla ya shilingi **624,415,131,530.00**. Kati ya fedha hizo shilingi **6,266,714,000** ni Fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi **610,469,888,530.00** zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya

Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **349,449,000,000.00** sawa na **asilimia 57** ni Fedha za Ndani ambapo kati ya fedha hizo, shilingi **158,500,000,000** ni za Mfuko wa Taifa wa Maji na shilingi **284,714,034,677** ni fedha zinazotokana na vyanzo vingine vya ndani. Aidha, shilingi **261,020,888,530** sawa na **asilimia 43** ni Fedha za Nje.

Mwenendo wa utolewaji wa fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2020 Wizara ya Maji (Fungu 49) ilikuwa limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi **6,266,741,000.00** sawa na **asilimia 73**, na ya kiasi kilichoidhinishwa. Aidha, kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa zilikuwa shilingi **453,697,256,871.41** sawa na **asilimia 72.2** ya Fedha zote za Bajeti ya Maendeleo zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi **175,036,818,847.08** sawa na **asilimia 50** ya bajeti ya Fedha za Ndani kati ya hizo fedha zilizotokana na Mfuko wa Maji ni shilingi **108,574,476,547.40**.

Maoni kuhusu Mwenendo wa Utilewaji Fedha za miradi ya maendeleo

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo juu, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 fedha za miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Maji Fungu 49 zilizotolewa ni **asilimia 74.2**, kikilinganishwa na **asilimia 51** ya Bajeti ya Mwaka 2018/2019. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga asilimia kubwa ya Fedha za Ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo sasa Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa Fedha za Ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji nchini. Hatua hii ni ya kupongezwa kwa kuwa inaonyesha dhamira ya dhati ya Serikali kusogeza huduma ya majisafi kwa wananchi ili kuhakikisha ifikapo Mwaka 2025 wananchi wote wa mijini waweze kuwa na huduma bora ya maji na wananchi wa vijiji kuwa na huduma bora kwa **asilimia 90**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko la bajeti na utoaji fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, bado lengo la Serikali kuhakikisha makundi yote ya jamii yanapata huduma inayoridhisha ya majisafi na usafi wa mazingira kwa kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo kufikia **asilimia 85** kwa wakazi wa vijijini na **asilimia 95** kwa maeneo ya vijijini ifikapo 2020 halijafikiwa kwa kiwango kilichotarajiwa. Takwimu zinaonyesha Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi Vijijini hadi **Machi 2020** ni **asilimia 70.1** ikilinganishwa na malengo yaliyoainishwa kwenye ¹Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 kuwa Serikali itahakikisha hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi waishio vijijini inafikia wastani wa **asilimia 85** ifikapo mwezi **Desemba 2020**. Aidha, malengo mengine ni pamoja na kuhakikisha kuwa majisafi na salama yanapatikana kwa umbali **usiozidi mita 400** kutoka kwenye makazi ya watu, na pia maji yawe yakutosheleza na ya uhakika.

Ukusanyaji wa maduhuli

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maduhuli, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Maji ilipanga kukusanya mapato yenye jumla ya shilingi **7,678,502,000.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Machi, 2020, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **7,917,721,588.30** sawa na **asilimia 103** ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato hayo na kuvuka lengo la ukusanyaji kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha mwezi Juni.

Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2019/2020

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) inayoitaka Kamati kufanya ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha (2019/2020). Ili kutekeleza masharti ya kanuni hiyo, Kamati ilipanga

¹ Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015

kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maji katika Mkoa wa Mwanza katika Wilaya za Magu na Miswungwi. Hata hivyo ziara hiyo haikuweza kufanya kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa **COVID 19**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutofanyika kwa ziara hiyo, Kamati ilipokea taarifa kuhusu kazi mbalimbali zilizotekeliza kwenye sekta ya maji katika kipindi cha Julai – Desemba kwa Mwaka wa Fedha 2019/20. Kazi hizi ni pamoja na utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za maji, ufuatilaji wa ubora wa maji; miradi mbalimbali ya huduma za maji vijijini na mijini pamoja na miradi ya usafi wa mazingira na jinsi utekelezaji wa miradi ya maji ilivyosaidia hali ya upatikanaji wa huduma ya maji nchini pamoja na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Kamati imeridhishwa na namna Serikali inavyotekeliza miradi ya maji sehemu mbalimbali nchini. Kamati inaanini Serikali ikiimarisha utoaji wa fedha zilidhoidhinishwa na Bunge kwa wakati, miradi ya maji itakamilika kwa wakati na hivyo kuwezesha lengo lililowekwa na Serikali kufikiwa.

Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa spika, uchambuzi wa kamati umebaini kuwa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 ulikabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji. Changamoto hizo ni pamoja na:-

i) Changamoto ya Upatikanaji wa Rasilimali Fedha za Kutekeleza miradi kwa wakati

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza miradi ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira pamoja usimamizi wa rasilimali za maji nchini, kwa mwaka 2019/20 Wizara imekabiliana na changamoto ya fedha kutokupatikana kwa wakati. Athari zinazojitokeza kwa kutopatikana kwa fedha kwa wakati ni pamoja na kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi ambako huathiri kuendelea kwa utekelezaji wa miradi. Mfano, katika kipindi cha Julai – Desemba 2019, jumla ya madai ya

wakandarasi na wataalam washauri ambao hawajalipwa Hati za Madai ni **Shilingi 19,135,029,386.67**.

ii) Uharibifu wa Vyanzo vya Maji Unaosababishwa na Shughuli za Kibinadamu

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake imebaini kuwa bado kuna ongezeko la uvamizi wa vyanzo vya maji kunakosababishwa na ongezeko kubwa la shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji ikiwemo kilimo, ufügaji na ujenzi wa makazi na viwanda. Hali hiyo inasababishwa na ukosefu wa miundombini ya kusambaza maji; kilimo cha umwagiliaji; na unyweshaji wa mifugo katika maeneo ya vijijini na matokeo yake ni vyanzo kukauka, mabwawa ya maji kujaa mchanga (*siltation*) na baadhi ya maeneo kuwa na migogoro.

iii) Upotevu wa Maji

Mheshimiwa Spika, licha ya Serikali kujiwekea lengo la kupunguza upotevu wa maji katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Miji Mikuu ya Mikoa hadi kufikia **asilimia 25** ifikapo mwezi Juni 2020. Bado changamoto ya upotevu wa maji ni kubwa, kwani tafiti zinaonyesha hadi kufikia mwezi Desemba 2019 wastani wa upotevu wa maji umefikia **asilimia 31**.

iv) Mtazamo wa Wananchi kuhusu Huduma ya Maji

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maji ya mwaka 2002 imeeleza umuhimu wa jamii kuchangia gharama ya uendeshaji na matengezo ya miradi ya maji vijijini. Jitihada mbalimbali zimechukuliwa katika kuhamasisha wananchi kushiriki katika kuchangia gharama za miradi ya maji. Hata hivyo, kumeendelea kuwepo kwa mtazamo tofauti ambapo baadhi ya wananchi wanaona si haki kulipia maji kwa kuwa ni rasilimali ya asili.

v) Uwezo mdogo Jumuiya za Watumia Maji (CBWSOs)

Mheshimiwa Spika, utafiti wa Kamati umebaini kuwepo kwa idadi kubwa ya Jumuiya za Watumia Maji (*CBWSOs*) ambazo zina uwezo mdogo katika kusimamia kikamilifu utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini hali

inayochangia baadhi ya miradi ya maji vijijini kutoa huduma hafifu na kutokuwa endelevu.

vi) Upungufu wa Wataalam wa Sekta ya Maji

Mheshimiwa Spika, Sekta ya maji kwa muda mrefu imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa wataalam. Taarifa iliyotolewa na Wizara kwa Kamati, inaeleza kuwa Wizara ilifanya zoezi la kubaini idadi ya wataalam wanaohitajika ili kutoa huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira kikamilifu. ²Taarifa ya zoezi la *HR Audit* iliyofanyika katika mwaka 2018/2019 ilibaini upungufu wa Watumishi 2,019. Aidha, zoezi hilo lilibaini pia, Wahandisi Wataalam na Wahandisi 344 sawa na **asilimia 50.95** ya wataalam hao walipo bado hawajakamilisha taratibu za usajili za *Engineering Registration Board*.

Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021-Fungu 49

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali ya maji ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 yenye kulenga kuinua hali ya maisha ya wananchi na kulifikisha taifa katika uchumi wa kipato cha kati. Dira hii inatekelezwa kupitia nyenzo mbalimbali, zikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 na llani ya CCM ya Mwaka 2015-2020. Aidha, Tanzania inashiriki kikamilifu katika kutekeleza malengo ya kimataifa, ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals - SDGs 2016 - 2030*). Katika malengo hayo, sekta ya maji ni moja ya sekta za kipaumbele kutokana na umuhimu mkubwa wa huduma ya maji kwa ajili ya maisha ya binadamu, wanyama, mimea na mazingira. Aidha, maji ni injini ya shughuli za maendeleo ya kijamii na kiuchumi na ni nyenzo muhimu katika kutokomeza umaskini na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ili kuishauri Serikali kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 pamoja na kuhakikisha nchi yetu

² Taarifa ya Wizara ya Maji kwa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai – Desemba, 2019

inatekeleza kikamilifu lengo Namba Sita (6) kati ya malengo 17 ya Malengo Maendeleo Endelevu ambalo linazitaka nchi wananchama wa umaja wa Mataifa kuhakikisha kila Serikali inawapatia wananchi wake wote majisafi na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mionganini mwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa na inatekeleza lengo hili kupitia Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kisekta pamoja na Mipango mbalimbali ya kibajeti. Katika kutekeleza jukumu la Bunge la kuishauri na kuisimamia Serikali kwa niaba ya Wananchi, tarehe 27 Machi, 2020 Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Maji na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Mpango ambaao umezingatia pamoja na mambo mengine Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Malengo ya Bajeti na Kazi Zilizopangwa Kutekelezwa

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, kazi zitakazofanyika zimejikita katika maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo: -

- a) Kuendelea kutambua, kutunza, kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini kwa kufanya tathmini na ufuutilaji wa rasilimali za maji; kuhifadhi na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vyaa maji; kugawa na kuendeleza rasilimali za maji; kuimarisha usimamizi wa rasilimali za majishirikishi na kuimarisha Taasisi zinazosimamia rasilimali za maji nchini;
- b) Kukamilisha miradi inayoendelea katika Halmashauri mbalimbali na kuanza miradi mipya ya maji vijijini; kutekeleza miradi ya maji vijijini katika maeneo kame na yenye shida kubwa ya maji; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa mabwawa pamoja na upanuzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye mabwawa na visima vilivyocheimbwa; na kuendelea na ujenzi wa miradi mikubwa ya maji vijijini katika maeneo ya Same- Mwanga- Korogwe na Kigoma;
- c) Kukamilisha miradi inayoendelea na kuanza utekelezaji wa miradi mipya ya majisafi na usafi wa mazingira katika:-

- (i) Jiji la Dar es Salaam;
- (ii) Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tinde na Shelui, mradi wa maji wa Simiyu;
- (iii) Mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na majitaka katika Jiji la Dodoma na Ikulu ya Chamwino;
- (iv) Kuendelea na ujenzi wa mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Arusha;
- (v) Mradi wa kuboresha mfumo wa majitaka katika Mji wa Musoma na Bukoba;
- (vi) Mradi wa usambazaji maji na usafi wa mazingira katika Mji wa Shiyanga.
- (vii) Miradi mingine ya maji katika Miji Midogo, Miji Mikuu ya Mikoa na Wilaya mbalimbali na Miradi ya Maji ya Kitaifa; na
- (viii) Mradi wa kutoa maji safi mto Ruvuma kupeleka Mtwara Mikindani na vijiji vilivyo umbali wa kilomita 12 kutoka bomba kuu;
- d) Kuanza kutekeleza miradi mipya yenye kuleta matokeo makubwa kutoka kwenye vyanzo vya uhakika ukiwemo mradi wa kutoa maji ziwa Victoria kupeleka Singida hadi Dodoma;
- e) Kuboresha huduma ya maji safi na salama katika taasisi za umma ikiwemo vituo vya afya na shule;
- f) Kuimarisha mfumo wa uvunaji maji ya mvua na kutekeleza mkakati wa ujenzi wa bwawa moja kwa kila Wilaya zenyne mazingira yanayofaa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa;
- g) Kuboresha huduma ya maji kwa kujenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji katika Miji mikuu ya Mikoa, Miji mikuu ya Wilaya, Miji midogo na miradi ya kitaifa.

- h) Kujenga mabwawa ya kimkakati ambayo ni Farkwa (Dodoma), Kidunda (Morogoro Vijiji) na Ndembera (Iringa) na ukarabati wa mabwawa ya ukubwa wa kati ya Itobo (Nzega) na Enguikment (Monduli);
- i) Kuendelea kukiimarisha Chuo cha Maji ili kiweze kuzalisha wataalam wa sekta ya maji nchini; na
- j) Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa Ubora wa Maji.

Fedha zinazoombw a kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza kazi zilizopangwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Maji - Fungu 49 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **28,275,145,000** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **11,171,714,000 sawa na asilimia 40** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC), na Shilingi **17,103,431,000 sawa na asilimia 60** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya Watumishi.

Fedha zinazoombw a kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Wizara ya Maji kupitia fungu 49 inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 705,008,930,000:00**. Kati ya fedha hizo, shilingi **349,449,000,000:00** sawa na **asilimia 49.6** ni Fedha za Ndani na shilingi **355,539,000,000:00** sawa na **asilimia 50.4** ni Fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo za maendeleo zinaombwa kugharamia miradi ya kipaumbele ikiwemo miradi ya maji Vijiji. Aidha, kipaumbele kimetolewa kwenye miradi na kazi zinazohusu uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji ikiwemo ujenzi na ukarabati wa mabwawa, uboreshaji wa huduma za ubora wa maji ikiwemo kujenga uwezo wa maabara za maji pamoja na miradi na kazi za kujenga uwezo wa Taasisi na Watumishi.

Makusanyo ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Maji kupitia Fungu 49 imekadiria kukusanya shilingi

8,187,042,210.00 kutokana na vyanzo vya mauzo ya nyaraka za zabuni, leseni kwa makampuni ya utafiti na uchimbaji wa visima vya maji, tozo mbalimbali kwa wateja wanaopata huduma ya maabara za ubora wa maji na vibali vya matumizi ya maji katika mabonde. Kati ya fedha hizo Shilingi **400,000,000.00** ni tozo za maabara za maji, Shilingi **1,000.00** ni mauzo ya nyaraka za zabuni, Shilingi **240,000,000.00** zinatokana na leseni kwa makampuni ya utafiti na uchimbaji wa visima vya maji na Shilingi **7,787,041,220.00** zitatokana na vibali vya matumizi ya maji katika mabonde.

Tathimini ya Kamati kuhusu Malengo ya Bajeti na Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Maji - Fungu 49.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia, imechambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2020/2021. Malengo haya ni ya msingi na ya kuridhisha. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa malengo yanayowekwa na Wizara yamekuwa yakijirudia kila mwaka nahii inatokana na Serikali kutegejemea mipango iliyojiwekea kutekelezwa na wadau wa maendeleo. Kamati ilipokuwa ikipitia taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2019/2020 Wajumbe walitaka kufahamu hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa mabwawa ya kimkakti ya Farkwa (Dodoma), Kidunda (Morogoro Vijiji) na Ndembera (Iringa) majibu ya Serikali yalikuwa ³"Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mipango inaendelea kufanya majadiliano na wafadhili mbalimbali ili kupata fedha za ujenzi wa mabwawa ya kimkakti ya Farkwa, Ndembera na Kidunda".

Mheshimiwa Spika, kwa Mfano; katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 moja ya malengo ya kipaumbele cha Wizara ilikuwa kujenga mabwawa makubwa ya kimkakati ya Farkwa (Dodoma), Kidunda (Morogoro Vijiji) na Ndembera (Iringa) na ukarabati wa mabwawa ya ukubwa wa kati ya Itobo (Nzega) na Enguikment (Monduli). Ukipitia hotuba ya Waziri

³Taarifa ya Wizara kuhusu Majibu ya Hoja za Wajumbe wa Kamati Waziri wa Maji akiwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Nusu Mwaka wa Fedha 2019/2020- Tarhe 22 Januari, 2020

wa Maji kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 utaona lengo hili limejirudia tena likiwa kama mojawapo ya lengo la kipumble.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hiyo niliyoeleza hapo juu na changamoto zingine, Kamati inatambua jitihada kubwa zilizofanywa na Serikali katika utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira nchini. Dhamira ya Serikali kuwapatia wananchi huduma bora za maji safi na usafi wa mazingira inaweza kuonekana pale ambapo Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019 ilianzisha Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine Sheria hii imehamisha uwajibikaji wa Watumishi wa Sekta ya Maji kutoka OR-TAMISEMI, Tawala za Mikoa na pia kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenda Wizara ya Maji. Sheria hii pia imehamisha majukumu ya utekelezaji na usimamizi wa utoaji wa huduma ya maji katika maeneo ya vijijini, Miji Midogo na Makao Makuu ya Wilaya kwenda Wizara ya maji.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya yanadhihirisha jitihada za Serikali ambazo zinaonesha nia njema ya kisiasa na hitaji la kuwaondolea wanachi hasa wa vijijini adha ya upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira. Licha ya jitihada na mabadiliko haya, sekta ya maji bado inakumbana na changamoto za kifedha na ongezeko la uhitaji unaotokana na ongezeko la watu na ukuaji wa miji unaosababisha sekta hii kuwa na 'uhaba wa fedha' katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia tathimini hii, Kamati, imejiridhisha kwamba fedha zinazotengwa na Serikali pamoja na ahadi za wafadhili kwa sekta ya maji viko wazi tatizo ni kuwa fedha hizo hazitolewi kwa wakati na kama zillivyoidhinishwa na Bunge. Changamoto hii iko wazi na inajulikana kinachotakiwa tu ni kurekebisha upungufu uliopo ili kuifanya sekta hii kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati imebaini ukuaji wa uchumi mkubwa wa taifa (7.1% kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na 7% mwaka 2018) na ongezeko la ukusanyaji mapato (Kodi kwa uwiano wa GDP wa 13.1%, kwa kulinganisha na makadirio yaliyofanywa mwaka 2018/19 ya 12.1%); haujaakisiwa vya kutosha katika sekta ya maji kwa muongo uliopita.

SEHEMU YA TATU

MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa Bajeti ya Mwaka 2020/2021. Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

i. **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Rural Water Supply and Sanitation Authority – RUWASA). Kuanzishwa kwa Wakala huu ni juhudhi za Serikali katika kutatua changamoto ya utoaji wa huduma ya maji kusimamiwa na Wizara mbili, hali iliyosababisha kuwepo kwa maelekezo yanayokinzana. Usimamizi usioridhisha wa utekelezaji wa miradi na utoaji wa huduma zilizopelekea kukwamishwa kwa upatikanaji wa haraka wa huduma ya maji vijijini. Tangu kuanzishwa kwa RUWASA mwezi Julai 2019 kumepekekea kuongezeka kwa utekelezaji wa miradi kutoka **asilimia 53** mwezi Julai 2019 na hadi kufikia **asilimia 64.8** mwezi Novemba 2019.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Wakala huu hakutakuwa na manufaa endapo Serikali haitaweza kushughulikia changamoto zinazoikabili RUWASA ili iweze kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa kisheria kwa ufanisi. Kwa sasa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini unakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

- a) Upungufu wa watalaam (*technical and supporting*) - RUWASA inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa watumishi katika ngazi zote kuanzia makao makuu hadi ngazi

ya wilaya ikilinganishwa na mahitaji ya watumishi kwa mujibu wa Ikama katika kada mbalimbali

b)Uhaba wa vitendea kazi na Ofisi – tangu ilipoanza utekelezaji wa majukumu yake tarehe 01 Julai 2019 kumejitokeza changamoto ya uhaba wa vitendea kazi kama vile magari, pikipiki, compyuta pamoja na majengo kwa baadhi ya Ofisi za RUWASA za Mikoa na Wilaya.

ii. Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Sekta ya Maji imekuwa ikitabiliwa na upungufu wa wataalam, kuna upungufu wa Watumishi takribani 2,019 katika kada mbalimbali. Uhaba huu mkubwa wa Watumishi katika sekta ya maji umekuwa ukikwamisha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira kutolewa kikamilifu. Kamati inaishauri Wizara ya Maji kupeleka maombi Ofisi ya Rais –UTUMISHI ili kuomba kibali cha kuajiri. Ni muhimu kwa Serikali kuona ukubwa wa tatizo la uhaba wa wataalam katika sekta ya maji na kutenga fedha kwa ajili ya kuajili Watumishi ili kukabiliana na upungufu uliopo.

iii. Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini katika kutekeleza miradi ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira pamoja usimamizi wa rasilimali za maji nchini, kwa mwaka 2019/20 Wizara imekabiliana na changamoto ya fedha kutokupatikana kwa wakati. Athari zinazojitokeza kwa kutopatikana kwa fedha kwa wakati ni pamoja na kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi ambako huathiri kuendelea kwa utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kushughulikia mapema iwezekanavyo Hati za Madai ya Wakandarasi ambazo hazijalipwa ili madai hayo yalipwe na hatimae kukamilisha miradi ya maji iliyosimama kutokana na ukosefu wa fedha.

iv. Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya mapitio ya sekta kuu tano za kipaumbele cha matumizi ya Serikali na kubaini kuwa licha ya kuwepo kwa ahadi kwa umma kukuza uchumi wa nchi na kuboresha mazingira ya biashara kupitia kuboresha

upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu na ujuzi, chakula na lishe pamoja na maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini sekta kuu tano zilizotengewa fedha nydingi kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo (2014/2015 - 2019/2020) ni Elimu, Miundombinu, Kilimo, Afya na Nishati. Kamati inaishauri Serikali kama kweli Sekta ya Maji ni moja ya sekta kuu ntano za kipaumbele ni vyema ikaitengea sekta hii bajeti ya kutosha kama ambavyo inatenge kwa sekta za Elimu. Miundombinu, Afya, Nishati na Kilimo.

v. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza miradi ya majisafi na usafi wa mazingira pamoja na usimamizi wa rasilimali za maji nchini, kwa mwaka 2019/20 Wizara ya Maji imeendelea kukabiliwa na changamoto ya kucheleva kupatikana kwa misamaha ya kodi kwa miradi inayostahilli kutokana na makubaliano ya kifedha katika Serikali na watoa fedha.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo imesababisha kusuasua kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi na kutishia adhima ya Serikali kufikia malengo yaliyokusudiwa. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kufuata taratibu zote katika utoaji wa misamaha ya kodi ili kuhakikisha upatikanaji wa misamaha hiyo kwa wakati.

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyevitii wa Bunge, kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkituongoza kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge la Kumi na Moja na kuliwezesha Bunge letu kutimiza wajibu wake wa kuvisimamia Serikali kwa niaba ya Wananchi kwa mujibu wa Katiba. Aidha, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa katika kipindi chote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hiki ni kikao cha mwisho katika Bunge hili la Kumi na Moja, napenda kutumia fursa hii kuwatachia Wajumbe wa Kamati na Wabunge wenzangu wote kila la kheri katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2020 na panapo majaliwa ya Mwenyezi Mungu, turejee sote kama tulivyo katika Bunge la Kumi na Mbili ili kuendeleza gurudumu la ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Kutokana na kazi kubwa walioifanya natamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na utaratibu tuliojiwekea hapa Bungeni naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni kama ifuatavyo: -

- | | |
|--|--------------|
| 1. Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb | " |
| 5. Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani, Mb | " |
| 6. Mhe. Kangi Alphaxad Lugola Mb | " |
| 7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | " |
| 8. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb | " |
| 9. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb | " |
| 10. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb | " |
| 11. Mhe. Lucy Simon Magereli, | " |
| 12. Mhe. Justine Joseph Monko | " |
| 13. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb | " |
| 14. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb | " |
| 15. Mhe. Pascal Yohana Haonga | " |
| 16. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb | " |
| 17. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb | " |
| 18. Mhe. Devotha Methew Minja, Mb | " |
| 19. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb | " |
| 20. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb | " |
| 21. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb | " |
| 22. Mhe. Juma Ali Juma, Mb | " |

- | | |
|----------------------------------|---|
| 23. Mhe. Emmanuel Papian John, | " |
| 24. Mhe. Kunti Yusuph Majala, | " |
| 25. Mhe. Anthony Calist Komu, Mb | " |
| 26. Mhe. Jitu Vraijal Soni, Mb | " |

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji Mhe. Prof. Makame Mbarawa, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Jumaa Aweso (Mb), Katibu Mkuu Prof. Kitila Mkumbo na Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Sanga pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Maji kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge Ndg. Gerald Magili, kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kwa namna ya kipekee naishukuru Sekreterieti ya Kamati amba ni Ndg. Virgil Mtui na Ndg. Rachel Nyega wakisaidiwa na Ndg. Jane Ndulesi kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumiziya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa katika hoja ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**

27 APRILI, 2020

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa. Tunakushukuru sana kwa uwasilishaji wako mzuri, hiyo sauti msishtuke mwezi Mtukufu huu swaumu kali. (*Kicheko*)

Sasa tunaingia *session* ya uchangiaji na tunaanza na Mheshimiwa Leah Komanya.

WABUNGE FULANI: Bado.

SPIKA: Ooh, nimemruka Mheshimiwa Sakuru, yuko Msekwa. Hebu tupate mawasiliano ya Msekwa tumsikilize Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wakati huo Mheshimiwa Leah Komanya ajiandae atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza. Afadhali sasa nakuona, endelea una dakika 20.

MHE. ZUBEDA H. SAKURU - MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAJI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2019/2020 pamoja na Mpango wa Maendeleo na Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa kuwa hotuba yangu ni ndefu, naomba hotuba iliyowasilishwa kwenye meza yako iingie kwenye Katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tunatumia barakoa kila mmoja ajitahidi kuongeza sauti kidogo na kuweka microphone sawasawa.

MHE. ZUBEDA H. SAKURU - MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu hoja iliyo mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi Hai, kwa imani yake kwangu kuwa Msemaji Mkuu wa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuwapa moyo Watanzania wote hasa viongozi na wanachama wenzangu pamoja na wanaharakati wanaokabiliwa na kesi za aina mbalimbali nchini katika mapambano ya kudai haki na demokrasia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa maji. Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa kwa ushirikiano wa Shirika la Afya Duniani (*WHO*) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), mabilioni ya watu duniani wanaendelea kutaabika kutokana na kukosa huduma bora za maji na masuala ya usafi. Takribani watu bilioni 2.2 duniani hawana maji safi na salama; watu bilioni 4.2 hawana huduma salama za usafi; na watu bilioni 3 wanakosa huduma za msingi na sehemu za kunawa mikono. Vilevile inakadiriwa kuwa kati ya watu 10 mmoja hana huduma za msingi na watu milioni 144 hunywa maji yasiyo safi na salama. Takwimu hizi zinadhahirisha kwamba watu 8 kati ya 10 katika maeneo ya vijijini wanakosa huduma hizo muhimu.

Mheshimiwa Spika, hivyo ripoti hii imeweka wazi kuwa endapo nchi zitashindwa kuweka juhudhi katika masuala ya usafi, maji salama na huduma za kujisafi basi tutaendelea kuishi na maradhi ambayo kitambo yangekuwa yamebakwa kuwa kumbukumbu za kihistoria. Hivyo, ni dhahiri kuwa 'maji ni uhai'.

Mheshimiwa Spika, takribani 60% ya Watanzania wanapata maji lakini swali kubwa la kujiuliza, je, maji hayo ni

safi na salama? Zaidi ya 50% ya Watanzania wanatumia zaidi ya dakika 30 kufuata maji. Ikumbukwe kuwa wahanga wakubwa wa ukosefu wa maji safi na salama ni kina mama na watoto kwani hutumia muda mwingu na kutembea umbali mrefu ambayo bado si salama.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoainisha awali katika taarifa hii kwa nchi zinazoendelea makundi ambayo ni wahanga wakuu wa tatizo la maji ni wanawake na watoto. Wanawake wamekuwa wahanga wakubwa katika tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama. Hii ni kutokana na shughuli nyingi za kifamilia zinazohitaji maji kama vile, matumizi ya maji katika uzalishaji na uandaaji wa vyakula, matumizi mahsusini ya maji kwenye afya ya uzazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo halina ubishi wa aina yoyote ni kuwa wawanake ndiyo wanapoteza muda mrefu sana kwenda kutafuta maji hali inayodunisha vipato vyao pamoja na kuhatarisha ustawi wao. Wanawake pia ndiyo wamekuwa wahanga wakubwa kwa matukio ya udhalilishaji pamoja na kukumbana na shida mbalimbali katika safari za kutafuta maji. Pia kuna ushahidi wa kutosha kuwa ndoa nyingi zimevunjika kutokana na changamoto za maji, hivyo inatosha kusema kampeni ya kumtua mwanamke ndoo kichwani imeshindwa.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa kipaumbele na umakini katika kutatua changamoto za sekta ya maji nchini unaweka rehani ustawi wa sekta muhimu zinazotegemea maji kama chanzo hasa sekta ya uzalishaji, umwagiliaji, kilimo, viwanda na nishati ya umeme. Bila kuwa na vyanzo vya uhakika vya maji hasa katika kipindi hiki tunapokabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni dhahiri kuwa kama nchi hatutaweza kufanikisha lengo lolote la Malengo ya Maendeleo Endelevu (*SDGs*) kwa sababu maji yanagusa kila lengo na mfumo mzima wa maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya maji. Hivi sasa matumizi ya maji hapa nchini kwa sekta mbalimbali za huduma na uzalishaji yanakadiriwa kufikia mita za ujazo 40. Takwimu

zinaonesha kuwa kiasi cha maji kwa mtu kwa mwaka kimeendelea kupungua kutoka wastani wa mita za ujazo 7,862 mwaka 1962 wakati nchi ikiwa na idadi ya watu milioni 10.6 hadi kufikia wastani wa mita za ujazo 2,250 mwaka 2018 nchi ikiwa na idadi ya watu wapatao milioni 56. Jambo hili linasababisha nchi yetu kuwa juu ya mstari wa uhaba wa maji dunia (*water stress*). Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji Serikali, je, ni mikakati ipi endelevu ya utunzaji wa vyanzo vya maji imewekwa na Serikali nchini?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na TWaweza chini ya ripoti yake ya Safi na Salama? Maji, Usafi na Afya Mazingira (2017) inaonesha kuwa changamoto kuu tatu zilionekana katika sekta ya maji nchini hasa katika maeneo ya vijiji ikiwemo umbali wa vyanzo vya maji, uhaba wa vyanzo vya maji na maji machafu. Tunapofikia ukomo wa miaka mitano ya Awamu ya Tano ambayo ni mwaka 2020, je, ni kweli Serikali imeweza kufikia asilimia 85 kwa vijiji na asilimia 95 kwa mijini kama ilivyoahidi pia katika llani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2015 au bado tunaendelea na hekaya za abunuwasii?

Mheshimiwa Spika, tumefanya nukuu ya takwimu za matumizi ya fedha za awamu ya kwanza ya WSDP kwa lengo kuonesha wingi wa fedha ambao tayari umetumika, lakini ukweli na hali halisi ni kuwa tija yake ni ndogo sana na hajatatua changamoto katika kuhakikisha kila Mtanzania anapata maji safi na salama. Hili linatokana na usiri unaogubika katika miradi hii ikiwemo gharama za miradi yenye, utoaji wa zabuni na hata ushirikishwaji wa wananchi katika kuhakikiisha nao wanakuwa sehemu ya miradi ya hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoweza mazingira ya usiri na ubabaishaji katika kutekeleza miradi ambayo inalenga kuwapa wananchi maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa majitaka. Ni bahati mbaya sana kuwa Serikali imeshindwa kuwekeza vya kutosha katika kukabiliana na tatizo la majitaka nchini hali inayopelekea mifumo ya maji taka kuingiliana kwa kiasi

kikubwa na mifumo ya maji safi na hivyo kuhatarisha afya na mazingira kwa ujumla hasa kwa miji mikubwa.

Mheshimiwa Spika, ni ajabu kuona mpaka sasa, Serikali imeweka lengo la kuwa na mifumo ya majitaka katika miji na makao makuu ya mikoa kufikia asilimia 30 ifikapo mwaka 2025. Hii inatoa taswira kuwa, Serikali haina mpango wa kuhakikisha usalama wa watumiaji wa maji kwa asilimia 70 kufikia mwaka 2025. Hivyo bado kuna hatari kubwa kwa maeneo yanayoendelea kuwa na mvua kubwa kukumbwa na mafuriko kwa kuwa miundombinu ya sehemu hizo itaendelea kuelemewa na maji taka yanayotokana na kutapishwa kwa vyoo na kufanya tatizo hilo kuzaa matatizo mengine ikiwemo matatizo ya kiafya.

Mheshimiwa Spika, tafiti zilizofanywa na TAWASANET (“*no one left behind*”) zinaonesha kuwa 35% ya vyanzo vya maji katika maeneo mengi ya Dar es Salaam na 52% kwa maeneo ya Mkoa wa Morogoro yalionesha uwepo wa mchanganyiko wa vinyesi katika mifumo ya maji yanayotumiwa na wananchi. Hii ina maana kuwa kuna hatari kubwa ya magonjwa ya milipuko hasa kwenye vipindi vya masika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Dar es Salaam 57% ya kinyesi (vyoo vya shimo) kinaingia kwenye mfumo wa mazingira bila kuwekewa dawa ya alia yoyote na ujazo wa 2164m^3 ya maji taka yasiyotiwa dawa unaingia kwenye mfumo wa maji safi katika Jiji la Dar es Salaam kila siku. Kwa takwimu hizo za kutisha zinachangia kuongezeka kwa gharama za kukabiliana na magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo safi na salama. Toka Agosti mwaka 2015 nchi imeshuhudia wagonjwa 33,421 na vifo 542 kutokana na kipindupindu.

Mheshimiwa Spika, inabashiriwa kuwa janga kubwa la mafuriko hasa kwa mijini linaweza kuchangia takribani anguko la 2% ya *GDP* kutokana na mabadiliko ya tabianchi tufikapo mwaka 2030. Hivyo, kutokuwa na mifumo mizuri ya majitaka kuna athari kubwa katika maisha ya jamii ya kila

siku kwa kuwa majitaka yamekuwa kero kubwa kwa biashara kama yadi, mama ntilie, masoko, matumizi ya barabara na hata kuleta athari kubwa kwenye mazingira ya shule ambapo wanafunzi huathiriwa na uchafuzi wa mazingira unaotokana na mifumo duni ya majitaka.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi ni kutokana na Ripoti ya Tanzania *Water and Sanitation Network* ya mwaka 2019 na *Water Sector Equity Report* ya mwaka 2019. Takwimu za randama zinaonesha kuwa tangu tupate uhuru hadi Desemba mwaka 2018 kaya ambazo zilikuwa zimeunganishwa katika mifumo wa majitaka nchini ni 48,566 tu na kufikia Desemba 2019 ziliongezeka kaya 1,842 na hivyo kufanya jumla kuwa kaya 50,408.

Mheshimiwa Spika, kaya hizo zipo katika miji 10 tu ambayo ndio yenye mitandao ya majitaka. Maana yake ni kwamba itatuchukua tena miaka hamsini mingine kuweza kuweka mtandao wa majitaka nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Maji kuweka mikakati madhubuti itakayoweza kukabiliana na mahitaji ya kuwa na mifumo imara ya majitaka kwa kiwango kikubwa, hasa katika maeneo korofii nchini ili kukabiliana na changamoto za kimazingira na kiafya zinazoweza kujitokeza kwa kushindwa kuwa na mifumo hiyo katika kipindi cha mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Taifa wa Usambazaji Maji (*National Water Supply Grid*); kumeanzishwa Mfumo wa Taifa wa Usambazaji Maji ambao umelenga kuhusisha utoaji wa maji katika vyanzo vya uhakika ikiwemo Maziwa Mkuu matatu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa ili kuyafikisha katika baadhi ya mikoa yenye uhaba wa maji ikiwemo Mikoa ya Singida na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ni mara nyingi Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiiasa Serikali juu ya utirishaji wa maji yenye *heavy metals* kama vile *cyanide* na zebaki kwenye

vyanzo vya mito inayomwaga maji ake hasa kwenye Ziwa Victoria lakini hatujawahi kupatiwa jibu kuhusianana jambo hio. Tukumbuke kuwa shughuli za wachimbaji wadogowadogo wa madini, hasa dhahabu zinazofanyika sana kwenye mito na maziwa pale mvua za masika zinapoanza, mabaki yote ya zabaki na *cyanide* yanelekea kwenye Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, unafuu wa ankara za maji kukabiliana na janga la kidunia la Corona; wakati huu ambao dunia nzima inapambana na janga kubwa la Virusi vya Corona (*COVID-19*) kumekuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya maji nchini, hasa ukizingatia kuwa kumekuwa na kampeni mbalimbali za kuwataka wananchi kutumia maji yanayotiririka kama nja mojawapo ya kukabiliana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, mamlaka mbalimbali duniani na Afrika zinajitahidi kuwaondolewa wananchi kadhia ya ukosefu wa maji safi na salama kuhakikisha kuwa kuna upatikanaji wa maji safi na salama muda wote. Baadhi ya Nchi zilizochukua hatua hiyo ni pamoja na Ghana, Kenya, Chad na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuchukua jukumu la kulipia ankara za maji kwa muda wote huu ambao tuko katika mapambano dhidi ya *COVID-19*.

Mheshimiwa Spika, hatua hii sio tu itaweza kuwaokoa wananchi bali pia itasaidia kuwapa wananchi ahueni ya kiuchumi na kwa maana nyepesi ambayo ilitolewa na aliyekuwa Rais wa Marekani Abraham Lincoln *Government of the People, for the People, by the people*.

Mheshimiwa Spika, na kwa kumalizia kwasababu ya muda naomba nijielekeze katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2020/2021. Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2020/2021 kwa asilimia kubwa ni mwendelezo wa miradi ambayo ilikuwepo na miaka yote tokea Awamu ya Nne ya Serikali ilipoanza lakini mpaka sasa haipatiwi fedha. Ni dhahiri kuwa Serikali imeendelea kuweka mipango ambayo haiwezi

kutekelezwa na kwa kuwa haina fedha za kutosha kuweza kuietekeleza unakuwa ni mwendelezo wa hila za Serikali dhidi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha nimalizie kwa kuitaka Serikali kujitafakari kwa kina ni kwa kiwango gani imeweza kutatua changamoto za maji nchini. Lakini vilevile niwatake Wheshimiwa Wabunge, hasa ambaao walitumia tatizo la uhaba wa maji katika majimbo yao kama kete ya kuombea kura kwa wananchi kujitafakari; je, ndani ya miaka mitano tumeweza kutatua kero za maji katika majimbo hayo?

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatakia Waislam wote mfungo mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani *Ramadan Kareem*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
MHESHIMIWA ZUBEDA HASSAN SAKURU (MB) KWA WIZARA
YA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2019/
2020 PAMOJA NA MPANGO WA MAENDELEO NA MAPATO
NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*)

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuweza kusimama mbele ya ukumbi huu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu hoja iliyo mbele ya Bunge letu.

2. Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe (Mb), ambae pia ni Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi Hai, kwa imani yake kwangu kuwa Msemaji Mkuu wa Wizara ya Maji.

3. Mheshimiwa Spika, kwa kipekee kabisa napenda kuchukua fursa hii kuwapa moyo Watanzania wote hasa viongozi na wanachama wenzangu pamoja na wanaharakati wanaokabiliwa na kesi za aina mbalimbali nchini katika mapambano ya kudai haki na demokrasia katika nchi yetu. Mapambano yanaendelea.

4. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi kuhusu Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021.

B. UMUHIMU WA MAJI

5. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa kwa ushirikiano wa Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), mabilioni ya watu duniani wanaendelea kutaabika kutokana na kukosa huduma bora za maji na masuala ya usafi. Takribani watu bilioni 2.2 duniani hawana maji safi na salama ya kunywa, watu bilioni 4.2 hawana huduma salama za usafi na watu bilioni 3 wanakosa huduma za msingi na sehemu za kunawa mikono. Vilevile inakadiriwa kuwa kati ya watu 10 mmoja hana huduma za msingi na watu milioni 144 hunywa maji yasiyo safi na salama. Na takwimu zinadhahirisha kwamba watu 8 kati ya 10 katika maeneo ya vijiji wanakosa huduma hizo muhimu.

6. Mheshimiwa Spika, hivyo ripoti hii imeweka wazi kuwa endapo nchi zitashindwa kuweka juhudhi katika masuala ya usafi, maji salama na huduma za kujisafi basi tutaendelea kuishi na maradhi ambayo kitambo yangekua yamebakii kuwa kumbukumbu za kihistoria. Hivyo, ni dhahiri kuwa 'MAJI NI UHAI'.

7. Mheshimiwa Spika, Maji ndio roho ya uchumi wa dunia, 19% ya matumizi ya maji ni kwa ajili ya viwanda na 70% zaidi ni katika matumizi ya mnyororo wa uzalishaji kwenye sekta ya kilimo. Hivyo basi kuna jukumu la msingi kuhakikisha malengo ya maendeleo endelevu (Sustainable Development Goals) kwenye sekta ya maji yanatekelezeka au yanatimizwa.

Kwa mwaka 2018 hasara ya kifedha iliyotokana na maji duniani ilikadiriwa kufikia dola za Kimarekani bilioni 36.¹

8. Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji safi na salama hupelekea kuwa na watu wenye afya bora ambacho ndio kichocheo cha ukuaji wa uchumi, vilevile afya bora inasaidia kuwepo kwa viwango bora vya elimu kwa wanafunzi. Takwimu zinaonesha kuwa upatikanaji wa maji safi na salama unaweza kuokoa kiasi cha takribani shilingi bilioni 521 kwa mwaka kwenye uchumi wa nchi. Au kuokoa tija yenye thamani ya 1% ya pato ghafi la Taifa ambayo ingepotea kutokana na magonjwa yanayosababishwa na matumizi ya maji yasiyo safi na salama.

9. Mheshimiwa Spika, takribani 60% ya Watanzania wanapata maji, lakini swali kubwa la kujuliza je, maji hayo ni safi na salama? Zaidi ya 50% ya Watanzania wanatumia zaidi ya dakika 30 kufuata maji. Na ikumbukwe kuwa wahanga wakubwa wa ukosefu wa maji safi na salama ni kina mama na watoto kwani hutumia muda mwingi na kutembea umbali mrefu kufuata maji ambayo pengine pamoja na upatikanaji wake bado si salama. Tumeshuhudia katika majiji makubwa ikiwemo Dar Es Salaam, upangaji wa foleni, kutembezwa maji katika madumu yasiyokidhi usafi ili kuweza kuhudumia familia zenye uhitaji wa maji. Hali ni mbaya kwa maeneo ya vijijini ambapo wananchi wameendelea kufuata maji kwa umbali mrefu, foleni zenye kuleta kero na fedhea ili kupata huduma muhimu ya maji ambayo bado tunatafsiri kuwa si safi na salama! Watanzania wengi wanalazimika kutumia takribani 5% ya matumizi yao kwenye maji kulinganisha na kiwango cha kimataifa cha 2%. Hii maana yake ni kwamba maji bado ni tatizo kubwa katika maisha ya Watanzania.

10. Mheshimiwa Spika, taarifa ya hali halisi ya sekta ya maji kama ilivyotolewa mwaka 2017 (National Environmental Status Report 2017) inaonesha kuwa kwa mwaka 2016, watu

¹ RIPOTI YA MAJI DUNIANI “Global Water Report 2018”

²Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET) March 2019,
Water Sector Equity Report 2019,

6 kati ya 10 ambaao ni sawa na 59.7 % wanapata maji kutoka kwenye vyanzo vya maji safi na salama. Lakini kwa maeneo ya mijini ni takribani watu 9 kati ya 10 wanapata maji ya kunywa kutoka vyanzo salama³.

11. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoainisha awali taarifa hii kwa nchi zinazoendelea makundi ambayo ni wahanga wakuu wa tatizo la maji ni wanawake na watoto.

12. Mheshimiwa Spika, Wanawake wamekuwa wahanga wakubwa katika tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama. Hii ni kutokana na shughuli nydingi za kifamilia zinazohitaji maji kama vile, matumizi ya maji katika uzalishaji na uandaaji wa vyakula, matumizi mahususi ya maji kwenye afya ya uzazi na kadhalika.

13. Mheshimiwa Spika, jambo ambalo halina ubishani wa aina yoyote ni kuwa wawanake ndio wanapoteza muda mrefu sana kwenda kutafuta maji hali inayodunisha vipato vyao pamoja na kuhatarisha ustawi wao.

14. Mheshimiwa Spika, Wanawake pia ndio wamekuwa wahanga wakubwa kwa matukio ya udhalilishaji na ukatili kama vile ubakaji na kesi nyininge nydingi za kudhuru mwili wanazokumbana nazo wakiwa katika safari za kutafuta maji⁴. Pia kuna ushahidi wa kutosha kuwa ndoa nydingi zimevunjika kutokana na changamoto za maji, hivyo inatosha kusema kampeni ya *kumtua mwanamke ndoo kichwani imeshindwa*.

15. Mheshimiwa Spika, ukosefu wa kipaumbele na umakini katika kutatua changamoto za sekta ya maji nichini unaweka rehani ustawi wa sekta muhimu zinazotegemea maji kama chanzo hasa sekta ya uzalishaji, umwagiliaji na kilimo, viwanda na nishati ya umeme. Bila kuwa na vyanzo vya uhakika vya maji hasa katika kipindi hiki tunapokabiliana na

³Sectors Ministers' meeting 2019, San Jose' –Costa Roca 4-5 April, Tanzania Country Report.

⁴ Chama cha Demokrasia na Maendeleo(Chadema), Sera ya Wanawake - Machi 2020

mabadiliko ya tabianchi ni dhahiri kuwa kama nchi hatutaweza kufanikisha lengo lolote la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kwa sababu maji yanagusa kila lengo na mfumo mzima wa maisha ya binadamu.

C. MAHITAJI NA MATUMIZI YA MAJI

16. Mheshimiwa Spika, Hivi sasa matumizi ya maji hapa nchini kwa sekta mbalimbali za huduma na uzalishaji yanakadiriwa kufikia mita za ujazo 40. Takwimu zinaonesha kuwa kiasi cha maji kwa mtu kwa mwaka kimeendelea kupungua kutoka wastani wa mita za ujazo 7,862 mwaka 1962 wakati nchi ikiwa na idadi ya watu milioni 10.6 hadi kufikia wastani wa mita za ujazo 2,250 mwaka 2018 nchi ikiwa na idadi ya watu wapatao milioni 56⁵. Jambo hili linasababisha nchi yetu kuwa juu ya mstari wa uhaba wa maji dunia (water stress). Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji je, ni mikakati gani endelevu ya utunzaji wa vyanzo vya maji imewekwa na Serikali nchini?

17. Mheshimiwa Spika, Sekta ya maji ina muongozo wake juu ya matumizi na namna gani ya kuendeleza sekta hiyo chini ya programu ya maendeleo ya maji ya mwaka 2006 - 2025 (Water Sector Development Programme 2006 - 2025). Programu hii ni jumuiko la Sera ya Taifa ya Maji-NAWAPO ya mwaka 2002 pamoja na mkakati wa Taifa wa kuendeleza sekta ya maji wa mwaka 2006 (National Water Sector Development Strategy – NWSDS, 2006). Programu ilikuja kama utekelezaji wa mkakati na sera ya maji ili kukidhi malengo ya MKUKUTA kwenye sekta ya maji.

18. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa fedha zilizotumia kutekeleza awamu ya kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Maji (WSDP Phase I (2007-2015) takwimu zinaonesha kuwa zilitumia bilioni 1.6 za Kimarekani wakati sekta ilihitaji takribani bilioni 3.33 za Kimarekani kuondoa kabisa mapungufu katika kupanga utekelezaji wa awamu ya II ya WSSD ambayo ilitakiwa kutekelezwa hadi mwaka 2021. Kati ya kiasi hicho Serikali na wadau tayari walikuwa na kiasi cha bilioni 1.93 za

⁵RANDAMA YA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA 2020/21- Machi 2020

Kimarekani na hivyo kuwepo na upungufu wa bilioni 1.4 za Kimarekani ambacho kinefidiwa kwa ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi⁶.

19. Mheshimiwa Spika, Katika Randama ya Wizara inaonesha kuwa Wizara imepanga kufanikisha malengo ya muda wa kati kwa kuhakikisha kuwa makundi yote ya jamii yanapata huduma inayoridhisha ya maji safi na usafi wa mazingira kwa kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo kufikia asilimia 85 kwa wakazi wa vijijini na kufikia asilimia 95 kwa maeneo ya **mijini ifikapo 2020**; lakini katika taarifa ya Mkutano wa Mawaziri wa Sekta ya Maji, inaonesha kuwa **ifikapo mwaka 2025** upatikanaji wa maji safi na salama kwa vijijini utafikia 95%; makao makuu ya mikoa na Jiji la Dar es Salaam itafikia 100%. Uwiano kwa nyumba za vijijini ambazo zitakuwa na huduma bora za usafi wa maji kwa 85%; makao makuu ya mikoa na wilaya 70% na Dar es Salaam 60%.

20. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na TWaweza⁷ ulibaini changamoto kuu tatu katika upatikanaji wa maji vijijini ambazo ni umbali wa vyanzo vya maji, uhaba wa vyanzo vya maji na maji machafu. Tunapofikia ukomo wa miaka mitano ya awamu ya tano ambayo ni mwaka 2020, je, ni kweli Serikali imeweza kufikia asilimia 85 kwa vijijini na asilimia 95 kwa mijini kama ilivyoahidi pia katika ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2015 au bado tunaendelea na hekaya za abunuwas?

21. Mheshimiwa Spika, Tumefanya nukuu ya takwimu za matumizi ya fedha za awamu ya kwanza ya WSDP kwa lengo kuonesha wingi wa fedha ambao tayari umetumika, lakini ukweli na hali halisi ni kuwa tija yake ni ndogo na hajitatua changamoto katika kuhakikisha kila Mtanzania anapata maji safi na salama. Hili linatokana na usiri unaogubika kuanzia mradi wenyewe, gharama zake na utoaji wa zabuni kwa

⁶Sector Ministers' Meeting 2019, San Jose' –Costa Rica 4-5 April

⁷ Safi na salama? maji, usafi na Afya Mazingira (2017)

mkandarasi. Je, wananchi walishirikishwaje katika kuhakikisha nao wanakuwa sehemu ya miradi hiyo ya maji? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoweke mazingira ya usiri, ubabaishaji katika kutekeleza miradi ambayo inalenga kuwapa wananchi maji safi na salama.

D. MFUMO WA MAJI TAKA

22. Mheshimiwa Spika, Ni bahati mbaya sana kuwa Serikali imeshindwa kuwekeza nya kutosha katika kukabiliana na tatizo la majitaka nchini hali inayopelekea mifumo ya maji taka kuingiliana kwa kiasi kikubwa na mifumo ya maji safi na hivyo kuhatarisha afya na mazingira kwa ujumla hasa kwa mijji mikubwa.

23. Mheshimiwa Spika, Ni ajabu kuona mpaka sasa, Serikali imeweka lengo la kuwa na mifumo ya majitaka katika mijji na makao makuu ya mikoa kufikia asilimia 30 tu iflikapo mwaka 2025. Hii inatoa taswira kuwa, Serikali haina mpango wa kuhakikisha usalama wa watumiaji wa maji kwa asilimia 70 kufikia mwaka 2025. Hivyo bado kuna hatari kubwa kwa maeneo yanayoendelea kuwa na mvua kubwa kukumbwa na mafuriko kwa kuwa miundombinu ya sehemu hizo itaendelea kuelemewa na maji taka yanayotokana na kutapishwa kwa vyoo na kufanya tatizo hilo kuzaa matatizo mengine ikiwemo matatizo ya kiafya.

24. Mheshimiwa Spika, Aidha, tafiti zilizofanywa na TAWASANET (*“no one left behind”*) zinaonesha kuwa 35% ya vyanzo nya maji katika maeneo mengi ya Dar Es Salaam na 52% kwa maeneo ya Mkoa wa Morogoro yalionesha uwepo wa mchanganyiko wa “vinyesi” katika mifumo ya maji yanayotumiwa na wananchi. Hii ina maana kuwa kuna hatari kubwa ya magonjwa ya milipuko hasa kwenye vipindi nya masika.

25. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Dar Es Salaam 57% ya kinyesi (vyoo nya shimo) kinaingia kwenye mfumo wa mazingira bila kuwekewa dawa ya aina yoyote na ujazo wa 2164m^3 ya maji taka yasiyotiwa dawa unaingia kwenye mfumo wa maji ya Dar Es Salaam kila siku. Kwa takwimu hizo

za kutisha zinachangia kuongezeka kwa gharama za kukabiliana na magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo safi na salama. Toka Agosti mwaka 2015 nchi imeshuhudia wagonjwa 33,421 na vifo 542 kutokana na kipindupindu.

26. Mheshimiwa Spika, Inabashiriwa kuwa janga kubwa la mafuriko hasa kwa mijini linaweza kuchangia takribani anguko la 2% ya GDP kutokana na mabadiliko ya tabianchi tufikapo mwaka 2030. Hivyo, kutokuwa na mifumo mizuri ya majitaka kuna athari kubwa katika maisha ya jamii ya kila siku kwa kuwa majitaka yamekuwa kero kubwa kwa biashara kama yadi, mama ntilie, masoko, matumizi ya barabara na hata kuleta athari kubwa kwenye mazingira ya shule ambapo wanafunzi huathiriwa na uchafuzi wa mazingira unaotokana na mifumo duni ya majitaka⁸.

27. Mheshimiwa Spika, Takwimu za randama zinaonesha kuwa tangu tupate uhuru hadi Desemba mwaka 2018 kaya ambazo zilikuwa zimeunganishwa katika mifumo wa majitaka nchini ni 48,566 tu na kufikia Desemba 2019 zikaongezeka kaya 1842 na hivyo kufanya jumla kuwa kaya 50,408.

28. Mheshimiwa Spika, Kaya hizo zipo katika miji 10 tu ambayo ndiyo yenye mitandao ya majitaka. Maana yake ni kwamba itatuchukua tena miaka hamsini kuweza kuweka mtandao wa majitaka nchi nzima.

29. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuititia Wizara ya Maji kuweka mkakati madhubuti utakaokabiliana na mahitaji ya kuwa na mifumo imara ya majitaka kwa kiwango kikubwa hasa katika maeneo korofi nchini ili kukabiliana na changamoto za kimazingira na kiafya zinatojitokeza kwa kushindwa kuwa na mifumo hiyo hasa katika kipindi hichi cha mabadiliko ya tabia nchi.

⁸Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET) March 2019,
Water Sector Equity Report 2019

E. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

30. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara iliomba na kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 610.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 349.4 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi bilioni 261.0 zilikuwa ni fedha za nje. Hadi Februari 2020, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 312.7 sawa na asilimia 51.2 ya fedha zote za miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani zilizokuwa zimetolewa ni shilingi bilioni 151.3 sawa na 43% tu na fedha za nje shilingi 161.5 sawa na 57%. Hii inaonesha kuwa Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kategemea fedha za wahisani na kushindwa kuhudimia sekta ya maji ambayo ndio sekta ya muhimu kwa fedha zake za ndani na hivyo kuendeleza utegemezi wa bajeti kwa wahisani.

31. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa muda mrefu imeendelea kuwa na miradi ambayo imeshindwa kuisimamia kikamilifu ili iweze kukamilika na kuwa na tija kwa muda wa miaka minane mfululizo ikiwemo mradi wa Bwawa la Kidunda na wa Visima vya Mpera na Kimbiji. Madhara yake ni kwamba ghamama zinazidi kuongezeka kila kukicha kutokana na ukweli kwamba thamani ya shilingi yetu dhidi ya dola ya Kimarekani inazidi kuporomoka. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kukamilisha miradi hii ambayo imeendela kuwa kiporo kabla ya kuanzisha miradi mingine ili kuongeza ufanisi, tija na kutimiza ahadi zake kwa wananchi.

32. Mheshimiwa Spika, Kwa mradi wa Bwawa la Kidunda ambao ungesambaza maji kwa Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Pwani ni mradi ambao ungeweza kupunguza madhara ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa maeneo mengi ya Mkoa wa Morogoro ambao tumeona ni jinsi gani wananchi wa kata nydingi za vijijini wanavyopata taabu sana na upatikanaji wa maji safi na salama.

33. Mheshimiwa Spika, kuna mradi ambao pia ulikuwa katika mpango wa kwanza wa maendeleo wa miaka mitano wa kuboresha upatikanaji wa maji katika miji ya Same na

Mwanga ambao ulikuwa umetengewa jumla ya shilingi 29,281,000,000.00. Lakini hadi mwezi Februari zilikuwa zimetolewa jumla ya shilingi 2,135,860,946.18 sawa na 7.3% ya fedha zilizombwa na kuidhinishwa na Bunge.

34. Mheshimiwa Spika, pia kuna mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Shinyanga/Kahama hadi Tabora wa shilingi 23,500,000,000.00; hakuna hata shilingi iliyotolewa na tukumbuke kuwa wakandarasi wako site. Jambo hili linazidisha gharama za mradi. Aidha, kuna mradi wa Ziwa Victoria, Shinyanga hadi Kahama wa shilingi 23,810,000,000.00 hadi Februari zimetolewa shilingi 3,332,861,207.50 tu sawa na 13.99%.

35. Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Masasi/Nachingwea ulioihinshiwa kiasi cha shilingi 1,500,000,000.00 lakini hadi kufikia mwezi Februari 2020, hakuna hata shillingi iliyotolewa kwa ajili ya mradi huo. Ni dhahiri kuwa Serikali imeshindwa kutekeleza majukumu yake kwa kushindwa kuwa na vipaumbele vya msingi hususani katika kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama.

36. Mheshimiwa Spika, Sambamba na hilo la kutokutolewa fedha za miradi ya muda mrefu ya upatikanaji wa maji safi na salama, Randama inaonesha kuwa zilitolewa jumla ya shilingi 5,909,000,000.00 kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Mamlaka za Maji Mijini ili kutekeleza programu ya WSDP.

F. MFUMO WA TAIFA WA USAMBAZI MAJI (NATIONAL WATER SUPPLY GRID)

37. Mheshimiwa Spika, Kuwepo kwa mfumo wa Taifa wa Usambazi Maji umelenga kuhusisha utoaji wa maji katika vyanzo vya uhakika vya maji ikiwemo maziwa makuu matatu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa na kuyafikisha katika mikoa yenye uhaba wa maji ikiwemo Mikoa ya Singida na Dodoma.

38. Mheshimiwa Spika, Ni mara nyingi tumekuwa tukiiasa Serikali juu ya utiririshaji wa maji yenye **heavy metals** kama

vile **cyanide** na **mercury** kwenye vyanzo vya mito inayomwaga maji yake hasa kwenye Ziwa Victoria, lakini hatujawahi kupatiwa jibu kuhusiana na jambo hilo. Tukumbuke kuwa shughuli za wachimbaji wadogo wadogo wa madini hasa dhahabu zinafanyika sana kwenye mito na pale mvua za masika zinapoanza, mabaki yote ya mercury na cyanide yanaelekea kwenye Ziwa Victoria. Kwa maneno mengine mfumo huo wa usambazaji wa maji wa Taifa usiposimamiwa kikamilifu ikiwemo kuyatibu maji hayo ipasavyo basi itakua ndio chanzo kikuu cha ugonjwa wa kansa kwa Watanzania.

G. USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA RASILIMALI ZA MAJI

39. Mheshimiwa Spika, Kati ya kiasi cha maji cha mita za ujazo bilioni 126 zinazokadiriwa kupatikana hapa nchini kwa mwaka, asilimia 43.4⁹ ya maji hayo yapo katika vyanzo vya majishirikishi. Vyanzo hivyo vipo katika mabonde saba kati ya tisa yaliyopo nchini ambavyo ni Maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa, Natron, Chala na Jipe pamoja na Mito ya Kagera, Mara, Malagarasi, Momba, Mwiruzi, Umba, Ruvuma na Songwe. Usimamizi wa rasilimali za majishirikishi unafanyika kuititia Taasisi za Kikanda na Kimataifa zilizoundwa kwa ushirikiano wa nchi wanachama. Tanzania ni mwanachama katika Taasisi zifuatazo: Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika, Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (Zambezi Watercourse Commission - ZAMCOM); Taasisi ya Mpito ya Bonde la Mto Nile (Nile Basin Initiative - NBI); Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe; Mamlaka ya Usimamizi wa Bonde la Ziwa Tanganyika (Lake Tanganyika Authority – LTA); na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria.

40. Mheshimiwa Spika, Kutokana na ushirikiano huo wa maji, ghamama za usimamizi na uendelezaji wa kamisheni hizo nazo zinakuwa ni shirikishi, jambo hilo linatoa unafuu mkubwa kwa Tanzania. Na ukweli ni kuwa majirani zetu wao wanathamini sana sekta hii ya maji hivyo wanafanya juhudu kubwa kuhakikisha kunakuwepo na uendelevu wa kamisheni hizo za usimamizi wa mabonde hayo.

⁹ Randama ya wizara ya maji 2020/21 uk.22

41. Mheshimiwa Spika, Ni muhimu sana kuwepo kwa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji hapa nchini, lakini rasilimali za maji ambazo zimezoleka kwa wengi ni zile ambazo ziko juu ya ardhi. Taktamu zinaonesha kuwa na wastani wa **mita za ujazo bilioni 105¹⁰**, na **mita za ujazo bilioni 21** chini ya ardhi.

42. Mheshimiwa Spika, Mojawapo ya sababu zinazoongeza ukiritimba mkubwa katika matumizi ya rasilimali maji iliyo chini ya ardhi, Serikali inasema kwamba; *Udhhibit wa uchimbaji holela wa visima udhibiti wa uchimbaji holela wa visima umeendelea kwa kuratibu na kusajili kampuni za utafiti na uchimbaji wa visima pamoja na kutoa leseni na vibali vya uchimbaji kwa makampuni yanayokidhi vigezo. Aidha elimu imeendelea kutolewa kwa wananchi wanapotaka kuchimbiwa visima waombe vibali vya kuchimba visima kutoka katika Bodi za Maji za Mabonde. Vibali hivyo vinawawezesha kulindwa kisheria na kupata taarifa sahihi za uwepo wa maji na ubora wake katika maeneo yao kabla hawajachimba. Hadi mwezi Februari 2020, leseni mpya 52 za utafiti na uchimbaji wa visima na vibali 225 vya kuchimba visima vya maji katika maeneo mbalimbali nchini vimetolewa.*

43. Mheshimiwa Spika, maana yake ni kuwa hata wale ambaao wanahitaji kuwekeza kwenye kilimo hawataweza kuchimba visima kwa ajili ya kuendeleza kilimo kulingana na aina ya mazao anayolima. Hii ni changamoto kubwa kwa kuwa kwani jambo hili limekuwa la jumla mno na pia linaweza kuleta migogoro mkubwa pale mkulima anapotoa fedha kwa ajili ya kuchimbiwa kisima na matokeo yake inakuwa kama ile miradi ya visima kumi kila wilaya, ambavyo hadi leo havitoi maji na hiyo hasara ilikwenda kwa walipa kodi.

44. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka mfumo madhubuti na imara wa uratibu kwenye matumizi ya rasilimali ya maji yaliyo ardhini chini ya Idara ya Umwagiliaji na sio kuhusisha makampuni binafsi ya wafanyabiashara.

¹⁰ Randama ya Wizara 2020/21 uk.9

H. UNAFUU WA ANKARA ZA MAJI KUKABILIANA NA JANGA LA KIDUNIA LA KORONA

45. Mheshimiwa Spika, Wakati huu ambao dunia nzima inapambana na janga kubwa la Virusi vya Korona yaani COVID-19, kumekua na ongezeko kubwa la matumizi ya maji nchini hasa ukizingatia kuwa kumekuwa na kampeni mbalimbali za kuwataka wananchi kutumia maji yanayotiririka kama njia mojawapo ya kukabiliana na ugonjwa huu.

46. Mheshimiwa Spika, Mamlaka mbalimbali duniani na Afrika, zimechukua hatua zaidi kwa kuwaondolea wananchi kadhia za ukosefu wa maji safi na salama kwa kuhakikisha kuwa kuna upatikanaji wa maji safi na salama muda wote. Baadhi ya nchi zilizochukua hatua hizo ni pamoja na Ghana, Kenya na Chad. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuziagiza mamlaka za maji nchi kutokata maji kwa wadalwa wa maji kwa kipindi hiki pamoja na kuchukua jukumu la kulipia ankara za maji kwa wananchi wote kwa kipindi cha miezi sita toka kampeni za kujikinga kwa kunawa zilipoanza yaani mwezi Machi, 2020.

47. Mheshimiwa Spika, Hatua hii si tu itaweza kuwaokoa wananchi, bali itasaidia kuwapa wananchi ahueni ya kiuchumi. Kuna maana nyepesi ya Serikali iliyotolewa na aliywahi kuwa Rais wa Marekani, Abraham Lincoln '*government of the people, by the people, for the people'* yaani "*Serikali ya watu, kutokana na watu kwa ajili ya watu.*" Serikali haiwezi kuwa Serikali ya watu iwapo itashindwa kutoa ahueni kwa watu wake ili kuwaokoa na janga hili la korona kwa kutoa msamaha wa ankara katika kipindi hichi kigumu.

I. MAPITIO YA BAJETI KWA MIRADI MAENDELEO YA MAJI KUANZIA 2015/2016 HADII 2018/2019

48. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara ya Maji na Umwagiliaji Fungu 49 na Fungu 05 iliidhinishiwa jumla ya shilingi **bilionti 565.9**. Fungu 49 iliidhinishiwa jumla ya shilingi **bilionti 512.5** kati ya fedha hizo shilingi **bilionti 27** ni fedha za matumizi ya kawaida (fedha hizi zinajumuisha mishahara shilingi **bilionti 18** na matumizi

mengineyo shilingi bilioni 9. Na kiasi cha **shilingi bilioni 485.3** zilitengwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

49. Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 Fungu 49 lilikuwa limepokea fedha za maendeleo **shilingi bilioni 137** tu kati ya **shilingi bilioni 485.3** zilizotengwa ambazo ni sawa na asilimia 28 ya bajeti yote ya maendeleo.

50. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Fungu 49 likiidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 938.3**. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 913.8** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

51. Mheshimiwa Spika, lakini hadi mwaka huo wa 2016/2017 unamalizika Wizara Fungu 49 ilipokea fedha za **maendeleo jumla ya shilingi bilioni 231**. tu sawa na **asilimia 25.7** ya bajeti yote ya maendeleo.

52. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Fungu 49 liliidhinishiwa na Bunge fedha za maendeleoz jumla ya **shilingi bilioni 624**. Lakini hadi mwezi Machi, 2018 fedha za maendeleo zilizokuwa zimepokelewa ni **shilingi bilioni 135.2** sawa na asilimia 22 ya fedha zote za bajeti ya maendeleo kwa Wizara ya Maji-Fungu 49.

53. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019 Bunge lilinaombwa kuidhinisha fedha za miradi ya maendeleo yenye jumla ya **shilingi bilioni 673.2** kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 443.2** sawa na asilimia 66 zilikuwa ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 230** sawa na asilimia 34 zilikuwa ni fedha za nje.

54. Mheshimiwa Spika, Hadi mwezi Februari 2019 jumla ya **shilingi bilioni 100.1** sawa na 15% ndizo zilizokuwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 95.3** sawa na asilimia 22 ya fedha za ndani. Fedha za nje zilizotolewa ni **shilingi bilioni 4.7** tu sawa na asilimia 2.06 ya fedha za nje. Takwimu hizi zinaonesha kuwa fedha za maendeleo zinazotolewa zinakuwa zikipungua kila mwaka hii ni dhahiri kuwa maji sio kipaumbele kwa Serikali ya CCM.

55. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2019/20 Wizara iliomba fedha za maendeleo jumla ya **shilingi bilioni 610.5** au 610,469,888,530.00 kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 349.45** au 349,449,000,000.00 ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 261.021** au 261,020,888,530 ni fedha za nje. Bajeti ya maendeleo ilikuwa ni pungufu kulinganisha na ile ya mwaka 2018/2019 kwa **shilingi bilioni 62.7** au 62,744,145,147.00 sawa na asilimia 9.32

56. Mheshimiwa Spika, Hadi mwezi Februari, 2020 fedha za maendeleo za ndani zilizokuwa zimetolewa ni shilingi 151,284,580,290.00 sawa na 43.29% tu, ya fedha za ndani zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge na fedha za nje zilizokuwa zimetolewa hadi Februari 2020 ni shilingi 161,485,277,389.00 sawa na 61.9% ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Hii maana yake ni kuwa Serikali imeshindwa hata kufikisha asilimia 50 ya fedha zake za ndani katika kutekeleza miradi ya maendeleo huku fedha za wahisani zikivuka asilimia 50 katika miradi ya maendeleo. Hii inaonesha kuwa kuna utegemezi mkubwa wa fedha za wahisani katika miradi ya maendeleo na Serikali imeshindwa kuipa sekta ya maji kipaumbele kinachostahili.

57. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, fedha zinazombwa kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni shilingi 697,085,149,000 kupitia Fungu 49 (Wizara ya Maji). Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi 349,449,000,000 sawa na asilimia 50.1 ni fedha za ndani na shilingi 347,636,149,000 sawa na asilimia 49.9 ni fedha za nje.

58. Mheshimiwa Spika, ukifanya ulinganisho wa fedha zinazombwa mwaka 2020/2021 kiasi cha shilingi 697,085,149,000.00 na zile zilizoidhinishwa mwaka 2019/2020 shilingi 610,569,888,530.00 kunatofauti ya jumla ya shilingi 86,515,260,470.00. Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2019/2020 haukufikia asilimia 55, sasa inawezaje kuongeza bajeti kwa kiasi hicho na wakati huu duniani kumekuwa na anguko kubwa la uchumi kutookana na janga la Korona na hivyo kuathiri makusanyo yetu ya kodi kuliko miaka yote?

J. MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2020/21

59. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa asilimia kubwa ni muendelezo wa miradi ya ambayo ilikuwepo na miaka yote tokea awamu ya nne ya Serikali ilikwishaanza lakini imekuwa haipatiwi fedha.

60. Mheshimiwa Spika, Miradi ambayo kwa bajeti inayomalizika hakuna fedha iliyotengwa lakini mwaka huu zimetengwa fedha zile zile au zimeongezwa ni kama ifuatavyo; Mradi wa Maji wa Masasi Nachingwea, ulikuwa umetengewa jumla ya shilingi 1,500,000,000.00 sasa kwa mwaka 2020/2021 umetengewa jumla ya shilingi 2,000,000,000.00; Mradi wa Maji toka Ziwa Victoria kwenda Kahama na Shinyanga ulikuwa na shilingi 23,810,000,000. Zikatolewa shilingi 3,332,681,207.50 tu, sasa umetengewa shillingi 26,491,000,000.00; ujenzi wa Bwawa la Kidunda mwaka jana ziliidhinishwa jumla ya shilingi 3,000,000,000.00 lakini haikutolewa hata senti moja, mwaka huu wa fedha zimetengwa tena shilingi 3,000,000,000.00; uchimbaji wa Visima vyta Mpera na Kimbiji zilikuwa zimeidhinishwa jumla ya shilingi 3,000,000,000.00 lakini hakuna hata senti moja iliyotolewa, mwaka 2020/2021 zimeombwa tena shilingi 3,000,000,000.00; kuboresha upatikanaji wa maji katika miji ya Mwanga na Same zilikuwa zimeidhinishwa shilingi 29,281,000,000; zikatolewa shilingi 2,135,860,946.10 tu. Mwaka huu wa fedha zinaombwa shilingi 29,200,000,000.00. Sasa hii ni mifano tu na tukumbuke mazingira ya upatikanaji wa fedha za kodi kwa mwaka huu yatakuwa ni magumu sana kutokana na hali halisi ya maambukizi ya ugonjwa wa Corona ulivyo athiri biashara nydingi hapa nchini.

61. Mheshimiwa Spika, Ni dhahiri kuwa Serikali imeendelea kuweka mipango ambayo haiwezi kutekelezwa kwa kuwa haina fedha za kutosha kuweza kuitekeleza. Huu unakuwa ni muendelezo wa hila za Serikali kwa wananchi.

K. HITIMISHO

62. Mheshimiwa Spika, Nimalizie kwa kuitaka Serikali kujitafakari kwa kina ni kwa kiwango gani imeweza kutatua

changamoto za maji nchini hasa kwa kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata maji safi na salama. Lakini kwa kuwataka Waheshimiwa Wabunge hasa ambao walitumia tatizo la uhaba wa maji katika majimbo yao kama kete ya kuombea kura kwa wananchi, je, ndani ya miaka mitano ya awamu ya tano wameweza kutatua kero ya maji katika majimbo yao? Je, mwanamke ametuliwa ndoo ya maji kama kaulimbiu illivyokuwa inataka? Tunaporudi kuomba kura kwa mara nyingine..... mjiulize, tulipowaahidi kuwatatulia changamoto ya maji, tulitekeleza ama ndio yatakua yale yale ya Mfalme Juha na watu wake?

63. Mheshimiwa Spika, napenda kuwatakia Waislam wote Mfungo Mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, Ramadhan Kareem.

64. Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Zubeda Hassan Sakuru (MB)
**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-WIZARA YA
MAJI**
27.04.2020

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sakuru kwa kuwasilisha mawazo hayo ya upande wa Upinzani Bungeni, asilimia za TAWASANET hatari kwelikweli.

Tunaendelea na uchangiaji sasa, kama nilivyokwishesasema awali, tunaanza na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya na atafuata Mheshimiwa Edwin Sannda ambaye yuko kule Msekwa. Mheshimiwa Leah Komanya.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yangu. Lakini nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu katika kipindi changu chote cha miaka mitano nilichokuwa hapa Bungeni ameniwezesha nimeweza kuwawakilisha wanawake wa Mkoa wa Simiyu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nianze na kumpongeza Waziri wa Maji pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanazozifanya za kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maji. Kupitia Kamati yangu nimeona yapo mabadiliko katika matumizi ya fedha kwa kuwa miradi sasa inatekelezwa kama ilivyokusudiwa. Kwa dhati ya moyo wangu nampongeza Waziri kwa hatua mbalimbali alizochukua ikiwemo kudhibiti bajeti ambazo zilikuwa zinatolewa za ajabuajabu katika kutekeleza miradi ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee nishukuru kwa ajili ya Mkoa wa Simiyu; tumeweza kutekelezewa miradi mbalimbali ya maji katika maeno tofauti, mpaka sasa miradi hiyo imekamilika na inatoa maji. Kwa mfano nikiongelea Mradi wa Maji Lamadi uliogharimu shilingi bilioni 12.8, mradi huu umeombwa katika awamu hii na umetekelizwa ukakamilika katika awamu hii, kwa hiyo, maji yanatoka kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini katika mkoa wetu tumepokea shilingi bilioni 10.2 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji, kwa sasa hivi mkoa unatekelezwa miradi 43 ambayo iko katika hatua mbalimbali. Kwa hiyo, niendelee kuishukuru Serikali kwa kuuona Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee nishukuru kwa ajili ya mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria na kuyasambaza katika Mkoa mzima wa Simiyu, mradi huu ambao umekusudia kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi. Niungane na hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba tayari tumeshapata mfadhili wa maji ambao utagharimu euro milioni 171 ikiwemo Serikali ya Tanzania inachangia euro milioni 40 na nguvu za wananchi euro milioni 1.5, na hatua za mradi huo zinaendelea ikiwemo tathmini kwa ajili ya fidia kwa wananchi, ikiwemo tangazo la kumpata mkandarasi mshauri.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali; ninaomba kwa kuwa rasimu ya fidia ya wananchi imeshafikishwa Wizarani, tathmini hiyo ifanyike vizuri ili isiwepo mwananchi ye yote ambaye atapunjwa au hatalipwa fedha hiyo. Maana

yake ipo tabia baadhi wanalipwa au baadhi wasilipwe. Ili mradi wetu uweze kutekelezwa bila kero yoyote kutoka kwa mwananchi. Kutokana kwamba kama mambo yatakwenda vizuri tunatakiwa kuanzia Januari, 2021 tuwe tumempata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, lakini changamoto ninayoionna ni katika kumpata mkandarasi mshauri ambaye tangazo lake la siku 60 tayari limeshatoka tuweze kumpata. Najua huwa kuna taratibu nyingi, ninaomba Serikali sasa ichukue hatua za dhati ili mkandarasi mshauri aweze kupatikana, tukizingata toka tunaingia kwenye Bunge hili 2016, mradi huo umeweza ukitajwa kila wakati kwamba unatekelezwa na mpaka leo 2020 ndiyo sasa tumepata mkandarasi. Ninaamini Serikali yangu sikivu itachukua hatua za dhati.

Mheshimiwa Spika, lakini awamu ya kwanza inaanzia Wilaya za Busega, Bariadi na Itlima ambapo itabaki Wilaya za Maswa na Meatu na wilaya hizi mbili ndizo hasa zilizoathiriwa kabisa na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mfano nikiongelea Wilaya ya Meatu; wilaya hii inaongoza kwa athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi. Serikali inatuletea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji lakini tunashindwa kutokana na vyanzo hafifu vya maji kwa sababu vyanzo vyetu vingi visima vikichimbwa maji yanakuwa ni ya chumvi, kwa hiyo tuna uhaba wa vyanzo vya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwishoni mwa mwezi Oktoba mwaka jana, Mji wa Mwanuzi ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Meatu ulikumbwa na kadhia ya ukosefu wa maji ambapo Bwawa tunalolitegemea na Mwanyainai lilitauka. Lakini kuititia vyombo vya habari, *TBC*, nimshukuru Rais wetu alichukua maamuzi ya haraka alimtuma Waziri wa Maji akafika mara moja na wataalam wake lakini pia tukiwa tumepeva visima kumi vya maji ili kuweza kukabiliana na upungufu wa Bwawa la Mwanyaina.

Mheshimiwa Spika, bwawa hilo mvua ilipokuja, mvua moja tu ililijaza bwawa. Kwa maana hiyo kabla hata ya mwezi wa kumi mwaka huu mji wetu pia hautakuwa na maji.

Nichukue ombi langu kwa Serikali basi ifanye jitihada tuweze kupata hata kisima kimoja ambacho kitasaidiana na Bwawa lile la Maji la Mwanyainia.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa wakati huohuo, ule mpango wetu wa wilaya wa kwamba tunatoa chanzo katika Mto Semu ambao mto huo una mchanga mwingu uendelee kutekelezwa. Serikali isiuache kwasababu ndiyo tunautegemea na tayari wataalam wetu wamefanya makadirio kutoka fedha ya mkandarasi hadi kutumia *force account*, kutoka bilioni moja mpaka milioni 800. Naomba Serikali iridhie, isitoe fedha hizo ili tuweze ku-rescue situation ambayo tunategemea mwezi Oktoba tutaiona. Na wewe unajua mwezi Oktoba kuna nini. Chondechonde tunusuru wananchi wa Wilaya ya Meatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia Waziri alipokuja aliona uwezekano wa kukarabati lile Bwawa la Mwanyainia. Ni muombe, badala ya kutoa tope ashirikiane na wataalam waliopo Meatu tufanye kama walivyofanya Maswa, walilongezea tuta ule usawa wa tope likawa kama ndiyo *base*. Kwa hiyo, pia tuna uhakika na yale maji kwa kuwa mradi wa Ziwa Victoria hautafika leo au kesho katika Wilaya ya Meatu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Busega kabla ya Kiloleli kuna mradi uliogharimu bilioni 1.6 ambayo Mheshimiwa Makamu wa Rais aliuzindua mwezi Februari mwaka jana, lakini toka alipouzindua ule mradi haujaendelea na hatua yoyote. Tunaomba Serikali basi kwa kuwa chanzo ni Ziwa Victoria na tenki limeshajengwa, ilete fedha kwa ajii ya kusambaza maji katika Mji wa Kiloleli.

Mheshimiwa Spika, na wakati huohuo Makamu wa Rais aliweka jiwe la msingi katika Bwawa la Mwanjolo lililopo Wilaya ya Meatu. Lakini kutokana na tathmini...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Leah Komanya.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa tunakwenda Msekwa ambako yuko Mheshimiwa Edwin Sannda.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie fursa hii adhimu kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehemu leo tuko tena hapa tukiwa na afya njema, na akiendelea kutunusuru na ugonjwa huu hatari wa Corona basi pia na sisi tuendelee kuzingatia yale yote ambayo tunaendelea kuelekezwa katika kujihadhari na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, lakini pili nimshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na timu yake kwa kazi nzuri sana ambayo wanaendelea kufanya ya maendeleo kwa Watanzania kupitia Serikali yake ya Awamu ya Tano, tunakwenda vizuri sana. Kwa kweli tunamshukuru na kumpa pongezi nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, na tatu nikushukuru wewe mwenyewe pamoja na wasaidizi wako; Naibu Spika, Wenyeviti na wengine wote kwa jinsi ambavyo tumeendelea kufanya kazi vizuri kama Bunge, kama mhimili na tumeendelea kuwatendea haki Watanzania kupitia mhimili wetu huu; nakupongeza sana Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Prof. Mbarawa kwa hotuba yake nzuri, yeye pamoja na timu yake yote wamefanya kazi nzuri, wameendelea kufanya kazi nzuri kwa kipindi chote hicho; tunakupongeza sana, tunatambua jitihada nyingine zinahitajika , maendeleo bado ni safari ndefu; tumepeiga hatua lakini tunastahili kuendelea kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Wabunge wenzangu lakini pia pamoja na wananchi wa Kondoaa ambao siku zote wameendelea kutupa ushirikiano katika kuleta maendeleo haya.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia katika mchango wangu, nitumie fursa hii kuwatachia ndugu zangu, Waislam wote hapa Bungeni, pale Kondoa lakini na nchi nzima kwa ujumla Mfungo mwema wa Ramadhani na iwe sehemu ya toba na maombi mema katika kuhakikisha kwamba janga hili la Corona pia linatuondokea.

Mheshimiwa Spika, leo nataka nizungumze na watalam wenzangu, *ma-architect* wenzangu, wako *ma-engineer* wako *ma-planner* ambao wako kwenye Wizara hii ya Maji. Nataka tuzungumze lugha inayoweza kufanana kidogo; tumekuwa tunakwenda na mipango ya utekelezaji wa miradi ya maji wakati mwingine *randomly*, *randomly* kwa maana ya kwamba inategemeana na kelele, labda Mbunge mmoja amepiga kelele, kuna presha sehemu fulani ndiyo tunakwenda kutekeleza miradi kwa namna ile, pamoja na mipango ambayo wakati mwingine inakuepo.

Mheshimiwa Spika, nataka nishauri jambo moja kubwa sana na la msingi kwenye maendeleo yoyote yale; tutengeneze *master plan* ya huduma ya maji kwenye kila halmashauri, kila wilaya. Hizi mamlaka tulizoiunda za RUWASA lakini pamoja na zile huduma za mijini, tuwe na *master plan* kamili, miradi yote inayotekeliza iende kutekelezwa kufuatana na jinsi *mater plan* ilivyoandalialiwa.

Mheshimiwa Spika, *master plan* inachukua *thinking* kubwa, kuna *planning* ya kutosha, inaangalia vigezo vingi sana, matokeo yake kunakuwa na tija kwa miradi ile inayokwenda kutekelezwa. Tunazungumza maeneo yetu yana jiografia mbalimbali, mtawanyiko umekaa mbalimbali, mgawanyiko umekaa mbalimbali. Sasa unapokwenda kwa mtindo wa *random* au dharura uwezekano wa kupata tija kwa usambazji wa huduma kwa watu wengi zaidi ambao wako kwenye eneo lile husika, labda ni Wilaya au halmshauri unakuwa kidogo una walakini.

*(Hapa Mhe. Edwin M. Sannda alivua barakoa aweze
kuongea vizuri)*

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Spika, uwezekano wa kupata tija sahihi kwa ule mtawanyiko na mgawanyiko wa miradi ile na kusogea huduma karibu na wananchi unaweza ukawa una walakini. Unakuta upande mwingine umepeleka maji maeneo *concentrated* umesahau maeneo mengine ambapo watu wanakosa au wanahitaji kwenda umbali mrefu zaidi. Kwa hiyo, ninawaomba Wizara kwa kutumia *machinery* zilizokuwepo na mipango ambayo tunayo. Maeneo yetu yana jiografia mbalimbali, kila Wilaya iwe na *master plan* ya huduma ya maji kama msingi namba moja wa maendeleo, kama tunavyotengeneza *strategic plan* na vitu vingine vya namna hiyo; hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili nataka kuongelea *value for money* kwa maana ya kwamba tukiacha ile *scope* na *magnitude* ya kazi kutokana na gharama za mradi halisi, unakuta tumepeleka fedha au tumetumia, tumewekeza fedha nydingi sana mahali fulani, nikichukulia mfano kwangu Kondoa, mpaka sasa toka mwaka 2016 tuna zaidi ya billioni 6 lakini kero ya maji ambayo bado inaendelea kuwepo, hususani pale mjini huwezi kuamini kama tumepokea fedha nydingi kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, ina maana fedha zile labda zingefanyiwa *planning* na *design* nzuri zaidi, nikichukua mathalani pale mjini tuna chanzo cha chemchemi, tumechimba visima vitano vipyta na kukarabati vingine viwili kwa ajili ya ku-*complement* upatikanani wa maji pale, lakini unakuta miundombinu ya usambazaji bado ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, umewekeza kiasi cha kutosha lakini bado vile visima ulivyotengeneza haviwezi kwenda kulisha kwenye gridi kubwa ilipo kutoka kule kile chanzo cha asilia ambacho labda ndiyo mnaki-*complement* sasa. Haya ndiyo mambo ambayo nasema kwa fedha ileile tungepata *more value for the same amount of money* ili yotumika kuwekeza kwenye maji pale ... mjini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwasihii na hii pia inapandia kwenye lile wazo langu la mwanzo la *master plan*;

planning nzuri ikifanyika uwekezaji utakuwa na *efficiency*, utakuwa *effective* kwasababu pia utaangalia mtawanyiko na mgawanyo ili kunufaisha watu wengi zaidi kwa fedha mahususi ambazo zitakuwa zimebekwa.

Mheshimiwa Spika, unaweka bilioni sita halafu bado unakuta kelele za maji na tatizo bado liko kubwa, kwa kweli hapa ni lazima turudi nyuma kama wataalam tukaangalie ile *design* iliyofanywa kwa nini Serikali imetumia hela nyingi kiasi hiki mpaka leo na bado kilio ni kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nawasihi sana tuone ni namna gani *proper plan* na *design* itafanyika kuanzia mwanzo; lakini hapo hapo nazungumzia kitu kinaitwa *effectiveness* na *efficiency*. Unakuwa na visima vingi tu, mwisho wa siku gharama ya uendeshaji pia inakuwa kubwa. Kumbe ungeweza kuwa na visima vichache, ukafanya *design* nzuri ya matenki makubwa na vizimba vyta usambazaji vikawafikia watu wengi kwa mfano kisima kimoja na gharama ya uendeshaji mwisho wa siku ikiwa ndogo, utakuwa umefanikisha kupata tija ambayo mwisho wa siku ndiyo hii, tunazungumza *value for money that brings efficiency* na *effectiveness*.

Mheshimiwa Spika, namsihi Mheshimiwa Waziri, najua naye ni mtaalam, tumeshakaa *several times* na namna ambavyo anaongea, anaongea kitaalam kabisa. Kwa hiyo,...

(Hapa, kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, turudi nyuma tuone ni namna gani tunaweza tukafanikiwa kupata *efficiency* kwa fedha...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sannda, tunakushukuru sana.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Edwin Sannda, ujumbe wako umefika, umesikika vizuri kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, walioomba kuchangia Wizara hii ni wengi sana. Nawashauri kila mmoja wenu ajitahidi afikishe ujumbe, afikishe mchango wake kwa maandishi kupitia *tablets* zetu ili watakaopata bahati ya kuzungumza humu ndani, basi waweze kuzungumza. Wale ambao hawatapata nafasi, naamini kwenye afya, inakuja huko mbele. Afya na maji bado ni mambo yale yale na Mheshimiwa Waziri ataendelea kuwepo ili kuendelea kuchukua michango. Kwa hiyo, nawasihi tufanye hivyo.

Mheshimiwa Aisharose Matembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Aster Bulaya.

MHE. AIS HAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii muhimu ya maji. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema, mwangi wa neema kwa kutujalia uzima na afya njema na kwa kuendelea kutulinda dhidi ya janga hili la *corona*. Nawasihi Watanzania wote tuendelee kuchukua tahadhari huku tukimwomba Mwenyezi Mungu na ni imani yangu kwamba na hili nalo litapita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee kwa dhati ya moyo wangu nawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Singida kwa ridhaa walijonipa kuwawakilisha Bungeni kwa muda wa miaka mitano. Ikiwapendeza ninawaomba wanipe ridhaa kwa kipindi kingine ili tuweze kushirikiana katika mambo mengi zaidi. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, Profesa Mbarawa, Naibu wake - Mheshimiwa Juma Aweso, Katibu Mkuu - Profesa Kitila Mkumbo na watendaji wote wa Wizara hii ya maji kwa kazi nzuri

wanayoifanya ya kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa mageuzi makubwa aliyofanya katika Wizara ya Maji. Katika kipindi chake cha miaka mitano tumeshuhudia miradi mbalimbali ikitekelezwa na mingine imeshakamilika. Mfano, katika Wilaya yangu ya Iramba upo mradi wa meli katika Kata ya *Old Kiomboi* na ule wa Mgungia Kaseria, miradi yote imekamilika na wananchi wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yangu ya Ikungi umefanyika ukarabati mkubwa wa maji wa Vijiji vya Mwaru na Ulyampichi na miradi yote hii pia nayo imeshakamilika na wananchi wanapata maji safi na salama. Naipongeza sana Serikali. Katika Wilaya ya Manyoni upo mradi mkubwa wa Kintku Lusilile wa vijiji kumi. Mradi huu pia nao uko katika hatua za mwisho za kukamilika.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye alifanya ziara mwaka 2019. Mheshimiwa Waziri Mkuu ziara yako imeleta tija kubwa sana, kwani mradi huu sasa upo katika hatua nzuri za kukamilika. Naiomba Serikali basi iharakishe ili sehemu iliyobaki iweze kukamilika kwani wananchi wa Jimbo la Manyoni Mashariki wameteseka kwa muda mrefu kwa adha ya ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Singida Kaskazini upo mradi wa uchimbaji wa visima virefu katika Vijiji vya Mughamo na Misingo. Mradi huu tayari usanifu umeshafanyika. Naiomba Serikali ifanye haraka kuleta fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya visima hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia napongeza sana Wakala wa Maji Vijijini (*RUWASA*) kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya. Kwa muda mfupi tumeshuhudia utekelezaji wa miradi mbalimbali huko vijijini. Kwa kazi nzuri hii wanayoifanya naiomba Serikali yangu sikivu, basi hawa *RUWASA*

waongezewe fedha za kutosha ili miradi mingi iweze kukamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile naiomba sana Serikali, taasisi za afya na elimu katika Wilaya yangu ya Singida, nikimaanisha Shule za Sekondari pamoja na Vituo vya Afya, hazina miundombinu ya maji. Basi katika bajeti hii, naomba sana Wizara izingatie, itoe kipaumbele ili taasisi hizi nazo ziweze kuunganishwa na huduma ya uhakika ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, mfano katika Kituo cha Afya cha Kintinku ambacho kimejengwa vizuri sana, kuna adha kubwa ya upatikanaji wa maji, lakini pia kipo Kituo cha Ihanja. Mheshimiwa Waziri, Profesa Mbarawa, alikitembelea kituo hiki mwaka 2019 na alituahidi kutupatia fedha katika Kituo hiki cha Ihanja ili kiweze kuunganishwa na miundombinu ya maji. Namwomba sana jambo hili liweze kufanyika haraka ili wananchi wa Mkoa wa Singida katika vituo hivi vya Afya waweze kupatiwa maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia suala la *Corona* kwamba anaziamrisha Mamlaka za Maji ziweze kuhakikisha kwamba maji yanapatikana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kwamba kwa kuwa kuna miradi ya maji ambayo imefikia katika hatua za mwisho, basi wahakikishe kwamba miradi hiyo inapelekewa fedha za kutosha ili wananchi waweze kupata maji na waweze kunawa mikono kwa ajili ya kujikinga na janga hili baya la *Corona*.

Mheshimiwa Spika, mwisho nawatakia Waislamu wote mfungo mwema na tuendelee kumwomba Mungu atukinge na janga hili baya la *Corona*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe. Nilikwishamtaja Mheshimiwa Ester Amos Bulaya na atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Maji ambayo mwisho wa siku imeshika uhai wa Watanzania kwa sababu maji ni uhai.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia Mpango wa Miaka Mitano kuanzia mwaka 2010 – 2016, 2016 – 2021. Kama Taifa tulijiwekea malengo kwamba, ikifika mwaka 2021 upatikanaji wa maji vijijini tufikie asilimia 80, mijini tufikie asilimia 90 kutika asilimia 72 mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, nilipitia taarifa mbalimbali za Wizara kupitia Wizara ya Maji, nikapitia taarifa nyingine pia ya Wizara ya Fedha, lakini na rejea mbalimbali kwenye ripoti mbalimbali za CAG. Sasa ukiangalia kwenye Taarifa ya Wizara ya Maji inaonesha mpaka sasa mwaka huu wa 2020 upatikanaji wa maji vijijini umeshuka kwa asilimia 13 kutoka asilimia 72 mpaka asilimia 58.7. Ndiyo maana changamoto na kelele za maji bado zinaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilijuliza, kwa nini upatikanaji wa maji umeshuka? Nilipitia ripoti mbalimbali; kama Taifa, kuanzia mwaka 2011 mpaka 2014 tulitumia shilingi triliioni 2.8 kwenda kuwekeza kwenye Sekta ya Maji na dhamira ilikuwa njema tu, kuhakikisha kama Taifa tunaondokana na tatizo la maji. Taifa lenye miaka zaidi ya 50. Cha kusikitisha kwenye pesa tulizowezeka shilingi triliioni 2.8, asilimia 46 ya miradi ya maji haifanyi kazi kama ilivyokusudiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii inamaanisha nini? Inamaanisha asilimia 46 ya shilingi triliioni 2.8 imetupwa chini. Leo tunawakamata akina Tito Magoti tunawapa kesi za uhujumu uchumi za shilingi milioni 17. Kuna watu wamesababisha uzembe wa matriliioni ya Watanzania, wapo ofisini na wengine walikuwepo kwenye Wizara tukonao humu, hatulitendei haki Taifa letu. Nasema kwa unyenyekevu

mkubwa, tunahitaji mabadiliko. Hata mkitoka ninyi, watakaoingia watimize wajibu wao ili tulitendee wema Taifa letu na tuwatuue akina mama ndoo kichwani kama kweli tuna dhamira hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini tumeshuka? Nilikuwa napitia ripoti mbalimbali; ukiangalia katika visima 1,485 vilivyochimbwa, visima virefu vya Kitaifa 1,485 vilivyochimbwa visima 490 havitoi maji na vimekauka. Sasa kama Wabunge, kama Wawakilishi wa Watanzania tunahitaji kujua hivi kweli kuna ufanisi?

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Ester, unapewa Taarifa na Mheshimiwa Mlinga.

TAARIFA

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe Taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza kuwa Serikali hii inaacha watu ambao wamekula mabilioni ya pesa. Nataka nimpe taarifa kuwa Serikali hii haiwezi kuacha, hata aliyekuwa mmiliki wa Bilicanas alikuwa anadaiwa shilingi bilioni moja na *point*; alinyang'anywa jengo na anapelekwa Mahakamani na vifaa vyake vyote vimechukuliwa. Ahsante.

SPIKA: Unapokea Taarifa hiyo Mheshimiwa Ester?

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na mchango wangu. Niko hapa kwa ajili ya kulihutubia Taifa na Watanzania wanansikiliza.

Mheshimiwa Spika, leo visima 490 havitoi maji. Sasa tunajiliza, tatizo kubwa ni nini? Tatizo ni athari za utafiti wa ki-haidrolojia usiojitosheleza. Tuna wataalam kwenye Wizara; sasa leo tuijulize, kisima kimoja kinagharimu shilingi ngapi?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimeenda mbali zaidi. Ukienda kwenye mikoa saba kati ya visima 554 vilivyochimbwa, visima 139 havitoi maji, tuna wataalam hapo. Mheshimiwa Waziri pia kwenye hotuba yake nimemsikia anakiri ooh, kuna uzembe umesababishwa na wataalam kwenye Wizara ya Maji. Wapo, mnachekanao hamwachukulii hatua. *Real? Kweli mna dhamira nyie ya kumtua mwanamke ndoo kichwani? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Baraza la Wanawake la CHADEMA tumeandaa Sera ya Wanawake na kama chama tumesema, tukichukua nchi ni namna gani tutamaliza tatizo la maji katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukizungumzia changamoto ya Wakandarasi kutokuwa na vigezo vya kupewa tenda. Mkandarasi anapewa tenda, hana uwezo, hana vifaa; kwa tatizo hilo Wakandarasi kutokuwa na vigezo ambapo ni kinyume kabisa na kanuni zetu, wameisababishia hasara Serikali zaidi ya shilingi bilioni 30. Mmewachukuliwa hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa natolea mfano mradi wangu wa Bunda. Zaidi ya miaka 12 Mkandarasi mnamuweka ndani, mnamtoa, mnampa tenda tena aendelee na miradi, *shame!* Nguvu zenu nyie ni kushughulika na upinzani, timizeni wajibu wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni aibu Taifa lenye umri zaidi ya miaka 50 tuna mfumo wa majitaka 9%, *real?* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazunguka tunaenda nchi mbalimbali, tunaona wenzetu wanafanyaje. Ukipanga kueneza maji, unahakikisha kuwe na mfumo wa majitaka. Leo kukiwa na mafuriko ndiyo viwanda wafungulie, huko kwenye nyumba nyingine uswahilini huko wafungulie, mwisho wa siku Jiji linanuka kinyesi. Aibu! Taifa kama hili 9% mfumo wa majitaka. Dar es Salaam lile ni Jiji la kibiashara, lina 4% tu. Nilikuwa nasoma ripoti ya mwaka 2012, Serikali ilitumia zaidi ya shilingi bilioni 300 kutibu maradhi mbalimbali

yanayotokana na matatizo hayo ya kutokuwa na mfumo wa majitaka. Timizeni wajibu wenu, acheni kiburi. mkichoka Watanzania tutawatoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ester Amos Bulaya. Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Andrew John Heche.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Spika, naweza kuthubutu kukuita Spika wa karne ijayo. Nitakapopata nafasi ya kuelezea, nitakuelezea kwa nini ni Spika wa karne ijayo.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza leo siungi mkono Hoja ya Serikali yangu. Nitaandika kwa Katibu Mkuu kwa nini siungi mkono hoja. Kwa mara ya kwanza atatokea Mbunge wa CCM kwenye hoja kuu ya Waziri wa Fedha atakayesema hapana, kwa sababu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nitasema mambo matatu tu, yako mengi sana. Wamejitätidi kidogo, lakini nianzie na hili la mkopo wa India ambao tumesomewa kwa kirefu leo. Bahati nzuri mkopo huo wakati Mheshimiwa Profesa Maghembe ana-negotiate nilikuwa India kwa *mission* nyingine, lakini tulifanya *consultation for the good intention of this country*. Kwa kawaida, *on average*, mradi wa maji hauwezi kugharimu dola milioni 17 kwa mji.

Mheshimiwa Spika, nitatoa takwimu. Misungwi, Mji ambao umepata maji na baada ya kupata maji kuna mashine tatu zina-pump maji na kuna matenki makubwa, tumetumia shilingi bilioni 12. Mji wa Magu ambao umepata maji sasa hivi wametumia shilingi bilioni 16. Chukua hizo dola milioni 500 gawanya kwa mijji 28 plus mmoja wa Zanzibar utapata dola milioni 17.2 ambayo ni sawasawa na shilingi bilioni 39 point something. Bila kufanya marekebisho kwenye

hilo, sitaunga mkono hoja ya Serikali Kuu kwa sababu, najua kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, nilishaweka makaratasi hayo; jinsi tulivyompata yule Mkandarasi, anaitwa *WAPCOS*, kama mlisema kuhusu Lugumi *that is more than Lugumi*. Siku nitakapopata nafasi ya kumzungumzia Lugumi, mtajua; kwa sababu hata ripoti ulipounda tume ya kwenda kuchunguza, baada ya kuona yule mliyekuwa mmemtafuta hayumo, mlimweka pembeni. *That is one. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, *second*, mradi wa maji kutoka Shinyanga kwenda Nzega, Igunga na Tabora; ule mradi uliota maji kutoka kijiji lhelele, Wilayani kwangu, ultumia shilingi bilioni 25, lakini waliweka mashine tatu ambazo zinatoa maji ziwani, zinayachuja, zinayasafisha na zina-pump kwenda kwenye *tank* lenye eneo kubwa zaidi ya uwanja wa mpira na kuyasukuma kwenda Kahama na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, hebu waulize leo hii, huo mradi wa kutoka Shinyanga usiokuwa na mashine za aina hiyo na ma-*tank* ya namna hiyo na *distance* ya kutoka Shinyanga kwenda Nzega, Igunga na Tabora, shilingi bilioni 600 *against* shilingi bilioni 250 na pale tulichakachuliwa, *we can not accept this*. Wafanye upya! *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, huu Mradi wa Vijiji 28 kutoka mkopo wa India, bila hesabu ya kujidanganya yoyote, unaweza uka-save miji 54. Wafanye hesabu upya. Bahati nzuri Tanzania mimi wakati nakua kulikuwa na Chuo cha Maji Rwegarulila, tuna wataalam wazuri, tuna Wahandisi wazuri, *why are you not using those engineers and technicians?* Mnakimbilia *WAPCOS*, *WAPCOS is almost a de facto name* ndani ya ile Wizara. Waiondoeni *WAPCOS*, nilishakuletea jinsi alivyopatikana kusimamia mradi ule, *it's a shame!* Siwezi kukubaliana na hicho. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, la tatu na la mwisho, katika Wilaya yangu sehemu ya Usagara pamoja na Wilaya ya Nyamagana na Ilemela pamoja na Magu tuna mradi. Mradi

huo nilishasema, siku Rais anatoka Sengerema akatoka pale Kigongo, akawaambia wananchi huyu Mbunge wenu anafahamiana na watu wengi mno, mnashindwaje kupata maji? Nikatafuta wafadhili, wakapatikana *for better terms* kuliko hizo za AFD wanazosema. Wale watu walisema hivi, tunawapa huu kama mkopo kwa sababu tunaamini tukiwapa grants mtazi-misuse, *they are my friends!*

Mheshimiwa Spika, wakakataliwa, nikashtakiwa mpaka kwa Mheshimiwa Rais kwamba Kitwanga ana *interest* na nilishasema hapa, yes, nilikuwa na *interest* kwa sababu nilikuwa nataka watu wa Koromije na watu wa Usagara wapate maji, *that is my only interest!* Wakaleta, AFD, Wafaransa waanze kujadiliana kusaini mkataba. Wameanza mwaka 2017, hapa ninavyoongea leo hii mkataba haujapitishwa, lakini ni *additional fund ya only 30 million Euro*, mkataba mkuu ulishakuwepo. Mwaka 2017, 2018, 2019, 2020.

*Halafu niunge mkono ujinga huu? (Makofi/Kicheko)
[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

SPIKA: Mheshimiwa Kitwanga...

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Spika, sorry napandwa na munkari kidogo kwa sababu ya hasira. Naomba tu unisamehe...

SPIKA: Endelea kuchangia, hilo lingine la ujinga nimelitoa kwenye Hansard, endelea.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Spika, nimelitoa. Nimelitoa kwa bahati mbaya tu, najua wale watu wanahitaji maji, hawahitaji maneno; mpaka tunawapa sifa hawa wanasema sema, hawa huwa hawana cha kusema! Hawa huwa hawana hoja, tunawapa sisi hoja! Sisi katika Wizara zote tatu ambazo zinagusa wananchi Elimu, Afya, na Maji, maji mwende kaburini, wale wenzeni wako huko ju, *they are super stars*, hii elimu zimepelekwa hela, malipo bure, hakuna malalamiko makubwa. Kwenye afya, ujenzi wa vituo vya afya, *everywhere*, kila mtu anajisifia, tujisifie na nini nyie?

SPIKA: Mheshimiwa malizia, kengele ya pili.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba niseme hivi, siungi hoja ya Wizara hii na sitaunga hoja ya Serikali Kuu mpaka niwe nimehakikishiwa hiyo miaka minne sasa imeisha, wamesaini ule mkataba na kwamba wame-reviewbadala ya vituo vya miji 28 na mmoja wa Zanzibar, haki itendeke, *we need value for money!* Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga kwa mchango wako kwa uchungu mkubwa. Kwa kweli hoja ya kwamba Wizara ya Maji miradi yake huwa ni ya fedha nyingi sana, ni hoja ambayo Bunge hili limekuwa nayo kwa muda mrefu. Hata kwa Wilaya nyingine, yaani unaangalia mamilioni, unaangalia kilichofanyika, kwa kweli! Hatuwezi kukulaumu Mheshimiwa Waziri umeyakuta haya mambo, lakini mfumo huo lazima ufile mahali fulani, *it has to stop*, kwa sababu tuna shida nyingi, yaani miradi ya mamilioni, halafu kinachofanyika, ndiyo hivyo bwana.

Mheshimiwa Chenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula. (*Makofi*)

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nichangie kwa ufupi tu kwenye hoja ilio mbele yetu. Nimshukuru sana mtoa hoja Profesa Mbarawa; Naibu Waziri Mheshimiwa Aweso; Katibu Mkuu, Profesa Mkumbo; Naibu Katibu Mkuu, Sanga; Wakurugenzi wote na watendaji wa taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii. Hongereni sana kwa kazi nzuri mnayofanya. Changamoto ni nyingi sana kwenye sekta hii muhimu, lakini angalau tunaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Serikali, asilimia 74 ya fedha ambazo Bunge liliidhinisha zimetolewa na Serikali mpaka Machi mwaka huu. Wizara ya Fedha tunawashukuru sana kwa sababu ndiyo *priority* ambayo tulisema moja ya vipaumbele vyetu maji, maji, maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi natoka kwenye maeneo ya ukame sana kama Dodoma. Naendelea kuishukuru sana Serikali kwa kuwa na mpango huu unaohakikisha maeneo ambayo yana maji mengi, maji hayo yatoke kwenye maeneo hayo, yaende kwenye maeneo mengine ambayo ni kame kama Simiyu, Shinyanga, Tabora, Dodoma na Singida na maeneo mengine kama Babati. Ningependa sera hii *inclusive* tuiendeleze kwa sababu inajenga umaja na mshikamano kwa Taifa hili. Maji ni uhai, maji ni kila kitu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, *charity begins at home*. Niishukuru sana Wizara hii, nilikuwa mnyonge sana miaka ya nyuma kwenye suala la maji kwa sababu kuna visima vilivyo chimbwa tangu Mwaka wa Fedha 2012/2013, vilipata maji lakini wananchi walikuwa hawana maji. Katika mwaka huu wa fedha, Kijiji cha Igaganulwa, Sengerema, Masewa, Mwamulapa, Kasoli, wananchi hawa watapata maji. *Centre* kubwa sana ya Wilaya ya Bariadi, Nkololo tulifadhiliwa na Serikali ya Misri tukapata maji mengi sana, safari hii na wenyewe wanaanza kusambaza maji ili wapate wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa Nkololo naendelea kuomba kisima au visima vingine virefu ni *centre* kubwa sana. Wewe hukubahatika kufika Nkololo, huwa unaishia Bariadi pale tu lakini hii ni *centre* kubwa sana. Profesa Kitila Mkumbo na Profesa Mbarawa wanajua, ni *centre* kubwa sana, mahitaji ya maji ni makubwa, lakini nashukuru kwa haya ambayo tunayapata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna visima viko tayari, tuna maji, tunaomba fedha tu kwa Bunamhala, Gudui, Mahaha, Mbiti na Ezunya. Naishukuru Serikali kwa Mradi wa Mahina Sanungu, tumepata milioni 157, itatusaidia tukamilishe, tuwapatie wananchi maji. Nangokola hivyo hivyo, nimeambiwa mchana huu tumepata milioni 40 tukamilishe, mradi ulikuwa umesimama. Hata hivyo, naiomba sana Serikali kwa Mradi wa Bupandagila, mkandarasi tumesha-*terminate* mkataba, tungependa sana sasa tukamilishe mradi huu kwa kutumia *force account* ili wananchi wapate maji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya na niseme hapa siku ile wakati wa TAMISEMI sikupata nafasi ya kuchangia. Mimi nahudumia halmashauri mbili, Mheshimiwa Masaba siku ile alisema nazeeshwa, nachoshwa kuhudumia Halmashauri mbili. Nataka niwaambie Watanzania kupitia kwako, ni heshima kubwa sana kwangu kuhudumia halmashauri mbili, wala sijisikii vibaya, unatoa huduma kwa wananchi hawa na hadi hapo Serikali itakapoona kuna umuhimu wa kuligawa Jimbo hilo, watafanya hivyo lakini nina kata 31, tangu 2005 hadi leo, tunakwenda vizuri. Siwezi kuja hapa na kulalamika, tunawatumikia wananchi kwa moyo safi kabisa, *it is a public service.* (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi, kuna visima 20. Naomba tu pesa hizi zipatikane katika mwaka huu wa fedha kwa sababu pesa ile ilitengwa, fedha zipo kuweza kukamilisha, kuwachimbia wananchi hawa maji tufanye vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ziwa Victoria; amesema vizuri sana Mheshimiwa Leah Komanya na Serikali inasema kwenye hotuba hii tunaenda vizuri. Matamanio yetu ilikuwa kwamba mradi huu unaanza mwaka ujao wa fedha, Tarehe 1 Julai ilikuwa tuanze, lakini unapopewa msaada kama huo na Serikali yako inachangia milioni 40, *Euro* na wananchi watachangia 1.5 million *Euro* na ile sehemu kubwa ni pesa ya mwingine anayekusaidia, si lazima ukubali kusubiri kidogo! Kwa hiyo tunavumilia na wenyewe taratibu zao zikamilike, lakini naamini mradi huu sasa unafika mahali pazuri, tathmini ya ardhi inafanyika vizuri, tunataka wananchi wetu waweze kulipwa fidia kwa maeneo ambayo yatachukuliwa na mradi huu.

Mheshimiwa Spika, naungana na Wabunge wengine, huu Mradi wa Mkopo wa India umechukua muda, lakini sasa baada ya Bunge kuwezesha yale ambayo tuliombwa na Serikali masuala ya kodi na kadhalika tukawezesha, sasa twende kwa kasi ili miji hiyo 28 na wenyewe iweze kupata maji kama ilivyokusudiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, sisi ni Bunge, hasa hali hii ya *corona virus* sio jambo la kawaida. Tunapitisha Mafungu haya kwa mwaka ujao wa fedha, lakini tukijua kabisa kwamba Mafungu haya tunayoidhinishga pesa, hali haitakuwa kama kawaida. Ushauri wangu kwa Serikali, ni vyema tulione hili sasa kama Bunge, tunapofika mwishoni kabla ya Bajeti Kuu, Mafungu yote haya, Serikali iwe imejipanga, lazima tuangalie maeneo maalum ambayo lazima tuendelee kutoa pesa kama mradi wa *Standard Gauge*, *Nyerere Dam*, lakini pia tulinde mafanikio makubwa ambayo tumepata katika upande wa afya na upande wa elimu na upande wa maji, haya ambayo tunasema. Maeneo mengine yote Waheshimiwa Wabunge, lazima tukubaliane sasa tutoe jasho, kwa sababu hali haitakuwa kama kawaida, na ni vyema tukatumia Kanuni ya 105 mwishoni...

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa, mallizia sasa.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuiomba Serikali na kuishauri kwamba wafanye tathmini mapema sana lakini na sisi kama Bunge tuwe sehemu ya kushauri kabla ya kuitisha bajeti kuu ya Serikali ili tujue yanayokuja ni yapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hiyo na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Andrew J. Chenge. Kabla ya mchangaiji anayefuata, nimkumbushe Mheshimiwa Charles Kitwanga pamoja na hasira yako yote, itakapofika Bajeti Kuu, sikushauri kabisa kujaribu kuikataa kwa sababu kwanza ni *three line whip*, lakini pia Serikali ya Awamu ya Tano yenyewe kwa upande wake imetekeleza wajibu wake, imetenga fedha nydingi kwa ajili ya maji. Tunacholalamikia Bunge wakati wote ni kwamba haturidhiki na wataalam wa Wizara ya Maji kwamba miradi yake inakuwa ya mabilioni ya shilingi, yaani haturidhiki. Serikali kama Serikali, imetekeleza wajibu wake, imetenga fedha nydingi sana mpaka mikopo hiyo tunapata ambayo tunaamini kwamba fedha hizo zinaweza zikaenda

katika miji mingi zaidi badala ya hiyo miji michache ambayo iko *targeted*. Kwa hiyo hii ni *challenge* kwa wataalam wa Wizara ya Maji, kujitathmini na kujitazama zaidi.

Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja liyoko mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametupa uzima na kwamba tunaendelea kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii vile vile kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri kwa kutembelea Mkinga, kuja kujonea changamoto tunazopambana nazo. Hivi tunavyozungumza kuna timu ya wataalam, Wahandisi wa Maji kutoka Wilaya mbalimbali za Mkoa wa Tanga, wako Maramba, wanaendelea na kazi ya usanifu wa Miradi ya Mapatano ambayo inatakiwa kupeleka maji kwenye Kijiji cha Bantu, Machimboni, Kwangena na Miyenzani. Vile vile, wanasanifu Mradi ule wa Maramba ambao umekuwa ni mradi wa muda mrefu, Waziri Mkuu alipotembelea pale, tulieleza hitaji la mradi ule kufanyiwa mapitio na chanzo kile kuangaliwa upya. Nashukuru sana Serikali imefanya uamuzi wa haraka kulishugulikia jambo lile, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, timu ile inafanya kazi kwenye miradi ile miwili, lakini mradi muhimu sana mmoja umesahaulika; Mradi wa Mhinduro na Bosha ambapo mwaka jana nilisema kwamba hawa ndiyo wanaotunza chanzo cha maji kinachopeleka maji kwenye Jiji la Tanga, lakini wao hawana maji. Namwomba sana, Mheshimiwa Waziri atumie busara na weledi wake, timu ile isiondoke mpaka ikamilishe kufanya usanifu wa Mradi ule wa Mhinduro na Bosha, namsihi sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, sasa nirudi kwenye mambo ambayo nimekuwa nikiyazungumzia mara kwa mara. Mwaka jana wakati nachangia bajeti ya Wizara

hii nilizungumzia maeneo manne ambayo yamekuwa ni changamoto kubwa sana kwetu watu wa Mkinga. Nilizungumzia Mradi wa Mbuta, nikasema huu ni mradi ambao tulisaini mwaka 2016, ukiwa na thamani ya bilioni 1.9 na kwamba wakati ule nachangia, mkandarasi alikuwa ameamua kuvunja mkataba, lakini wakati huo alikuwa tayari amekwishalipwa milioni 800. Nikaomba Wizara ione uwezekano wa kuwatuma Wakala wa Visima ili waweze *ku-take over.*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, timu ile imekwishakwenda, imefanya tathmini, imeonekana kwamba ili kumalizia mradi ule, zinahitajika takriban milioni 700 na kitu hivi. Namsih sana, fedha hizi zitoke, nimeambiwa taarifa tayari iko mezani kwake. Naomba fedha hizi zitoke, tuweze kumaliza mradi huu ambao ulianza tangu mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni wa Mwakijembe. Nashukuru tarehe 3 Aprili, 2020 ulifika Mwakijembe baada ya ziara ile ambayo tulikwenda na Naibu Waziri. Niliambiwa ulipofika pale ulitoa maagizo *DCC* wafanye tathmini ya kuona mkandarasi anastahili kulipwa alichokuwa anastahili kulipwa ili kazi iendelee. Nimeambiwa tathmini imekamilika iko ofisiini kwako na zinahitajika karibu shilingi milioni 720 ili kazi ile iendelee. Vilevile mkoani zipo tayari shilingi milioni 300, zilisimama kulipwa mpaka uhakiki wa kazi iliyofanyika ufanyike. Kwa hiyo, nakuomba kwa mujibu wa mapendeleko yaliyotolewa basi utekelezaji wa mradi huu uendelee.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine nililozungumzia ilikuwa ni mradi wa Horohoro. Nilizungumzia eneo hili kwamba ni aibu kwetu kama nchi kwa sababu wananchi wetu walikuwa wanalamizika kwenda kuchota maji upande wa pili wa Kenya. Nashukuru Serikali ilifanya haraka kushughulikia jambo hili zikatengwa takribani shilingi milioni 370 na kazi imeendelea vizuri. Nimeambiwa *DCC* wamefanya kazi pale na wenzetu wa Tanga-UWASA wamefanya tathmini, wamebaini kuna baadhi ya mapungufu. Wamekuja na mkakati wa muda

mfupi na mrefu. Mkakati wa muda mrefu unahitaji bwawa lile lijengwe upya maana linavujisha maji. Nakusih i sana na naiishi Serikali ifanyie kazi jambo hili. Kama mnavyoona sasa mpaka imefungwa, kama tungekuwa hatukushughulikia mradi ule, sijui hali ya watu wetu inge kuwa namna gani. Nawasihi sana tufanyie kazi jambo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ni changamoto kubwa tunayopata watu wa Mkinga kwa kukosa mradi mkubwa wa kupeleka maji U坎da wa Pwani. Mwaka jana wakati nazungumza hapa, nilisema tayari Wizara ilikuwa imeshatafuta mkandarasi wa kufanya usanifu. Kilichokuwa kinatakiwa ni kufanya majadiliano ili kusaini mkataba. Nikaahidiwa kwamba ndani ya kipindi kifupi jambo lile lingefanyika lakini mpaka hivi tunavyozungumza hatujui nini kinaendelea.

Mheshimiwa Spika, mradi ule wa kutoa maji kwenye Mto Zigi kwenye eneo la Mabayani kwenda mpaka Horohoro ungehudumia vijiji 37, tunazungumzia watu takribani 45,000 mpaka 50,000. Nawasihi sana Serikali oneni umuhimu wa jambo hili. Najua Mheshimiwa Waziri una nia ya dhati ya kuhakikisha tunatumia hata uwezo wa ndani wa kutekeleza jambo hili kwa haraka lakini jambo hili ni la muda mrefu. Naomba hiyo dhamira yako sasa igeuke kwenye vitendo ili wananchi wa Mkinga waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi mingine ambayo ilitekelezwa, mradi wa Daluni, mradi ule ulikuwa na matatizo tangu mwanzo ulipoanzishwa kwa sababu ulivyokuwa umebuniwa baadaye ulipunguzwa *specifications* zake na mahitaji yake matokeo yake baadhi ya maeneo yaliyokusudiwa kufikishiwa maji hayakufikiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile tulikuwa tuna changamoto ya usimamizi. Sasa kipindi cha uhai wa mradi ule kimeisha, nawasihi Serikali muone umuhimu sasa wa kufanya upya mapitio ya jinsi ya kuboresha mradi ule, tuondokane na changamoto zilizopo ili wananchi wetu waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru ndugu zetu wa *Islamic Help* kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutusaidia kuchimba visima kule Mkinga. Wametuchimbia visima na sasa hivi wanaendelea na kazi hiyo, wamesema wapo tayari kutuchimbia karibu visima 20 mpaka 30 hivi. Changamoto tunayopambana nayo ni fedha ya utafiti wa maeneo yenye maji. Ikkupendeza Mheshimiwa Waziri, tuwatumie *DCC* waje wafanye utafiti ule ili wenzetu hawa ambao wamejionesha wapo tayari kutusaidia kwenye kuchimba visima, waweze kufanya jambo lile.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dunstan Kitandula. Mheshimiwa Joseph Selasini atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Monko ambaye yupo kule Msekwa. Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa nafasi hii ambayo nimepata. Hii ni mara yangu ya kwanza kabisa kusimama katika Bunge lako hili tangu bajeti hii ilipoanza kujadiliwa. Nakushukuru sana kwa nafasi hii, pia namshukuru Katibu wa Bunge letu Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuwasilisha ombi langu mbele yako.

Mheshimiwa Spika, leo natoa mchango wangu nikiwa nimetengwa na familia ya kisiasa *group* la *WhatsApp* la Wabunge wa chama changu ambamo pia wapo viongozi wakuu wa chama changu bila kupewa taarifa ya kukemewa au ya hatua hiyo iliyochukuliwa. Hii ni dhahiri kwamba nafasi hii nisingeipata bila kuititia katika meza yako na bila kufikishwa kwako na Katibu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, nitumie nafasi hii kuipa pole familia ya Ndg. Evod Herman Mmanda aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, wananchi wa Kata ya Mengwe na Kijiji cha Manda Juu kule Rombo kwa kuondokewa na mpandwa wetu

ambaye pia atazikwa Mtwara kama ambavyo familia imeafiki mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, natumia fursa hii kutoa pole kwa Watanzania wote ambao jamaa zao wamefariki kwa ugonjwa wa *Covid 19* unaosababishwa na virusi vya *Corona* na wagonjwa wote. Nampongeza Waziri Mkuu kwa kuratibu vizuri timu ya Taifa inayopambana na janga hili. Nampongeza Waziri wa Afya na timu ya wataalam, madaktari, manesi pamoja na wahudumu wote wa afya wanaohusika moja kwa moja na huduma hii.

Mheshimiwa Spika, natumia pia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kusimamia shughuli ambazo zinafanyika dhidi ya jambo hili. Aidha, nakupongeza wewe kwa hatua mballimbalil ulla zochukua na unazoendelea kuchukua ili kuhakikisha Wabunge na Mkutano huu wa mwisho wa Bunge la Kumi na Moja unamalizika salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naungana pia na Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa ushauri wake kwamba janga hili lisichukuliwe kisiasa. Ndiyo maana nami najisikia kuwa na wajibu wa kuwaomba Watanzania; moja kupokea ushauri wa Serikali wa namna ya kujikinga na kuutekeleza; pili, kuchangia juhud za Serikali kwa hali na mali; tatu, kuacha kubeza juhud zozote zinazochukuliwa kubwa au ndogo badala yake tutoe ushauri wa namna ya kuboresho yanayofanyika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu na wanyama na mabadiliko ya tabia nchi, uharibifu wa vyanzo vya maji, kukosekana kwa mradi mkubwa wa maji toka ule uliojengwa tangu tulivyopata uhuru; katika Jimbo la Rombo kuna shida kubwa sana ya maji. Kwa muda mrefu nimeiomba Serikali na ombi hili lilletwa hasa na wananchi kuititia Halmashauri yao na mimi Mbunge wao

kwamba tunaiomba Serikali ianzishe Mamlaka ya Maji katika Halmashauri ya Rombo.

Mheshimiwa Spika, ninayo taarifa kwamba hatua zinaanza kuchukuliwa ingawa kasi yake ni ndogo sana, jambo ambalo linasababisha wananchi waendelee kulalamikia Jumuiya ya Usambazi wa Maji maarufu *Kili Water*. Naiomba na kuitafadhalisha Serikali iongeze kasi katika kutekeleza jambo hili, litakuwa la manufaa makubwa sana kwa wananchi wa Rombo.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, Serikali immeanzisha mradi wa maji kutoka katika Msitu wa Rongai kwa ajili ya kunufaisha Mji wa Tarakea na Vijiji kama Nayeme, Kibauni, Urauri na Msangai. Mradi umekamilika lakini tatizo tulilonalo ni fedha kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya kuwafikishla maji wananchi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri kazi hii isipotee bure, ikikupendeza na ikipendeza uwezo wa Wizara yako kazi iliyokwishaanza ipewe fedha ili wananchi waweze kupata maji yale.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Kumi na Nane, nilisimama kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri, kwa kukubali ombi la watu wa Rombo ambalo lilifkishwa Serikalini na Wabunge wote waliokwishakuongoza Rombo na halikutekelezwa, limetekelezwa baada ya mimi Mbunge wao kulisukuma vizuri na Serikali ya Awamu ya Tano kulikubali. Mradi wa maji wenye thamani ya shilingi bilioni 40 utatekelezwa na tayari usanifu umeshafanyika na fedha za awali shilingi bilioni 1.5 zimeshapelekwa ili wananchi wa vijiji 21 vya ukanda wa chini waweze kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilipoishukuru Serikali wakati swalii hili liliyokuwa linajibowi niliitwa msaliti. Naomba niweke wazi kwamba kwangu mimi Joseph Roman Selasini, tofali halitaitwa mkate hata siku moja na kupongeza ni kuomba mara ya pili na kuhimiza utendaji. Niweke wazi pia kwamba mimi ni Mkatoliki na katika Ukatoliki tuna amri ya nane inayosema usiseme uongo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini nikumbushe marehemu Shaaban Robert alisema na nanukuu: "Msema ukweli ni mpenzi wa Mungu, sitaikana kweli nikichelea upweke wa kitambo, nikajinyima ushirika wa milele unaotazamiwa baada ya kuushinda uongo". (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tulipoanza mageuzi, tulianza na msemo kwamba upinzani siyo uadui na tutapingana bila kupigana. Hatukusema kwamba yote yanayofanywa tuyapinge isipokuwa tunaweza tukapongeza na tukasema kwamba tutafanya zaidi sisi mkitupa nchi. Serikali imejenga visima 1,000 lakini sisi mkitupa nchi tuna uwezo wa kujenga visima 3,000. Bado tutaendelea kuwa wapinzani na bado tutaendelea ku-*acknowledge* kile ambacho kimefanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukushukuru, kukutakia wewe pamoja na Wabunge wote kheri na baraka tele ili muweze kurudi katika Bunge lijalo kujenga nchi yetu. Pamoja na hayo, nawatakia ndugu zangu Waislamu wote popote walipo mfungo Mtukufu wa Ramadhan wenyе kufaa, mfungo ambaо utatusaidia kufanya toba na malipizi ya dhambi zetu ili Mwenyezi Mungu aweze kuleta baraka katika familia zetu, nchi na dunia kwa ujumla kwa sababu pamoja na yote ugonjwa huu wa *Corona* na nasisitiza, nimeona kwenye mtandao watu wakibea tunapoambiwa tufanye ibada, hakuna yejote aliyesema kwamba tusifuate taratibu tunazopewa na wataalam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza hotuba za viongozi wetu. Nimemiskiliza Waziri Mkuu, Waziri wa Afya na Rais mwenyewe hajawahi kusema kwamba tusivae barakoa, tusinawe, tusiweke *distance* na hajawahi kusema kwamba tusichukue hatua za kitaalam. Pamoja na hatua za kitaalam, tunapaswa kumlilia Mungu kwa sababu Mungu ndiye muweza wa yote na huruma ya Mungu haina mipaka. Huruma ya Mungu ipo kwa ajili ya watu wote wanaomlilia ili aweze kufungua akili za wataalam na watafiti ili waweze kutupatia dawa na kinga dhidi ya janga hili, peke yetu hatuwezi kufanikiwa. Ndiyo maana narudia na nasisitiza

maneno ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika hili tuache siasa, katika hili tuache kutumia vitabu vya dini kwa ajili ya kubeza. Mimi ni Mkristo, Biblia inatumika vibaya katika kuhalalisha tamaa za watu, tuache. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri kabisa. (*Makofii*)

Bado tupo Msekwa ambapo sasa ni zamu ya Mheshimiwa Justin Joseph Monko anatafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Philip Gekul wote wakiwa Msekwa.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara yetu hii ya Maji ambayo ni bajeti muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa neema na baraka zake ambazo ameendelea kutupatia sisi Watanzania kwa kutuepusha na gongwa hili la *Corona*. Nikushukuru sana wewe kwa maelekezo mengi ambayo umekuwa ukitupatia na kutufanya sisi tuendelee kutekeleza wajibu wetu tukiwa na afya njema na salama.

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nichangie kidogo katika bajeti yetu hii ya Wizara ya Maji. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli pamoja na wewe mwenyewe kupitia Bunge lako Tukufu kwa juhudi kubwa ambazo mnazonesha kwa kutaka kuwapatia Watanzania maji, mkitekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi ya kufikia mwaka 2020 angalau vijijini asilimia 85 na mjini asilimia 95. Nakushukuru sana wewe, Mheshimiwa Rais pamoja na viongozi wengine ambao wanafanya juhudi kubwa katika kutekeleza hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, bado tuna changamoto kadhaa. Kama ulivyoona mwenyewe kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, zipo changamoto nyingi ambazo zinakwamisha na mpaka sasa kwa taarifa aliyoisoma leo, tumefikia kiwango cha asilimia 70.1 kwa maeneo ya vijiji na asilimia 84 kwa maeneo ya mijini. Kiwango hiki utaona kwa kasi hii mpaka tutakapokuwa tunamaliza Bunge lako na mpaka kufikia uchaguzi ambao ilitakiwa ndiyo tutekeleze llani yetu ya CCM, tutakuwa hatujafika kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi kama tulivyoahidi.

Kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali, ni muhimu sana sasa tukafanya Mapinduzi makubwa kupitia kwenye Bunge lako hili Tukufu linaloendelea sasa na kuona namna ambavyo tunaweza tukawasaidia Wizara ya Maji ambayo kwa kiwango fulani tunaweza tukasema imeshindwa kutekeleza llani vizuri kufikia hapo ambapo tulikuwa tumetarajia.

Mheshimiwa Spika, tumeona miradi mingi bado haijakamilika, hata katika miradi iliyotangazwa kwamba inaendelea zaidi ya miradi 588, bado miradi mingi haijakamilika na muda uliobakia sasa hivi katika kutekeleza hiyo miradi ni mfupi mno. Tatizo hapa Wizara imekuja na changamoto ya upatikanaji wa fedha, inazungumzia habari ya uwezo mdogo wa wakandarasi, upotevu wa maji na mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukiyazungumza mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, nadhani lipo tatizo lingine pengine zaidi ya hili kwa sababu fedha tulitenga kwenye bajeti iliyopita na kwa mujibu wa maelezo ya Waziri ni kwamba Serikali imeendelea inaendelea kutoa fedha lakini tunafika mahali tunakaa tunalalamika tena kwamba fedha hazitoki kwa wakati. Tuna Mfuko wa Maji ambao ulitakiwa fedha hizo ziwe zipo muda wote; kila tunapovyoendelea kukusanya kwa ajili ya miradi ya maji lakini kinachosikitisha wakandarasi walio wengi hawapewi fedha kwa wakati. Fedha hazitoki, *certificate* zinatoka, watu wanazunguka watakwendwa wilayani kujiridhisha na mkoa unarudi kujiridhisha, Wizara na yenyeewe inataka ipite, zimekuwa ni fedha zinatumika kwenye

kuchungulia badala ya kuwaamini walioko huku kwenye wilaya ili waweze kutekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, sasa hili limesababisha wakandarasi wengi wameshindwa kutekeleza miradi kwa wakati na ndiyo sasa Waziri anaanza kulalamika anasema uwezo mdogo wa wakandarasi sasa tunajiliza maswali mengi tunao utaratibu mzuri wa kupitia manunuzi wa kutafuta wakandarasi wenye uwezo na Wizara inasimamia inakuwaje leo tufike mahali tuanze kusingizia wakandarasi inawezekana ikaja ikawa ndiyo sababu ya wananchi kutokupata maji nadhani Bunge lako tukufu linapaswa kabisa kipingana na jambo hili na kuitaka Wizara kufanyakazi ya kuhakikisha kwamba miradi yote ya maji inasimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, hatuvezi kuwalaumu Wizara ya Fedha kutokutoa fedha kwasababu fedha zinatoka baada ya miradi kuwa imekamilika tuna urasimu mkubwa kwenye Wizara ya Maji yenewe. Niliwahi kufuatilia zaidi ya miezi minane kwa mradi uliokuwa pale Mtinko na mradi wa Ngamo zaidi ya miezi minane Mkandarasi hapewi fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yapo maeneo ambayo ningemuomba Mheshimiwa Waziri na timu yake wajirekebishe wanaurasimu mkubwa hata ukipensa wale wa *DDCA* waende wakachimbe visima kule mizunguko ni mingi utaenda *DDCA* unaambiwa mara *RUWASA* sijui mara wapi hakuna mtu mmoja ambaye anauwezo wa kutoa maelekezo sahihi juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukijaribu kuangalia hata kwenye bajeti ambayo imewasilishwa Jimbo la Singida Kaskazini au Halmashauri ya Singida *DC* hakuna kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakuna mradi hata mmoja unao unaendelea. Sasa ningetamani sana baadaye Waziri atakapokuwa anajibu atuambie Singida Kaskazini atafikia namna gani 85% kwa wananchi wale ambao nao ni watanzania wanaotakiwa waweze kupewa huduma sawa na watanzania wengine.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia hata katika Jimbo lako wewe mwenyewe pale kuna kijiji kimoja tu kinaitwa sijui kijiji cha Vihungo uko mradi mmoja tu wa kunufaisha wananchi 3962 hatuwezi na wenyeewe ndiyo unaendelea uko kwenye asilimia ndogo hatuwezi tukafika mahali tukatoa huduma kwa wananchi tukiendelea na utaratibu huu tulionao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba sana Bunge lako liweze kuazimia sana katika kuhakikisha Wizara hii inatimiza wajibu wake na tuhakikishe wananchi wetu wanapata maji. Kule kwangu viko vijihi vya Ntondo, Msisi Ughandibee, Mitula, Migugu, Nongwa Mpoki, Mwalala, Makuro, Msikii, Gairo, Mughanji, Lamba na Mkulu hakuna miradi ya maji. Sasa tunapambana na corona wananchi hawa wanakwenda kuchota maji kule kwenye mabonde na ni bahati kwasababu sasa hivi kuna mvua zinazoendelea sasa lakini yale maji si safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri awaambie wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini tunawezaje kufikia lengo la kutekeleza llani ya CCM kwa utaratibu huu tunaokwenda nao. Ningemuomba sana Mheshimiwa Waziri wakae wajitafakari na walilettee Bunge lako Tukufu tatizo ni nini sasa tumeanza kuwatupia watendaji kwamba ndiyo hawatekelezi wajibu wao. Pale ninaye *engineer*mmoja mzuri sana *engineer* Mkalimoto, hana gari, hana pipipiki, hana baiskeli wako pale wanatekelezaje miradi ya maendeleo vijijini? Nimekwenda kwa Waziri mara nydingi nimeonana na Mheshimiwa Katibu Mkuu hawatoi magari. Magari waliyonayo yako wao tu wanakwenda kutembelea hiyo miradi ili waweze kuona kama miradi imetekelezwa au vipi. Ningeomba sana wahakikishe vitendea kazi kwa watendaji wetu hawa ili waweze kutekeleza wajibu wao vizuri.

Mheshimiwa Spika, RUWASA wamekuwa wakifanya kazi nzuri katika hatua za mwanzo ambao tumeanza lakini wanachangamoto nydingi kwenye vitendea kazi, lakini vile vile fedha sasa hivi kuna mradi pale katika Jimbo langu Mughamo pale tunaambiwa sasa RUWASA wale hawana uwezo wa

kufanya manunuzi hata ya kutengeneza tu ile DP huo mradi manunuzi yote yanakuja kufanyiwa huku makao makuu.

Mheshimiwa Spika, urasimu huu ndiyo unaofanya utekelezaji wa miradi unakuwa ni mgumu tunaomba sana viongozi wa mikoa na wilaya waweze kuaminiwa. Tumewaweka ni wasomi wazuri hatuwezi kutegemea Katibu Mkuu

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Monko nakushukuru sana ahsante sana watu wanamachungu kweli kweli na mambo haya ya maji. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Justin Monko kwa mchango wako na nakushukuru kwa kunisema bwana kamradi kamoja kakijiji kimoja katika jimbo lenye watu 400,000. Mheshimiwa Pauline Philip Gekul atafatiwa na Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maji, lakinia pia nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kutupa nafasi tena tukiwa wazima wenye afya tukiendelea kutimiza majukumu yetu najua ni kwa neema tu na wala si kwa nguvu zetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu Dkt John Pombe Magufuli kwa jinsi ambavyo analiongoza Taifa letu na kwa jinsi ambavyo amekuwa akitutia moyo wakati wa matatizo lakini kwa jinsi ambavyo amekuwa ni mtu anayemcha Mungu na akimtegemea siku zote. Nimpongeze sana na Mheshimiwa Rais wetu Mwenyezi Mungu ataendelea kukutia nguvu ukitimiza wajibu wako na sisi watanzania tukikuombea.

Mheshimiwa Spika, nipongeze Mawaziri wetu Mheshimiwa Waziri wa Maji Prof. Mbarawa, Mheshimiwa Naibu Waziri Jumaa Aweso, pamoja na Katibu Mkuu mwalimu wangu Prof. Kitila kwa jinsi ambavyo pia mnatumikia Wizara

hii. Wizara hii ni Wizara ya mfano mionganoni mwa Wizara zingine Wizara hii ni Wizara ambayo katika bajeti ya bilioni 705 ambayo wanaiomba, ni kama bilioni 28 tu ndiyo zinakwenda kwenye mishahara na *OC* lakini zaidi ya 80% zinakwenda kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze kwa dhati hii inaonyesha ni kwa jinsi gani Serikali yetu inawajali watanzania na wanania njema ya kutua ndoo kwa mama ambaye siku zote amekuwa akihanganya kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nipongeze Serikali kwa *delivery* ya pesa 75% katika Wizara hii fedha zake zimekuwa *delivered* hii inaonyesha ni jinsi gani ambavyo miradi ya maji tulioipitisha katika Bunge lililopita inaendelea kutekelezwa katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika leo nina mambo manne yakuchangia katika Wizara hii. Kwanza nipongezi na shukrani ambazo nimezitoa, lakini wana Babati mjini wamenituma mambo matatu. Jambo la kwanza niwashukuru Wizara hii pamoja na Serikali kutupatia fedha kwa muda huu wa miaka mitano kuna mambo mengi yamefanyika katika mji wa Babati kupitia Wizara hii ya Maji. Tumekamilishiwa miradi ifuatayo na wana Babati wanawashukuru nisiposema hili inawezekana nisiwatendee haki kwasababu miradi hii ilikuwa hajakamilika.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Malangi wa zaidi ya milioni 680 umekamilika, na mradi wa Nako wa milioni 801 umekamilika Haraa milioni 594 umekamilika na Ngara milioni 262 umekamilika Managa milioni 535 umekamilika, mradi wa maji Kiongozi milioni zaidi ya 400 umekamilika mradi wa maji wa kijiji cha Himiti zaidi ya milioni 400 umekamilika, mradi wa maji Imbilili Mheshimiwa Waziri ulifika wewe, Naibu wako, Katibu Mkuu mradi uliokuwa unatusumbua Mheshimiwa Waziri na siku ile ukamuweka yule mkandarasi ndani akaongeza kasi leo wanakijiji cha Imbilili wanakunywa maji zaidi ya milioni 506 umekamilika na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Ng'wang'warai milioni 51 umekamilika mradi wa maji Hala kisima milioni 155, mradi wa maji Bonga milioni 250. Nisipo shukuru zaidi ya bilioni 6 ambazo zimeletwa katika Jimbo la Babati mjini, nitakuwa mtu wa ajabu sana wana Babati wanawashukuru Mheshimiwa Waziri wetu pamoja na Serikali na kazi inaendelea. Naomba nishukuru wenzetu wa Tanesco kwa kutuletea pia nguzo kupeleka sasa kwenye mradi huu wa Bonga ambaa ulikuwa unasubiri fedha wanasubiri Tanesco wapeleke umeme pale.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya nguzo 1000 zimeingia mji wa Babati na nimpongeze meneja wangu wa Tanesco dada Khadija *engineer* Khadija kwamba anakwenda kupeleka sasa nguzo kwenye ule mradi na maji yanakwenda kuwafikia wana Bonga. Tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka kuzungumzia ni suala la mradi wa maji wa Singu. Mheshimiwa Waziri kwa namna ya pekee nikushukuru ulifika wewe Naibu wako, Katibu Mkuu mkipita pale mnapita Singu. Lakini nishukuru mlinitumia wataalamu kutoka Wizarani wakaenda Singu wakaona maji pale hayapatikani wakaenda Bacho, Babati Vijijini kwa pacha mwenzangu Mheshimiwa Jitu wakakubali kuunganisha Kata mbili, Kata ya Sigino na Kata ya Ari tupatiwe maji. Lakini siyo hilo tu kwamba miradi inayotekelizwa na Wizara ya Maji kwamba haifanyiwi *review*. Miradi hii inafanyiwa *review* mradi wa Singu mapendekezo ilikuwa bilioni 9 lakini wataalamu waliotoka Wizara ya Maji wakaja wakafanya *review* wakasema tunawapatieni huu mradi *uta-cost* kama bilioni 5.

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana Wizara mmefanya haya na nimeona kwamba mna nia ya dhati mmeniambia mwezi huu wa tano mnanipatia milioni zaidi ya 400 ule mradi wa Sigino Singu vijiji vitatu vilivyobaki uanze. Naiomba Serikali yangu Mheshimiwa Waziri nakuomba naamini katika vitabu hivi vinaonyesha mradi wa Signu ndiyo kipaumbele chetu cha Babati mjini. Niombe sasa hizi milioni 400 zije mwezi wa 5 ili tuanze kujenga kisima pale Mheshimiwa Naibu Waziri

engineer wetu wa BAWASA Iddi amekuwa akionyesha nia njema na ameshaanza kupeleka *material site*. Ninachoomba hizo milioni 400 ziflike halafu hizo bilioni 5 zifuate, na nishukuru hata katika bajeti hii mmekumbuka mradi huu wa vijiji vitatu katika Kata ya Sigino.

Mheshimiwa Spika, mradi huu utatusaidia sana kuondoa maji ya chumvi ambayo sasa yako mji wa Babati mradi huu ukikamilika wana Babati wataepukana na mabomba yao, sufuria zao kuharibika kwa chumvi Mheshimiwa Waziri na ulifika Babati walikueleza kuhusu maji ya Babati kuwa na chumvi. Mradi huu sasa ni *solution* ya wana Babati kuondokana na maji ya chumvi kwasababu tunatoa kwenye chanzo cha Bacho na ni maji matamu mazuri hayana chumvi kwa hiyo, ninaomba hizo milioni 400 na hizo bilioni 5 sasa ziende.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka niende kwenye jambo la tatu kuhusu mradi wa KFW ambao sisi pamoja na Mtwara tumekuwa tukitengewa fedha kwenye bajeti kwa muda mrefu.

Niombe Mheshimiwa Waziri kutoka moyoni nikuombe huu mradi umetumia miaka 12 tangu 2008 mmekuwa mkiweka *token amount* kwenye bajeti kila mwaka hata mwaka huu mmeweka bilioni mbili na milioni 500 lakini hakuna *delivery* ya hizi fedha. Mheshimiwa Waziri niombe pamoja na Serikali yangu na Waziri wa Fedha mtusaidie ni wapi mmekwama kwasababu kama kila mwaka tunaweza tukaweka kwa miaka 12 na huu mradi ulikuwa na lengo la kwenda kusaidia mfumo wa maji taka katika mji wa Babati na mji wa Mtwara na mwaka jana nilizungumza lakini hakuna majibu ya wapi mmekwama kwenye mkataba niombe hili sasa kwenye bajeti hii mtuambie. Hizi bilioni 2.5 zinakuja kweli na Mheshimiwa Waziri kama hao wenzetu Wajerumani hawatupi hizi fedha basi hizi bilioni 2 na milioni 500 tuongezee kwenye mradi wa maji wa Sigino kwa fedha zetu za *own source* maana kwenye bajeti yenu 49% ni *own source* hela zetu wenyewe ninaomba sasa mliangalie hili na mtupatие majibu baada ya kuwekea kwa miaka 12 bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, la mwisho Mheshimiwa Waziri bili za maji mji wa Babati bado ziko juu, nimeongea, nimeliwasilisha kwenu mkasema subirini tuangalie mchakato wa Ewura umefikia wapi na janga hili la corona bado wananchi wanatumia maji na bili za Babati ziko juu. Mheshimiwa Waziri unajua kabisa fika kwenye *list* ya bei za maji kwa *unit 1* kwa mikoa yote Tanzania Mji wa Babati ni miongoni mwa *top 5* ambazo bili zao ziko juu. Wana Babati wanakuomba Mheshimiwa Waziri tupatie majibu mnatupunguzia hamtupunguzii? Kwa sababu pia nimeshalisema mwaka jana mwaka huu naendelea kulisema tunaomba wana Babati kwa unyenyekevu mtusaidie kushusha bili za maji maana zimetushinda ziko juu ya uwezo wa wananchi wa Babati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niunge mkono hoja songeni mbele watanzania tunawaamini chapeni kazi na kwa miji tumeona taarifa zaidi ya 84% tumeshafika. Mji wa Babati zaidi ya 84% tuna maji sasa, lakini ni vijiji vitatu tu vimebakti katika mji wangu wa Babati. Kwa hiyo, niitie moyo Serikali yangu changamoto hazikosekanagi hata siku moja lakini ni jinsi gani tuna-*solve* hizo changamoto ndivyo ambavyo wananchi watakuwa wanaendelea kutuamini. Mheshimiwa Rais hongera, Mheshimiwa Waziri hongera, Serikali yetu hongereni tunasongambele tunaendelea kutekeleza ilani na naamini watanzania wanatuelewa tutatue hizo changamoto chache ambazo zimebaki, ahsanteni sana. (*Makofii*)

SPIKA: ahsante sana Mheshimiwa Gekul na hongera sana kwa miradi ya maji ulioipata kwa kweli ni mingi kweli kweli sijui unatumia mbinu gani mwenzetu kwasababu kwa kweli ukiangalia kuna *distribution asymmetry* kubwa fatilia hata Jimbo la Spika nimekaa hapa 20 years Wizara ya Maji yaani inafanya vitu vya ajabu kabisa vimiradi vya kuokota okota tu hapana hatuwezi kwenda namna hiyo lazima mkoa kama wa Dodoma ndiyo mkoa *the driest in the country* yaani huhitaji kuambiwa ukiwa katika Wizara ya Maji labda tunashindana na Shinyanga sijui nani zaidi na Simiyu labda unatarajia na miradi yetu sisi ni ya fedha kidogo kwasababu

maji yako chini siyo umbali yaani ukikuta mbali sana ni 120 meters that's all kama kule Kongwa mita 90, mita 70 mita ngapi lakini nasikia tu kama wanavyosema akina Mheshimiwa Gekul sijui wapi milioni mia ngapi mia ngapi ngapi 800 mia ngapi milioni, sasa lazima turekebishe hii hali huko tunako kwenda. Mheshimiwa Kiza Mayeye nilikutaja anafata Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Zedi ajandae.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia siku hii ya leo lakini awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya, amenipa uzima na kuweza kusimama siku hii ya leo hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee kabisa nitoe pole kwa mwenyekiti wangu wa chama Prof. Ibrahim Haruna Lipumba, familia na wanachama wa chama cha wananchi CUF kwa kuondokewa na Katibu Mkuu wetu Mheshimiwa Khalfa Suleiman Khalifa, Mwenyezi Mungu ampe kauli dhabiti mbele zake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijakwenda kwenye hoja nitoe pole kwa watanzania kwa janga hilli la corona. Hilli janga ni letu sote haliangalii chama, haliangalii rangi niombe tuungane kwa pamoja tupigane kwa ajili ya uhai wetu na uhai wa watanzania wote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nimepitia ripoti ya bajeti ya Waziri wa Maji nimpongeze anafanya kazi nzuri pamoja na Naibu Waziri lakini siku zote hata kama mtu anafanya kazi vizuri changamoto zikiwepo ni lazima tuseme ndiyo kazi yetu ambayo imetuleta hapa.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai lakini kila mtu anafahamu kwamba pasipokuwa na maji hakuna ambalo linaweza kufanyika. Na sisi hapa bila maji sidhani kama kuna shughuli yoyote ambayo inaweza kufanyika, ni ukweli usiopingika bado tuna changamoto kubwa ya maji katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nikianza tu na maeneo ya mjini kwa wale ambao tunaishi maeneo ya Goba Dar es Salaam watakuwa ni mashahidi bado kuna shida ya maji katika baadhi ya maeneo. Lakini hata kule Kimara bado maji ni changamoto wakazi wanapata shida ya maji. Lakini nikirudi katika Mkoa wangu wa Kigoma pamoja na kwamba ni mkoa ambao tumebarikiwa kuwa na Ziwa Tanganyika, Mto Malagarasi, lakini wakazi bado wanateseka kwa shida ya maji. Vipo vijiji ambavyo mpaka sasa toka nazaliwa mpaka umri huu havijawahi kuona maji safi na salama. Vijiji vya Mkabogo, Kiziba, Kalinzi, Mkigo na Pamila. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niombe sana Mheshimiwa Waziri kuna mradi huu wa Ziwa Tanganyika ambao sasa umeanza Mkoa wa Kigoma muweze kuwafikiria wakazi wa vijiji hivi na wao waone faida ya kuwa na Ziwa Tanganyika katika mkoa wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka mwaka 2019 nilisimama hapa nikamwomba Mheshimiwa Waziri, kuna kijiji cha Mwandiga ambacho natokea, ndicho kijiji ambacho nimezaliwa. Ni kijiji ambacho ni Mji Mdogo lakini kinahudumia wakazi wengi. Tulimwomba Mheshimiwa Waziri kwamba maji haya ya mjini, ya Manispaa ya Kigoma Ujiji yaweze kufika katika Mji huu Mdogo wa Mwandiga.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na kumshukuru kwamba tayari wameanza kazi pale, lakini kwa taarifa ambazo ninazo, bado haujakamilika kwa sababu kuna *pump* ambazo wameagiza nje na wameahidi zitakuja mwezi wa Nne na mwezi wa Nne ndiyo huu unakwenda kwisha, naomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe Kijiji hiki cha Mwandiga kinapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kijiji hiki kwa ufupi ndicho ambacho kwa sana wagonjwa wa *corona* itakuwa ni *center*, lakini bado akina mama wanaendelea kuhangaika kutafuta maji safi na salama. Sasa kama mradi huu utachelewa kama walivyosema mwezi wa Nne wanaleta *pump* na wakachelewa na tuna janga la *Corona*, maana yake mama

zetu uwezekano wa kuambukizwa ugonjwa huu ni mkubwa kwa sababu wataendelea kwenda kupanga foleni, kuweka mikusanyiko kwa ajili ya kutafuta maji safi na salama. Naomba sana kadri tutakavyoweza, Mheshimiwa Waziri basi tupate maji katika kijiji hiki.

Mheshimiwa Spika, hapa hapa niongezee na naiomba Wizara, Kijiji cha Mwandiga tupo Kigoma Vijiji, lakini tayari tumeingia kwenye mradi wa Mkoa wa Kigoma Manispaa, kama itampendeza Mheshimiwa Waziri, basi mradi huu utakapakamilika na kuunganishwa na wananchi wote, basi tuweze kuingia katika *system* ya KUWASA badala ya RUWASA.

Mheshimiwa Spika, niongelee jambo lingine kuhusu undeshaji wa miradi ya maji kwa kutumia *diesel*/katika baadhi ya maeneo. Natambua kwamba kuna maeneo ambayo wanatumia *solar*, kuna maneno ambayo wanatumia *diesel*, lakini katika Mkoa wangu wa Kigoma wilaya ninayotokea, yapo maeneo ambayo wanatumia *diesel*; ni hasara. Mbali na hasara, kutokana na uendeshaji wa *diesel*, bado mfumo wake unasababisha wananchi hawa kukosa maji kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mheshimiwa Waziri na nimshauri kitu hapa, hebu katika maeneo haya ambayo wanayotumia *diesel*/katika Wilaya ya Kigoma Vijiji, wajaribu ku-practice *solar* waone mafanikio yake yatakwendaje? Yapo maeneo kwa mfano jirani zetu wa Katavi tangu mwaka 2016 wanatumia *solar* katika mradi wao maji na mpaka sasa wanapata maji safi na salama bila tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili tuweze kuepuka gharama hizi, naomba sana suala hili Mheshimiwa Waziri aweze kulichukua tuweze kutumia *solar* na tayari kuna maeneo ambayo wanatumia, watu wa *Water Mission* wamefunga kwa mfano Kijiji cha Kalalambago na Matiazoo tayari wanafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, nikugusie miradi hii ambayo inachelewa. Wamezungumza Waheshimiwa wengine. Mbali na kwamba Wakandarasi hawapewi fedha, lakini yawezekana miradi hii inachelewa kwa sababu hatuna *master plan* nzuri ambazo zinaweza kupanga hatua kwa hatua. Kwa hiyo, nafahamu Mheshimiwa Waziri anafanya kazi vizuri na wala sina wasiwasi naye baba yangu, hebu jaribuni kuweka *master plan* ambazo mtafanya kwamba leo tunaanzia hapa, mwaka huu tutafanya eneo hili; nadhani itaweza ikasaidia miradi hii kukamilika kwa wakati na kuepuka milundikano ya kuwa na miradi ambayo haitekelezeki. Kwa sababu toka nakua nafuatilia Bunge, lakini kila Mbunge anayesimama ana-*complain* suala la maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana suala maji; maji ni uhai hakuna chochote bila maji. Nawaomba sana Wizara mjitahidi maeneno mengi yapate maji.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Wakandarasi. Yapo maeneo ambayo kuna uhaba wa Wakandarasi, lakini tunao Wakandarasi na vijana ambao wame-*qualify* katika maeneo na wanaweza wakatusaidia katika kutatua changamoto hizi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri kama itakupendeza, najua ajira ni changamoto, mpaka kibali cha ajira kitoke Utumishi, basi toeni kibali katika maeneo kama mkoa waweze kuajiri vijana ambao wapo *competent* na wanaweza wakatusaidia maeneo yetu katika suala la maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitatoa shukrani. Sisi ni Wabunge ambao tumeingia kwa miaka mitatu kama siyo miaka miwili na nusu. Nawashukuru Wabunge wote kwa kutupokea vizuri, mmekuwa ni mfano mzuri kwetu, tumejifunza mengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuwa pamoja nasi na kutuelekeza mambo mbalimbali. Nawatakia kila heri na

ninamwomba Mwenyenzi Mungu atusaidie tuweze kurudi wote, kutuweze kuwatumikia Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nawatakia Waislamu wote Ramadhani Kareem. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Felister Aloyce Bura na kwamba atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Zedi. Mheshimiwa Bura tafadhalii.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi na ninamshukuru Mwenyenzi Mungu kwa afya njema aliyonijalia siku ya leo. Sitawatendea Wana-Dodoma jambo la busara nisipompongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ya maendeleo kwa nchi yetu. Wengine walidhani ni moto wa mabua, wakabeza tulipoanza, lakini kwa utendaji wake uliotukuka, amefunga vinywa vya wabezaji na sasa kila mmoja anampongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, utawala na kazi hazikosi changamoto. Kwa hiyo, changamoto tunazoziona ni za kawaida kabisa, lakini utawala wa Awamu ya Tano unafaa kupongezwa. Mbali ya kupongezwa, kumwombea kwa Mwenyezi Mungu Rais na Wasalidizi wake wote, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na hata Mawaziri wote tuwaombee kwa Mwenyenzi Mungu waendelee kufanya kazi yao ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipokupongeza wewe. Umefanya mambo makubwa mno katika Bunge letu; umeleta maboresho makubwa mno katika Bunge letu. Wabunge wa awamu hii hatutakusahau. Tulizoea kubeba vitabu, tulizoea kununua mabegi kwa ajili ya vitabu, lakini maboresho ulioleta katika Bunge hili, Mungu akubariki sana, Mungu akulinde sana.

MBUNGE FULANI: Amen.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kongwa wanajua kazi unazozifanya hapa Bungeni, lakini hata kazi unazozifanya kule uliko kwenye Jimbo lako, naamini hawatakusahau. Tetesi ninazosikia ni kwamba utapita bila kupingwa. Nawapiga debe wako tupo kwa ajili ya kuwa Spika kwa kipindi kinachokuja. Mungu akubariki sana. (*Makofi/Vigelele*)

Mheshimiwa Spika, bajeti tunayozungumza ni Bajeti ya Wizara ya Maji. Nampongeza Waziri mhusika na timu yake kwa kazi nzuri wanayofanya na niendelee kuwaombea mtekeleze wajibu wenu kwa wananchi kwa sababu maji ni uhai na bila maji hakuna uhai kwa viumbe, wanyama na wanadamu pia.

Mheshimiwa Spika, tumeongea sana habari ya kuvuna maji ya mvua. Nitoe mfano, ukitoka katikati ya Makaravati na Mbande kuna maji mengi sana pale; ukitoka pale mpaka ufikie Kibaigwa; na ukitoka kibaigwa mpaka Pandambili kuna maji mengi sana kipindi cha mvua. Sasa hivi tunaona kila eneo watu wanalamika madaraja yamesombwa, nyumba za watu zimejaa maji. Kwa sababu hatuna mpango mahsuswa kuvuna maji, hili tumelizungumza sana kwamba tuwe na mpango mahsuswa kuvuna maji.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Kiangazi maeneo yetu hasa Kanda ya Kati Mkao wa Dodoma na Mkao wa Singida na pengine Tabora kuna matatizo makubwa sana, wanawake wanahangaika kutafuta maji kipindi cha Kiangazi, wanyama wanahangaikiwa kutafuta maji. Kwa hiyo, ukisikia tuna shida ya maji, ni katika mikoa ya *central zone*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ingekuwa busara kama tungejenga mabwawa. Haya maji ya mvua yanakwenda wapi? Tungevuna haya maji kwa sababu mwaka huu tuna neema ya maji, lakini je, mwakani kama tuna Kiangazi tutaanza kuhangaika, wanyama watahangaika na wanadamu watahangaika, kwa sababu hakuna maji na hatukuyakinga. Tulisema tuyakinge maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Bunge la bajeti iliyopita ulishauri kwamba tuyajenge mabwawa. Serikali ijenge mabwawa kukinga maji kwa matumizi ya kipindi cha kiangazi. Maji haya yanaingia kwenye majumba ya watu, yanavunja madaraja kwa sababu hayana pa kwenda. Yangekuwa na mahali pa kwenda yasingeingia kwenye majumba ya watu wala madaraja yasinge bomoka. Tutafute namna ya kukinga maji au kujenga mabwawa kwa ajili ya matumizi ya wanadamu na wanyama ili watu wasiendelee kuhangaika. Maji ni mengi na mwaka huu kuna maji mengi mno, sana, sana na yanafanya uharibifu.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka pia Bunge hili lilishapendekeza kwa Serikali na lilishaamua kwamba taasisi za Serikali tuwe na matenki ya kuvuna maji ya mvua. Nyumba za Umma zinazojengwa, taasisi, shule, zahanati, Vituo vya Afya wajenge miundo mbinu ya kuvuna maji. Naona taasisi zinajengwa, tunashukuru sana na tunaipongeza Serikali sana, kwamba Vituo vya Afya vingi vimejengwa, lakini hakuna miundombinu ya kuvuna maji na wala taasisi zetu zisingehangaika na bili ya maji, kwa sababu kuna kivuna maji kama matenki, ni makubwa, wanaweza kutumia kwa kipindi kirefu bila kutafuta maji kama ya DUWASA, RUWASA na maji ya maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, naona taasisi hizo zinajengwa, shule zinajengwa, lakini hakuna miundombinu ya uvunaji maji. Nadhani Serikali iangalie jambo hili la kuvuna maji katika taasisi zetu, lakini hata kwenye nyumba za Umma. Naomba sasa katika Mji wetu wa Dodoma ndiyo Makao Makuu na maji ambayo tunayo kwa sasa ni ya kutosheleza idadi ya watu waliopo kipindi hicho kabla ya Serikali kuhamia Dodoma. Najua kule kwenye Mji wa Werikali wamechimba visima, lakini kuna Vyuo Vikuu vitano vinajengwa njia ya Singida. Vyuo Vikuu vitano hakuna maji kule, pale Nala hakuna namna ya kupata maji, pale Chigongwe hakuna namna ya kupata maji, Vyuo Vikuu vitano hivyo ninavyovijua.

Mheshimiwa Spika, kuna taasisi wawekezaji binafsi wanatamani kujenga viwanda Dodoma. Kampuni ya Bia

wanajenga kiwanda kikubwa Afrika Mashariki, kinajengwa Dodoma. Kama hakuna maji, hawataweza, hawatafanikiwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali ya Awamu ya Tano, kuna haja ya kuiangalia Dodoma kwa upande wa maji kwa jicho lingine. Hizo taasisi zinazokuja wapate maji, Vyuo Vikuu vinavyojengwa, vipayate maji; wawekezaji wanaoingia Dodoma wapate maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, milituambia mnachimba bwawa la Farkwa na bwawa la Farkwa limekuwa kama ni hadithi. Muda mrefu tunalizungumzia, hakuna ufanisi katika hili. Fedha zitengwe. Nimengalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya kujenga bwawa la Farkwa. Kwa Farkwa tulisema litasidia Wilaya ya Chemba, Wilaya ya Chamwino, Wilaya ya Dodoma Mjini na Wilaya Bahi. Karibu wilaya nne za Dodoma hakuna kinachoendelea na fedha zimetengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba wananchi wamelipwa lakini bado wananchi 256 hawajalipwa fidia. Kwa hiyo, kwa sababu wale hawajalipwa fidia, hawawezi kutoka na fedha hazijatengwa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bahi imechelewa sana kuendelea kwa sababu ya ukosefu wa maji. Imechelewa sana, watu hawajengi pale. Sasa hivi ndiyo angalau baada ya maji ya kupatikana; lakini maji hayatoshelezi. Mbunge wa Jimbo amempa Mheshimiwa Waziri barua ya kuomba, kuna vijiji vyetu vitatu; Kijiji cha Chalinsanga, Kijiji cha Chaligongo na Kijiji cha Lukali. Tumechimbiwa visima pale, hakuna miundombinu. Namwomba Mheshimiwa Waziri, tunaomba fedha au tunaomba miundombinu iwekwe pale ili wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya chemba ni Wilaya ya siku nydingi sana, lakini hakuna maji pale. Waziri Mkuu alipotembelea alipokuwa kwenye ziara pale alituahidi takribani shilingi bilioni 10, kwamba zitapekwa pale kwa ajili ya kuchimba maji, wananchi Wilaya ya Chemba wapate maji, lakini mpaka leo hatuoni kitu chochote kinachoendelea.

Naiomba Serikali yangu sikuvi basi Makao Makuu ya Wilaya zote, Serikali ione namna ya wananchi wanawenza kupata maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho nampongeza sana Mheshimiwa Ummy na Wizara yake na Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa ya kuamua wanachi waendelee kuabudu. Hii ameisema Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba wananchi waendelee kuabudu. Hajafunga Misikiti wala Makanisa, watu wamwombe Mungu kwa ajili ya ugonjwa wa *Corana*. Tuzingatie masharti...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, tuzingatie masharti ya Wizara ya afya, lakini pia tumwombe Mungu ili gonjwa hili alipitishie mbali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Felister Aloyce Bura kwa kuisemea Dodoma. Tunakushukur sana.

Mheshimiwa Bura nikwambie tu, kwenye miradi inayoendelea Kongwa, kijiji kimoja tu, tena kijiji kidogo sana kinaitwa Vihingo basi; mh! Hakuna mradi mpya mwingine wowote ule. Wilaya nyingine vijiji 27, vyingine vijiji 30 vyingine vijiji 20, sisi wengine kijiji kimoja. Sasa hii Profesa, yaani hii ni hatari kubwa kabisa. (*Kicheko*)

Yaani mnamtaka na Spika naye awe anafanyaje? Naye ni Mbunge wa Jimbo vilevile. Ndiyo maana nikasema kuna *distrubition asymmetry* kubwa sana na hii ndiyo inaleta nchi nyingine kudai mambo ya Sera za Majimbo ili bajeti ya Taifa katika kugawana keki iende ili kila watu mahali pao angalau waweze kujipangia hali fulani. Ninyi ndiyo mnaleta

hizo fikra za watu tugawane. Yaani Bunge liwe la kugawana keki ili turudi kwenye kanda zetu au mikoa yetu sasa tukapange mipango. (*Makofii*)

Maana yake ukipanga kitaifa, matokeo yake ndiyo haya, kwamba wengine tukae hapa; na ninyi mnatuharibu kuiita ya CHADEMA. Kabisa! Ni jambo zuri tu, lakini mnapo *privatize* eeh! Matokeo yake ni haya, kupanga *national cake*; matokeo yake ni haya. Spika mzima unarudi na kijiji kimoja. Wale wengine mabilioni ya shilingi, mabilioni, mabilioni *year after year* mabilioni, mabilioni, wengine vimilioni ambavyo havieleweki, *this is very wrong*. (*Makofii*)

Lazima kwenye jambo la maji na mambo haya ya huduma za jamii tuwe na mtazamo wa Kitaifa. Tuwe na huruma na watu. Wataalamu ambao mpo kule lazima mwangalie haya mambo. Halwezekani namba hii, mabilioni ya shilingi mwengine hakuna kitu, wengine miradi inapotekelvezwa; *this is very wrong*. Hatuwezi kwenda namna hii! Ndiyo maana nikasema, Serikali siyo ya kulaumiwa. Hili tatizo lipo Wizara ya Maji, siyo Wizara ya Fedha, lipo lipo Wizara ya Maji. Hili ni tatizo la *distribution*. *Very unfair distribution!* Tunakwendaje namna hii? Haiwezekani! Profesa tutakupitishia bajeti yako, lakini *you have to know, we are not happy*, kabisa! Mgao gani huu? Hovyo kabisa!

Profesa Suleiman Zedi.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia, kwenye Wizara hii muhimu sana ya Maji. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya ambayo imeniwezesha kusimama na kuweza kutoa mchango wangu kwa niaba ya wananchi ninaowawakilisha katika Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuipongeza Wizara ya Maji na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa sana ambayo wamefanya hasa nikiwa mwakilishi ninayetoka katika Wilaya ya Nzega. Kwa muda mrefu sana

tumekuwa tukisemea matatizo ya maji ambayo yamekuwa yakiwakabili wananchi wa Jimbo langu la Bukene na hata Wilaya nzima ya Nzega, tulikuwa na tatizo sana la upatikanaji wa maji chini ya ardhi, lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi kubwa sana. Hivi ninavyoongea Mradi mkubwa wa kuyatoa maji ya Ziwa Victoria – Kahama kuyafikisha Tabora umeshafika katika Wilaya ya Nzega. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita tu Mamlaka ya Maji ya Kahama na Shinyanga ilisaini mkataba na Mamlaka ya Mji wa Nzega pale (*NZUWASA*) kwa ajili ya sasa kuanza kuuziana maji na baadhi ya maeneo kwa kweli huduma hii imeshaanza. Niseme tu kwamba maji yanayotoka katika Ziwa Victoria ni maji ambayo ni chanzo cha uhakika na chanzo salama. Hili ndo lilikuwa tatizo letu kupata chanzo cha uhakika cha maji, kwa hiyo liliobaki sasa ni *distribution* tu. Huu mradi sasa hivi unatupatia maji kwenye vijiji 54 katika Wilaya nzima ya Nzega lakini nina uhakika kabisa vijiji vilivyobaki sasa havitakuwa tena na tatizo la maji kwa sababu sasa kitakachofanyika ni kuyasambaza tu kwa sababu sasa chanzo tunacho, hatutahangaika tena kama ambavyo tulikuwa tunahangaika miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji Profesa Mbarawa ambaye baada ya kipindi kirefu cha maombi yangu ya kupatiwa chanzo cha maji cha uhakika, alifunga safari hadi Bukene kwenye Jimbo langu kuangalia kero na changamoto za maji. Baada ya hapo mchakato wa kiserikali ulifanyika na sasa zimeidhinishwa zaidi ya bilioni sita ambazo sasa zinakwenda kutupatia maji kwenye vijiji 20 katika Jimbo la Bukene. Nafahamu kwamba mchakato wa Wizara kwa kuititia *RUWASA* umeshafanyika kwa maana ya kufanya tathmini ya kina lakini ninazo taarifa kwamba (*procurement*) ununuzi wa vifaa na jema ni kwamba mradi huu sasa unakwenda kutekelezwa kwa *Force Account* siyo kutumia mkandarasi tena.

Mheshimiwa Spika, Wizara inanunua vifaa na ninafahamu kwamba mradi huu ni *package* moja na Mradi

ule wa kupeleka maji Goweko na kupeleka maji Nkinga kule kwa Mheshimiwa Gulamali. Kwa hiyo nafahamu kwamba Wizara iko kwenye hatua ya kufanya manunuzi ya vifaa na vifaa vitakavyopatikana *RUWASA* wenywewe chini ya usimamizi wa Wizara watatekeleza mradi huu, hautatekelezwa na wakandarasi na hivyo nina uhakika kwa sababu tumeshaona *Force Account* zinaishia kuokoa fedha.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Wizara kwa uamuzi huu wa kutupatia zaidi ya bilioni sita ambazo zinakwenda kupeleka maji katika vijiji 20; Kijiji cha Shigamba, Kagongwa, Itobo, Lakui, Chamwabo, Bukene yenywewe, Kijiji cha Kabanga, Uduka, Usongwahala, Kayombo, Mwamala, Kishili, Seki, Chamiwa, Kasela, Senge, Lububu na Uduto. Vijiji vyote hivi vinakwenda kupata maji ya uhakika kwa ajili ya shughuli za wananchi. Hili ni jambo kubwa sana kwa sababu kero ya maji katika maeneo yetu huko ilikuwa ni kero ambayo inashindwa kupatiwa ufumbuzi kwa sababu tulikuwa hatujapata chanzo cha uhakika, lakini sasa Ziwa Victoria limetuletea chanzo cha uhakika na tatizo la maji linakwenda kuwa historia katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda nilizungumzie ni kwamba, baada ya miradi ya maji kupatikana, kujengwa na kukamilika kinachofuata sasa ni usimamizi wa hii miradi ili miradi iwe endelevu.

SPIKA: Mheshimiwa Zedi nataka kukwambia tu kwamba, kwanza nakupongeza, wakati wewe unapata bilioni sita na vijiji vyote hivyo sisi Kongwa hakuna hata Kitongoji kimoja chenye hiyo *Force Account*, lakini nakupongeza, Wanyamwezi endeleeni kupata maji. (*Makofi/ Kicheko*)

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipongeza...

SPIKA: Kwa hiyo pamoja na yote, ni vizuri kwa kweli *nationally* pamoja na kwamba mnapata Waheshimiwa Wabunge na mnajipongeza kuendelea kuishauri hii Wizara

iache upendeleo. Kwani ingepunguza kijiji kimoja kwako ikatuletea na sisi kijiji kimoja ungepungua nini!

Endelea tu Mheshimiwa Zedi, ni tatizo kubwa sana unaweza ukawa wewe unayepata ugali unaona kwamba wewe unashiba, lakini mwenzako katika familia ile ile hapati hata tonge moja, hili ni tatizo kubwa kabisa hili. Endelea Mheshimiwa Zedi.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipongeza kupata maji kwenye vijiji 20 ambapo Serikali inapeleka zaidi ya bilioni sita. Kwa hiyo nilichokuwa nasema ni kwamba jambo linalofuata sasa ni usimamizi wa hii miradi ili iwe endelevu. Kwa kipindi kirefu tunafahamu kwamba mradi wa maji ukikamilika inatakiwa iundwe Jumuiya ya Watumia Maji ambayo ndiyo itasimamia huu mradi kuhakikisha unakuwa endelevu. Nina taarifa kwamba mwongozo mpya wa uundwaji wa hizi Jumuiya za Watumia Maji unaelekeza kwamba kila jumuiya inatakiwa iajiri wataalam wawili. Mtaalam wa kwanza ni fundi ambaye anatakiwa awe na elimu ya kidato cha nne na cheti cha ufundi (*Technician*), mtaalam wa pili ni Mhasibu ambaye anatakiwa awe na elimu kidato cha nne lakini na elimu ya uhaisibu. Huyu Mhasibu atashughulikia shughuli zote za ukusanyaji wa mapato na huyu fundi atashughulikia shughuli zote za ufundi.

Mheshimiwa Spika, huyu fundi na Mhasibu watakuwa wanalipwa kutokana na makusanyo yanayopatikana kwenye mradi husika. Sasa miradi inatofautiana, mingine mikubwa mingine midogo, kwa mfano, Mradi wa Bukene Mjini unaweza kujitosheleza, makusanyo yao ni mazuri, lakini kuna vijiji vingine nahisi makusanyo yao yanaweza yasiweze *sustain* kuwalipa; fundi na Mhasibu. Ukisema tu wanalipwa kima cha chini laki tatu tatu maana yake ni kama 600,000 kwa mwezi. Kwa hiyo ushauri wangu ni kwamba, vijiji vingine, hizi jumuiya ziunganishwe. Kwa mfano ushauri wangu ni kwamba maeneo kama ya Vijiji vya Lakui, Itobo na Chamwabo vinaweza vikaunda jumuiya moja badala ya kila kijiji kuwa na jumuiya yake. Kwa hiyo wakaajiri fundi mmoja

na Mhasibu mmoja kwa vijiji vyote. Hata Kijiji cha llagaja na Champipulu kwa mfano badala ya kila kijiji kuunda jumuiya yake wanaweza wakaunganisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ushauri wangu ni kwamba huyu fundi na huyu mhasibu...

SPIKA: Mheshimiwa Zedi ni kengele ya pili malizia.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, ushauri wangu hapo ni kwamba Jumuiya za Watumia Maji zisijali mradi mmoja mmoja, maeneo mengine ni kwamba hata vijiji vitatu au vinne viunganike viwe na Mhasibu mmoja na fundi mmoja ili waweze kuwalipa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii kwa sababu kwa kweli kwa Wilaya ya Nzega, Wizara ya Maji na Serikali ya Chama cha Mapinduzi wametutendea haki. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa John Heche atafuatiwa na Mheshimiwa William Mganga Ngeleja na Mheshimiwa Christopher Chiza ambao wote wako Msekwa watafuatia.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa kuweza kuchangia. Nataka nikuunge mkono kwenye hoja ya Serikali ya Majimbo kwamba itakuwa suluhu kwa matatizo mengi madogo madogo. Haiwezekani Bunge likakaa hapa kujadili choo kwenye shule ya msingi fulani kule kijijini, haya mambo yote, keki ingegawanywa hapa halafu Mabunge madogo madogo kwa maana ya halmashauri washughulike kule kupeleka miradi hii ya maji; miradi ya kitaifa ibaki michache ili kusaidia wananchi kupata maendeleo kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Kitwanga ameongea Kibunge na umetufundisha hapa, umemkanya kidogo kwamba asije akazungumza akapiga kura ya hapana kwa sababu ni *three line whip*. Kwa hiyo

nafikiri na Wabunge wa CCM mtuelewe sisi tunapopiga kura ya hapana kukataa bajeti yenu kwa sababu utaratibu ni huo, lakini pia mnakuwa mambo mengi hayako sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni jambo la *corona*, Mheshimiwa Waziri Mpango alituambia hapa tulipoanza kwamba wameunda Kamati mbalimbali zinashughulika na haya masuala halafu watatuletea hapa taarifa. Hili ndio Bunge la wananchi, hiki ndio chombo kikuu, *supreme organ* ya wananchi ambayo inaweza kuja hapa ikaangalia suala hili kwa undani na kuishauri Serikali na hata kutafuta Mafungu kutoka sehemu mbalimbali ikamega ikapeleka hapo. Hili suala linazidi kuwa na taharuki na kwa siku mbili, tatu hizi ambazo hakuna *update* yoyote mitandao ya kijamii, mambo yanazidi kuchanganya sana.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi imeonekana kule Dar es Salaam maiti imetupwa barabarani, imechukua muda mrefu sana kuja kuokotwa, *video* zinasambaa, nafikiri na wewe umeziona. Naomba sana Bunge hili lifanye kazi hii ya muhimu ya wananchi, tujadili hili suala tuelekeze Serikali na hili suala siyo la chama siyo la nini, tusije tukaingia kwenye matatizo makubwa ya kupoteza watu wengi, nakusihii sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tunapozungumza hapa maji yamechuruzika Nyamongo, maji ya sumu kutoka kwenye *TSF* inayotunza maji ya sumu pale yameingia kwenye miji ya watu. Mgodi umechukua hatua za dharura na niliongea na Waziri wa Mazingira asubuhi, lakini naongea na Wizara hii kwa sababu ndio inahusika na maji haya machafu. Mgodi umechukua hatua za dharura kuchukua *pump* na kuweka kwenye *TSF*, ume-*pump* maji kutoka kwenye *TSF* unapeleka kwenye sehemu inaitwa *Ramapity*. Sasa *Ramapity* kule chini hawajatandika lile zulia gumu ili kuzuia yale maji *ku-penetrate* kwenda chini ambayo yanakwenda kwenye visima moja kwa moja na yataua watu.

Mheshimiwa Spika, juzi Serikali iliupiga mgodi faini kwamba wamekuwa wakichuruzisha maji ya sumu ambayo yamesababisha mauaji ya watu wa Nyamongo. Sasa kwa

sababu yale maji yalikuwa yanakwenda kukithiri, hapa nina *video* za maji yanachuruzika kwa *speed* yanakwenda mpaka Mto Mara na pengine yatakwenda Ziwa Victoria, yataleta athari kubwa sana kwa maisha yetu. Naomba sana Waziri hili ni jambo la kidharura, atuambie ni hatua gani wanachukua kwa dharura ku-rescue maisha ya watu wa Nyamongo. Hatutakubali tena watu wafe kwa wingi kiasi kile kwa sababu ya maji ya sumu yanayochuruzika kwa sababu ya uzembe wa watu kushindwa ku-*anticipate* masuala haya ambayo ni ya usalama wa maisha yetu, hilo ni jambo la pili.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, Mheshimiwa Aweso alikuja Sirari na alikuja wakati kaka yangu amefariki, lakini kwa uzito wa Mradi ule wa Maji wa Sirari ambao tulipewa fedha na *African Bank* tangu mwaka 2009. Huo mradi fedha zikapitia *East Africa*, wenzetu wa Kenya walishakamilisha mradi wao tangu mwaka 2012, leo tunazungumza ni mwaka 2020. Halmashauri sisi tumejitalahidi, tumenunua eneo tukajenga *tank* wameshindwa kuleta shilingi bilioni moja na milioni mia mbili mradi ambao ungesaidia kutatua matatizo ya maji kwenye kata tatu. Kata ya Legicheri, Gwitiryo na Sirari ambazo zina watu zaidi ya 75,000. Mheshimiwa Waziri alikuja pale, tukiwa na yeye tumezungumza, amekagua mradi, imekuwa kimya kama anachozungumza Mheshimiwa Spika hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hapa baadaye mtu anasimama anatuambia sisi tumpongeze, hivi mimi nakupongeza kwa lipi hapa! Nakupongeza kwa kunyima watu wa Sirari maji ambao wanaendelea kuteseka hasa kipindi hiki cha *corona*. Fedha hizi ambazo tumepeewa wengine wameshazitumia, Kenya mradi wao unafanya kazi, sisi ambao Halmashauri yetu tumejitalahidi tumetoa fedha, kuleta fedha tu kwa ajilli ya kusambaza maji kwenye miji ya watu imekuwa ni kero.

Mheshimiwa Spika, mambo haya yanakasirisha sana na haya mambo yanababisha watu wanazungumza mambo ya kuhoji mambo mengi sana. Kwa sababu kwa mfano leo tunazungumza, maji yametoka Ziwa Victoria

yamekwenda mpaka Shinyanga, maji yametoka Ziwa Victoria yanakuja Tabora lakini leo tunazungumza watu wa Mkoa wa Mara ambao kuna Ziwa hakuna maji, tukiwaambia mnatubagua, mnasemaje hapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serengeti hakuna maji, Tarime hakuna maji tena katika hili mngeweza kufanya *propaganda* eti ooh huko ni Wabunge wa Upinzani, lakini tunazungumza Serengeti hakuna maji, Rarya ambako kuna Mbunge wa CCM miaka yote ziwa liko Ryarya hakuna maji. Mheshimiwa Spika wetu hapa analalamika hamjampeleke maji mpaka Spika, sasa haya mambo hayawezi kukubalika, hatuwezi kuendesha nchi kwa ubaguzi na kwa upendeleo. Tunataka maji haya ya Ziwa Victoria na sisi watu wa Mkoa wa Mara ambao ndiyo maji tuwe *priority* namba moja kwenye haya maji. (*Makofi*)

TAARIFA

SPIKA: Mheshimiwa Heche pokea taarifa.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika,...

SPIKA: Mheshimiwa Heche subiri kuna taarifa.

MHE. RICHARD P. MOGO: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa rafiki yangu Mheshimiwa Heche analalamika kwamba kwake hakuna maji, lakini Halmashauri yake wanapokea fedha toka kwenye mgodi siyo chini ya shilingi bilioni tatu ambazo angeweza kuzipangia katika miradi ya maji. Vilevile ukiangalia kwenye Randama kila Halmashauri zote 185 zimetengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maji.

SPIKA: Mheshimiwa Heche unapokea hiyo taarifa?

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, naomba niendelee tu kwa sababu ndugu yangu ametaka tu asikike, kwa sababu fedha ambazo Halmashauri inapokea siyo hisani, ni fedha za mapato ya ndani. Ni makusanyo kama ninyi

mnavyokusanya kwenye *service levy*, ni fedha ya *service levy*, kwa hiyo usiseme tunapewa fedha kutoka mgodini hakuna fedha tunayopewa sisi kutoka mgodini. Kwa hiyo hizi fedha nazo zimepangiwa ndiyo maana sisi tuna vituo tisa vipyta vyta afya na hospitali ambayo tumejenga. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla anajua alikuja kukagua pale kwa *own source* hiyo hiyo ambayo ni fedha ya nanihii, kwa hiyo, asilete hayo mambo hayahusiani kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi tunataka mradi mkubwa Ziwa Victoria kwa sababu sisi ndiyo tuna ziwa liko Mkoa wa Mara, haiwezekani maji yakanaka Mkoa wa Mara yakaenda mpaka Tabora, huu ni ubaguzi kwa watu wa Mkoa wa Mara wote na siyo kwenye Jimbo la Tarime Vijijini peke yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Nyamongo; Mheshimiwa Rais alikuja pale na Mheshimiwa Profesa Mbarawa alikuwepo, mtu mwema sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa kwa kuzungumza. Mheshimiwa Rais akamwita pale akamwelekeza kuhusu ule mradi ambaulikuwa ni *white elephant* pale na akaahidi ndani ya wiki mbili atakuwa ameushughulikia, tangu mwaka 2017 mpaka leo...

TAARIFA

SPIKA: Kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Margaret Sitta.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji, namheshimu Mheshimiwa Heche tafadhalii sana kama unaomba maji, omnia maji lakini kuanza masuala ya ubaguzi wakipeleka maji Tabora inakuumma nini wewe? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Heche pokea taarifa hiyo.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, mama najua hata wewe una shida na maji ndiyo maana tunayalililia wote, sisi ndiyo tunatoa haiwezekani wewe upate ambaye hauna maji, sisi ambaulayo hatujapata, ndiyo hoja yangu iko

hapo, kwamba tuanze sisi kwanza wenye maji kwa sababu sisi ndiyo chanzo kiko pale. Maji hayajaanza Misri yalianza kutolewa hapa ndiyo yakaenda Misri kule. Sasa wewe upeleke maji Misri wapate kabla ya sisi kupata maji inawezekana wapi hiyo, hiyo ndiyo hoja yangu mimi, sijasema msipate. Mimi nia yangu na miaka yote na nimesema hapa watu wote nchi nzima wapate maji, lakini kwanza sisi wenye chanzo ndiyo wawe wa mwanzo sisi kuwekewa maji pale kwa sababu yako karibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maji ya Nyamongo na Mheshimiwa Profesa Mbarawa kwa sababu hiyo ndio maana mimi nimesema kuhusu hili suala la sumu ambalo maji yameingia jana, itakuwa *disaster* kwa sababu tungekuwa tumekamilisha ule mradi ambao aliahidi pale mbele ya Mheshimiwa Rais kwamba ataushughulikia ndani ya miezi miwilli, mitatu leo tusingekuwa tunazungumza kuhusu hilo suala. Sasa yale maji ya sumu yanayokuwa *pumped* pale *Ramapity* yakilingia kwenye ardhi huko yatachafua visima. Nyamongo ina *population* ya watu zaidi ya 50,000 itakuwa ni *disaster* kubwa sana kwenye maisha ya watu, kwa hiyo, namwomba sana, namwomba sana...

TAARIFA

SPIKA: Kuna taarifa kutoka kwa Naibu Waziri Mheshimiwa Nyongo.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa anayechangia kwamba *TSF* ile ya Nyamongo anayolalamikia kwamba inavujisha maji ya sumu ni kweli kwamba mwanzoni palikuwa na *technical problems* ambazo lile bwawa lilikuwa linavujisha maji ya sumu ambayo kwa kweli tulichukua hatua na kuna *group* la Makatibu Wakuu walikwenda kuchukua hatua na tumedhibiti.

Mheshimiwa Spika, msemaji anasema kwamba ile *TSF* kwa chini inapitisha maji ambayo yanakwenda kwenye vyanzo vingine vya maji. Nipende tu kumwambia kwamba,

hilo suala tumeshalidhibiti sasa hivi halivujishi na maji yanayotokea sasa hivi yamesababishwa na mvua inayonyesha ambayo imekwenda kwenye maeneo mengine ya wachimbaji wadogo ambayo kwa kweli hayana ile sumu ambayo Mheshimiwa anazungumza. Kwa hiyo nipende tu kutoa taarifa hiyo wananchi wasipate tataruki, ni kwamba sisi na wataalam wetu tumedhibiti hiyo hali. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Heche, pokea taarifa hiyo.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana tunafanya siasa kwenye maisha ya watu. Hili Mheshimiwa Nyongo nimetumia Waziri wako picha, nimetumia na *internal memo* ya mgodi ya jana ambayo wanasema maji yanamwagika kutoka *TSF* kwa sababu ya mvua lakini yanatoka kwenye *TSF*. Wao wamechukua hatua ya kununua *pump immediately*, hivi sasa wana-pump maji yanakwenda kwenye Ramapiti ambako huko ndio hakuna ile *cover anayoizungumzia*. Mimi nimezungumzia Ramapiti ambayo ipo huku juu ambapo makazi ya watu yapo, ndio wame- *pump* maji kwenda pale bila kuchukua hatua za kuweka kwanza hilo zulia chini ili lizuie yale maji yasi-*penetrated* kwenda chini. Hivi tunavyozungumza tangia jana tayari wana-pump maji yanaingia kwenye ardhi huko chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kabla ya kujibu asikilize kwanza aelewae na hili nimetumia Mheshimiwa Waziri wake na Waziri wa Mazingira na ndio maana nazungumza pia na Waziri wa Maji lichukuliwe kwa udharura wake lisije likaletea wananchi wa Nyamongo madhara kwa sababu watu wale kwa miaka mingi sana wameumizwa na yale maji ya sumu. Nazungumza hivi kwa uzito mkubwa sitaki kutoa matamko mengi lakini katika hili nataka niseme Mheshimiwa Nyongo msipochukua hatua kipindi hiki hatutakubali kufa kizembe kiasi hicho, tafadhali sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Heche, hiyo ni kengele ya pili.

Nilishakutaja Mhshimiwa William Mganga Ngeleja ambaye yuko Msekwa na atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza na Mheshimiwa Hawa Abrahaman Ghasia ajiandae.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote nikupe pole. Wewe ni Kiongozi wetu Mkuu, Kiongozi wa Mhimili huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, licha tu ya kwamba unastahili kilicho bora kuwahudumia wananchi wako lakini kweli kilichojitokeza hapa na naamini sisi sote ye yote yule kama lingemkumba lile jambo ambalo unalalamikia la mgao angepata maumivu kama unayoyapata.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo maisha yanaendelea na nafahamu kwamba uzuri wa utaratibu huu wa bajeti tulio nao hili bajeti tunayoizungumza kwa mijadala inayoendelea sasa ni kama vile tunafanya mjadala wa awali, hitimisho litafuatia mwishoni. Nachotaka kushauri tu ni kwamba kwa sababu Kamati ya Maji ipo, Kamati ya Mheshimiwa Mgimwa, Kamati ya Bajeti ipo lakini na Serikali yenye we inasikia naamini kwamba bado tuna fursa huko tuendako kurekebisha hizi kasoro ambazo zimejitokeza. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wengine kukupa pole sana kwa hili lililoitokeza.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote naunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema. Naunga mkono kwa sababu kama ilivyo ada hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, Prof. Mbarawa na timu yake nzima ina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni taarifa ya utekelezaji kwa bajeti ile ambayo tunaihitimisha sasa lakini pia wanaomba fedha kwa ajili ya miradi itakayoanza kutekelezwa kuanzia kipindi cha Julai mwaka huu hadi mwezi wa sita mwaka kesho.

Mheshimiwa Spika, kwenye hii sehemu ya kwanza ya taarifa ya utekelezaji, tunaunga mkono hotuba hii kwa sababu yako mambo yaliyofanyika Jimboni Sengerema. Kwa mfano, nafahamu kwa kadri ambavyo hotuba imezungumza

tumetengewa fedha kwa ajili ya ukarabati wa visima 70 na fedha imeshafika Sengerema, kwa hivyo, ni jambo jema na ndio tunaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, lingine nafahamu kwenye Kata ya Kasenye na Kata ya Nyamizeze tayari ujenzi wa miundombinu unaendelea maeneo ya Busuangili kule Kata ya Tabaruka lakini Kata ya Nyampande, Kata ya Buyagu pia inahusu Mradi wa Buyagu unaokwenda mpaka Kata ya Gichocho kupitia Kalangalala na Kata ya Busisi nafahamu kwamba kuna shughuli inaendelea ya ujenzi wa mradi. Pia kule Sengerema kuna Kijiji kimoja kinaitwa Kalumo fedha zilishatoka ukarabati umefanyika na wananchi wanaendelea kupata huduma. Hili ni jambo linalotufanya sisi tuendelee kuiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia pale Sengerema Mjini kimiundombinu tuna uwezo wa kupata maji zaidi ya asilimia 90 sasa kwa sababu toka mwaka 2017 tulizindua mradi mkubwa sana wa maji lakini yako baadhi ya maeneo ambako huduma haijafika. Kwa mfano, eneo la Misheni pale Sengerema Mjini, asubuhi nilikuwa naongea na Injinia Lupoja sasa wako kwenye hatua ya kumpata mkandarasi atakayefanya ununuzi wa vifaa ili tuanze kujenga *booster* pale Misheni Sengerema. Ni jambo jema na hili ni kwa sababu pia Wizara imekuwa ikifuatilia kwa karibu kusimamia huu mradi. Pia tuna eneo la Mwabalugi pale Zanzibar, kule kwetu Sengerema pia kuna eneo linaitwa Zanzibar, Kata ya Mwabalugi na yenye we inaendana na huu mradi ninaozungumza wa Misheni.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii pia imezungumzia utaratibu ulioanzishwa, Mheshimiwa Waziri anasema timu yake wameanzisha utaratibu wa kutekeleza miradi kupitia wahandisi wa ndani na kwa kiasi kikubwa wanatumia *force account*. Wanasema katika ujumla wake, ukiangalia aya ya 89 - 94 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema baada ya kupitia miradi iliyokuwa itekelezwe kwa utaratibu wa wakandarasa wameokoa zaidi ya shilingi bilioni 48. Ni jambo la kuipongeza Serikali kuwa wamefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, kati ya waathirika wa hilo zoezi la kupitia miradi hiyo upya ni sisi Sengerema na hasa Mradi wa Nyasigu, Lubungo hadi Ngoma A, huu mradi ulikuwa utekelezwe kuanzia mwaka 2018 lakini hadi sasa haujatekelezwa. Faraja niliyonayo kwa wana Sengerema ni kwamba jana saa mbili kasoro dakika nne jioni Mheshimiwa Waziri Prof. Mbarawa alinitumia *message* akiniarifu kwamba sasa lile zoezi la kupitia zile gharama za utekelezaji wa Mradi wa Nyasigu, Lubungo hadi Ngoma A limekamilika na siku tatu zijazo atatuma fedha, kwa sababu amesema kufikia mwisho wa mwezi huu atatoa shilingi milioni mia tatu za kuanzia. Kwa hiyo, niwataarifa wana Sengerema na hasa Kata ya Igalula Vijiji vya Nyasigu, Lubungo na Ngoma A kwamba ile habari ambayo tuliyokuwa tunaisubiri sana imeshaiva na tunaipongeza Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika hili pia nlishukuru sana Serikali kwenye aya ya 189 inazungumzia mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria na hasa katika vijiji ambavyo vinagusa Ziwa Victoria. Sasa mradi huu unahusu vijiji 301 na Mikoa mitano ya Mwanza, Kagera, Geita, Mara pamoja na Simiyu. Naamini kwa sehemu fulani pia utakuwa unagusa maeneo ambayo Mheshimiwa Heche alikuwa analalamikia lakini hiyo haiondoi hoja aliyozungumza yeze kwa kadri ambavyo uhitaji wa maji ulivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa sisi wana Sengerema katika mradi huu mkubwa wa vijiji 301, sisi tuna Kata za Kasenyi, Kifumfu, Katunguru, Nyamatongo, Ngoma, Kahumulo, Kasungamile, Busisi, Buyagu na Igalula. Kwa hiyo, ni jambo jema na kwa sababu sasa hivi tumeaarifiwa na Serikali kwamba tayari Mtaalam Mshauri ameshakamilisha usanifu wa kina tunajua hatua ifuatayo sasa ni ya kutangaza tenda kwa ajili ya kupata mkandarasi atakayeendelea kujenga huo mradi.

Mheshimiwa Spika, kwa yote haya, natumia nafasi hii kwa kweli kuipongeza sana Serikali, Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Waziri Aweso, Katibu Mkuu Prof. Kitila Mkumbo lakini pia Naibu Katibu Mkuu Injinia Sanga ambaye

alikuwa *MWAWASA* Mwanza lakini Wakurugenzi wa Wizara ya Maji tumekuwa tukiwasiliana nao sana na katika vitengo vyote kwa maana Wizara kwa ujumla wake lakini pia *RUWASA*, Mama *Emmaculata* pale Mwanza *Regional Manager* wa *RUWASA* kule Jimboni Sengerema kuna Injinia Lupoja kama nilivyosema lakini kuna Injinia Witike wanafanya kazi kubwa na wanastahili kupongezwa kwa namna ambavyo mmejipanga. Ombi langu kwa kutumia fursa hii pia ni kuwakumbusha, tunafundishwa katika taratibu zetu hapa tusitumie jina la Mheshimiwa Rais pasipokuwa na ulazima wa kulitumia lakini hii naweka kwenye kumbukumbu tu kwamba pale Sengerema kuna Kata moja ya Sima kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ni kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Ngeleja.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, naikumbusha Serikali ikumbuke ombi hilo, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nakupongeza sana Mheshimiwa Willam Mganga Ngeleja, Mbunge wa Sengerema. Umezungumza vizuri na kwa kweli kama alivyoitungia Mheshimiwa Mama Sitta hatuhitaji kuona wivu kwa wengine lakini nakupongeza kwa kupata vijiji 70 miradi ya maji. Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza.

MHE. DKT. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii uliyonipa niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana, maji ni uhai. Wataalam wanasema miili yetu hii zaidi ya asilimia 70 ni maji, unaweza ukaona umuhimu wa maji.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Prof. Mbarawa na timu yake nzima Mheshimiwa Naibu Waziri Prof. Mkumbo, Katibu Mkuu na wenzake kwa sababu wamenifanyia kazi nzuri katika Jimbo langu. Napenda pia

niwapongeze wenzangu walioko katika Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko. Mabilioni yale takribani 4.7 mlituletea kwa ajili ya kutekeleza miradi ambayo sasa hivi inaendelea kutekelezwa katika vijji 14 hayangeweza kutekelezwa bila mchango mkubwa wa Mkurugenzi Mtendaji ndugu yangu Masumbuko Stephano akisaidiwa na Meneja wa RUWASA, kwa kweli watu hawa wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, changamoto ninayoiona na *declare interest* mimi niko katika Kamati ya LAAC kila tunapokwenda kukagua miradi ya maji tunakumbana na changamoto ya uhaba wa wahandisi wazoefu kwa sababu wengi wako makao makuu. Wale ambao ni wazuri lakini bado hawajawa na uzoefu ndio wako katika Halmashauri. Kwa hiyo, napenda sana Mheshimiwa Waziri uliangalie hili kwamba wataalam wale kwa maana ya wahandisi wapatikane katika ngazi za halmashauri.

Mheshimiwa Spika, lakini si wahandisi tu, wahandisi wakiwa wengi peke yao bila kuwa na mafundi mchundo na *technicians* kazihaziendi. Tumeshuhudia hata kwenye miradi ya ujenzi wa madarasa au inayosimamiwa na TARURA wanashindwa kwenda hata kutazama jinsi gani kazi zinatekelezwa na timu zile zinazosimamia fedha kwa *force account* kwa sababu unakuta Injinia ni mmoja katika halmashauri na mimi nawaona huruma sana kwa sababu kazi hizo nazijua.

Mheshimiwa Spika, injinia mmoja hawezi kwenda kukagua miradi yote ya maji, injinia huyo huyo mmoja hawezi kwenda kukagua kama ni miradi yote ya ujenzi, *dispensary*, sijui tunajenga vituo vya afya unakuta sehemu nyingi tunasema imejengwa chini ya kiwango. Suala ni kwamba hatupeleki wataalam na *technicians* wa kutosha kuwasaidia. Zaidi ya hayo, unaona kabisa mapungufu ambayo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanayazungumzia, kuna mapungufu ya menejimenti ya mikataba. Naomba eneo hili mlisimamie kwa sababu mikataba isiposimamiwa ndiyo unakuta miradi haikukamilika vizuri, miradi inaingia katika *validation order* halifu mnapti matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kuwapongeza, naomba nishauri Wizara. Sasa hivi kuna tatizo la mafuriko ukifanya *trend and periodicity* yaani ukiangalia mwenendo wa ukame na mafuriko katika nchi hii kwa miaka mingi utakuta kwamba takribani kila baada ya miaka minne au mitano nchi hii tunapata ama ukame au mafuriko kama ilivyo sasa. Tukipata ukame tunapata shida ya chakula, tukipata mafuriko matokeo yake ndio hayo ambayo leo hi kila mtu akifungua *TV*yake anayaona; vifo vyta watu wanaosombwa na maji, madaraja yamechukuliwa, reli zinaharibika na mazao yanaharibika.

Mheshimiwa Spika, sasa tufanye nini? Naungana na Mheshimiwa Bura alivyosema, Mheshimiwa Waziri mimi ningekushauri changamoto hizi zinazotupata sasa zinazotokana na mafuriko zibadilishwe ziwe fursa. Fursa yenyewe ni ile aliyoisema Mheshimiwa Bura kujenga mabwawa. Mabwawa hayo si kwa ajili tu ya kuhifadhi maji kwa ajili ya kiyatumia baadaye lakini kiutalaam yanaweza kutusaidia kupunguza mafuriko ambayo yanayokwenda kuharibu miundombinu yetu. Kubwa zaidi mabwawa haya tukiyajenga yatahifadhi maji ambayo baadaye tutayatumia kwenye kilimo cha umwagiliaji, utaona sasa *yata-solve* lile tatizo la njaa maana ukija ukame tayari tuna maji ya umwagiliaji. Maji hayo tutayatumia kwenye matumizi ya maji ya majumbani na kufugia samaki. Kwa hiyo, nashauri kabisa kwa nguvu zote kwamba lazima tuangalie suala la kujenga mabwawa.

Mheshimiwa Spika, tatizo letu kama walivyosema wenzangu ni kwamba tunapopanga wakati mwingine tunasahau. Ukitazama kwa mfano Bwawa la Farkwa, Bwawa la Kidunda, nizungumzie hasa Farkwa iko kwenye *master plan* ya miaka ya 80 ambayo tuliiandaa. Sasa kama tungejenga Bwawa la Farkwa miaka hiyo ya 80 ambapo nadhani ilikuwa kama takribani dola 800,000 au 1,000,000, zamu hii sasa tusingetakiwa kujenga bwawa hilo kwa mabilioni ya fedha ambayo hatuwezi. Kwa hiyo, naona nisisitiza kwamba lazima tujenge mabwawa tuweze kuyatumia baadaye.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa tunamalizia, naomba nirudi kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kweli umenitendea haki, niliporudi Bungeni tarehe 4/9 ulikuja kunitembelea Wilaya ya Kakonko na nikakutembeza na nikakwambia ajenda yangu namba moja katika Jimbo lile ni maji, namba mbili maji, namba tatu maji na mengine yanafuata. Nakushukuru kwa kweli kwa kuwa umetusaidia zile shilingi bilioni 4.7 hazikutoka zote tu Serikalini tume-mobilize kama ulivyoshauri tumepata fedha ya Serikali, *UNFPA, UNICEF*, Mashirika ya Wakimbizi wote tumechang'a na tumepata miradi takribani 14. Nashukuru kwamba sasa umetutengea tena shilingi billioni 2.95 naamini zinakwenda kumaliza tatizo la maji katika Wilaya ya Kakonko.

Mheshimiwa Spika, naweza tu nikataja kama wanansikiliza wenzagu, mradi wa Kidudwe unaendelea una shillingi millioni 127, Nyagwijima shillingi millioni 208, Gwanumpu shillingi millioni 623, Muhange shillingi millioni 309, Kasongati shillingi millioni 191 na juzi tumepita tumekagua umekamilika wanakunywa maji, Kakonko Mjini shillingi milioni 300, Nabibuye shillingi milioni 650. Najua haya yanamuumiza kidogo, Katanga na Ilabilo shillingi milioni 107, Kizibuzigu Enabeli tumepata *package* ya shillingi billioni 1.6 na taarifa niliyonayo sasa wameanza kuchimba visima. Pia programu inaendelea ya *PforRya Rumashi*, Churazo, Kinyinya, Gwarama na Bukilo pia mmetutengea shillingi milioni 566. Kwa kweli nina kila sababu ya kimshukuru Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, ombi langu sasa Mheshimiwa Waziri wataalam waendelee kwenda ili miradi hii ikamilike.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja na namwomba Mheshimiwa Waziri arejee kwenye bajeti na wewe wakuongezee vijiji mpate maji. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza. Huyu ni Engineer wa masuala ya mambo ya umwagiliaji kwa hiyo ametupa mchango mzuri sana.

Mheshimiwa Hawa Ghasia nilikutaja basi atamalizia Mheshimiwa Senetor George Lubeleje. Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, nichukue fursa hii kutoa pole kwa wananchi wa Wilaya ya Mtwara, Mkoa wa Mtwara kwa kuondokewa na Mkuu wetu wa Wilaya; Mheshimiwa Evod Mmanda. Nitoe pole pia kwa familia yake, kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Rais wetu pamoja na ndugu na jamaa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi na daima tutaendelea kumkumbuka, amina. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa salamu za rambirambi kwa kifo cha Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, napenda na mimi niungane na wenzangu kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji. Napenda nimpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wamekuja katika Wilaya yangu ya Mtwara zaidi ya mara mbili. Nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa jinsi wanavyoiongoza nchi yetu na hivyo kutuwezesha kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuamua kuanzisha Wakala wa Maji *RUWASA*. Nazungumza hivyo kwa sababu kwenye Jimbo langu katika kipindi cha miaka mitano tumepata pesa za maji kwa kiasi kikubwa sana lakini matokeo ya utekelezaji wa miradi kwa kweli ilikuwa haionekani, baada ya kuanzisha *RUWASA* tumeanza sasa kuona kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji ni ya kuridhisha. Ndiyo maana nasema naipongeza Serikali yangu kwa kuanzisha Mamlaka ya Maji yaani *RUWASA*. Ni imani yangu kabisa kwamba kupitia *RUWASA* miradi ya maji itatekelezeka katika maeneo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninao mradi wa maji wa Mpapura Liowa ambao tangu mwaka 2016 uko asilimia 95 na mpaka leo ninapozungumza bado mradi ule na Mradi wa Msanga Mkuu upo asilimia 5 hiyo hiyo. lakini ninafurahi na ninaishukuru RUWASA baada ya kuanzisha kwasababu mradi wa Maji wa Mpapura Liowa kilichokuwa kimebaki ilikuwa ni ununuzi wa pampu maji yaweze kufika Liowa. Miundombinu mingine yote ipo tayari, nashukuru kwamba pampu hiyo imeagizwa na kama sio Corona nina uhakika kabisa kwamba pampu ingekuwa imefika na maji wananchi wangekuwa wanayapata. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali sana kwa pesa ambazo zimetengwa katika Jimbo langu la Mtwara Vijiji. Tunao mradi wa Maji wa Kilombero ambao umetengewa shilingi milioni 451, na tayari mkataba umesainiwa na tayari shilingi milioni 150 zimetolewa kwa Mkandarasi tayari kwa kuanza kutekeleza huo mradi.

Mheshimiwa Spika, tunao Mradi wa Nalingu ambao utapeleka maji katika Kijiji cha Nalingu, Miramba, Mnene na Mnazi. Ambao wenyewe una gharama ya shilingi 781,499,000 na tayari Mkandarasi ameshalipwa shilingi milioni 180. Tunao mradi wa maji wa mitambo Msimbati, ambao utapeleka maji katika Vijiji vya Mitambo, Litembe, Mngoji, Mnuo, Msimbati, Mtandi na Luvua na tayari Mkandarasi ameshalipwa shilingi milioni 200. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia tumeshaagiza pampu kwa ajili ya mradi wa Maji wa Msanga Mkuu ambao umeanza kutumika lakini pampu na yenyewe kidogo huwa inasumbua. Ninashukuru kwamba Mradi wa Liowa ambao umechukua muda mrefu sana tayari shilingi milioni 360,266,512 zimeshalipwa na pampu tunaitegemea kwamba itafika wakati wowote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mradi wa kuchimba visima 30 tulitengewa shilingi milioni 957 na tayari shilingi milioni 398 zimetolewa. Visima 15 vimeshachimbwa na visima 11 vimekutwa na maji ya kutosha. Niiombe sana RUWASA

iharakishe mchakato, wa kuandaa maandiko ili pesa ziweze kuletwa na hiyo miradi iweze kutekelezwa. Kwasababu kama visima hivi vlivyochimbwa vya Mngoji, Mitambo, Kilombero, Kawawa, Moma, Makome, Mwindi, Mmangopacha nne, Mkutimango, Mtama, Likwidi, Mnyija, Mkonye na Changarawe. Kama miradi hii itatekelezwa nna uhakika kabisa asilimia ya upatikanaji wa maji katika Jimbo langu la Mtwara Vijijini itaongezeka sana kutoka ile 57 tuliyonayo nina uhakika kabisa kwamba tunaweza tukafika hata asilimia 70.

Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Serikali yangu, kama ambavyo nilirudia kusema kwamba kuititia mradi wa RUWASA tuna matumaini makubwa sana tuendelee usimamizi na tuendelee kuwapatia pesa za kutosha ili waweze kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, niombe kuna miradi ambayo ni ya muda mrefu sana. Tunao mradi wa kutoa maji katika Kijiji cha Namanjere kupeleka Njumburi umechukua muda mrefu sana. Pia tunao mradi wa maji wa Kitere ambao nao umechakaa, Mradi wa Mkunwa kwenda Mbuo Mkunwa nao unahitaji kupanuliwa. Nashukuru kwamba wamepewa MTUWASA kwa hiyo, naomba tuendelee kuwasimamia ili kuhakikisha kwamba maji yanapatikana katika maeneo yote. Mradi wa Mbawala tumewapa MTUWASA ni matumaini yangu kwamba wataukarabati ule mradi na watafikisha maji katika maeneo mbalimbali ambayo yanahitajika kufikiwa na huu mradi.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kuipongeza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, kumpongeza Mheshimiwa Rais sana kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kuiongoza nchi yetu. Nimpongeze Waziri wa Maji, Katibu Mkuu wake, Naibu Waziri wake na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya. Tumechelewa sana kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini, muda mrefu ambao miradi ya maji ilikuwa katika halmashauri yetu kwa kweli uwezo ulikuwa ni mdogo pesa ni nyingi zimepelekwa lakini matokeo yaliyopatikana ni madogo sana ukilinganisha na pesa zilizotoka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nirudie tena kuiomba Serikali, mradi wa maji wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kuja Manispaa ya Mtwara ambao utapeleka maji katika Vijiji 26 vya Jimbo la Mtwara Vijijini. Ningependa Waziri atakapokuja kutuelezea atuambie ule mradi hatima yake. Kwasababu kuna wananchi wamepitwi na ule mradi, nyumba zao wameahidiwa fidia mpaka leo mashamba yao wanashindwa kuyaendeleza wakisubiria hatima. Kama ule mradi haupo basi tuambiwe ili wananchi waendelee na shughuli zao lakini pia wananchi wa Vijiji vile vya Mtwara Vijijini basi watafutiwe mradi mwingine ambao utapelekea maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, basi niishukuru sana sana Serikali yangu kwa yale ambayo wameyafanya katika Jimbo la Mtwara Vijijini. Nina imani kabisa kwamba wananchi...

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, asante naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga upo humu ndani! Haya nakuruhusu umalizie hizi dakika.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi niweze kuwa mmoja kati ya wachangiaji katika hoja hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali, kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa na nzuri wanayoendelea kuifanya katika kuiletea maendeleo Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, bila kumung'unya maneno, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watumishi wote na Watalaam katika Wizara ya Maji kwa kazi kubwa walioifanya katika kipindi hiki cha miaka minne ya kuhakikisha nchi yetu inapata maji safi na

salama kwa wananchi ili tuweze kuondokana na matatizo mengine yanayotokana na ukosefu wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa na taadhima niseme naipongeza Wizara hii kwa sababu katika Taarifa yake Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 10 inaonesha ni kwa kiasi gani upatikanaji wa maji umeongezeka kwa kiasi kikubwa sana na hasa vijiji. Kutoka mwaka 2015 upatikanaji wa maji vijiji ulikuwa asilimia 47 lakini sasa hivi tupo kwenye asilimia 70.1 jambo hili ni kubwa sana tunahitaji kuwapongeza sana wao pamoja na Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mjini hali kadhalika upatikanaji wa maji umeongezeka kutoka asilimia 74 hadi 84 mambo haya ni makubwa yanayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano tuna kila sababu ya kuipongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kipekee kabisa kuishukuru Serikali kwa kazi hii iliyofanywa hasa kwa upande wa Jimbo langu la Chilonwa. Yamefanywa mambo mengi sana, pamoja na shida ya maji iliyokuwepo. Nikupe pole mwenzangu Mheshimiwa Spika kwasababu kwako inaelekea wamekusahau sana. Lakini nimepata visima 36 katika miaka hii minne. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi walivyotuangalia kwa jicho la karibu sana. Katika visima hivyo 36, visima 12 vyote viko katika Kata za Buigiri na Chamwino. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunajua ni kwa sababu gani, sasa hivi ikulu yetu ipo Chamwino. Lazima kuwe na maji ya uhakika pale anapoishi Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli pamoja na haya yote yaliyofanyika bado upatikanaji wa maji si kwamba umetosheleza kwa watu wote, mapungufu yaliyopo hiyo asilimia 30 iliyobaki bado ni tatizo kubwa kwa wananchi wetu na ukiangalia sana ni wale walio ndani sana Vijiji ambao tunahitaji sana kuwaangalia.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Timu yako, nimeyaomba haya kama walivyosema wenzangu wengine walitangulia. Tunaishukuru Serikali kwa kuja kuunda *RUWASA* ili iweze kushughulikia masuala ya matatizo ya maji huko Vijijini. Naipongeza sana. Kupitia *RUWASA* kwanza tuna mawasiliiano nao ya karibu sana kama vile ilivyo *TARURA*. Tunaweza kuzungumza mambo mengine huko chini na tukaelewana, nimeomba kupitia *RUWASA* kuweza kupatiwa maji katika maeneo mengine ambayo bado yana uhitaji sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ukaribu kabisa kuna maeneo ambayo yana shida sana. Nimeomba kwa karibu kabisa na naomba Mheshimiwa Waziri katika hili nisaidie. Nimeomba kwenye Kata ya Magereko kuna Kijiji cha Chinangali kuna Kitongoji cha Mhata wako mbali sana na wana shida sana ya maji. Nimeomba Kata ya Dabalo, Kijiji cha Igamba Kitongoji cha Slalee kiko mbali sana, hawa watu wanatembea umbali mrefu sana kutafuta maji. Wakipatiwa maji nao angalau watajisikia kwamba nao Serikali yao imewakumbuka.

Mheshimiwa Spika, nimeomba sana Kata ya Haneti kuna Kijiji cha Mpakani, Ekwahemu Kitongoji cha Mpakani, Kata ya Haneti kuna Kijiji cha Umeku hawa wanakunywa maji yasiyokuwa safi wala salama. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri, nimeomba kupitia *RUWASA* lakini naomba hawa hebu waangalie ni namna gani wanaweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, katika suala la visima vilivyoimbwa na hasa eneo lile la Ikulu. Kuna Kijiji cha Msanga ambao walichimba kisima. Kisima kile kimepata maji mengi sana na mazuri baridi lakini kisima kile hakina miundombinu, hakina umeme. Tumejitahidi tunaendelea kuongea, nimeongea na *TANESCO* Wilaya, tumeongea na *TANESCOM* koa lakini kwa kweli bado hawajapatiwa umeme naomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili uwezekano wa kuwapatia umeme katika Kisima kile cha pale Msanga.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache niliyoweza kuongea kwa kumalizia muda huu, naomba sana nikushukuru lakini niunge mkono hoja kwa asilimia 100 huku nikisema kwamba mwaka huu 2020 ni mwaka wa uchaguzi na sisi wa Jimbo la Chilonwa kwa kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano tunamwambia Mheshimiwa Rais, kwasababu yupo kwetu. Jimbo la Chilonwa asihangaike sisi tupo asilimia 100 atapata kura zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana asante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa. Tutaendelea na uchangiaji kesho siku ya pili ambapo wakina Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Eng. Edwin Ngonyani, Mheshimiwa Edward Mwalongo, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na wengine wote ambao mmejiandikisha na upande wa pili pia tutapata nafasi ya kuweza kuchangia hoja ilio mbele yetu.

Nisitisite tu kwamba kwa kweli, Wizara ya Maji Waziri wake Mheshimiwa Prof. Mbarawa na Naibu Waziri Aweso ni watu rahimu sana, watu wema sana. Lakini Wizara hii ina changamoto kubwa na changamoto hii sio ya jana wala juzi imeanza zamani, mna kazi kubwa kweli. Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana nami kwamba hata Mheshimiwa Rais akifanya ziara nchini, hakuna kitu huwa kinampa tabu na kumchefua kama shida za maji.

Wale wasioamini wakumbuke ziara ya Mheshimiwa Rais katika Mkoa wa Lindi hali ilivyokuwa! Inakera mpaka inafika mahali ambako sitaki kuendelea kueleza kilichotokea. Kwa upande wa sisi wengine natumaini Mheshimiwa Waziri umenisikia, bado tupo pamoja kesho natumaini panapowezekana panaweza pakafanyiwa marekebisho. Kama wataalam wenu wanawapa taarifa ambazo za kujipendekeza, Wabunge tunaweza tukawapa taarifa za hakika za matatizo makubwa yapo wapi. Maana wapo watu

wakiambiwa lete taarifa, wanaleta taarifa kwa kuogopa na kutetemeka hasemi ukweli, huenda huo ugonjwa nao upo.

Waheshimiwa Wabunge, nafurahi kuwajulisha kuwa Mheshimiwa Ritta Kabati alitunukiwa Shahada ya heshima ya PHD, kutoka *Africa Graduate University* ya Zambia kwa jitihada zake za kutetea Walemaru na Shughuli za Kijamii. Kwa maana hiyo kuanzia sasa atajulikana kama Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati. (*Makof/ Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu nampongeza sana Mheshimiwa Kabati na nawasihi Wabunge wengine kuendeleza jitihada za kusaidia Jamii pamoja na kujendeleza kielimu kwani elimu haina mwisho. Hongera sana Mheshimiwa Ritta Kabati. (*Makof/ Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, natumaini mmeshapata habari za kwamba Mbunge mwenzetu katika kipindi kilichopita. Aliyekuwa Mbunge wa Mafia Mheshimiwa Abdulrahman Shah amefariki dunia na kwa jinsi hiyo basi tunamuomba Mwenyezi Mungu aipokee na kuiweka roho yake mahali pema peponi.

Lakini tumepokea taarifa sasa hivi kutoka kwa Mbunge wa Mtwara Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwamba DC wa kule ndugu Evord Mmanda na yeye amefariki, tunatoa pole sana kwa familia ndugu, jamaa na marafiki na yeye tunamuombea Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kumalizia tatizo la Corona lipo, na kwa hiyo tunawaomba kila mmoja wenu maelekezo ya wataalamu si mengi sana ukizingatia ni kupunguza safari au kuziacha kabisa zisizokuwa za lazima. Hili ni *serious* kabisa kwamba safari isiyo ya lazima usiende. Nawa mikono kwa maji tiririka mara kwa mara na sabuni tumia *sanitizer*, epuka misongamano. Si maagizo mengi, sio maelekezo mengi sana lakini ni vizuri kuyazingatia. Mbunge yoyote ambaye hajisikii vizuri nasisitiza tuwasiliane na kuhusu mambo mengine nilishasema na narudia tena yanayohusu

utaratibu hayo Spika wenu anayazingatia sana, kuhakikisha kwamba hupati matatizo yoyote. (*Makofi*)

Kwa hiyo, badala ya kuja huku ukiwa na homa aina moja au nyingine ni bora tukapeana taarifa kutoka kule ulipo. Nirudie tena mambo yanayohusu utaratibu ndio maana Spika ni Mbunge mwenzenu kwa hiyo naelewa. (*Makofi*)

Tuambiane tu tutahakikisha unapata kila aina ya msaada unaohitajia. Basi baada ya maneno hayo kwa vile shughuli za leo zimekamilika na tunaendelea kesho na hoja hii hii basi nihairishe shughuli za Bunge hadi kesho saa nane kamili mchana.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumanne,
Tarehe 28 Aprili, 2020 Saa Nane Mchana)*